**30 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini na Saba– Tarehe 30 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibeti, Mbunge wa Busokelo.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Daktari Samia Suluhu Hassan imefanya mambo makubwa na kuzidi. Hivi karibuni ulifanya ziara Mkoani Mbeya na ulitembelea halmashauri zetu ikiwemo Busekelo, tunakushukuru sana. Lakini mojawapo ya changamoto ulizokutana nazo kwa wananchi wote kwa ujumla ni kwamba, katika nchi yetu kumekuwepo na tatizo la kutolewa kwa hati za ardhi za kimila ambazo hazithaminiwi na taasisi za kifedha za kibenki, hususan wanapokwenda kukopa na wamekuwa wakizungushwa mara njoo leo mara njoo kesho na hatimaye wanakata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wananchi wanaoishi vijijini wameendelea kuwa maskini kwa sababu hawapati mikopo kupitia hati za kimila za ardhi na tatizo hili limetokana na sheria Na. 5 ya mwaka 1999 ambayo ndio inayotoa hati hizi. Je, ni mkakati gani wa Serikali ili kuwarahisishia wananchi hawa wa vijijini waweze kupata hati kama wanavyopata mijini na ziweze kuthaminiwa na benki kwa kubadilisha sheria hii Na. 5 ya mwaka 1999? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye anaendelea kutupa afya na kutekeleza majukumu yetu kama hivi leo tumekutana hapa pamoja, tunaamini Mwenyezi Mungu ataendelea kutujalia kutupa neema zake.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakibete Mbunge wa Busekelo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria zetu za ndani ya nchi, hati zetu zote, zile zinazotolewa na Wizara yenyewe, zile zinazotolewa kama hati za kimila zote hizi ni hati zinazotambulika kisheria. Hati zote hizi ikiwemo na hati za kimila zinayo fursa ya mwenye hati hiyo kupata mikopo kwenye taasisi zote za kifedha. Inaweza kuwa yako maeneo ambayo ziko taasisi ambazo hazikubali tu kwa sababu ya matakwa yao au mpango kazi wao lakini kwa mujibu wa sheria hati ya kimila ambayo yenyewe pia inatolewa kwa vipindi kama vile vya hati inayotolewa na Wizara yenyewe, miaka 33, miaka 66, hata miaka 90, zote hizi zinatambulika kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nitoe wito kwa taasisi zote za kifedha ambazo zimeridhiwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya kazi yake nchini kwa mujibu wa sheria za nchi, waendelee kutumia na kutoa fursa kwa wale wenye hati za kimila au hata hizi hati ambazo zinatolewa na Wizara ya Ardhi kuwa ni hati halali zinatambulika na zinatoa fursa kwa mtanzania au kwa mmliki wa ardhi nchini kupata stahiki yake ya mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaendelea chini ya Wizara ya Ardhi kufanya kazi ya upimaji wa ardhi yetu kwenye ngazi za vijiji tunapima mashamba, tunapima maeneo ya makazi, tunapima maeneo ya taasisi na maeneo yote yanayotolewa hati na Wizara imeshaanza na inaendelea inapita kila halmashauri kuendelea na kazi ya upimaji wa ardhi kwa maana ya kupanga matumizi bora ya ardhi kwenye ngazi za vijiji na hati hizo zinatolewa. Kwa hiyo, hati hizi watanzania waendelee kuziona kama ni hati kamili na

inatambulika kisheria na inatoa fursa ya mikopo kama ambavyo nimeeleza awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza hayo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu imepata nafasi adhimu ya kuandaa michuano ya *AFCON* mwaka 2027. Ukifatilia maandalizi ya michuano hii kwenye mataifa mengine ilivyofanyika kama Ivory Coast inafanyika katika upana mkubwa na inagharimu mambo mengi sana. Sasa Serikali kuna maandalizi ambayo yanatakiwa yafanyike ya ujenzi wa viwanja vya kuchezea, ujenzi wa viwanja vya mazoezi, *transport facilities* kwa maana ya mabasi pia *emergency hospitals.* Serikali haioni haja ya fedha zinazotokana na magawio, fedha zinazotokana na CSR kwa asilimia kadhaa na fedha ambazo zinatokana na *betting* kwa asilimia kadhaa, ikaelekeza kama ni mfuko maalum kwa ajili ya maandalizi ya *AFCON* kwa kipindi cha miaka mitatu kama mkakati wa makusudi wa Serikali kujiandaa na tukio hili kubwa ambalo linakwenda kuheshimisha nchi yetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sanga Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme nilitegemea kupata swali hili kutoka kwake, kwa sababu ndio Mwenyekiti wetu wa michezo hapa Bungeni na ni mwanamichezo halisi.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali hili nataka nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu

amewezesha Taifa hili kutambulika sasa katika michezo kwa kiwango cha juu ambako tunaiona michezo imeshamiri na Watanzania wanashiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo pia na michezo ya kukimbia na mpira na mpaka imetufikisha kuwa na ligi bora Afrika na kuwa kwenye nafasi ya tano. Tunaona ligi ya Zanzibar nayo imeshamiri, tumeshapata bingwa, tumeona pia ligi ya Bara tumeshapata bingwa pia tumeona bingwa wa muungano ameshachukua kombe na yeye. Kwa hiyo, tunaona michezo namna inavyoshamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameridhia Taifa letu kuungana na nchi za Kenya na Uganda kuwa wenyeji wa mashindano ya *AFCON* mwaka 2027. Hii ni heshima kubwa na muono wa mbali kwa sababu michezo kama hii inapofika mahali ni nchi inapewa heshima ziko fursa nyingi zinatumika na hakika Taifa lazima lijipange vizuri ili kuweza kumudu kupokea wageni, kuhimili mashindano ndani ya nchi na mpaka kukamilika kwakwe na ikiwezekana basi Taifa wenyeji tuwe mabingwa ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameshauri Serikali tutumie mapato kadhaa *CSR* zetu katika kuimarisha ujenzi wa viwanja. Leo hii tumeshaweka mikataba ya kujenga uwanja Jijini Arusha. Tunaendelea na ujenzi tutaweza kuanza wakati wowote hapa Dodoma lakini tunakarabati viwanja kadhaa, ikiwemo Uwanja wa Benjamini Mkapa, Uwanja wa Uhuru kule Mwanza Kirumba, Uwanja wa Majimaji Mkoani Ruvuma na upande wa Zanzibar Uwanja wetu wa Amani utatumika pia kwa ajili ya michezo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nauchukua ushauri huu na Wizara iko hapa wiki mbili zilizopita tulikutana tukaweka mpango wa kuunda kamati kuanzia sasa ili kuanza maandalizi. Nitoe wito kwa watanzania heshima ambayo nchi hii tumeipata ambayo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameridhia michezo hii kuchezwa hapa Tanzania, sisi tutakuwa tumepata fursa na kwa hiyo kila mmoja ajiandae katika kuhakikisha kwa pamoja tunaiandaa timu yetu kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kila mmoja anajiandaa kupokea ugeni mkubwa wa timu mbalimbali kutoka duniani kote; tatu, tufungue fursa za kibiashara kwa sababu hawa watakapokuja watalala, watakula, watakunywa na watapata huduma mbalimbali ikiwemo na usafiri hapa nchini. Kwa hiyo, fursa hii na ushauri ambao tumeupata hapa utatusaidia pia katika kuboresha. Kwa hiyo, niahidi kwamba ushauri tumeupokea na tutaufanyia kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, iliwahi kutolewa pendekezo hapa Bungeni kwamba mfumo wetu wa elimu ubadilishwe kidogo kiasi kwamba mwanafunzi anapojiunga na chuo kikuu, anapomaliza mwaka wa kwanza mtaala uwe katika namna ambapo, ule mwaka wa kwanza akimaliza afuzu kupata *cheti (certificate)*. Kwa hiyo, kama atapata changamoto zozote akalazimika kukatisha basi anaondoka angalau na cheti. Akiingia mwaka wa pili mtaala umuoneshe kuwa amefuzu ngazi ya stashahada ili hata akipata changamoto akiamua kuondoka basi awe angalau ameondoka na cheti cha stashahada. Atakapomaliza mwaka wa tatu ndio aweze kupata shahada.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vile pendekezo hili mimi naliona kama lina tija, je lini Serikali italifanyia utafiti na kuweza kujenga mazingira ya kufuata utaratibu huo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba samahani Mheshimiwa alirudie niweze kujua dhana ya cheti, diploma, digrii ile namna alivyoweza kuainisha niweze kuielewa vizuri, niweze kujibu vizuri swali hilo, naomba samahani arudie tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, pendekezo hili lililetwa katika muktadha kwamba, mtaala wetu uwe katika namna ambapo mwanafunzi anapojiunga na chuo kikuu mfano kozi ya miaka mitatu, mtaala uwe kwa namna ambapo anapomaliza mwaka wa kwanza, awe amefuzu mambo ambayo yanamwezesha kupata cheti *(Certificate)* katika ile taaluma ambayo anasoma. Kwa hiyo, kama atapata changamoto, labda ameshindwa kulipa ada akikatisha masomo pale angalau aondoke na kitu mkononi, cheti chake. Wakati anamaliza mwaka wa pili, awe tena ameshafuzu katika mazingira ambayo kama atalazimika kukatisha masomo pale angalau aondoke na stashahada*(diploma).* Sasa anapokamilisha mwaka wa tatu anakuwa sasa anapata ile shahada *(Degree)*. Hii itasaidia kwamba kama mtu alipata changamoto katikati ya masomo asiondoke mikono mitupu, ndio dhana hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali hili lilivyoulizwa kwa sababu mimi nilikuwa mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam naona linampasa Waziri wa Elimu ndio alijibu, kwa sababu lina mambo mengi maana hata mimi ningekuwa na maswali ya kumuuliza Mheshimiwa Mbunge. Sasa itanirahisishia akijibu Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo swali lako tutalileta kama swali la msingi ili tupate nafasi ya kumsikia Mheshimiwa Waziri wa Elimu akitueleza kuhusu jambo hilo. Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

**JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni lini Serikali itaboresha Sheria ya Uhamiaji ili kuwezesha urahisi kwa wawekezaji wa kimkakati kusudi waweze kupata uraia wa uhamiaji kutokana na heshima ya uwekezaji wao kwenye Taifa

letu, kama ambavyo wanafanya mataifa mengine? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahawanga, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inayo mifumo pia inayo sheria za uhamiaji nchini kama nchi nyingine zote duniani. Sheria zetu hizi zinaruhusu pia watu kutoka nje kuja nchini kwa vibali maalum na kufanya shughuli mbalimbali. Wako ambao wanakuja kwa lengo la utalii, wako ambao wanakuja kikazi, wako ambao wanakuja kwa uwekezaji. Serikali yetu imeweka sheria lakini imefungua milango ya wawekezaji kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuja kuwekeza kwenye sekta mbalimbali. Ni kweli kwamba wawekezaji hawa tumewaweka kwenye madaraja wakiwemo wale wawekezaji wenye miradi ya kimkakati ambayo ni miradi ya gharama kubwa na ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, anahitaji kujua kama Serikali ina mpango upi wa hawa wawekezaji wa miradi ya mikakati na ya muda mrefu na gharama kubwa, kuwa na wao wapate hadhi ya Taifa hili. Serikali yetu pamoja na sheria zetu tulizonazo tumeweka eneo ambalo mwananchi yoyote kutoka nje anahitaji kuishi nchini anafuata sheria za nchi yetu na zipo sheria na zinaruhusu na hii pia inatoa fursa hata kwa wawekezaji wakubwa. Moja kati ya sheria zetu awe ameshaishi nchini kwa miaka 10 na uwekezaji huu mkubwa kimkakati hauwezi kuwa mwaka mmoja, miwili, mitatu, minne.

Mheshimiwa Spika, hawa wa miaka 10 ni wale ambao wameishi hapa kwa muda mrefu na wanahitaji uraia lakini kwa wawekezaji kupitia Wizara ya Mipango na Uwekezaji na chombo chetu cha Taasisi ya Uwekezaji Nchini *(TIC)* tunapojiridhisha kwamba huyu ni mwekezaji wa mradi wa gharama kubwa na ni wa muda mrefu unahitaji usimamizi wa karibu hawa nao tumewafungulia dirisha lao la kuona umuhimu wa wao kuwa

sehemu yetu. Lakini tunachofanya ni kumpa fursa mbalimbali za kikodi, kufanya biashara katika mazingira rahisi pia kumpa ushirikiano katika uendeshaji wa biashara hiyo na atakapoishi hapa zaidi ya miaka kumi anapata nafasi ya kupata kuomba uraia na anafikiriwa ili mradi tu atakapopata uraia lazima akubali kuendelea kuwa Mtanzania. Pia awe ni miongoni wanaochangia uchumi, kwa kuwa umekuwa na mradi mkubwa na wa gharama kubwa huyu atakuwa mmoja kati ya wanaochangia uchumi wetu, lakini pia azungumze lugha yetu ya Kiswahili na lugha ikiwa ya kiingereza na haya yote yanapokuwa yanafikishwa uhamiaji hakuna shida kwa sababu pia anasimamiwa na Taasisi ya Uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tunapojiridhisha kwamba huyu ni mwekezaji wa mradi mkubwa, gharama kubwa na ni wa muda mrefu unahitaji usimamizi wa karibu, hawa nao tumewafungulia dirisha lao la kuona umuhimu wa wao pia kuwa sehemu yetu. Tunachofanya ni kumpa zile fursa mbalimbali za kikodi kufanya biashara katika mazingira rahisi lakini pia kumpa ushirikiano katika uendeshaji wa biashara hiyo na atakapoishi hapa zaidi ya miaka kumi anapata nafasi ya kuomba uraia na anafikiriwa ili mradi tu atakapopata uraia lazima akubali kuendelea kuwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini awe ni miongoni mwa watu wanaochangia Uchumi, kwa kuwa na mradi mkubwa na wa gharama kubwa huyu lazima atakuwa ni mtu mmoja kati ya wanaochangia uchumi wetu. Pia azungumze Lugha yetu ya Kiswahili au na Lugha nyingine ya Kingereza na haya yote haya yanapokuwa yanafikishwa uhamiaji, hakuna shida kwa sababu pia anasimamiwa na Taasisi ya Uwekezaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, basi nitoe wito kwa wawekezaji ambao wako tayari kuja kuwekeza nchini kwamba, Serikali yetu imefungua milango, lakini pia imetoa fursa kwa Wawekezaji wakubwa miradi ya kimkakati wanapata nafasi lakini pia zile fursa za kupata punguzo kwenye maeneo kadhaa ikiwemo na masharti ya kikodi yanapungua. Pia kupata ardhi, ule urasimu nao

umepungua na hii ndiyo kwa sababu sasa tunashuhudia sasa wawekezaji wengi wanaingia hapa nchini. Kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha na kuboresha sheria zetu kama ambavyo imeshauriwa na Mheshimiwa Mbunge. Pia, tutaendelea kufungua milango ya uwekezaji wote kutoka nje na kwa kuangalia kuwa hawa wanaowekeza wana uzalendo lakini pia ni salama kwa usalama wa Taifa letu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia majukumu au shughuli za Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye nchi nyingi duniani kumekuwa na sera lakini sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ambayo inatoa nafasi kwa wahitimu wa vyuo mbalimbali kujitolea kufanya kazi Serikalini na kupewa posho kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye nchi yetu tunayo Taasisi ya Wakala wa Ajira wa Serikali *(TaESA)* ambayo inapeleka wahitimu wachache kwenye maeneo mbalimbali ya kazi na kule wanapewa posho kidogo, lakini walio wengi wanajiombea wenyewe, kwa baadhi waajiri wanawalipa lakini wengine hawalipwi kabisa. Je, Serikali haioni ni muhimu wa kuwa na sera, sheria, kanuni na miongozo kama hii ili wale wote ambao wanajitolea (wahitimu) waweze kulipwa posho? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba Jijini Dar es salaam, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwenye michakato ya ajira ambayo pia inasimamiwa na Wizara ya Kazi iliyoko Ofisi ya Waziri Mkuu.

Tunatambua kuwa tunayo makundi yanayopata ajira rasmi na wale ambao hawajapata ajira lakini wanatamani na wanapenda kujitolea. Kitendo cha kujitolea kinamsaidia sana mwajiriwa, kwanza kuimarisha uelewa wa sekta anayojiajiri, ambayo pia anakwenda kujitolea lakini pia anapata uzoefu mkubwa sana na waajiri wanatusaidia kubainisha watu wenye weledi, uaminifu, uadilifu katika utumishi wa ajira hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi na Ajira iliyoko Ofisi ya Waziri Mkuu nayo inafanya kazi kwa karibu na Baraza la Ajira *(LESCO), LESCO* iko kwenye Wizara yetu. Baraza hili lina ratibu pia ajira za kujitolea kupitia Sheria zetu za Kazi na Ajira. Tunafanya kazi pamoja na chombo ulichokitaja Mheshimiwa cha *TaESA* ambacho chenyewe ni chombo ambacho kinaratibu hawa wote wanaokwenda kwenye ajira za kujitolea na wakisubiri fursa za kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafasi hizo kama nilivyosema, wanapata nafasi ile ya kuwa wanapata uzoefu wa ajira zao, wawe wanatambuliwa kwenye chombo kile na kinasimamia maslahi yao. Kinahamasisha waajiri wale ambao wamewapokea wanaokwenda kujitolea kupata motisha wanapotekeleza majukumu yao, ile inasaidia sana kwa sababu hata mwajiri huyu iwe ni sekta ya umma au sekta binafsi anapohitaji waajiriwa, kuajiri watu ambao wanataka kufanya kazi kwenye taasisi yake anaanza na wale ambao wanajitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sheria zetu zinaruhusu watu kujitolea kupitia chombo chao cha *TaESA* akiamua kujiunga na chombo kile anasimamiwa kwa maslahi yake na motisha kwa kujenga mawasiliano kati ya *TaESA* pamoja na mwajiri. Kwa hiyo, kuwepo usimamizi natambua kwamba wako wengine hawaja kitambua hiki na wanajitolea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia swali hili ni vyema sasa wale wote ambao wanajitolea kwenye sekta mbalimbali wakajua kwamba tunacho chombo kinaitwa *TaESA* ambacho wao wakijitambulisha na kujisajili watasimamiwa wao wanaojitolea

pamoja na kile chombo kinafanya mazungumzo, kinamtambua pia mwajiri na kumhamasisha mwajiri kuona kuwa hawa wanapofanya kazi wanahitaji huduma zao kama vile chakula, mavazi na huduma nyingine muhimu kama afya. Kwa hiyo, mwajiri lazima atenge kidogo motisha kwa ajili ya kuwafanya hawa waweze kufanya kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, chombo tunacho na baraza tunalo na Wizara ya Kazi na Ajira ipo, iko Ofisi ya Waziri Mkuu. Jukumu lake moja ni kusimamia na kuhamasisha pia hawa ambao wamesoma kwenye ngazi fulani au wana ujuzi wa aina fulani pale ambapo wanasubiri ajira wanaweza kujitolea kwenye eneo ambalo ajira yake anaweza kuitumia vizuri na vyombo hivi vinafanya kazi ya kuungana na hawa waajiri kwa kuona motisha zao wakati wote wanapokuwa kazini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Igalula.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan inatekeleza miradi mikubwa katika nchi hii ukiwemo Mradi wa Reli wa *SGR* Loti Na. 3 wa Makutupora – Tabora, Loti Na. 4 Tabora – Isaka na Loti Na. 5 Isaka – Mwanza. Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwepo na changamoto kubwa ya mradi huu kwa sababu unapita katika maeneo mbalimbali ya watu, lakini tathmini ilikwishafanyika na watu waliambiwa wasiendeleze maeneo hayo kwa sababu mradi uko tayari. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika tathmini zilizofanyika zaidi ya mwaka mmoja watu wameshindwa kulima mashamba yao, nyumba zinaanguka wanashindwa kukarabati kwa sababu tathmini imeishafanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini kibaya zaidi watu walipisha mradi kwa kuondoa wapendwa wao, (makaburi) tayari yamekwisha ondolewa lakini mpaka leo wananchi hao hawajalipwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu nini kauli ya Serikali kwa wananchi ambao wanadai fidia zao hasa wa makaburi waliopisha tayari

mradi huu ili kutoa sintofahamu inayoendelea katika wananchi wetu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ni swali la muhimu lakini nilikuwa natafakari hapa kama ni la kisera ama swali ambalo inabidi lijibiwe na Waziri wa Kisekta kwa sababu linahusu jambo maalumu eneo maalumu. Kwa hiyo, kwa taratibu zetu za kikanuni hapa zinataka maswali yanayoelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni yale ambayo ni kisera na yapo chini ya utawala wake ama yako chini ya Ofisi yake. Mheshimiwa Daud Protas Venant, swali lako litakuja kama swali la msingi Wizara inayohusika itapata nafasi ya kutoa ufafanuzi juu ya swali hilo.

Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi. *(Makofi)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni dhahiri wote tunajua uwekezaji mkubwa ambao umefanywa na Serikali yetu hasa katika Bandari ya Dar es Salaam tukitegemea kwamba mizigo mingi inapita kwenye *central corridor* kuelekea katika nchi jirani hasa Burundi, Rwanda na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na *check points* za polisi zaidi ya 44, Mizani, *TRA* zaidi ya tatu lakini pia kuna mizani zaidi ya nane kwenye *lane* ya *central corridor* kutokea Bandari ya Dar es Salaam mpaka kuelekea Rusumo. Serikali kuweza kupunguza *trans time* na kuwasaidia wasafirishaji wasisafirishe mizigo kwa gharama hatimaye wakashindwa wakaona ni mzigo mkubwa. Ilianza kujenga *one-stop inspection centers,* tunacho cha Vigwaza pale Pwani lakini tuna kingine Dumila pale Morogoro. Kulikuwa na ujenzi ilibidi ufanyike Manyoni – Singida na ujenzi mwingine ilibidi ufanyike Nyakanazi – Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, lakini baadhi ya vituo bado havijajengwa na ujenzi wake uliishia njiani umesimama. Sasa ili kuweka azma nzuri ya Serikali ni lazima vitu hivi vimalizike ili viweze kutusaidia

kwenye kusafirisha hiyo mizigo na hatimaye uwekezaji tuliofanya kwenye Bandari ulipe kwa watu kupitisha mizigo katika Bandari yetu ya Dar es Salaam. Sasa ni nini kauli ya Serikali kwenye kumalizia ujenzi wa hivi vituo ili hatimaye Bandari yetu iweze kufanya kazi katika malengo ambayo Serikali inayatarajia? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, uko mpango wa kuimarisha ukaguzi, lakini mbili mapato kupitia mizigo inayoingia ndani ya nchi kupitia Bandari ya Dar es Salaam na kwenda nje ya nchi yetu na inapita pia ndani ya nchi lakini pia kwenda kwenye mipaka yetu. Mkakati ambao Serikali umefanya ni kujenga vituo vya ukaguzi kwa malengo yote mawili, usalama lakini pia kupata mapato na vituo hivi vimejengwa kimkakati.

Mheshimiwa Spika, tunapopeleka magari Nchi za Burundi, Kongo na Rwanda za ukanda huu maana yake lazima tuimarishe vituo kwenye barabara kuu inayotoka Dar es Salaam inapita Dodoma - Singida na kwenda Mkoa wa Kagera kule Ngara kupitia Biharamulo, lakini pia hatujajenga kwenye barabara hii tu hata maeneo yote yanayoingia na kutoka kwenye mipaka yetu nchini kama vile Horohoro – Holili – Mtukula na huku Tunduma tunaimarisha, kujenga na kazi ya ujenzi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuna vituo vingi vina mahitaji haya yote na ni lazima tujenge vituo kwa ajili ya ukaguzi kwa usalama lakini pia kwa ajili ya mapato. Kazi ya ujenzi inaendelea na ujenzi huu unaendelea kadiri tunavyopata fedha za kujenga vituo hivi. Kwetu kama Serikali ni muhimu sana kwa usalama wa nchi lakini ni muhimu sana katika kukusanya mapato ipasavyo ili tuweze kutunisha mfuko wetu kwa ajili ya ujenzi wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango mkakati upo wa Ujenzi wa Vituo hivi vyote vya ukaguzi kwenye maeneo haya. Pia, sasa tumeamua tunapojenga katikati ya nchi tunajenga kwa umbali ambao hauwezi kuleta usumbufu kwa wasafirishaji kwa kukaguliwa kila mahali wanapopita bali watakuwa wanakaguliwa kwenye vituo hivyo maalumu kama vile Vigwaza, Dodoma labda Manyoni kama ulivyosema Manyoni na huko Nyakanazi – Biharamulo na hata kule mpakani Ngara.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kufanya haya kwa kuhamasisha mataifa ya nje kutumia Bandari yetu ya Dar es salaam na bado tunao mpango wa kuimarisha Bandari za Mtwara na Tanga na sasa Serikali inao mpango wa kujenga Bandari Bagamoyo na kule tutaimarisha hiyo *corridor* yote, kuhakikisha kwamba usalama wa nchi tunapoingiza nchi nyingi kuja kuchukua mizigo hapa unaimarika. Pia, upatikanaji wa mapato pia na wenyewe tunauimarisha. Kwa hiyo, mipango hii yote ipo ndani ya Serikali, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 479

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mlowo Mbozi**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mlowo Wilayani Mbozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2023/2024, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa maboma katika vituo vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itatenga shilingi milioni 600 kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mlowo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kata ya Mlowo ina wakazi zaidi ya laki sita na wakazi hao wote wanahudumiwa na zahanati moja tu na sisi kama Wabunge tumekuwa tukiomba sana kuweza kupatiwa Kituo cha Afya kwenye Kata ya Mlowo. Sasa nilitaka niiulize Serikali kwa nini sasa haijaona umuhimu wa kutenga hizo fedha kwenye mwaka wa fedha ujao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Kalembo pamoja na Malangali kwenye Wilaya ya Ileje? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali imeweka mpango mkakati wa ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati ikiwemo Kata hii ya Mlowo – Mbozi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha ambayo itatengwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni muda wa matazamio kwa maana ya *maximum duration* ambayo tumeweka, lakini tunaweza tukapata fedha wakati wowote na kupeleka kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo hiki cha afya. Kwa hiyo, nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tunatambua umuhimu wa kituo hiki na tunaendelea kutafuta fedha ili twende kujenga kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kuhusiana na Kituo cha Afya cha Malangali na katika kata hiyo nyingine naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tulishawaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini kuanisha maeneo ya kata za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwa kata zile ambazo zinakidhi vigezo. Kwa maana ya idadi ya wananchi, umbali kutoka kituo cha afya cha karibu zaidi lakini pia na hali ya kijiografia. Kwa hiyo, kama Kata hizi zinakidhi vigezo hvyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Rais – TAMISEMI tutachukua orodha yake tuweke kwenye mpango mkakati kwa ajili ya kwenda kujenga vituo hivyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini kwenye hiki Kituo cha Afya cha Mlowo Serikali inakuwa na majibu mengi tofauti tofauti? La kwanza mlituambia kwamba mimi nilipouliza kama Mbunge wa Jimbo mlisema itajengwa kwa kutumia fedha za *World Bank*. Leo dada yangu Mheshimiwa Juliana Shonza ameuliza unatuambia kitajengwa 2026. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Mbozi alipiga simu TAMISEMI tukakubaliana kuna fedha zimekuja za ujenzi wa Serikali zitaenda kujenga kwenye hiki Kituo cha Afya cha Mlowo sasa kituo kimoja cha afya majibu matatu, sisi tushike lipi kwenye hili jibu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mwenisongole, amefuatilia kwa karibu sana kuhusiana na Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Mlowo na nimewasiliana naye mara kadhaa na nimemhakikishia tu kwamba Serikali ina vyanzo vingi na vyanzo mbalimbali vya ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, tuna vyanzo vya *World Bank* ambavyo tunatarajia wakati wowote fedha zikipatikana zitakwenda kwenye vituo vilivyoainishwa, lakini tuna mipango ya Serikali kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya miaka inayofuata 2024/2025 na 2025/2026 na hata tukipeleka fedha za *World Bank* mwaka huu wa fedha ujao bado tuna awamu ya pili ya Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mlowo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mbunge hii ni faida kwake kwamba tuna mpango wa *World Bank* fedha zikipatikana kituo hiki kitaanza kujengwa wakati wowote kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna mpango wa 2025/2026 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kituo hicho ili kiweze kuwa *fully* na kuweza kutoa huduma vizuri zaidi. Kwa hiyo, majibu ya Serikali ni yale yale, dhamira ni ile ile kujenga Kituo cha Afya cha Mlowo na

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kujenga Kituo hicho, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo sasa aulize swali lake.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba swali langu lipate majibu.

**SPIKA:** Swali lako ni Namba 480.

Na. 480

**Kumalizia Ujenzi Wa Kituo cha Afya Itenka – Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Itenka – Nsimbo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Itenka ambapo majengo matano yamejengwa; jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD);* jengo la maabara; jengo la upasuaji, jengo la wazazi; na jengo la kufulia. Aidha, jengo la *OPD* na maabara yamekamilika na yanatoa huduma tangu Mwezi Oktoba, 2022. Jengo la wazazi, jengo la upasuaji na jengo la kufulia yapo katika hatua ya ukamilishaji ambapo ili kuyakamilisha, kiasi cha shilingi milioni 100 kinahitajika. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa hili swali ambalo limejibiwa.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Itenka sasa hivi kina takribani ya miaka miwili na kila siku tukiuliza kuhusu fedha zilizobaki kwa sababu tuliahidiwa milioni 850, lakini mpaka sasa hivi zimeletwa milioni 480, kiasi ilichobaki ni kingi. Wananchi wa Itenka wanatamani sana ile hospitali iweze kukamilika.

Je,ni lini Serikali itaweza kukamilisha? *(Makofi)*

Katika Kata ya Ugala kuna Kituo cha Afya, nacho tuliahidiwa milioni 850 mpaka sasa hivi zimekuja milioni 500. Je, ni lini Serikali wataleta fedha za Kituo cha Afya cha Ugala? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Mama Anna Richard Lupembe amefuatilia kwa karibu sana kuhusiana na fedha za awamu ya pili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Itenka na Ugala. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wakati wa ujenzi huo wa vituo hivi vya afya tuliweka mpango wa kujenga vituo hivi kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza tulipeleka milioni 500 kwa vituo vyote kote nchini na imekamilika majengo yale matano ya awamu ya kwanza. Awamu ya pili tutakwenda pia kwa vituo vyote ambavyo vimekamilika awamu ya kwanza kwa ajili ya majengo mengine kama wodi za wanaume, watoto na wanawake kawaida. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, vituo hivi viwili ambavyo vimeshapata fedha za awamu ya kwanza, tutakamilisha kwanza majengo ambayo hayajakamilika ya awamu ya kwanza na baadae tutaingia kwenye awamu ya pili na nimhakikishie kwamba, tutapeleka fedha kwa ajili ya kazi hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama nimewaona. Wale waliokuwa wamesimama mwanzo nimewaona watapewa nafasi lakini maswali mafupi, moja kwa moja kwenye swali.

Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Ikola ni miongoni mwa vituo ambavyo vimejengwa na Halmashauri ya Wilaya.

Je, ni lini watapelekewa fedha za kukamilisha hicho kituo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze Halmashauri ya Tanganyika kwa kujenga Kituo cha Afya cha Ikola kwa mapato ya ndani na niombe kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri kutuletea taarifa rasmi ya kiasi cha fedha ambacho wanahitaji ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI itafute fedha na kupeleka kwa ajili ya ukamilishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, Serikali ina mapango gani wa kuipandisha hadhi zahanati ya Toangoma kuwa Kituo cha Afya kwa kuwa Kata ya Toangoma ina idadi kubwa ya watu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tulikwishatoa maelekezo na mwongozo unaelekeza hatua za kufuata kwa zahanati ambazo zina sifa ya kupandishwa hadhi kuwa vituo vya afya. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni, kufanya tathmini kwa kushirikiana na Mganga Mkuu wa Halmashauri na Mganga Mkuu wa Mkoa, kuona kama vigezo vyote kwa maana ya eneo na idadi ya wananchi vinakidhi kuwa na zahanati na

kupandishwa hadhi kuwa kituo cha afya ili tuweze kuanza hatua za upandishaji wa kituo cha afya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nyarioba kama ilivyoahidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali iliahidi na ni maelekezo ya Mheshimiwa Makamu wa Rais aliyatoa tukiwa kwenye ziara kule Kigoma, Nyarioba. Tayari tumeshakiweka kwenye orodha ya vituo ambayo vitapata fedha za umaliziaji kupitia Benki ya Dunia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 481

**Kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itagawa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na kupata Halmashauri mpya ya Kingonsera?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mahitaji na umuhimu wa kuanzisha maeneo ya kiutawala ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, uanzishaji wa maeneo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya

Serikali ya Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na (Mamlaka za Miji) Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadae kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA I. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kuweka haya maeneo ya kiutawala ni pamoja na kusogeza huduma kwa wananchi. Kwa kuweka hiki kipaumbele cha kuboresha miundombinu wakati wananchi wanaifuata hiyo huduma mbali, haioni kwamba inapingana na kipaumbele cha kusogeza huduma kwa wananchi?

Je, Serikali inaahidi nini Wananchi wa Tarafa ya Hagati na Mbuji wanaopata huduma hii mbali sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba, Serikali imeanzisha maeneo mengi sana ya kiutawala, maeneo mengi bado hatuna Ofisi za Halmashauri. Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuomba hapa na Serikali imeendelea kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Wakurugenzi, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Ofisi za Kata, Ofisi za Vijiji, bado tuna gap kubwa sana kwenye ujenzi wa miundombinu ya ofisi za utawala ambazo zipo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, tuliona ni busara tukamilishe kwanza miundombinu katika mamlaka zilizopo ili ziweze kutoa huduma na baadaye tuendelee na hatua ya kuanzisha mamlaka nyingine,

kwa sababu haina faida kuanzisha mamlaka ambazo hazina miundombinu na haziwezi kuhudumia wananchi kwa ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hilo Serikali inalitambua na dhamira yake ni kusogeza huduma pamoja na kuwa na miundombinu bora zaidi na tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili niwahakikishie wananchi wa Tarafa ambazo Mheshimiwa Mbunge umezitaja katika Jimbo la Mbinga Vijijini kwamba Serikali inatambua changamoto zao na Mheshimiwa Mbunge amezisemea na Serikali inaendelea kuzifanyia kazi, kuhakikisha wanapata huduma karibu zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea imekuwa zaidi ya miaka 10 sasa na tumefuata taratibu zote ambazo tulipaswa kufuata.

Je, Serikali ipo tayari sasa kupandisha Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea iwe Mji kamili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsnate sana. Serikali ilikwishafanya tathmini ya Mamlaka za Miji Midogo kote nchini. Zipo Mamlaka ambazo zina sifa au zinakidhi vigezo vya kupanda kuwa Halmashauri, mamalaka hizo zinasubiri muda na taratibu nyingine zipandishwe hadhi kuwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pia zipo Mamlaka ambazo kimsingi hazikidhi vigezo vya kuwa Halmashauri, kwa hiyo, Serikali inafanya utaratibu wa kuona hatua zaidi za kuchukua kwa zile Mamlaka

ambazo hazikidhi na hazina sifa za kuwa Halmashauri na bado zipo na taarifa rasmi itatolewa na Serikali kuhusiana na hatua ambazo zitafuata. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Chinguile tutalifanyia kazi suala la Nachingwea tuone kama linaangukia kwenye *category* gani na hatua gani inafuata, baada ya hapo utapata taarifa rasmi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ina Halmashauri ya Mji Mdogo wa Lusewa ambayo ilitangazwa toka Mwaka 2014, mpaka sasa hivi haina watumishi walio kamili kwa maana ina waliokaimu tu.

**SPIKA:** Swali.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Je, Serikali inaweza sasa kuhakikisha kwamba, tunapata watumishi katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewa ili ifanye kazi yake iliyokusudiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Mkurugenzi na Menejimenti yake kuhakikisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewe inafanyakazi kwa kupata Wakuu wa Idara ambao kwa ngazi ya Mamlaka ya Mji wanapatikana ndani ya Halmashauri. Kwa hiyo, naomba nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, kuhakikisha mapema iwezekanayo anatafuta wataalam ndani ya Halmashauri yake wenye sifa za kukaimu nafasi hizo waendelee kushika nafasi hizo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lusewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Masanja, swali la nyongeza.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itaharakisha kuligawa Jimbo la Magu kuwa Majimbo mawili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ugawaji wa Majimbo unafanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwa ni sehemu ya wadau.

Mheshimiwa Spika, naomba nipokee hoja ya Mheshimiwa Mbunge Mary Masanja na tutaiwasilisha Serikalini ili vigezo hivyo viweze kuzingatiwa na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 482

**Ujenzi wa Barabara za Jimbo la Mlalo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha kuweka changarawe katika barabara inayounganisha Tarafa za Umba, Mlalo, Mtae ya Hekicho, Lugurua hadi Manolo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayotajwa na Mheshimiwa Mbunge yapo katika barabara ambayo imesajiliwa kwa jina la Kwekanda – Hekicho - Mkomazi yenye urefu wa kilomita 20.5 inayounganisha Tarafa za Umba, Mlalo, Mtae ya Hekicho, Lugurua hadi Manolo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga barabara tajwa kwa kiwango cha changarawe pamoja na kujenga miundombinu ya kupitisha maji ya mvua, ambapo mwaka 2021/2022 Serikali ilitumia shilingi milioni 500 kuifungua ili iweze kupitika.

Aidha, katika mwaka 2022/2023, shilingi milioni 201.5 zilitumika kujenga vivuko 14 vya maji, kuweka changarawe kilomita 8 na tabaka la zege mita 80 kwa baadhi ya vipande vyenye miinuko mikali. Ndani ya Mwaka 2023/2024 shilingi milioni 300 ilitumika kwenye uwekaji wa changarawe kilomita 7.2, tabaka la zege mita 110 na kujenga vivuko 5 vya maji.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa jumla ya kilomita 15.2 zimeshawekwa changarawe. Katika Mpango na Bajeti wa Mwaka 2024/2025, Serikali imetenga shilingi milioni 313 ili kukamilisha uwekaji wa changarawe, tabaka la zege mita 200, kujenga vivuko 7 vya maji ambapo barabara hiyo itaweza kupitika katika kipindi chote cha mwaka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa mara ya kwanza naomba nikiri wazi kwamba Serikali imejibu maswali kwa ufasaha sana, swali hili limejibiwa kwa ufasaha na hali ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa namna ambavyo amekuwa akiendelea kujibu kwa ufasaha maswali ya Wabunge hapa Bungeni, namuombea Mwenyezi Mungu aendelee kumbariki na fahamu zake zizidi kukua kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Barabara hii imekuwa ni mkombozi mkubwa haswa hivi karibuni tulipata mvua ambazo zilifunga barabara kubwa ya *TANROADS*, barabara hii ikawa ndiyo mkombozi. Lakini zipo kona kali ambazo magari makubwa kuanzia tani nne na kuendelea yanashindwa kupita kwa ufasaha.

Je, Serikali ipo tayari kurekebisha hizi kona takribani tatu ili barabara hii iweze kuwa na ufanisi zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kupokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge pia na mimi nimpongeze kwa utumishi wake uliotukuka kwa wananchi wake na hasa kwa sababu amekuwa akifuatilia sana masuala ya miundombinu ya barabara kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la nyongeza alilouliza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge *TARURA* inatambua uwepo wa hizo kona kali tano, ambazo kimsingi zinazuia magari yenye zaidi ya tani nne kuweza kupita. Katika mwaka 2024/2025 Serikali imetenga milioni 328 kwa ajili ya kuanza kurekebisha kona mbili kati ya hizo kona tano ambazo zimebainika ni kali sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kipindi cha mwaka 2024/2025 Serikali itatumia hizi fedha milioni 328 kupasua miamba na kuweka tabaka la zege ili magari yaweze yenye ukubwa wa kuanzia tani nne hadi 10 yaweze kupita. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itahakikisha inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu na hasa katika barabara uliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Van Zealand, swali kwa kifupi.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 tulipokea milioni 500 kwa ajili ya kujenga

barabara ya kiwango cha lami kutoka Manyinga kwenda Madizini yenye urefu wa kilomita moja, lakini jambo la kushangaza barabara hii imejengwa mita 500. Kipindi kifupi cha miezi sita barabara hii ikawa imeharibika.

Je, Serikali ipo tayari kufanya ukaguzi maalum wa kujiridhisha na matumizi ya hizi fedha milioni 500? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba inajenga na inakarabati barabara kwa viwango vinavyokubalika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala alilolitaja kuhusuana na hii barabara yake ya Manyinga, tumelichukua na tutaliweka katika vipaumbele kuhakikisha fedha zinatengwa na barabara zinarekebishwa na kujengwa kwa viwango vinavyokubalika, kwa sababu hiyo ndiyo dhamira ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu sasa aulize swali lake.

Na. 483

**Hitaji la Soko la Uhakika la Muhogo**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la uhakika la zao la mihogo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali imeendelea kuimarisha soko la Zao la Muhogo ndani na nje ya nchi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya Masoko ya Muhogo na kuandaa majukwaa ya biashara yanayohusu zao hilo ili kutafuta soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji huo, Wizara inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa Soko la Muhogo la Kahama (Musoka) na miundombinu ya kukaushia muhogo katika Mkoa wa Kigoma ili kuendeleza biashara ya zao hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imehamasisha wadau waliopo katika mnyororo wa thamani wa zao la Muhogo kujiunga pamoja na kuanzisha Chama cha Wazalishaji na Wasindikaji wa Zao la Muhogo Tanzania *(TACAPPA)*. Uhamasishaji huo umewezesha kuuza nje ya nchi tani 21,620 za muhogo mkavu wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 7.6 kwa mwaka 2023. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo kwa wananchi wa Wilaya ya Kakonko ambao ni wakulima wazuri wa Zao la Muhogo ni bei ya zao hilo. Hata wakulima wakipata mnunuzi bei inakuwa chini.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuanzisha Chama cha Wasindikaji wa Zao la Muhogo Wilayani Kakonko ikiwa ni pamoja na kuwapa mikopo ili waweze kuboresha zao hilo? *(Makofi)*

Swali la pili, zao la Muhogo ni zao la chakula na baishara kwa Mkoa wa mzima kwa maana ya Wilaya zake zote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri anayezungumza yupo nyuma yako. Mheshimiwa Naibu Waziri, urejee kwenye kiti ulichokuwa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Aloyce Kamamba malizia swali lako la pili.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, swali la pili lilikuwa kwamba zao la Muhogo kwa Mkoa wetu wa Kigoma linalimwa katika Wilaya zake zote. Sasa, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, zao hilo linafanyiwa utafiti ili kupata mbegu bora ambayo inatoa mazao mazuri zaidi? Ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali inatambua kuna changamoto ya bei ya zao la muhogo ndiyo maana katika moja ya jitihada kubwa tulizofanya ni kuanzisha Chama cha Wazalishaji na Wasindikaji wa Zao la Muhogo Tanzania *(TACAPPA)*. Kwa hiyo, kwa sasa hivi wanatakiwa washuke katika Wilaya na kwa sababu Mbunge ameomba hilo tutalifanya hivyo kwa kuhakikisha tutakuwa na tawi katika Halmashauri ya Kakonko ili iweze kuwasaidia kupata bei ya uhakikka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu tafiti nimthibitishie kwa asilimia 100 *TARI* wameshafanya tafiti ya zao la Muhogo na sasa hivi wana mbegu ambayo inaweza kuzalisha mpaka tani 50 kwa heka moja. Kwa hiyo, tutakachokifanya sasa hivi ni kuhakikisha *TARI* inapeleka mbegu katika maeneo ya Kigoma ili iweze kuleta tija zaidi kwa wananchi hawa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai sasa aulize swali lake.

Na. 484

**Kufufua Kipande cha Reli ya Kuingia Uwanja wa Ndege**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua kipande cha Reli kuingia Uwanja wa Ndege wa *KIA* kwa ajili ya kusafirisha Mizigo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K. n. y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRC* imeendelea kuboresha miundombinu ya reli iliyopo, ikiwa ni pamoja na kufufua njia za reli zilizokuwa zimefungwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, *TRC* imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 23 kwa ajili ya ukarabati wa njia ya Reli ya Kaskazini ikiwemo kipande cha njia ya Reli ya kuingia uwanja wa Ndege wa *KIA* na kwa sasa shirika linaendelea na taratibu za manunuzi ya reli nzito za ratili 80 kwa yadi kwa ajili ya matengenezo ya njia hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkitaka kuzungumza zungumzeni kwa karibu basi. Yaani mtu yuko mbali unazungumza naye; kweli tuko Bungeni hapa? Siyo sawasawa. Kelele zinakuwa zinazidi kwa sababu mnazungumza mtu mmoja yuko mbali mwingine mbali. Nenda kwenye kiti chake zungumza naye.

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, maswali ya nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kweli ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri mazuri mazuri sana. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuweka mpango wa kuunganisha reli ili iweze kusafirisha chuma, mradi unaotegemewa kukamilika wa chuma ya Liganga iweze kuja

mpaka kwenye kiwanda cha *Machine Tools* ambacho kina-*process* na kuunda vyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali iliahidi kujenga kituo kidogo cha kupandisha abiria na mizigo kwenye eneo la Rundugai pale sokoni. Je, Serikali ina mpango gani kutekeleza ahadi hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wazo alilotoa la kuunganisha reli aliyoitaja na kiwanda ama Liganga, kwa maana ya kutoka Kusini kwenda Kaskazini, tulichukue kama ni wazo jipya lianze kufikiriwa lakini tuna mipango mingi ya nijia za reli. Ninadhani wazo alilolitoa kuunganisha Liganga na Kiwanda cha *Machine Tools* litakuwa ni wazo jipya ambalo Serikali tulichukue kwa ajili ya kulifanyia *study*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la kufufua hiki kituo cha abiria, ninaomba pia Serikali tulichukue tuweze tuweze kulifanyia kazi ili kutoa huduma kwa wananchi hawa ambao watanufaika na hiki Kituo cha Reli cha Mgai, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaenda Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kunti Majala, swali kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Faustine.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Faustine Dugulile, ninaomba swali lake liweze kupata majibu ye Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali Na. 485? Mheshimiwa Kunti ...

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri Mheshimiwa Waziri. Ni swali Na. 485.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, 485.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinaeleza namna ya kuuliza swali. Sasa, usipotaja namba sijui unataka ujibiwe swali gani. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

Na. 485

**Kukamilika kwa Pantoni ya MV Magogoni**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza: -

Je, ni lini matengenezo ya pantoni ya *MV. Magogoni* iliyopo nje ya Nchi yatakamilika na kurejeshwa nchini ili ianze kutoa huduma kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa kivuko *MV. Magogoni* unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa wezi Desemba 2024 na kurejeshwa nchini ili kuanza kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, kivuko hiki kimetumia muda mrefu sana na wananchi wa Kigamboni na watumiaji wengine wa kivuko hiki wameendelea kupata adha kubwa lakini Serikali imekuwa na ahadi zisizotekelezeka.

Mheshimiwa Waziri umesema mwaka 2024 kivuko hiki kinakwenda kukamilika. Ni tarehe ngapi? Kwa sababu suala la miaka imekuwa kila leo mnatupa. Tunataka tarehe ili wananchi hawa waondokane na adha hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza ninamkumbusha tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kigamboni na Dar es Salaam kwa ujumla wake kwamba, ukarabati unaofanyika kwenye MV Magogoni ni kama kukijenga upya, kutokana na ukweli kwamba kivuko kilikuwa kimechoka na tunakileta katika hali ambayo ni mpya kabisa. Ndiyo maana kimeendelea kuchukua muda mrefu ili kuboresha kiwe kivuko cha kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tarehe ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge; sisi kivuko unaweza ukasema tarehe mbili lakini katika safari ikachukua muda. Tunachotaka kukuhakikishia ni kwamba, kabla ya mwisho wa mwezi Desemba 2024, kivuko kitakuwa kimefika na kuanza kutoa huduma Kigamboni na Dar es Salaam, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga, sasa aulize swali lake.

Na. 486

**Ujenzi wa Barabara ya Kisangara – Nyumba ya Mungu**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Kisangara – Nyumba ya Mungu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kisangara – Nyumba ya Mungu yenye urefu wa kilometa 17.5, inaendelea na inategemewa kukamilika mwezi Agosti mwaka huu wa 2024. Baada ya Usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri na yenye kutia matumaini ya Serikali kwenye swali hili lakini nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwanga – Kikweni – Vuchama, kilometa 28.98, kilometa 16.008 zimekamilika kiwango cha lami, kilometa 5.4 mkandarasi yuko *site*. Swali langu ni, kwa kuwa barabara hii iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025; je, ni lini basi Serikali itamalizia kipande kilichobakia cha kilometa 7.752? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nipokee pongezi za Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutengeneza miundombinu.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri barabara hii nimeitembelea na tunatambua ilikuwa ni ahadi ya Kiongozi wa Kitaifa kwamba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. Tumeendelea kufanya kwa awamu na kweli tumepokea maombi kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge lakini pia Mkoa wa Kilimanjaro, kuomba tukamilishe hii barabara yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumetenga kilometa mbili, zikawa zimebaki kilometa tano na ninamwagiza Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro aweze kuwasiliana na *TANROADS* pamoja na Wizara, kuona uwezekano wa kuijenga hii Barabara yote kwa kiwango cha lami ili tukamilishe hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyokuwa ameitoa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru, mwaka 2022/2023 tuliambiwa tuorodheshe barabara za kipaumbele, Jimbo la Rungwe tuliorodhesha barabara kutoka Katumba – Kapugi mpaka Ushirika kwenye Kata ya Mpuguso. Je, ni lini barabara hyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara aliyoiainisha tulikuwa bado hatujaifanyia usanifu. Kwa hiyo, tutakachofanya kwanza ni kuingiza kwenye utaratibu wa kufanyiwa upembuzi yakinifu na kisha kuifanyia usanifu ili sasa tuweze kujua gharama na kuingiza kwenye mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 487

**Ujenzi wa Barabara ya Utegi Hadi Kilongwe**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Utegi hadi Kilongwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Utegi – Kilongwe yenye urefu wa kilometa 47.4 imekamilika. Kwa sasa taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya barabara hiyo kuanzia Utegi – Shirati itakayokuwa na urefu wa kilometa 27 zinaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, barabara za kiulinzi zilizopo mipakani ni muhimu sana kwa ulinzi na usalama wa Taifa letu lakini kwa bajeti ambayo imewasilishwa jana kwa mwaka wa fedha 2024/2025, hakuna hata senti tano ambayo imetengewa barabara hizi kwa nchi nzima. Je, ni lini Barabara ya Kiulinzi inayoanzia Kirongwe Wilayani Rorya Mpaka Nyanungu Wilayani Tarime itaenda kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kipande kilichopo kwenye mradi wa ujenzi wa Barabara wa kuanzia Tarime mpaka Mugumu, kwa maana ya Tarime Mjini mpaka Mogabiri kimeharibiwa sana na mvua ambazo zinaendelea kunyesha. Ninataka kujua Serikali inachukua mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inaenda kuziba yale mashimo na mahandaki ambayo yamejijenga kwenye hicho kipande cha lami ili kuweza kurudisha usafiri na usafirishaji kwenye Jimbo la Tarime Mjini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli Barabara ya Ulinzi ya Kirongwe – Sirari ninajua inaenda mpaka Kegonga inaendelea kufanyiwa ukarabati kuhakikisha kwamba inapitika. Katika kipindi hiki tunachokifanya katika

barabara hii ni kuhakikisha kwamba inapitika kwa kiwango cha changarawe na inapitika muda wote, wakati Serikali tunatafuta fedha kuzijenga hizi barabara ambayo ni moja ya kipaumbele cha Wizara na Serikali kuhakikiksha kwamba Barabara za Ulinzi zinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, zipo Barabara za Ulinzi ambazo zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na siyo kwamba Barabara zote Tanzania za Ulinzi hazijengwi. Zipo ambazo zipo kwenye mpango. Maana yake amesema Barabara zote za Ulinzi; Hapana, siyo kweli. Zipo ambazo zinaendelea kujengwa na zingine zitatangazwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipande kilichoharibika cha kutoka Tarime kwenda Mogabiri, kipande hiki ni cha kiwango cha lami ambayo ni ya zamani. Ninamshakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika mkandarasi ambaye sasa anajenga kambi eneo la Serengeti pale Mugumu, ambaye atajenga, ndiye atakayejenga pia kipande hicho cha lami. Ataifumua na kuijenga upya. Kwa hiyo, tutakachofanya ni kuangalia uwezekano.

Mheshimiwa Spika, hatutaijenga kwa kuziba, bali tunaifumua yote na kuijenga yote. Kwa sasa Meneja wa Mkoa wa Mara ahakikishe kwamba yale mashimo ambayo yapo anayaziba kwa muda ili yasije yakaleta changamoto kwa watumiaji, wakati tunasubiri kuijenga hiyo barabara yote ambayo tulishaitangaza, ahsante. *(Makofi)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninaleta tangazo la wageni niko nalo hapa mbele.

Tunaanza na wageni waliokaa Jukwa la Spika; kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Anton Mwantona ambao ni Machifu

kutoka Wialaya ya Rungwe na Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi na Serikali. Machifu wanaongozwa na Chifu Edward Mwanjali. Machifu wanaweza kusimama na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia viongozi wa chama wanaongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rungwe, Ndugu Meckson Mwakipunga, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ally Said Kiumwa, Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Gabriel Mwakagenda ambaye ni Katibu wa Mbunge, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni wangu mmoja ambaye ni Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo kutoka *Serena Hotel*, Ndugu Seraphin Lusala, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa ... *(Makofi)*

Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na mimi sitasema sababu iliyowafanya mpige makofi. Kwa hiyo, sitaisema. *(Kicheko/Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu Waziri wa Ujenzi; hawa ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Ileje. Yupo Mheshimiwa Farida Mgomi ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Ileje. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo Ndugu Hassan Lyamba, Katibu wa CCM Wilaya, Ndugu Maoni Mbuba Katibu Mwenezi wa Chamba cha Mapinduzi Wilaya, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Wilaya, Ndugu Weston Ndabila, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa CCM Wilaya, Ndugu Glory Mjema na Ndugu Ubatizo Songa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje; karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwantona anao wageni wengine ambao ni Ndugu Meshack Mwaheleja, Katibu wa Jumuiya ya Vijana Chama Cha Mapinduzi Kata ya Rufingo. Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Kenny Laurance, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya, Ndugu Noel Sibonike, Mwandishi wa Habari na Ndugu Megy Bahesya, Mtangazaji, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Najma Giga ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ambao ni viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mvomero Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Twaha Mpembenwe ambaye ni Muasisi wa Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani, karibu sana Muasisi. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Simon Songe, wapiga kura wake kutoka Busega. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni Madiwani na mpiga kura wake kutoka Kasulu Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira *(IGUWASA)* kutoka Igunga Mkoa wa Tabora, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Igunga Mheshimiwa Sauda Mtondoo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni rafiki zake na wapiga kura wake kutoka Kishapu Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ambao ni viongozi wa Taasisi ya *Ruzinga Development* kutoka Jijini Dar es Salaam na Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni Wajumbe wa Vyama vya Ushirika kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana. Wageni 62 wa Mheshimiwa Cosato David Chumi ambao ni Timu ya Itifaki kutoka Jimbo la Mafinga Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni wanafunzi 70 na walimu watano kutoka shule ya wasichana ya Kiislamu Kilimanjaro *(Kilimanjaro Islamic Secondary School)* ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 70 ambao ni wanachama wa *Scout* kutoka Shule za Sekondari *St. Ritta* na Madale za Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matanganzo ya wageni ambayo tunayo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, leo Alhamisi tarehe 30 Mei, 2024, mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge Saa 7:00 Mchana kutakuwa na kikao pamoja na mimi na mimi niko chini ya Mwenyekiti. Kikao hicho kitafanyika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wanawake wote mnakaribishwa kwenye kikao hicho. *(Makofi)*

Baada ya Tangazo hilo Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na muda ninasimama kwa Kanuni ya 76 lakini ninaomba Mwongozo wako. Kwa muda mrefu umekuwa ukitoa angalizo au ukituasa na kutufundisha kama Mwanasheria lakini pia kama Spika.

Mheshimiwa Spika, kuna hili tatizo linajitokeza katika Ukumbi wako wa Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Msimamizi wa Shughuli za Serikali katika Bunge. Ndiyo utaratibu na tumekuwa tukisema na tukitoa Mwongozo mara kwa mara tukiomba Mheshimiwa Waziri Mkuu apate nafasi ya kutusikiliza tunapouliza maswali lakini Mawaziri wanapojibu maswali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo tunahitaji kwenda kwenye kiti chake kwa ajili ya kushauriana naye mambo madogo madogo. Wakati mwingine Waheshimiwa Wabunge wanatumia muda mrefu sana kwenye Kiti cha Mheshimiwa Waziri Mkuu na si tu Mheshimiwa Waziri Mkuu hata Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Hata wakati mwingine unaona kabisa anashindwa kusikiliza hotuba zinazoendelea kwa sababu watu wamekaa kwenye kile kiti kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako, baada ya maonyo uliyoyatoa na makatazo uliyoyatoa huko nyuma na hali bado inaendelea, kuna utaratibu gani unatakiwa kufuatwa baada ya kutokusikilizwa kwa ule ushauri uliyotupa? Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na kwa kweli alilolizungumza hata hapa linaendelea, Wabunge wanaendelea kuzungumza wakati nimesimama. Kwa hiyo, unaweza kuona namna ambavyo tunazikosea kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, kipindi hiki ni kigumu kidogo kwa Wabunge kwa sababu kuna yale mambo yanakuja hapo baadaye, kwa hiyo, kila mtu mawazo yake kidogo yanakuwa yamevurugwa. Pamoja na hayo ni muhimu sana kuheshimu mkutano huu ambao ni wa kwetu sisi wenyewe ambao kwa kweli tumepewa dhamana na nchi yote inatutazama sisi na maamuzi yetu hapa.

Sasa kwenye kipindi cha maswali, kwanza nilishawahi kusema hapa katazo, waacheni Mawaziri wasikilize kwa sababu kuna maswali ya nyongeza yanaulizwa ambayo yanagusa Wizara mbili, inabidi awe amesikia aweze kujibu na yeye, kuongeza majibu ili majibu yawe sahihi kwa huyu Mbunge na ili yawe majibu ambayo kwa kweli yanatosheleza hoja ya wananchi wake. Sisi sasa muda wa maswali wenzetu wanauliza sisi tunaongea na Mheshimiwa Waziri, yaani kama vile Mheshimiwa Waziri anapotea, yaani kama ama hana muda nawe ama huwa hakai Bungeni. Tunajivuruga sisi wenyewe kwa kweli. *(Makofi)*

Kimsingi nilishakataza kipindi cha maswali watu kuja upande wa Mawaziri, nilishakataza hapa ndani na leo nisisitize, upande wa Mawaziri Waheshimiwa Wabunge tuwe na utulivu kipindi cha maswali ili wasikilize kinachoulizwa humu ndani, moja.

La pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu anapoingia na kutoka humu ndani nilishatoa mwongozo, anapokuwa anatoka hujui ni nini kinamtoa hapa Bungeni, kwa sababu katika hali ya kawaida huwa anakaa na sisi hapa, anavyotoka maana yake lipo jambo la haraka ama la dharura ndilo linalomtoa hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, mnasimama mstari mzima mkitaka Mheshimiwa Waziri Mkuu asimame kuwasalimu, sasa mnatarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu atawapita wakati ninyi mmesimama? Wakati mwingine Mheshimiwa Waziri Mkuu analazimika kutoka wakati Mheshimiwa Waziri anasoma hapa hoja yake. Wewe unafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu hataki kusikiliza hoja ya Waziri wake? Anatoka kwa sababu kuna jambo la dharura, ninyi

mmesimama Waziri mwezenu hapa anasoma taarifa, haipendezi. *(Makofi)*

Ama Mwenyekiti anasoma, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana dharura inabidi atoke kabla hajasikiliza hoja ya Kamati, lakini ninyi mmesimama. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu anachelewa kutoka, kwa hiyo anachelewa na kurudi, kwa sababu anaporudi mnasimama tena. Humu ndani Waheshimiwa Wabunge nilishalisema hili mara kadhaa. Ninyi mnataka Mheshimiwa Waziri Mkuu awasalimie mara ngapi kwa siku? Ninyi mnaokaa hapo, kwa sababu akitoka mnasimama mumsalimu, akirudi mnasimama mumsalimu, awasalimu mara ngapi? *(Makofi)*

Sasa mmeanzisha mtindo, kuna watu mnatoka hata kule mbali mnasogea, ama wakati mwingine upande mzima mnasimama, yaani mimi hata siwaelewi kwa kweli. Mnamkosea Mheshimiwa Waziri Mkuu na mnalikosea heshima Bunge letu.

Hili nadhani limeeleweka, nimezungumza na watu wa Serikali kwa sababu ndio mnaokaa hapa mbele na ndio mnaoanzisha kusimama. Waheshimiwa Wabunge wanaokaa nyuma kule lazima wasimame kwa sababu ninyi mmesimama.

Sasa leo mmekumbushwa na nimekumbusha kwa maneno haya kwa kirefu, ninaamini tumeelewana. Mheshimiwa Mbunge atakayesimama ataambatana na Mheshimiwa Waziri Mkuu ili amsindikize kusikiliza simu ya Mheshimiwa Rais ambayo anakuwa ameitiwa huko nje. Hilo katazo ni la Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kuhusu hapo mbele, Waheshimiwa Wabunge kipindi cha maswali waacheni Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu wasikilize wanachouliza Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo kipindi kingine twende pale, hilo halijakatazwa, lakini usikae kupiga *story*, Bungeni si sehemu ya *story*. Kaa pale na peleka hoja yako kwa dakika chache ukijua kwamba Waheshimiwa WWabunge tupo 393, ukitumia wewe nusu saa hapo wenzako watapata nafasi saa ngapi? Tumia

dakika mbili, maliza hoja yako nenda. Kwa nini? Ni kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri pia wapo, wape hoja zako, si lazima kila hoja asikilize Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni ile ambayo Mheshimiwa Waziri ameshindwa ndipo unakwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa ninyi mnakaa hapo muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu anakaa humu ndani ili awasikilize Wabunge, siyo ili akusikilize wewe peke yako nusu saa. Dakika mbili uwe umetoka hapo na kama hukutoka nitakutaja mwenyewe hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelekezo haya hata Wenyeviti wanapokaa hapa mbele mtu anayekaa zaidi ya dakika mbili pale ni kama mchangiaji tunavyomkatia muda. Zaidi ya dakika mbili atajwe, atoke, apishe mtu mwingine.

Vilevile kwenda pale uende ukiwa na dharura, usiende tu kumsalimu, kwa nini? Na yeye anakaa hapa ndani ili asikilize, huyu ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Ataiongozaje Serikali ambayo hasikilizi inaambiwa nini na Waheshimiwa Wabunge? Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge huwa wanasema pisheni ili nisikilizwe. Sasa mimi hapa mbele nakaa kuwatetea, kwamba Serikali ipo, lakini watu wanataka wasikilizwe na viongozi wao na viongozi wao ni pamoja na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani hilo limeeleweka na kelele pia. Usizungumze mtu mpo meta kadhaa mbali, unaufanya mkutano wetu hapa uwe kama soko hivi, msogelee Mbunge mwenzio, zungumza naye, usizungumze yupo kiti kile unazungumza tu kila mtu akizungumza hivyo itakuwaje? Tuheshimu Bunge kama ambavyo sisi tunaheshimiwa, tujiheshimu sisi wenyewe. Kwa leo yanaishia hapo.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, huo ndiyo Mwongozo wangu kuhusu jambo hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa Mwongozo huo sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na Wizara hii kama ilivyokuwa jana, Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia hoja hii wapo wengi, kwa hiyo michango badala ya dakika 10 itakuwa dakika nane kwa kila Mbunge atakayeitwa. Kwa sababu leo majina ni mengi zaidi, ukishagongewa kengele na ukaona nimewasha basi ujue ukatishe sentensi yako.

Tutaanza na Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege ajiandae.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa zawadi ya uhai. Nikushukuru wewe pia kwa kunipa fursa ya kwanza siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi hii. Amefanya kazi kubwa ya miradi, Mheshimiwa Waziri amesema, sina haja ya kurudia kwa sababu muda ni mchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Waziri Bashungwa, amekuwa ni kijana mtulivu, msikivu, mwenye nidhamu na unyenyekevu wa hali ya juu na ni mchapakazi asiyetiliwa shaka. Katika Wizara zote alizopita tumemuona uchapakazi wake. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kutokana na mpango wa kuwajengea uwezo wakandarasi wazawa. Kwa kutekeleza mpango huu kutasaidia vijana wengi kupata ajira, hivyo itakuwa ni mapinduzi makubwa katika sekta ya ujenzi. Nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kuwa makini kwa kuteua Waziri wa namna hii. Kwa eneo hili la sekta ya ujenzi hapa pamepatikana mtu mahususi, hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa kuwajengea uwezo wazawa utasaidia kuimarisha uchumi wa vijana wetu na pia utasaidia kupunguza fedha za kigeni ambazo wanalipwa wakandarasi wa nje. Kwa hiyo, Watanzania tutakuwa tumejengewa uwezo mkubwa kwa uchumi wa ndani na tena tutakuwa tumeondoa umaskini katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wamekuwa wakitumia riba na kudai riba kubwa. Riba hizi zimekuwa zikipunguza mapato katika sekta hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu, niiombe Serikali ipunguze au wakati inapopanga mpango wa kujenga barabara au mpango katika sekta ya ujenzi iwe na uwezo kwanza wa fedha na iwe na uhakika wa fedha kuliko kutangaza *tender* na hatimaye tupate riba kubwa, wakandarasi waweze kupata hiyo riba na sisi Watanzania tunazidi kuathirika katika sekta hii ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ni ngumu sana, tumetembelea miradi mingi na tumekuta mapungufu hayo ya

riba katika maeneo kadhaa. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iangalie maeneo hayo kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu *TEMESA*, tunaiomba Serikali iweze kuijengea uwezo *TEMESA* na pia iweze kuitafutia ubia na hasa katika miradi ya vivuko. Kumekuwa na ile Kampuni ya *Songoro Marine* inafanya vizuri sana, kwa hiyo, *TEMESA* kama itajengewa uwezo na kuingia ubia na kampuni ile ya *Songoro Marine* itasaidia kujenga vivuko vingi na vilevile itakuwa na manufaa katika nchi zinazotuzunguka kwa kujenga vivuko vingi, si Tanzania tu bali na nchi zinazotuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee Mkoa wa Dar es Salaam; Mkoa wa Dar es Salaam sisi hatuna ruzuku na wala hatuna mashamba. Sisi tunahitaji barabara na mifereji, mito imeharibika, barabara zimeharibika, madaraja yameharibika, lakini bajeti mliyotutengea ni ndogo. Ukiangalia Mkoa wa Dar es Salaam na ukubwa wake na uchumi unaotokana na wafanyabiashara na wananchi wa Dar es Salaam ni mkubwa. Kwa hiyo, tunaomba hata bajeti wanazozipanga waiangalie Dar es Salaam kwa jicho la pembeni. Tunashida sana Mkoa wa Dar es Salaam. Siasa zetu za Dar es Salaam ni barabara, tumekuwa tukipiga kelele barabara, barabara, barabara. Sisi hatuhitaji kingine, ni barabara, barabara, barabara, ndizo siasa za Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa mradi wa mabasi ya mwendokasi, mradi ule ujenzi wake unakwenda kwa kasi sana. Tunaomba na zile awamu nyingine zifanyiwe kwa haraka ili kunusuru wakazi wa Dar es Salaam ambao wanakaa masaa mengi njiani, wanatumia zaidi ya saa nne kufika kwenye shughuli zao. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma wananchi wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam na ile bajeti ya vivuko au bajeti ya mito, maana kuna mito mingi Mkoa wa Dar es Salaam, tunaomba bajeti yake iwe kubwa, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, tumeona wamepanga kwamba watajenga daraja la pale Jangwani, lakini ikitokea siku mvua imenyesha mkoa mzima una-*collapse*, kunakuwa hakuna kazi. Kuna siku tumekaa kwa saa 12 magari hayatembei na watu hawafiki nyumbani mwao, vilevile watu hawafiki kazini. Hiyo inatokana na kile kiwango kidogo wanachotupatia kwenye bajeti ya ujenzi katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti iliyombele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na hasa kwenye kipindi hiki ambacho tulipata mvua zisizo za kawaida, wameonesha uzalendo wa hali ya juu sana kwa namna walivyowahudumia Watanzania, kwa hiyo, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo ninafurahi na ninampongeza Mheshimiwa Waziri vilevile na timu yake nzima ni suala zima ambalo wengi wameliongea hapa ndani, la namna ya kuwasaidia wakandarasi wa ndani. Nchi hii ina miradi mikubwa, bajeti ya Wizara hii ni moja ya bajeti kubwa sana, lakini fedha ambazo zingeweza kuongeza nguvu ya uchumi kwa wananchi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa zinaondoka kurudi nje ya nchi kwa sababu sehemu kubwa ya wakandarasi wanatoka nje. Kwa hiyo, wazo hili la kuwajengea uwezo wakandarasi wa Kitanzania limezungumzwa kwa muda mrefu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini natoa angalizo, mkakati huu wa kuwajengea uwezo, kwanza tukubaliane, wakandarasi wetu si kwamba hawana *skills* za kufanya kazi hizi, mimi naamini kabisa walio wengi *skills* wanazo. Wengi wanasoma shule hizo hizo ambazo na wenzetu wanasoma. Tatizo lao ni kupata uzoefu wa kutosha wa kufanya kazi hizo za kujenga Barabara na la pili uwezo wa kifedha. Haya ndiyo matatizo yao makubwa. Kwa hiyo hayo yaangaliwe. Kwenye kutunga huo mkakati au ku-*implement* huo mkakati nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tuendane na kuhakikisha kwamba mwisho wa siku miradi ambayo hawa wazawa wanapewa inakuwa na fedha ambazo kwa kweli zitawafanya waweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, tuna mifano ya kuonesha kabisa kwenye maeneo mengine, kama kwenye miradi ya maji ambako wakandarasi wa kizawa wengi wamefirisika, wameuza nyumba zao, wamekwenda kuwa na hali mbaya zaidi kuliko mwanzo. Kwa hiyo hilo lizingatiwe sana katika mkakati mzima.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimeiangalia bajeti hii, sina matumaini makubwa sana kwamba ina-*address* maeneo ya kimikakati ambayo ningetegemea katika kipindi hiki yangeangaliwa kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi imeongelewa ya kimikakati kama nane. Daraja la Kigongo Busisi, na kuna fedha nyingi zitakwenda kujaribu kuondoa misongamano. Ni tatizo linachelewesha uchumi na linachukiza kwa watu walio wengi. Vilevile kuna suala la viwanja na vivuko mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani kwamba ni vizuri tukaangalia, tukawa na mtazamo wa miradi ambayo inakwenda kufanya uchumi wetu ukue kwa nguvu zaidi na kwa haraka zaidi.

Kwa hiyo, nimeshangazwa kuona kwamba bado kuna maeneo ambayo kuna barabara ambazo kwa kweli zina mchango mkubwa sana kiuchumi ambazo zilitakiwa ziangaliwe kwa karibu na zipo nyingi, lakini mimi nitaongelea zile ambazo

zinatuhusu, hasa Nyanda za Juu Kusini, kwa maana ya mikoa ya Ruvuma na Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mkubwa sana wa Liganga na Mchuchuma. Kwanza tunaishukuru Serikali imeona umuhimu wa barabara hizo kukamilika. Lakini tukubaliane, unapofanya uwekezaji katika barabara ni vizuri ukahakikisha mradi huo unakamilika ili uanze kuona *value for money*. Sasa tumetumia fedha nyingi sana kwenye miradi, mradi mmoja wa barabara ambao ni *Lot II* kilometa 50 Lusitu Mawenge. Kuna mradi mwingine ambao ni barabara muendelezo, tulianza kujenga *Lot II* tukaacha *LOT I*. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais alipoingia moja ya miradi aliyokubali ianze haraka ni *Lot I* ambayo inaanzia Njombe inakwenda mpaka mpakani na Ludewa Lusitu.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mkubwa sana wa Liganga na Mchuchuma, kwa nza tunaishukuru Serikali imeona umuhimu wa kuwa na barabara hizo zikamilike. Lakini tukubaliane, unapofanya uwekezaji katika barabara ni vizuri ukahakikisha mradi huo unakamilika ili uanze kuona *value for money*. Sasa tumetumia fedha nyingi sana kwenye mradi mmoja wa barabaraba ambao ni *Lot two* kilometa 50 Lusitu Mawenge.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwingine ambao ni Barabara ya mwendelezo, tulianza kujenga *Lot two* tukaacha *Lot one*. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais alipoingia moja ya miradi aliyokubali ianze haraka ni *Lot one* ambayo inaanzia Njombe inakwenda mpaka mpakani na Ludewa Kusini, lakini ni barabara moja.

Mheshimiwa Spika, sasa barabara hii imeanza kujengwa na mkandarasi yupo *site*. Kwa kweli imesimama kwa muda mrefu kwa muda wa kipindi chote hiki cha mvua siyo muda mrefu kipindi cha mvua na niseme barabara za Nyanda za Juu Kusini kwa ujumla na hasa Mkoa wa Njombe, ili tuone *value for money* kwa wakati unaposema inajengwa kwa miaka miwili maana yake ni mwaka mmoja, kwa sababu kipindi cha cha mvua ni kirefu na ni mvua kubwa na ambazo haziishi, mkandarasi lazima simame.

Kwa hiyo, barabara hii imesimama kwa muda mrefu, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa kweli tutoe fedha kwa wakati ili barabara hii ianze ili iendelee kwenye kipindi hiki cha kiangazi, kwa sababu wana muda mfupi sana wa kujenga barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulisaini mkataba mwaka Machi, 2022, barabara hii inatakiwa ikamilike mwaka huu mwezi Disemba. Kwa hali ninavyoiona sioni ni kwa muujiza upi barabara hii itakamilika, lakini unaweza tukasukuma tukafika mahali pazuri. Tuangalie barabara nzima ambazo zinakwenda kufungua uchumi mzima wa Makaa ya Mawe pamoja na Chuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii imejaliwa utajiri huo, lazima tujiandae kimiundombinu. Miundombinu ni jambo la muhimu sana kwenye kukuza uchumi na uchumi huu wa nchi yetu unaweza ukakua kwa kiasi kikubwa na kwa haraka kama tutafungua Liganga na Mchuchuma. Nafahamu Serikali inakwenda kufanya kwenye maongezi, watakapokuwa tayari maongezi yamekamilika, miradi ya barabara haijakamilika, bado hatutaweza kuendelea na uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu tuna barabara ya pili barabara ya Makambako - Songea ni barabara kubwa wenzangu wameiongelea barabara hii ni kilomita 295, lakini tulidhani kwamba, wenzetu kule Songea tayari wameshakamilisha tumebakia kipande cha Njombe kwenda Makambako, mpakani mwa Songea mpaka Makambako lakini kumbe hata huku Songea bado na wenyewe wana matatizo fedha hazijapatikana.

Mheshimiwa Spika, niombe kwenye kipindi hiki angalau basi maeneo yaingizwe fedha angalau kuitanua maeneo ya Mjini maeneo ya Milima ya Kibena. Tumekuwa na ajali nyingi sana pale, kwa sababu ya barabara kuwa hatarishi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, atafuatiwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, ajiandae.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba nitumie fursa hii kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu kwa kuendelea kuweka pesa nyingi sana katika sekta hii ya ujenzi wa barabara zetu, hakika Mama yupo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Bashungwa na timu yake nzima ya Wizara kwa kazi nzuri. Vilevile, ninampongeza Mhandisi Malibe, ambaye ni *RM* wa Mkoa wangu, kwa kazi nzuri anayofanya na pia kwa ushirikiano wake mzuri sisi Waheshimiwa Wabunge. Hakika tumempata mtumishi mzuri katika Mkoa wa Mara, apate maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jimbo langu naishukuru Serikali kwa kukubali kuanza kutafuta pesa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la kati ya Kisorya na Ukerewe**.** Pia, kwa kuanza mchakato wa kuipandisha barabara ya Busambara kwenda Mugara kwa kuiweka katika *TANROAD* ili baadaye iweze kujengwa katika kiwango cha lami. Ahsante sana Mama, ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ianze kuangalia upya ujenzi wa barabara kipande cha Nyanguge kwenda Bunda, hiki kipande kimechakaa sana, kuna viraka vingi sana. Vilevile, barabara hii imekuwa ni nyembamba sana ilijengwa zaidi ya miaka 40 iliyopita. Naona sasa muda umefika wa kuweza kuibadilisha barabara hii iweze kuendana na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ujenzi wa barabara inayopita nje ya Mji wa Dodoma, sasa hivi utaangalia, jana mimi nimeshindwa nimechelewa hata kuuliza swali langu, kwa sababu ya msongamano kati ya *round about* ya Shabiby na hapa Bungeni,

kuna malori mengi sana, kuna mabasi mengi sana pia yanapita pale, sasa kuna msongamano umekuwa mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali yetu imalizie kipande kile ili yale mabasi na malori yaweze kupitia kule nje ya Mji. Vilevile, ninaomba Serikali ikamilishe ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Dodoma, huu wa Msalato, mahitaji ya usafiri wa ndege ni makubwa sana kama ambavyo watani wangu Wahaya wamezungumza nao wanapenda sana kutumia ndege. Sasa wanashindwa kutumia ndege, kwa sababu ndege hazifiki hapa. Kwa hiyo, ninaomba sana uwanja huu ukamilike ili uweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kuna tatizo la malipo ya wakandarasi, mimi ingawa nipo katika sekta hii, lakini sipo katika ujenzi wa barabara. Wakandarasi wengi sana wamefilisika na wengi sana sasa hivi wanaumwa magonjwa ya moyo, kwa sababu ya madeni waliyonayo. Kila siku Serikali inasema kwamba, itawalipa, sasa Serikali ituambie ni lini italipa haya madeni? Kama haiwezi kulipa madeni, kwa nini inaendelea kutoa hizi *tender* wakati inajua kabisa kwamba, haiwezi kulipa haya madeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninampenda sana Mheshimiwa Bashungwa, lakini katika hili nafikiri leo shilingi yake itabakia kwangu mpaka aje na mpango maalum wa kuweza kulipa haya madeni. Kwa kusema hayo machache.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru sana, kwa kunipa nafasi na mimi niweke mchango wangu kwenye hii Wizara ya Ujenzi. Kwanza, kabisa

ninamshukuru Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Naibu wake. Ahsanteni sana kwa kazi mnayoifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais, wetu Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwatimizia wananchi ndoto yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri nikushukuru sana kwa kweli kipindi hiki ambacho kumekuwa na mvua si za kawaida hasa kwenye maeneo mengi sana Dar es Salaam na Jimbo la Kawe, kwa ujumla tulikubwa na mafuriko, madaraja yakakatika, mito ikapanuka na barabara zikaharibika, kwa namna ambavyo wewe na Wizara yako mlikuwa wepesi sana. Mahali pale ambapo lile Daraja la Kunduchi, lilikatika pamoja na Daraja la JKT na Daraja la Mbopo. Mlipokuja mkanihakikishia kwamba, mtajenga ndani ya saa 72 na kweli mlifanya hivyo mlijenga ndani ya saa 72, hongereni sana kwa ajili ya kazi hiyo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa *TANROADS,* ndugu yangu *Engineer* Mohamed Besta, pamoja na Katibu Mkuu Balozi *Engineer* Aisha, kwa namna ambavyo na wao walifika kwenye matukio hayo wakashirikiana pamoja na wananchi na jambo likaenda vizuri ndani ya saa 72, madaraja yote na barabara zote zilikuwa zimejengwa, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa moyo wako huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninakushukuru, kwa sababu ya barabara inayotoka Bunju B kwenda Mabwepande, kwenda mpaka geti la Mabwepande mpaka Mpiji Magohe. Wakati huo wa mvua nyingi zilipokuwa zimenyesha Mheshimiwa Waziri wewe ulikuja pamoja na Watendaji kazi wako kwenye mvua tukapita wote kwenye matope ulionesha mfano mzuri sana wa uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nikwambie jambo moja; tuna Mawaziri wengi sana wazuri katika Baraza letu, lakini wewe ni mmoja wa Mawaziri wazuri tulio nao. Kwenye Kitabu cha 1 Petro 5:5 inasema hivi; *"Kwa maana Mungu huwapinga wenye kiburi na huwapa neema wanyenyekevu"*. Kitabu cha Yakobo

Sura ya 4:6 kinasema; *"Mungu huwapinga wajikuzao bali huwapa neema wanyenyekevu." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashungwa wewe ni kati ya Mawaziri tulio nao wanyenyekevu sana, Mungu akuinue na aendelee kukupa neema iliyozidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, ningependa kutoa ushauri kadha wa kadha, kwanza, nilikuwa ninaomba mfahamu kwamba, suala la barabara *is the matter of national concern* na hasa kwenye Miji mikubwa kama Mji wa Dar es Salaam, barabara zote zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, nimefanikiwa kutembea shina kwa shina Jimbo la Kawe, tuna mashina 1,000. Nimekwenda shina kwa shina barabara zote mbovu kila sehemu ziwe za *TARURA* na za *TANROADS* barabara zote mbovu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba ushauri mmoja kwamba, ni vizuri badala ya kutegemea utaratibu wa kawaida, mtengeneze *special supplement,* ambayo inaweza kufanya barabara za Dar es Salaam, zikapitika kwa urahisi zaidi. Kwa nini mfanye *special supplement* kama unavyojua Mheshimiwa Waziri, *road fund* (hela ya barabara) huwa tunapata hela ya barabara kwenye kila lita ya mafuta inapouzwa na Dar es Salaam, ndio mahala ambapo magari mengi sana yanaendeshwa.

Mheshimiwa Spika, barabara za Dar es Salaam, zikiwa nzuri magari mengi yataendeshwa na utapata hela nyingi ya *road fund* itakayokusaidia. Kwa hiyo, nilikuwa ninakuomba sana unapowaza kuhusu barabara ukitumia utaratibu wa kawaida wakutengeneza barabara za Dar es Salaam haitawezekani, lazima kuwe na *special supplement* itakayosaidia barabara zitengenezwe na magari mengi yaendeshwe na hela nyingi ya *road fund* iingie, kwa sababu kuna magari mengi Dar es Salaam. Ni *philosophy* ya kawaida Mheshimiwa Waziri, ng'ombe

anayekupa maziwa unampa majani ya kutosha. Kwa Dar es Salaam magari yanaendeshwa sana, kwa hiyo, hiyo lita moja ya *road fund* inapatikana kwa wingi zaidi, tupe majani ya kutosha ili tukupe mafuta ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninakuomba Mheshimiwa Waziri ni barabara nyingi, ile barabara ya kutoka pale Tegeta kwenda Basihaya mpaka Nyaishozi imejengwa bila mitaro ni barabara ya *TANROADS* hiyo. Barabara hiyo inaleta mafuriko kwa watu, ninaomba sana wakati mnajaribu kuangalia barabara muiangalie barabara hiyo kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuna hiyo barabara inayotoka Tegeta kwenda mpaka Kiwanda cha Wazo, hiyo barabara imekuwa nyembamba. Kwa hiyo, magari yanapangana kuanzia asubuhi mpaka jioni na watu wanapoteza maisha yao kwa ajili ya hiyo Barabara, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri iangalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote ninaomba sana suala la barabara katika Jiji la Dar es Salaam, liwekewe mkakati maalumu, kwa sababu barabara zote zimeharibika. Mungu akubariki sana. Mungu huwapinga wajikuzao huwapa neema wanyenyekevu. Mungu akupe neema hiyo Mheshimiwa Waziri na uendelee vilevile. Ahsante sana, kwa unyenyekevu wako, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, ajiandae.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi. Nami nianze kwa kusema moyo usiyo kuwa na shukrani hukausha mema yote. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, sisi Wanambeya, sisi Wanabusokelo pamoja na wasadizi wake Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri

wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote, kwa kutembelea Jimbo la Busokelo na kuona hali halisi ya miundombinu ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara mlipotembelea Mheshimiwa Waziri, mwaka jana mkiwa na Waziri wa Fedha, mliona ile barabara ya kutoka Katumba - Suma – Mwakaleli - Langwa - Mbambo mpaka Tukuyu Mjini, leo hii barabara ile tumesaini mkataba na tunasubiri Mkandarasi aanze kazi. Tunawashukuru sana tena sana, kwa sababu ni barabara ambayo hakika Waheshimiwa Marais wengi wamepita, lakini Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amethubutu. Maana tangu enzi za Mwalimu Nyerere ile barabara ilikuwa ikiahidiwa yenye kilometa 56. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni lango kuu la uchumi wa Wanarungwe, wa Wanambeya, kwa sababu kule tunalima mazao mengi, tunafuga, lakini zaidi ya yote gesi asilia inatoka kule aina ya Kabondayoksaidi. Kwa hiyo, uwepo wa mkandarasi ambaye ameshaonyeshwa *site* hii, tunaiomba Serikali, tunaiomba Wizara ya Fedha, *advance payment* iweze kufanyika mapema ili kazi ianze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze pia kwa kushukuru kwa barabara ya kutoka Mbambo mpaka Tukuyu, Bujesi yenye kilomita 10 ambayo imeshakwisha kamilika. Nashukuru pia barabara ya kutoka Tukuyu Mjini mpaka Kibanja yenye kilomita saba ambayo pia imekamilika na barabara ambayo bado ni ya kutoka Luteba mpaka Ipelele kwa wenzetu Makete. Mheshimiwa Waziri, ulivyokuja uliona, tunaomba sana barabara hii iweze pia kukamilika, kwa sababu inaunganisha kati ya Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Njombe. Tunaombeni sana Serikali iweze kuliona hili, kwa kuwa kule kuna fursa nyingi za kiuchumi pamoja na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri mambo yafuatayo machache; Waheshimiwa Wabunge, wengi wamezungumza suala la bajeti haitoshi. Ni kweli haitoshi, lakini nini tufanye kama

Taifa? Mataifa yote yaliyoendelea asilimia kubwa pamoja na *China* wana Benki maalum kwa ajili ya ujenzi. Tungekuwa na benki maalum kwa ajili ya ukandarasi wa Tanzania maana yake hata mafungu ambayo leo hii tunasema hayatoshi, huenda angalau yangeweza kukidhi kiwango kwa asilimia fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, katika ujenzi wa barabara tuna teknolojia nyingi ambazo zinatumika; duniani kote tuna teknolojia zaidi ya 100 teknolojia, lakini Tanzania teknolojia tunazozitumia hazizidi saba. Niwashukuru Wizara mmeshaanza ku-*practice* hata teknolojia nyingine mpya sasa hivi. Tuongeze kasi zaidi, kwa sababu zile teknolojia ndizo zinazopunguza gharama ya ujenzi wa Barabara, vinginevyo, tukiendelea kutumia teknolojia za zamani zile *automatically* gharama za barabara zitakuwa kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wewe ni mtu ambaye una *exposure* ya Kimataifa. *Technical* timu yako ikitumwa kwenye Mataifa ambayo wanatumia teknolojia ambazo wanatumia udongo katika maeneo ya barabara husika. Kwa mfano, mngekuja kule Busokelo mngetengeneza barabara ile ya Mbambo ile tunaizungumzia sasa hivi Tukuyu ama ya Katumba mpaka Suma kwa kutumia udongo halisi wa kule. *Automatically,* gharama zake zingeshuka na tungeokoa na tungetengeneza barabara nyingi zaidi ndani ya Taifa letu la Tanzania. Kwa hiyo, tukazanie tuweke mkazo zaidi katika suala la tafiti za teknolojia mpya katika kutengeneza barabara zetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana pia *Manage*r wangu wa Mkoa *TANROADS* na timu yake yote. Sasa hivi kule mvua zinanyesha na timu yako Mheshimiwa Waziri, mmezunguka sana. Hivi tunavyosema Rungwe mvua inanyesha na bado barabara zimeharibika. Tunaomba kama ambavyo mmetusaidia huko nyuma muweze kutusaidia tena.

Mheshimiwa Spika, kwenye barabara ya *TANZAM* ambayo ndio barabara kuu ya uchumi wa Wanambeya na Watanzania

wote na ambayo ndio inapitisha mizigo mingi na ndio lango kuu la uchumi wa *SADC*. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tunajua ipo kwenye *EPC+F*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ambayo ni ya kimkakati, kwa sababu ikiboreshwa ile *automatically* fedha nyingi za nchi za Congo, Zambia mpaka *South Africa* kwa kuwa mabasi au *trucks* zote zinapita kule. Barabara hii itafungua zaidi fursa za kiuchumi pamoja na nchi za Malawi. Kwa hiyo, tuipe uzito mkubwa barabara hii ya *TANZAM*, kwa sababu ni ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukija kwako wewe ambaye ni Rais wa Mabunge duniani, Mbunge wa pale Mbeya Mjini na Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuna barabara ya *by pass* sisi Waheshimiwa Wabunge wote tunapita pale mjini. Ili twende Majimboni kwetu lazima tupite Mbeya Mjini, sasa hivi mkandarasi anadai bilioni tisa hajalipwa, ndio maana ile njia ya *four-way* inachelewa, kwa sababu ya madai ya mkandarasi. Tunaomba Wizara muone kwa umuhimu katika kufungu lango hili la barabara katika Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niishukuru tena Wizara, nimshukuru Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo ametuona sisi Wanabusokelo, Wanambeya na Watanzania wote katika miundombinu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ataendelea Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, atafuatiwa Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, lakini Mheshimiwa Bidyanguze, kabla haujaanza kuchangia Mwenyekiti anakuja kunipokea hapa mbele. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi, ambayo ni Wizara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bashungwa, kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya kwenye Wizara hii, lakini pia akishirikiana na Naibu Waziri. Pia, nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na timu yote kwa kazi wanayoendelea kuifanya na tukijua kabisa barabara ni sawa na mishipa ya damu katika mwili wa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya kupeleka fedha kwenye Wizara hii ambayo kwa kweli tumepata shida sana kwa mwaka huu ambapo tulipata majanga mengi ya kuharibikiwa kwa barabara nyingi pamoja na madaraja. Mama ameendelea kupeleka fedha kwa ajili kuokoa na kuwezesha wananchi waweze kupita katika maeneo hayo ambayo yameharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwalike Mheshimiwa Waziri aje Kigoma. Tunayo Barabara ya Mpeta – Uvinza, hii barabara ndiyo kipande ambacho kimebaki kwa Mkoa wa Kigoma kuunganishwa na mikoa mingine hasa Mkoa wa Tabora. Ndiyo kipande ambacho kimebaki na kina kilometa 51.5. Mheshimiwa Waziri kipande hiki kiliwekewa fedha na mkandarasi yupo na anaendelea kufanya kazi na kwa kweli ana muda mrefu sana na wananchi mpaka wamefika mahali wamechoka sasa ninaomba uje uone kazi inayoendelea kufanywa. Naona kidogo kwa sasa ameanza kuweka lami lakini alikuwa amekwama kabisa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ukija utuambie Wabunge wa Mkoa wa Kigoma na sisi tushiriki kwenye ziara yako ili tuweze kuona namna ambavyo tutawasaidia wananchi kufungua hicho kipande ili tuondokane sasa na vumbi ukitoka Dar es Salaam, ukitoka Dodoma pita Tabora unafika Kigoma kwa kiwango cha lami lakini hicho kipande kwa kweli kinasumbua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mkoa wa Kigoma ipo barabara ambayo inaitwa Simbo – Kalya ambayo ipo Uvinza. Hii barabara ni kweli inakwenda Kalya, lakini ukweli ni kwamba hii barabara kuna kipande kule mbele ambacho ni cha *TARURA* ambacho kinaunganisha kwenye Mkoa wa Katavi na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri niliwahi kumwomba aje aione hiyo Barabara. Hii barabara aliipita na akavuka kwenda mkoa mwingine. Nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri hii barabara pia ifunguliwe, isiitwe tu Simbo – Kalya hapana. Katika Mkoa wa Kigoma tuna barabara tatu ambazo zinatoka kwenye mikoa mingine kuingia Mkoa wa Kigoma, lakini hiyo ni ya nne. Tunapoendelea kuwa na barabara nyingi za kutoka ndani ya mkoa kwenda mikoa mingine ni faida pale ambapo barabara moja inaweza ika-*broke* (ikavunjika) maana yake hapo sasa tunatumia njia nyingine mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii huwa ina shida sana hasa kwenye mwinuko. Nashukuru Naibu Waziri alipokuja alitoa maelekezo ya kuwekewa zege katika baadhi ya maeneo ya miinuko yaani mwananchi anashuka Basi la Saratoga na vijana wale wa Saratoga kwa kweli wamejitolea sana kuhakikisha kwamba wanahudumia eneo lile ambalo lina watu wengi. Eneo lile lina watu wengi karibuni 200,000 kwa sababu wapiga kura wangu ni karibu 450,000. Kule ndiyo kuna upande wa watu karibu 200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale vijana mpaka wanafika mahali wanajaribu kutengeza barabara wenyewe katika maeneo korofi. Sasa naomba katika maeneo haya korofi yawekewe zege, lakini barabara hiyo kwa sasa imefungwa kutokana na kwamba kivuko hakifanyi kazi kwamba maji yamejaa sana pale Ilagala. Mheshimiwa nikuombe, kwa kuwa tayari upembuzi yakinifu wa daraja lile umekamikika basi naomba utamke Serikali ina mpango gani katika kujenga daraja hilo? Kwa sababu wewe fikiria kwamba barabara ile sasa imekwama, imekwama kwa sababu kivuko hakifanyi kazi kutokana na maji kuwa mengi, upembuzi yakinifu umeshakamilika kwenye Daraja la Mto Malagarasi Chini, sasa mpango wa Serikali ni upi katika kuhakikisha kwamba hilo

Daraja sasa linakwenda kujengwa? Nitapenda Mheshimiwa Waziri ukija kuhitimisha uzungumze chochote na utakapokuwa unakuja Mkoa wa Kigoma naomba nikupeleke hapo Ilagala uweze kuona hiyo adha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeenda juzi Jumapili iliyopita ile kwa kweli wananchi wanasikitika sana kuona kwamba usafiri sasa katika barabara ile haupo watu wamesimama, maboti yalishaoza na meli hazifanyi kazi. Kwa hiyo watu 200,000 wamekaa hawatembei, wamesimama hakuna kinachofanyika. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri, kwa hilo niwe nimeliwekea msisitizo mkubwa, lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kutuletea fedha nyingi katika Jimbo la Kigoma Kusini kwa maana ya Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli napongeza sana kwa juhudi ambazo zinaendelea kwenye eneo la afya na elimu. Kwa kweli kuna haja ya hiyo barabara, kwa maana ikitengenezwa tukiweka daraja naomba nikuhakikishie kwamba kwa kweli itakuwa imeenda vizuri na tutakuwa tumewashika vizuri sana hawa wananchi kwa maana ya kwamba tumewashika kwenye eneo ambalo kwa kweli wanalihitaji. Ukienda pale Ilagala na wewe utakuwa shahidi yangu siku nitakayokupeleka watakwambia kilio chao ni daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba niunge mkono hoja, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anastazia James Wambura atafuatia Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimwa Aloyce Andrew Kwezi ajiandae.

Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu. Samahani kidogo Mheshimiwa Mgalu. Baada ya Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuata Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga.

Mheshimiwa Subira karibu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo na mimi kuchangia Bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi, Wizara muhimu kabisa. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Ujenzi kwa kazi nzuri. Wizara hii nimeona imepitia katika changamoto na kipimo kikubwa cha ku-*test* uwezo wao, uvumilivu na kujitoa kwao kutokana na mvua za *El Nino* pamoja na Kimbunga cha Hidaya, lakini binafsi niseme naona wamefaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu amewajalia wamefaulu kwa sababu tumewaona katika maeneo mbalimbali katika kuangalia namna gani ya kurejesha miundombinu katika hali yake ya kawaida. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Bashungwa kwa kufika katika Daraja la Mpiji Chini katika kuangalia namna gani ya kuweza kuendeleza ujenzi wa daraja hili. Nataka nimwombe Mheshimiwa Bashungwa nimeona kwenye hotuba yake kwamba ameeleza daraja hili ambalo linaunganisha Bagamoyo na Kinondoni. Daraja hili lilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli wakati anafungua Kituo cha Mafunzo Maalumu cha Kijeshi kule eneo la Mapinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa daraja hili kwa kweli mkandarasi tangu amepewa mkataba mwaka jana, Januari 2023 kazi haiendelei vizuri tunakushukuru kwa maelekezo yako, lakini nikuombe Mheshimiwa Bashungwa daraja hili ambalo pia linaingiliana na barabara ya Mingoi – Kiembeni, ulifika na uliona wananchi wanavyolalamika barabara inaenda mpaka kwenye Kituo hiki Maalum cha Mafunzo ya Jeshi na ambayo inaunganisha Vitongoji vya Kiembeni, Mingoi, Udindivu, Kiharaka na maeneo hayo katika Kata ya Mapinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimwombe Mheshimiwa barabara hii ni mbaya sana. Nikuombe kilometa

tano zinazobaki zihamie *TANROADS* ili Wananchi wa Msongola, Tungutungu, Minazi Minane wote ambao wanaunganishwa na daraja hili waweze kutengenezewa barabara hii na pengine hata kama isifike kiwango cha lami basi kiwango cha moramu. Nilitembelea kuona namna gani wanawake wanapata shida, Mbunge wa Jimbo naye ameisemea hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niipongeze sana Wizara hii kwa mara ya kwanza kwa kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka mipango ya kuwajengea uwezo wakandarasi wazawa na wakandarasi wanawake. Kwa mara ya kwanza tumeona dhamira ya dhati ya kuwainua wakandarasi wanawake kwa kuwatengea barabara ya lami kilometa 20 Mkoa wa Songwe na kazi hiyo imetangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na *Engineer* Aisha - Katibu Mkuu wa Wizara hii na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumpangia Katibu Mkuu mwanamke. Tunaona namna gani anavyopambana kuhakikisha maslahi ya wakandarasi wanawake na wahandisi wanawake katika Wizara hii yanazingatiwa. Kwa hiyo nimwombe sana, pamoja na azma nzuri ya kuwazesha lakini tuangalie namna gani taasisi za fedha zinaweza zikawapa mitaji wakandarasi hawa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee itazame pale watakapopewa kazi yale malipo ya *certificate* zao yazingatiwe. Kwa sababu kama nia ni kuwajengea uwezo basi mnyororo wa kuwajengea uwezo huo uzingatie namna ya kuwawezesha ili zile kazi watakazopewa wafanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda niishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa barabara unaondelea wa Tanga – Pangani na Mkange – Makurunge. Hapa naomba niwasilishe kilio cha madai ya fidia kwa kipande cha Mkange – Saadani – Makurunge. Mheshimiwa Mbunge

amefuatilia, Naibu Waziri wetu Mheshimiwa Ridhiwani lakini mimi pia naomba, shilingi milioni 840 siyo kiwango kikubwa. Naomba mmalizie kuwalipa fidia ili ujenzi huo uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba niishukuru sana Serikali kwa ujenzi unaoendelea wa Barabara ya Nyamwage – Utete, kazi inaendelea, pia Daraja la Mbambe. Kipekee kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge mwenyewe (Mheshimiwa Waziri Mchengerwa) amekuwa akifuatilia ndani ya Serikali lakini naomba Serikali iongeze kasi. Nishukuru sana kwa ubunifu na utayari wa Mheshimiwia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuelekeza kuanza kwa upembuzi yakinifu wa Barabara ya Chalinze – Utete ambayo itakuwa ni *shortcut*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kasi katika kuona barabara hii inaanza upembuzi yakinifu. Pia niishukuru sana Serikali yetu kwa kuamua kuanza upanuzi wa Barabara ya Mbagala – Vikindu kwa sababu ina foleni nyingi sana. Ina maana itarahisisha mawasiliano na uharaka kwa Wilaya za Mkuranga, Kibiti, Rufiji na hatimaye Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi naomba niielezee Barabara ya Makofia – Mlandizi – Maneromango – Vikumburu. Barabara hii imekuwa ikitajwa karibu kila Ilani, kuanzia Ilani ya 2010, 2015 na hii 2020. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, umesema sentensi moja tu kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami. Nikuombe sana, kuna malalamiko ya fidia katika kipande hicho cha Makofia – Mlandizi – Maneromango – Vikumburu, barabara hii ya muda mrefu. Niiombe Serikali iitazame, kwa sababu Serikali imejenga bandari kavu na inatarajia kujenga eneo la viwanda Bagamoyo, hii barabara inaweza ikasaidia. Kwa hiyo niombe uharaka wa fidia lakini pia kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho pamoja na changamoto zinazoendelea za madai katika Wizara hii lakini nina matumaini baada ya kukamilika kwa Mradi wa Bwawa la

Mwalimu Nyerere, Wizara hii na Serikali inaweza ikatenga fedha kwa ajili ya malipo ya wakandarasi. Niombe kasi ya malipo ya wakandarasi ili kuchachua uchumi wa ndani ya nchi yetu. Dhamira ni njema lakini tuangalie wakandarasi wanataka kufilisika. Kwa hiyo niombe kama Serikali namna gani mtakavyojielekeza hasa wakandarasi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa niendelee kumpongeza na kumshukuru Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Pwani kwa namna ambavyo amejipanga kuwezesha makundi ya wanawake. Utekelezaji wa 30% ya Sheria ya Manunuzi kwa ajili ya makundi maalumu, nakuomba Mheshimiwa Waziri mlisimamie hili. Nimefurahi kuona namna gani mnahusiana na Wizara ya Fedha katika mapitio ya Sheria ya Manunuzi tuliyoitenga hapa ili safari hii 30% ya manunuzi kwenye makundi maalumu hususan kwa wanawake iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wanawake wenzangu wakandarasi, wale wanaofanya masuala ya *labour based* katika mikoa mbalimbali Serikali yetu ya Awamu ya Sita imejipanga na sisi tuendelee kujipanga tusiiangushe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya napenda kuunga mkono na nakuomba Mheshimiwa Waziri urudi tena Mapinga kwa ajili ya Daraja la Mpiji Chini na barabara zake ili kazi iendelee, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Anastazia James Wambura ajiandae.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, mimi nina mambo mawili tu. Jambo la kwanza changamoto yetu ya Barabara ya Malinyi na pili ni suala la kuunganisha Wilaya ya Malinyi na Jimbo la Mlimba kwa Kivuko cha Kikove kwa maana ya kutumia pantoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea na mengine yote nitoe shukurani kwa Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kuweza kuhangika kufanya *recovery* ya mafuriko. Barabara nyingi nchini zimeathirika tunafahamu, ikiwemo Malinyi tumeathirika sana. Niseme tu, kufikia leo jioni barabara kubwa ya *TANROADS* kutoka Njiapanda au niseme Malinyi – Ifakara – Malinyi Mjini itapitika kwa maana ya hali ya udharura wakandarasi wapo pale wanarudisha hali kwa matengenezo ya muda mfupi wakati tunasubiri bajeti kubwa ya madaraja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kipande kilichobaki kutoka Njiapanda – Ngoheranga kule Kilosa kwa Mpepo njia ya Songea nacho wakitoka hapa Malinyi Mjini (Madumba) wataelekea kule nadhani ndani ya siku tano au sita kazi itaanza na baadaye kutakuwa salama. Kwa hiyo niwaambie tu Wana-Malinyi wenzangu waungane nami kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa ajili ya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri nimekuwa nawasiliana naye mara nyingi wakati wote kipindi cha mafuriko yeye na Naibu Waziri, Mheshimiwa Kasekenya amefika Malinyi zaidi ya mara tatu. Katibu Mkuu naye Mhandisi Aisha nimekuwa nawasiliana naye na kumsumbua mara nyingi ingawaje hajaweza kuja lakini amekuwa akitoa maelekezo mara kadhaa na *Engineer* wetu Meneja wa Mkoa Bwana Kiyamba na timu yake wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo kiukweli kama Wana-Malinyi tunafarijika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kuhusu changamoto yetu ya Malinyi nilikuwa nazungumza kipande cha kutoka Ifakara – Malinyi tunakuwa tunateseka masika wote mnafahamu na nimekuwa nikisema mara kadhaa, hili ni jambo la kwanza. Kwa hiyo naamini kuna kitu kitafanyika, lakini hata ukiacha hivyo ule mpango mkubwa wa barabara yetu ya kutoka Dar es Salaam – Mikumi – Ifakara – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Namtumbo ipo kwenye mtindo wa *EPC+F* kwa maana ya ujenzi wa mtindo wa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu iliyopita niliomba walau; najua Serikali inaweza ikabanwa uhitaji ni mkubwa nchi nzima. Niliomba walau kilometa 50 tujenge barabara hiyo ya Malinyi kwa vipande vipande pengine ndani ya miaka mitatu au minne tungeweza kuwa tumemaliza, lakini iliwapendeza Wizara ya Fedha na Ujenzi kuihamishia barabara hiyo kwenye huu Mfumo wa *EPC+F* kwa maana ya kujengwa yote kutoka Ifakara – Namtumbo – Ruvuma - Lumecha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nadhani mnafahamu mwaka jana tulisaini mkataba mwezi wa sita na tunasubiria wakandarasi wafike *site*. Sijajua uvunguni kuna nini hasa lakini shida ya wazi inaonekana kama mkandarasi anatudai *down payment*. Basi niombe Wizara kama ni hilo, basi alipwe tuweze kufanya hilo jambo liweze kwenda. Sisi barabara yetu hiyo ambayo tunaizungumzia mara nyingi ina umuhimu mkubwa sana. Kwanza kutuokoa Wana-Malinyi na changamoto ya masika. Sisi nadhani ndiyo watu pekee wakati wa masika hatuwezi kufika Halmashauri ya Mji, hatuwezi kufika mjini. Ndiyo hali ilivyo ya Malinyi na mara kadhaa nimekuwa hapa nikizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia umuhimu wa pili wa barabara hii mnafahamu Serikali na Chama ni mpango wetu kuunganisha barabara za mikoa na mikoa kwa kiwango cha lami nchi nzima, lakini sisi bado. Kwa hiyo maeneo ya Morogoro na Ruvuma hatujaunganika, hii ndiyo barabara pekee na tumeisemea mara kadhaa najua Serikali mnafahamu ndiyo maana mnaiweka kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wafanyabiashara na wananchi wa kawaida hasa kwa watani zangu Wangoni kule Ruvuma nao wanataka kupita Malinyi wafike kwao kiurahisi. Leo kwenda Ruvuma kwa maana ya Songea kupitia Masai kutoka Dar es Salaam kilometa karibia 1800. Kutoka Dar es Salaam kupitia Njombe kwenda Songea kilometa 950 lakini kutoka Dar es Salaam kwenda Songea kupitia Malinyi kilometa 785. Kwa hiyo unaweza kuona barabara hiyo ni fupi sana sana. Zaidi ya kilometa 200 zinaenda kuokolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Watu wa Malinyi uchumi utakuwa umechagizwa kwa kiwango kikubwa lakini hata ndugu zetu wale wa Ruvuma nao watakwenda kunufaika. Sisi ni wazalishaji wakubwa wa mpunga mnafahamu Bonde la Kilombero lote. Tunafahamu barabara yetu ya pale Ifakara, kupita Mlimba kwenda Njombe inaendelea na yenyewe tuombe tu Serikali wa-*speed up* na baadaye tukimaliza Malinyi kutoka pale Ifakara kupitia Mahenge kwenda Liwale nazo zote tunazihitaji ili kulifungua Bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna mpunga mwingi tunazalisha kabla ya mafuriko lakini bei zake mnafahamu ya mazao, bei zipo chini sana kutokana na kwamba hatuna *alternative roads*. Malinyi hatuwezi kufika, hatuna sehemu ya kupitisha watu kwa meli wala kwa treni, barabara pekee ndiyo hii. Kwa hiyo naomba nitoe changamoto Serikalini, Mheshimiwa Waziri mlichukuwe Watu wa Malinyi tuweze kusaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ilikuwa ni ahadi yangu mimi kama mgombea Ubunge wa CCM na CCM yangu kwenye uchaguzi wa 2020. Tuliwaahidi Wana-Malinyi na Wana-Mlimba tutaunganisha Mlimba na Malinyi kupitia Kivuko cha Kikove kwa maana tutaweka pantoni pale kivukoni jambo liweze kwenda. *TEMESA* wameanza kujenga hilo eneo lakini bahati mbaya mpaka sasa kipo 50% tu na mradi unasua sua na mafuriko sasa hivi yameenda kuharibu zaidi mambo hayaendelei, lakini hata kabla ya hapo kulikuwa na uzembe wa mkandarasi sijui kama Serikali pengine hamkuwa mnamlipa lakini mwaka wa tatu mradi ambao ulipaswa utumie miezi sita bado haujaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nikupe changamoto *deal* na watu wako wa *TEMESA* kama hamjawapa fedha naomba muwasaidie. Hata dharura ambayo imetokea hatuwezi kufika Ifakara – Mlimba watu wangepita *shortcut* kule nyuma, tunavuka pale Ngoheranga tunaingia Ngalimila tupo Mlimba tayari. Leo kutoka Malinyi tunaingiliana na Mlimba unatembea kilometa zaidi ya 300 mpaka ufike Ifakara Mjini uende Mlimba kutoka Malinyi lakini tukimaliza kile kivuko pale Kikove

maana yake tutatumia siyo zaidi ya kilometa 40 Malinyi – Mlimba kwa maana Ngoheranga, lakini leo kilometa 300 tunazunguka. Kwa hiyo mheshimiwa Waziri ninakupa hii *challenge* naomba utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri umeniahidi, ulikwama kuja Malinyi wakati mafuriko yalipokuwa makubwa maana sehemu nyingi Taifa lilikuwa linakuhitaji, tumelipokea hatulalamiki lakini naamini baada ya bajeti hii kama ulivyoniahidi tutakwenda wote Malinyi ukaone maeneo yote ambayo ninayazungumza. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie hili jambo liweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi mpya ambaye anapewa kazi kwenye kivuko, naomba mmuhimize atusaidie, kwa sababu wa kwanza naona amefukuzwa kwa sababu alikuwa mzembe, basi naomba huyu wa pili apewe muda. Matamanio yangu mimi, wananchi wa Malinyi na Mlimba, tunatamani hata Christmas ya mwaka huu tuweze kuvuka pale kwa mara ya kwanza tangu dunia imeumbwa, tuweze kuwa tumeunganika Mlimba na Malinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi lakini ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa naomba unisaidie katika haya, sitaki Bunge la Septemba tuje tuanze kugombana tena humu ndani, nakutunzia heshima na ninakuamini ninakuomba utusaidie watu wa Malinyi, Mlimba, Ulanga na Kilombero, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga. Atafuatia Mheshimiwa Anastazia James Wambura na Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi mchana wa leo kuweza kuchangia mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi, yenye bajeti ya trilioni 1.7 ambayo inaenda kuleta mabadiliko kwenye nchi yetu ya Tanzania. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa

kuteuliwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi lakini ninakuomba Kaka yangu au mdogo wangu, wewe unatokea Kanda ya Ziwa, unayaelewa maeneo yote tunayotokea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Ziwa tunayo changamoto barabara zetu ni mbaya sana, nyingi ni za vumbi, magari yanakata *chassis* kwa ajili ya ubovu wa barabara. Ninaiangalia hii bajeti ni kama ni kidogo sana, kama kuna uwezekano umuombe Mheshimiwa Rais iweze kuongezwa ili kusudu tuweze kutengeneza barabara zetu ziweze kuwa za viwango na zinazopitika kwa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa siwezi kujua kilichoko ndani yake kwenye upande wa fedha, ndiyo maana niko na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa, nimemsogeza karibu kujaribu kumuuliza tunatokaje huu mwaka wa uchaguzi kuelekea mwaka 2025, lakini amenihakikishia mambo yatakuwa mazuri na tutazidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na maeneo ambayo ni hatarishi. Mheshimiwa Waziri kwenye Wilaya ya Mbogwe ambayo ni Mkoa wa Kimadini, tumejaliwa kuwa na madini, mifugo pamoja na mazao mengine. Tunalo Daraja Mwabomba ambalo kila mwaka huwa linasumbua, ambalo naomba ulitengee hata kilometa moja ya lami ili kusudi likitengenezwa vizuri liwe linapitika kila wakati mvua zinaponyesha. Hii ni barabara muhimu sana, huwa inawapa shida sana wananchi na hii barabara ni ya *TANROADS*, tumeungana na Mheshimiwa Cherehani kwa upande wa Shinyanga na Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo daraja lingine la Budoda, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka mliniona nimebebwa na wananchi wa Budoda vijana wa kule, naiomba Serikali iweze kutenga hata nusu kilometa ili kusudi tukaondokane na huu usumbufu wa kila mwaka, kila mvua ikinyesha barabara inakatika wananchi wanateseka, kwa sababu tuna miaka 61 ya uhuru sasa hivi tunaiongoza nchi hii, ni vema tuwe na mtazamo wa haraka kuweza kusaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna daraja la Ilangale ambalo Wilaya hii imeungwanishwa na Wilaya ya Bukombe kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Ikalanga pamoja na Ilangale na penyewe kila mvua zikinyesha hili daraja linakatika. Mheshimiwa Waziri pia naomba unitengee nusu kilometa tu, hii barabara tumeiweka kwenye mapendekezo iingie kwenye *TANROADS* ili kusudi tuweze kuondokana na usumbufu, kwa kuwa labda pesa za kutengeneza lami hakuna, ndiyo maana naomba nusu nusu tu. Naibu Waziri Mheshimiwa Kasekenya unazifahamu hizi sehemu kwa kuwa wewe umewahi kufanya kazi kwenye hiyo Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mto Nyikonga, namshukuru Mheshimiwa Rais kupitia mradi wa *RISE*, tunaenda kutengeneza lami kutoka Nyikonga kuja Lulembela pamoja na Kashelo. Nakuomba Kaka yangu Mheshimiwa Kasekenya huu mpano uharakishwe haraka kama mlivyoniahidi mwezi wa nane, kwa sababu upembuzi yakinifu kila kitu kimeshaisha, sasa utekelezaji wake ukaanze haraka kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameniambia pesa zipo tayari na mikataba imeshafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mapendekezo ya barabara tatu, Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize sana, Mkoa wa kimadini wa Mbogwe ambao unazalisha dhahabu kwa wingi ukiitoa Geita na Chunya, huwa tunapata mali nyingi sana lakini magari yanayotumika yanabeba zaidi ya *tons* 30. Kwa sheria zetu kwenye barabara hizi za *TARURA,* hizi gari haziruhusiwi kutembea chini ya *tons* 10 kushuka chini. Kwa kuwa, wafanyabiashara wa Mbogwe wanayo malori yanabeba *tons* 35, sasa Barabara hii ya Kanegele - Mpakali - Mbizi, kuelekea Segese, naomba ipandishwe kuingia upande wa *TANROADS* ili wafanyabiashara hawa wasiwe wanagombana na watumishi wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mara hizi barabara zinapitiwa na haya maroli makubwa, wakati mwingine watumishi wa *TANROADS* wanapomaliza ubinadamu wanaingia kwenye zile sheria wanagombana, sasa haipo sababu ya kugombana wakati

hii nchi moja, Tanzania moja na sisi ni viongozi wananchi wametuamini kuweza kuwasaidia maisha yao waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo barabara ya Mwalo – Iyogelo kuja Iponya – Masumbwe hii tumepakana na Wilaya ya Bukombe na yenyewe naomba iingizwe *TANROADS* ili hawa wafanyabiashara wa marudio wanaobeba zaidi ya *tons* 30 waweze kuruhusiwa wawe wanapitisha magari yao, mpaka sasa huwa wanapitisha magari lakini ni kinyume cha sheria na huwa wanakamatwa, wanapigwa faini lakini mizigo iliyoko Iyogelo kuipitisha kwenda Masumbwe, haiwezekani bila kupitisha magari hayo ya zaidi ya toni 30, kwa sheria za *TARURA,* hayo magari yanazuiliwa kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara nyingine ya Bwerwa – Mwendamwizo, inatokea Bukoli, Mheshimiwa Kasekenya unaifahamu. Ukitoka Masumbwe kwenda Rugunga mpaka Makao Mkuu ya Wilaya ya Mbogwe, kuna kijiji kinaitwa hapo Bukoli ambacho tumeungana na Magesa, naomba hii barabara na yenyewe ni muhimu sana, wenye maroli wanaitumia lakini sasa hivi kwa vile iko kwenye kiwango cha *TARURA,* wenye magari makubwa wanazuiliwa kupita. Kwa hiyo, naomba na yenyewe ichukuliwe ili kusudi ikae kisheria ili watu hawa waweze kufanya biashara zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa zamani, yule aliyekuwepo kabla yako, mwaka jana alinifanyia *surprise* kitu kizuri sana, pale Mjini Masumbwe alinipa kilometa moja ya lami na wewe nakuomba ukiwa bado Waziri uniachie kumbukumbu ili niweze kukukumbuka kwamba uliwahi kuwa Waziri wa Ujenzi, unisaidie ili kusudi pale Mjini Masumbwe ipo barabara muhimu sana inayotoka lami kwa Moris pale kuelekea Shule ya Kasandalala. Mheshimiwa Waziri naomba hiyo kilometa moja kwa nguvu zako na uwezo wako uliopewa na Mwenyezi Mungu kwenye Wizara yako ya Ujenzi uweze kunisaidia ili kusudi na yenyewe iweze kuunganishwa na hii tuliyopewa na Mheshimiwa Mbarawa ili

kusudi wananchi wale waweze kuishi pale Masumbwe Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo Makao Makuu ya Wilaya ambayo yako Mbogwe, ninaiombea sana hiyo Wilaya iweze kupata kilometa mbili za lami kwa sababu pale ndiyo Makao Makuu, vilevile, barabara ni mbaya sana na watumishi bado tunaishi nao mjini, Mvua zinaponyesha wanapata kazi sana kwenda kufanya kazi kwenye Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nina malalamiko ya wakandarasi. Wakandarasi wamekuwa wakipata kazi kweli lakini pesa zinachelewa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba ujaribu kulifuatilia sana hili suala. Hasa wakandarasi wa ndani, wanapopata hizi kazi wana *rise certificate* wanapata usumbufu mkubwa kuweza kupata malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyoelewa wakandarasi wa ndani hawana mitaji, wanategemea pesa kutoka Serikali ili kusudi waendelee kufanya kazi vizuri. Nimezungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa na wewe utamfikishi, wakandarasi wa ndani wapewe kipaumbele ili kusudi wanapopewa hizi kazi za ujenzi waweze kufanya vizuri na waweze kuendeleza Taifa letu, tuweze kupata matajiri wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapa, ninaomba kwa vile hii barabara imeshapa lami kupitia Mradi wa *Rise* kutoka Lulembela; Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu huwa anapata shida sana kwenda pale kwake Bukombe. Serikali ione kila namna kuongezea lami hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ni mtu mkubwa. Barabara anayopita haifanani na Unaibu Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Serikali iangalie kila iwezavyo, iweze kuweka lami, ni kipande kadogo tu kama kilometa 38 ambazo zimebaki na hii barabara iliahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, pale alipokuwa anapita tarehe 27 mwezi wa

kwanza, kwamba itawekewa kiwango cha lami, kwa hiyo, Serikali isirudi nyuma iweze kuitengeneza hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa kuwa wewe Jimbo lako liko Magharibi, tuko mpakani na wewe. Ninakuomba siku moja uweze kusimama Masumbwe tuweze kuziangalia hizi barabara ambazo nazipendekeza ili kusudi uweze kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na wataalam wote, mameneja kwa maana ya Meneja wa Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga ili tuende tukaiunganishe Mbogwe yetu iweze kufanana na Mkoa wa kimadini ambao unaingiza pesa nyingi sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Naomba hitimisha tafadhari.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kwa kusema, Mheshimiwa Waziri hii trilioni 1.7 naona ni kidogo, fanya mpango Serikali iweze kukuongezea kwa sababu maeneo yote yameharibika ili kusudi iweze kupatikana pesa ya kwenda kukarabati barabara za Tanzania ziweze kupitika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anastazia James Wambura. Atafuatia Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Bashungwa na Naibu wake Mheshimiwa Kasekenya pamoja na Katibu Mkuu Injinia Aisha kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika hii Wizara na kwa namna ya pekee jinsi ambavyo waliweza kutatua changamoto za uharibifu wa miundombinu wakati wa kipindi cha *El Nino*, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza awamu zote za Serikali za Chama Cha Mapinduzi kwanzia awamu ya kwanza mpaka awamu ya sita. Naipongeza kwa sababu mnamo Juni, 2022 Nchi yetu ya Tanzania ilitangazwa kuwa ni nchi ambayo ni ya kwanza kabisa katika Afrika kwa kuwa na mtandao mrefu zaidi wa barabara *(Road Network)* katika nchi zote za Afrika, ambapo ilikuwa na kilometa 86,472 kwa ujumla wake na kati ya hizo kilometa 12,786 ni *trunk road* na 21,105 ni barabara za Mikoa, zilizobakia ni barabara za Wilaya, Miji pamoja na *feeder roads*. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu kwa awamu zote kwa sababu kazi hii imefanywa kwa awamu na imefanyika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia kwamba nchi yetu pamoja na kwamba ni kubwa lakini huwezi kulinganisha na nchi zile 10 ambazo ni kubwa zaidi katika Bara letu la Afrika. Kwa hiyo, ina maana kwamba Serikali yetu imeji-*commit* kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara inawasaidia wananchi katika ngazi zote kuanzia vijijini hadi mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kupongeza ukamilishaji wa uwanja wa ndege katika Mkoa wa Mtwara na kilichobaki sasa hivi tunaambiwa ni *control tower* pamoja na jengo la abiria, likishakamilika tutakuwa na uwezo wa kupokea ndege aina ya *Dream Liner* pale Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kazi ambayo inafanywa na *Engineer* wa *TANROADS*, *Engineer* Dotto. Kwa kweli anafanya kazi nzuri sana huyu *engineer* wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwamba, barabara ya Mnivata – Newala – Masasi sasa imeshapata wakandarasi wawili na wako *site*, ina maana kwamba sasa huu mtandao wetu wa barabara pamoja na barabara zingine katika nchi yetu utazidi kuongezeka na kuwa zaidi ya hizi kilometa 86,000 na pengine mpaka hata 90,000 au zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee niombe sana Serikali, hapa ndiyo mahali pekee ambapo tunaweza tukawasaidia wananchi wetu katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza ile Sheria ya manunuzi ya kutenga zile asilimia 30 kwa ajili ya makundi maalum. Siamini kabisa kwamba makundi maalum, wanawake, vijana na watu wenye ulemevu watashindwa kufanya *supply* hata ya *cement*. Kwa sababu naona kwenye barabara huwa tuna-*supply*, tunatumia *cement*. Kwa hiyo, niombe sana tuangalie kanuni zile ambazo nafikiri zinaruhusu yule *contractor* mkuu kuwa na *sub-contractors* ambao wanaweza wakafanya kazi ndogo ndogo. Tuangalie na kazi zingine ambazo zinaweza zikawasaidia wananchi wetu ili kusudi waweze kuinua kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bilioni zaidi ya 230, kusema zote zinaenda kwa mkandarasi mkuu kwa kweli siyo sawa. Naomba sana na wananchi waweze kunufaika kwa kutumia ile sheria yetu ya manunuzi ili kusudi tuweze kuhakikisha kwamba tunawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa uwezekano upo kwa sababu kuna mikopo yetu ya kina mama, vijana na watu wenye ulemevu, tunaweza tukaitumia hii mikopo tukawasidia hawa vijana, kina mama na watu wenye ulemavu angalau hata bilioni tano basi ziweze kwenda kwa hao wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza tena kwamba tuna barabara ya kutoka Mangaka kwenda Msimbati ambayo inafanyiwa sasa maandalizi kuanza utekelezaji wa ujenzi, lakini kwa namna ya pekee napongeza jitihada za *TANROADS* kupitia *Engineer* Doto, ambapo sasa wanakwenda kutoa kipaumbele kuwapa wakandarasi wanawake. Hii ni hatua nzuri sana. Nimesikia hata wachangiaji wengine wanasema kwamba, wakandarasi wanawake wanapewqa kipaumbele, naomba Serikali yetu iendelee na jitihada hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napongeza maandalizi ya barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi, tuna taarifa hizo kwamba maandalizi ya ujenzi yameanza, nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nilete ombi langu, barabara ya Kibiti – Lindi ni tatizo kubwa, ikiwa na maana kwamba mashimo yanapokarabatiwa na tumekuwa tukiuliza sana hapa ndani, ukarabati unafanyika lakini ndani ya siku chache yanabomoka tena yanatengenezwa mashimo makubwa zaidi na hii ni kutokana na magari ambayo yana uzito kupita ule uwezo wenyewe wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wakati wa kuhitimisha hoja yake Mheshimiwa Waziri atupatie majibu kwamba wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapofanyiwa matengenezo hazibomoki ndani ya muda mfupi. Vilevile, watuambie mkakati mahsusi ambao utasaidia kukabiliana na matatizo au athari za mabadiliko ya tabia ya nchi pindi mvua za *El Nino* zinapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia mara kadhaa Mheshimiwa Waziri akisisitiza kwamba maeneo yale ambayo yanakuwa na usumbufu yasirejee tena hasa katika hii barabara yetu ya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma hapa karibu na maeneo ya Jirani na Gairo hapa au Kibaigwa. Amekuwa akitoa msisitizo kwamba maeneo hayo yafanyiwe ukarabati wa kudumu au hatua za kudumu zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo eneo hilo pekee, Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameona ile Barabara ya kwenda kule kwetu Kusini imeleta matatizo makubwa lakini hata barabara zingine katika nchi yetu zitakuwa zina matatizo makubwa, kwa hiyo ninaomba wafanye mapitio kuona maeneo gani yana uwezekano wa kuathirika na mabadiliko ya tabianchi ili kusudi maeneo yote yaweze kufanyika utatuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nashukuru tena kwa kunipa nafasi na niseme naunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatia Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi kwa dakika hizi nane. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais, maombi ya Musoma Vijijini yamekubaliwa kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba barabara tumepewa. Tumeomba mambo ya umwagiliaji tumepewa, naomba kuwathibitishia kila mtu amemsifia Waziri Bashungwa na Naibu wake labda mimi ndiyo nitawathibitishia zaidi. Hawa nimefanya nao kazi kabla ya wao kuwa wanasiasa, wakavuka viwango vyangu vya utendaji. Narudia, wakavuka viwango vyangu, kwa hiyo msiwe na wasiwasi nao hawa wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara yangu ya Musoma – Makojo – Busekela, Waheshimiwa Wabunge nadhani wakati tunaomba barabara vilevile tuwe tunaweka na vigezo. Mimi barabara yangu ina vigezo vyote vya maana vya kiuchumi. Kilimo, tunalima pamba inatumia barabara hiyo hiyo, samaki wanaopelekwa viwandani wanatumia barabara hiyo, maziwa yanayopelekwa viwandani yanatumia barabara hiyo, kule Musoma Vijijini tunachimba dhahabu na shaba inatumika barabara hiyo hiyo, Makao Makuu ya Halmashauri yanatumia barabara hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina barabara moja ambayo inaunganisha vijiji 67, kwa hiyo Mheshimiwa Bashungwa na kijana mwingine japokuwa nimewasifia msisahau barabara yangu lakini mmenipa ahadi mko kwenye kumtafuta mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kilichonifanya mimi nisimame hasa ni mambo ya fedha. Wote tunakiri fedha hazitoshi, naomba unipatie muda niwaeleze mahali pa kutoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu ni kwamba fedha za miradi ni trilioni 1.69. Tumekumbushwa hapa madeni na riba ukipiga inafika karibu trilioni moja. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hii Wizara wanazo bilioni 700 za kutekeleza Barabara, zilizobaki ni bilioni 700, tuende kwa mahesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi shilingi imeshuka kidogo, barabara iliyokuwa inajengwa kilometa moja kwa shilingi bilioni moja sasa hivi nadhani inakaribia shilingi bilioni 1.5. Kwa hiyo kwa shilingi bilioni 700 ukigawa kwa vyovyote vile huyu Mheshimiwa Waziri anakazi ya kilometa 500 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shilingi bilioni 500 kwa mikoa 26 lazima tumuombee fedha. Ambao tumekaa Bungeni kwa muda suala la kumuombea fedha siyo geni wala siyo la ugomvi, ni sisi Waheshimiwa Wabunge tupendekeze kwamba kile kipindi cha majadiliano Mheshimiwa Waziri wa Fedha akikaa na Jirani yangu hapa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti lazima waongezewe fedha hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikuwa imependekeza wapewe shilingi trilioni tano. Mimi kwa udadisi wangu nikauliza *Engineer* wa barabara maombi yetu wanapaswa kuwa na shilingi trilioni 15. Hata hizi tano Kamati ilisema kwa kuwa hatuna fedha wapewe tano. Sasa Waheshimiwa Wabunge mimi nawashawishi tumuombee, tuombee hii Wizara ipewe angalau shilingi trilioni 3.5 ili akitoa shilingi trilioni moja kulipa madeni abaki na na shilingi trilioni 2.5 ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mahali pa kutoa fedha. Kwanza nampenda Mheshimiwa Mbunge wa Lindi aliongea jamani mwaka ujao na miaka inayokuja tusije tena kulumbana humu lazima Tume ya Mipango ifanye kazi yake. Yani kwenye

mambo ya uchukuzi na usafirishaji tuwaulize kipi kipaumbele? Kuna *surface transportation* yani ardhi inamaanisha reli na barabara halafu kuna *air* (ndege), kuna maji (meli); kipi namba moja tuwekeze hela nyingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Tume ya Mipango itusaidie sana kwenye hilo la vipaumbele. Kitu cha pili namalizia, utunzaji wa barabara tulizozijenga. Mtaalamu ameniambia *asset* (thamani) ya barabara zote tulizojenga zina thamani ya shilingi trilioni 40 na utunzaji wake unataka trilioni mbili. Kwa mwaka unaona yeye hata bajeti ya shilingi trilioni mbili za kutunza barabara hana. Kwa hiyo lazima tumuombee fedha. Sehemu nyingine ya kupata fedha ni kwenda nje. Hiyo wala hii tusione kwamba ni aibu na Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri aendelee kutafuta fedha nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zitapatikana *World Bank, IMF* na *Africa Development Bank.* Wenyewe riba yao ni kati ya 0% mpaka 2%; twende huko. Pengine pa kupata fedha ni hii ya *EPC+F (Engineering, Procurement, Construction and Finance)* lakini hatuwezi kuongea na hawa wa *EPC+F* bila sisi Watanzania kujua thamani ya hiyo barabara. Kama ukimuachia kila kitu tutapigwa. Isitoshe hii ni 100% *private* kwa nini tena wanataka Serikali iwasaidie kutafuta fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya kupata fedha ni Sheria yetu ya *$P^3$ (Public, Private, Partnership)*. Zinajengwa barabara kama ya Kigamboni zinakuwa na *road toll.* Ukienda miji yote Duniani watu wanapita kulipia hizo barabara. Kwa hiyo hayo ndiyo yalikuwa mawazo yangu kwamba tuombe wapewe fedha wakati wa majadiliano yetu na utakuwepo tuwaombee shilingi trilioni 3.5, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Professor* Muhongo ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya mimi kuchangia Wizara ya Ujenzi. Kama walivyosema wenzangu na mimi nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na viongozi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge humu wanaotaka kuthibitisha kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasikia na inafanyia kazi yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kiasi kikubwa. Watu wanafahamu mimi tangu nimekuwa Mheshimiwa Mbunge humu 2021, 2022 na 2023 kila nikisimama nazungumzia barabara yangu ya Ifakara – Kidatu kilometa za lami karibu 67 mpaka Serikali iliposikia imetatua changamoto zile akiwepo Mheshimiwa Waziri *Professor* Mbarawa na baadaye kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa amerithi kijiti kile. Katika utatuzi wa changamoto tayari ameshafanya ziara katika barabara hii tumeambatana nae amezungumza vizuri sana pale Mikumi kwa maana ya Daraja la Ruaha – Mang'Ula na amefika Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ungeweza kuwaambia Wananchi wa Kilombero chochote kile wakakuelewa lakini siyo barabara ya Ifakara – Kidatu. Hivi navyozungumza na mama yangu Mheshimiwa Aleksia yupo hapa tunatokea sehemu moja. Mheshimiwa Waziri unateleza tu sasa hivi na wewe umeona kiwango cha barabara kilivyo kipana na sisi kutoka Kata ya Kidatu mpaka Ifakara tuna kata karibu 10 ambapo kuna maporomoko ya maji kutoka milima ya Udzungwa lakini vimejengwa kwa *standard* nzuri changamoto zipo hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa hivi ukishatoka Hifadhi ya Mikumi unataka kuja Ifakara unatembea kuna kama kilometa moja tu haijakamilika katika kilometa 67; piga makofi kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tusishukuru kwa nini? Kwa hiyo tunataka kukushukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri. Siyo kwamba tukishukuru hatutaomba tena, tutaomba lakini kwa

jambo hili kubwa watu wanaweza wakaona lami wanateleza kwa lami, wanatembelea bajaji na pikipiki hawawezi kujua changamoto tulizopita mpaka kukamilika kwa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Kwa hiyo nataka kumshukuru pia *Chief of TANROADS Engineer* Mohamed Besta. Kwa kweli unamuona kabisa ana dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko katika nchi yetu ya barabara lakini ukitaka kumuongezea hata kipande cha kilometa moja unamuona yule mzee kama anatetemeka hivi kutokana na ufinyu wa fedha lakini ni *Engineer* mzuri tunampongeza. Mimi nimeona Mheshimiwa Waziri hakuna wa kukulaumu kwa kweli tulivyoona unahangaika kule Mtwara na Lindi unasafiri usiku kucha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wataalamu wako wa *TANROADS* akiwepo *Chief of TANROADS* yupo kwenye boti. Sasa wamepanda boti hata *life jacket* hawajavaa, mnatafuta matatizo huko. Sisi tunataka mtuhudumie lakini kwa kweli mnatuhudumia mpaka mnapitiliza. Kwa hiyo tunashukuru sana na tunawapongeza sana na natumia fursa hii kumualika Katibu Mkuu naye afike aone barabara ile Balozi *Engineer* Aisha Amour afike Kilombero aitazame barabara yetu nzuri ili tuweze kutatua changamoto zinazokabiliana na ile barabara kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mimi nataka kusema barabara hii ni muhimu sana. Pia, mimi kwa maoni yangu ni kwamba hizi barabara za Masaki - Dar es Salaam huko hatusemi kwa njia mbaya kuna barabara za kipaumbele kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Muhongo. Nchi hii ina barabara ya kuunganisha wilaya na wilaya hazijakamilika tupunguze hizi barabara ndogo ndogo huko. Angalia Kilombero unatoka Morogoro Mjini unafika Kilombero Ifakara huwezi kwenda Wilaya ya Malinyi huwezi kwenda Ulanga, huwezi kwenda Mlimba kama barabara hazijakamilika hizo ni wilaya nazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika vipaumbele na kufungua nchi yetu tunavyosema kilimo ni kipaumbele sisi Mkoa wa Morogoro tunaongoza kulima mpunga lakini *percent* kubwa inatoka Malinyi, inatoka Kilombero kwetu, inatoka baadhi Ulanga. Unasafirishaje mazao haya kama hatuna barabara? Mwenge kwa mara ya kwanza umetembezwa kwa mguu kilometa 46 Malinyi na tumeshasaini ile barabara ya Ifakara kwenda Malinyi mpaka Kiongozi wa Mwenge anasema sijawahi kuona hiki kitu katika historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali imetusikia barabara ya Ifakara kwenda Mlimba mkandarasi tunavyozungumza yupo *site*. Kwa hiyo tunasema pelekeni nguvu kule Morogoro chini katika kufungua mazao. Kwa hiyo kila barabara mnataka kujenga na Waheshimiwa Wabunge tunaomba barabara hata mimi Ifakara Mjini nina barabara ya *TANROADS*. Siombi sasa hivi kwa sababu kuna barabara kubwa Ifakara – Mlimba, kuna barabara ya Ifakara kwenda Malinyi ni barabara kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nataka kusisitiza hilo lakini pili nataka kusema fidia Mheshimiwa Waziri. Hii barabara yetu ya Ifakara – Kidatu kuna wananchi bado wana malalamiko na *Engineer* wetu Razack analijua hilo alikuwa anasema analifuatilia. Mheshimiwa Waziri niseme nimemsikia Dada yangu Mheshimiwa Ghati jana au juzi akichangia hapa anasema *Engineer* wa *TANROADS* wa mkoa wake ni bora nchi nzima; hapana siyo kweli. *Engineer* Razack wa Morogoro anaweza kuwa namba moja kwa nchi hii na wewe kama unataka kumpima *Engineer* bora aende Morogoro pale akaone. Mafuriko tuliyoyapata na changamoto tunazozipata kule ndiyo utajua kwamba huku kuna mwamba Razack.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anakuwa na uhaba wa pesa na changamoto lakini kwa kweli anajitahidi kwa kazi kubwa sana; tunataka tumpongeze sana. Kwa hiyo nataka kusema hilo la fidia Mheshimiwa Waziri timu ile iende Ifakara – Kidatu tumalizane na watu wale wenye nyumba za kijani wapewe fidia zao. Kuna fidia

ya Ifakara kwenda Malinyi ile barabara, kile kipande cha Ifakara kutoka Ifakara Kikwawila kwenda mpaka Daraja la Magufuli inapita Kata ya Mbasa, Kata ya Katindiuka wananchi miaka minne hawajaendeleza majengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia hiyo wanasema kila mwaka wana-*review* wana-*review*. Sasa hivi nikienda Mbasa kule hawataki kuniona kama Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ya fidia yao jambo ambalo watu wanadanganywa. Barabara hii mkandarasi yupo *site* sasa hivi wananchi wanalalamikia njia panda kwa sababu tuta ni kubwa. Barabara za kuingia kwenda kwenye kata zao zile hazipitiki. Kwa hiyo lazima mumsimamie mkandarasi vizuri tuhakikishe barabara hizi zinapitika zote kwa kiwango kizuri. Kwa mfano Signal nimepata taarifa jana kuna mtu ameanguka maevunjika kutoka kwenye barabara ya lami kuingia kwenye barabara ya kata kubwa wameweka tuta kubwa. Sasa msipokomalia watu wale hawasikii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusaidieni wekeni tuta vizuri ambalo linaweza kwanza likatunza barabara yenyewe. Hii barabara lazima tuilinde kwa ma-*culvert*, vituo kuna maeneo hayana vituo wananchi wanaenda kushukia mbali na taa za barabarani. Mheshimiwa Waziri umeniahidi taa Mang'Ula nakukumbusha, taa ya Daraja la Ruaha nakukumbusha na taa ya Ifakara mjini kuendelea kuziweka katika barabara ya *TANROADS* kutoka Ifakara kwenda Daraja la Magufuli kwenda Lumemo na kwenda Kibaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaziweka taa baadhi lakini umeniahidi ulivyofika pale ukanisaidia kuweka hizo taa nyingine. Kwa sababu ya muda nataka kusisitiza Mheshimiwa Waziri sisi tutakuombea fedha na naamini jambo lako litapita vizuri zaidi. Tunasisitiza sana fikirieni vyanzo vingine vya mapato na sisi kama Kamati ya Miundombinu na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Selemani Kakoso tumeshauri, *document* yetu ipo pale. Sasa hivi kuna hii mnaita *carbon 14* tunapata mapato. Kwa nini tusichangie kwenye barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ile *CIF* ya bandari ambayo inatozwa kwenye reli kwa nini isitozwe pia kwenye barabara? Hata ile shilingi 100 ya mafuta tunayotoza, tupendekeze ni shilingi 100 halafu ikusanywe yote iende kwenye mfuko wa barabara. Kwa hiyo sisi tunataka barabara, tunataka vitu vya barabara na tunataka pesa; lazima tufikirie nje ya *box* tunapataje fedha zaidi zinazotusaidia kukuza mfuko wako ili uweze kujenga barabara zinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusisistiza kwenye madeni. Tumezunguka Mheshimiwa Waziri umesema mwenyewe na umeona watu wanadai. Tuliona Mchina analia kule *Beijing – Mtwara construction* na kuna ma-*sub constructer* wanalia. Lipeni kwa awamu, hamuwezi kulipa yote tangazeni tunalipa mwezi huu hawa, wengine wasubiri watu wataendelea kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri kuhusu kutumika kwa Jeshi letu la Wananchi. Mimi ni miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge tulioenda kule JKT, kuna vijana kule *Engineers* wapo. Sasa kama tulivyofanya Suma JKT je, kwenye *construction* hii hatuwezi kuwa na kampuni ya Jeshi au utaratibu utakaoonekana unafanyika katika kupunguza gharama wakapewa baadhi ya barabara zinapotokea dharura ikafanyika kama baadhi ya nchi inavyofanya? Mheshimiwa Waziri mimi nakuunga mkono hoja mimi sina nongwa na wewe. Nina imani tutakupitishia bajeti yetu hapa. Waheshimiwa Wabunge wote mliosema mtashika shilingi nawaombeni sana, chonde chonde mimi nina lami kilometa 67 tusishike shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Hotuba

ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kipindi hichi ambacho tumepata mvua nyingi kwa kweli wewe na timu yako tumeona mmefanya kazi kubwa tunawapongeza sana. Pia, bado kuna kazi nyingine kubwa mbele ya kuhakikisha barabara zetu zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia sera yenu wenyewe mliyojiwekea Sera ya Wizara ambayo inaeleza kwamba mtahakikisha mnaunganisha mikoa na mikoa kwa kiwango cha lami. Sisi Wilaya ya Karatu tuna barabara kuu mbili muhimu ambazo zinaunganisha Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara inayotoka Njiapanda Karatu kwenda Mang'ola mpaka Lalago mpaka Simiyu inaenda kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu ni barabara ya muda mrefu sana ambayo mlituahidi mtajenga kwa kiwango cha lami kilometa 129 kwa upande wetu wa Karatu kabla kuunga upande wa Simiyu. Mmeahidi na mmekuwa mkituambia usanifu unafanyika na upembuzi yakinifu lakini miaka na miaka tunakaribia sijui miaka mingapi leo toka Waheshimiwa Wabunge waliopita toka 1995 mpaka leo mnatuahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni muhimu sana kwa uchumi. Hii barabara ndipo ambapo kuna bonde kubwa la umwagiliaji. Mnapeleka fedha nyingi kwa upande wa kilimo inajengwa miundombinu mikubwa ya umwagiliaji halafu hakuna barabara ya kufikisha hayo mazao kwenda sokoni. Kuna kilimo huku watu wanalima, tunapata wateja mpaka South Sudan, Uganda, Kenya wanakuja kuchukua vitunguu kule lakini barabara ni mbaya ni mbovu haipitiki mmetuahidi mtajenga kwa kiwango cha lami lakini hakuna. Hayo maneno yenu ya upembuzi yakinifu sijui usanifu tumechoka kuyasikia, tumechoka Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani kuona ile barabara mnaifungua kwa kiwango cha lami kwa sababu ni wenyewe kupitia sera zenu mnasema mtafungua kati ya mkoa na mkoa na ni kilometa 129 tu. Nina imani mkiamua kuweka nguvu na

kutokana na mapato yanayopatikana katika hilo bonde inawezekana. Gharama mnayotumia kufanya marekebisho ya mara kwa mara kwa miaka yote hiyo mimi naamini hiyo gharama mliyotumia tungeshapata angalau kupunguza hizi kilometa 129 mngepunguza angalau sasa tungekuwa tuna kilometa kadhaa baadaye mnaongezea hatimaye tunakamilisha hizi kilometa 129. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kusikia baadaye Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha hoja yako lakini usije ukatupiga *sound* hapa kwa sababu unaweza ukasema. Tumeshapigwa *sound* muda mrefu sana kuhusu hii barabara. Tunatamani na wananchi wanatamani kusikia ni lini kwa uhakika barabara hii mtajenga kwa kiwango cha lami hata kwa kuanza kilometa chache kwanza. Fungueni kilometa chache tu baadaye halafu muendelee, hiyo ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Karatu – Mbulu. Kwa sisi upande wetu wa Karatu – Mbulu ni kilometa 51 tu mlishakuja mkasaini pale na mkatuletea wakandarasi mkafanya kasherehe kadogo mpaka leo. Ndiyo maana nasema mnatupiga *sound,* mpaka leo hakuna. Najua kwa upande ule wa Manyara imeshaanza lakini upande wetu pia bado; ni lini? Au tuendelee kusikiliza habari ya upembuzi yakinifu sijui mchakato sijui na nini? Siku hizi mmetuletea na hichi kitu kinaitwa *EPC+F* yani kila siku mnatupiga maneno maneno fulani hivi ambayo yanatupa matumaini lakini kule *field* hakuna kinachotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara pia ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu inakutanisha Mkoa wa Manyara na Mkoa Arusha. Kumbuka Karatu ni kitovu cha utalii na barabara nyingine inayotoka Mang'ola watalii wanaenda kule kuangalia Wahadzabe ndipo walipo. Wahadzabe wanapatikana kule mtu anatoka *all the way from* Marekani wapi wapi anaenda kumtafuta Muhadzabe lakini akifika kwenye hiyo barabara ni balaa. Kwa hiyo mzingatie na hilo, mzingatie pale ni kitovu cha utalii tunataka hizi barabara zifunguliwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine. Hii barabara ya Makuyuni mpaka lango la Ngorongoro nataka nikwambie Mheshimiwa Waziri kwanza ukiacha kipande cha Makuyuni - Mto wa Mbu ambacho sasa hivi kinasumbua lakini kipande kingine chote kilichobaki ni miongoni mwa barabara *the best* ndani ya nchi hii. Ina miaka 20 ukipita pale haina hata tobo haina ukiacha hii ambayo inasumbua kati ya Makuyuni na Mto wa Mbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa imepewa muda wa matazamio miaka 15 imeshaisha sasa hivi ina miaka 20 ni barabara nzuri na barabara bora sana. Nataka nikuulize huyu mkandarasi aliyejenga hapa na hawa wakandarasi wanaojenga barabara za siku hizi hivi kwa utaalamu ni ule ule au kuna utaalamu uliobadilika ukaongezeka? Kwamba huu utaalamu wa siku hizi barabara haina hata miezi imeshaanza kuwa na matobo. Barabara ikishakuwa na mwaka inakuwa siyo barabara tena ni kichaka gharama yote iliyowekwa pale haipo. Nataka kuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi kwa nini ule ujuzi uliyokuwa umetumika kwenye mfano wa hii barabara moja kwa nini usitumike kwenye barabara za leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweka fedha nyingi, tunatumia fedha nyingi za Watanzania walipa kodi lakini barabara ni chakavu ni mbovu inatengenezwa kiujanja ujanja mno. Halafu mbaya zaidi barabara zikiwa wakati wa mvua sasa ndiyo eti mnaanza wakandarasi ndiyo wanaanza. Yaani kukiwa na mvua nyingi ndiyo tunaona ma-*grader,* ndiyo mnaanza kukwangua wakandarasi ndiyo wanaanza kufanya. Kwa nini msisubiri wakati ambao ni mzuri zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ule wakati mbovu nyie ndiyo mnaanza kutengeneza. Kwa nini ule wakati mbovu barabara zisitazamwe kuangaliwa maji yanapitaje yanafanya nini halafu ikishakamilika mtengeneze wakati ambao siyo wa mvua ili itengenezeke katika ubora ule unaotakiwa *then* baadaye mkague wakati wa mvua? Je, kile ambacho kimetengenezwa ndicho ambacho kitakidhi mazingira yote wakati wa mvua na wakati wa kiangazi? Ni muhimu sana mkaangalie haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ya Makuyuni – Ngorongoro kuna baadhi ya maeneo mmeweka *drift* kuna baadhi ya maeneo hakuna *drift*. Wataalamu wanasema wameifanya hivyo kwa sababu sisi tunapakana na hifadhi kwa maana kuna wanyama wanaotoka Ngorongoro wanaenda Manyara; ni sawa sawa lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo hiyo *corridor* haipo. Tunaomba mtuwekee drift.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo ndani ya mji kabisa hakuna hizo *drift* kwa sababu mvua zikiwa nyingi tope linatoka nje linapita kati kati ya barabara. Barabara ile ni ya watalii, magari yanakwama muda mrefu utalii nao unadorora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna baadhi ya maeneo hakuna ile mifereji mikubwa waliyoijenga. Sasa yale maeneo ambayo si *corridor* za wanyama tunaomba watujengee mitaro, mitaro iwepo ili maji yaweze kupita kwa sababu hii barabara iko chini sana, maji mengi yanasimama barabarani hali ambayo inaleta usumbufu kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kuna wananchi wetu wa Manyara Kibaoni walipisha upanuzi wa uwanja wa ndege. Baadhi wamewalipa fidia na wengine hawajawalipa fidia. Wale waliowalipa fidia waliwaahidi watawalipa riba, lakini hawajawalipa riba mpaka leo na ukisoma miongozo yao inaelekeza kabisa kuwa kuna riba. Wananchi wale wanataka kujua, je, ni lini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:**…watalipwa fidia zao na riba zao ili waweze kuzipata wamesubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, atafuatia Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata ajiandae.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nimesimama katika Bunge hili Tukufu nikianza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Vilevile nimpongeze sana Waziri wetu kwa kazi nzuri aliyoifanya ya ujenzi mkubwa sana wa barabara katika nchi yetu. Mimi nisiwe mchoyo wa fadhila, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mtendaji Mkuu pamoja na Meneja wangu wa Mkoa wa Tabora. Viongozi hawa kwa kweli sisi watu wa Tabora wanaendelea kutuheshimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kuwapongeza viongozi kwa sababu katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia, pale Kaliua tulikuwa na kipande cha kutoka Kaziramba kwenda Chago, kilometa 36. Kipande kile, kwenda Kigoma, chote kimekamilika kwa kiwango cha lami na wametumia karibu shilingi bilioni 38 na ndiyo maana nasimama kifua mbele kuanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia shilingi 11,700,000,000 kwa ajili ya kujenga kilometa saba za lami kutoka katika Kijiji cha Ugansa kwenda kwenye mji mkubwa wa Usinge na ndiyo maana kwa mara nyingine ninasimama kwenye sekta ya barabara kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatu, Mji wa Kaliua pale katikati hatukuwa hata kipande cha lami, lakini kupitia *TANROADS* tayari wamekwishamaliza takribani kilometa tatu na sasa tunavyoongea mkandarasi yupo *site* na anaendelea kutokea

Ushokola kwenda Relini. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kaliua kusema tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru sana Mtendaji Mkuu, tunamshukuru sana *engineer* wetu wa mkoa na tunamshukuru zaidi Mama Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi mema na wananchi wa Kaliua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, meneja wangu wa mkoa, wengi walikuwa wanaongea hapa, mimi nilifikiri wale ambao wamemaliza kufanya kazi kubwa kama hizi ndio wanaostahili hata *promotion*, ndio wanastahili hata makofi mengi sana. Mheshimiwa Waziri hajaja pale, lakini Naibu wake amekuja, kazi iliyofanyika kule sio kazi ya kawaida. Kwa hiyo, mimi nisimame na niendelee kusifu kazi nzuri inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo la mwisho kwa niaba ya wananchi wa Kaliua, hivi karibuni tulipata tangazo, sisi pale Kaliua barabara imepita nje ya Kaliua, lakini kabla ya ujenzi walitaka kupitisha katikati ya mji kwa ajili ya kubomoa zile nyumba za wananchi pale. Wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Dkt. Kikwete, wananchi wa Kaliua tuliomba kwamba barabara ipite mbali kule ili kuepusha athari hizi. Sasa *TANROADS* walikwishakamilisha kujenga na wanaendelea kujenga. Hivi karibuni tulipata tangazo kwamba zile nyumba ambazo ziko karibu na barabara zivunjwe ndani ya siku 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa hekima zake Mheshimiwa Waziri, mimi nilimpigia Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* na nikampigia wa kwangu wa mkoa, kwa kweli wamefanya uamuzi sahihi wa kuona kwamba jambo lile kwa sasa halina afya wala hata kwa mwakani halina afya, kwa sababu tuliomba na tukakubaliwa. Niwaombe wananchi wa Kaliua pamoja na kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekubali, niombe sasa tusiendelee kujenga nyumba mpya kwenye hifadhi ili kulinda vizuri barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaombi kubwa sana moja, nilikwishazisoma Ilani tatu za Uchaguzi za Chama Cha Mapinduzi, zinaongelea barabara ya kutokea Mpanda, zinaongelea barabara ya Kaliua, zinaongelea barabara ya Ulyankulu, zinaongelea barabara ya Katavi na zinaongelea Kahama.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa, Mheshimiwa Ngassa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngassa, tafadhali.

**TAARIFA**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa mchangiaji kuhusu huyu Meneja wa Mkoa wa Tabora, *Engineer* Mlimaji, ni miongoni mwa mameneja ambao wanakwenda *extra miles,* tofauti hata na fedha anazopewa na Wizara. Ni meneja anayefanya vizuri. Kwenye Mkoa wetu kila Wilaya tumewekewa taa za barabarani na kwa Igunga tumepata kilometa nane, anafanya vizuri sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ngassa. Mheshimiwa Aloyce Kwezi unaipokea Taarifa?

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea Taarifa hiyo kutoka kwa Mbunge makini, Mheshimiwa Ngassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo moja kubwa, niombe pale Ukumbi Siganga na Zugi Mlole mkandarasi aliye *site* wambane vizuri ili aweze kukamilisha, kwa sababu kata mbili hazipitiki mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine ni taa za barabarani kutoka Kaliua kwenda Kasungu, Kamsekwa na Igagala. Jimbo hili ndilo jimbo kubwa katika Mkoa wa Tabora lenye idadi kubwa ya watu, kwa hiyo, niombe waliangalie kwa macho mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye ile barabara wanayojenga kutoka Ushokola kuja Relini kipo kipande cha barabara yao kuna miji mingi sana ya watu, niombe kilometa moja ya lami kuelekea Zugi Mlole. Wakitupatia kilometa moja ya lami na hili ninajua ni dogo kwa Mheshimiwa Waziri, najua ni mchapakazi, halafu anafanana na mimi, kwa hiyo, ni jambo ambalo ni jepesi. Nimwombe sana kwa hekima zote, ninaomba atuongezee kilometa moja na itapendeza kama utatoa maelekezo hata jioni ya leo unamaliza, mimi hata sina shida na ninawashawishi Wabunge wenzangu sisi tumwombee ili apate hizo trilioni tatu ili nyongeza iende ikajenge Mpanda - Katavi, Mpanda – Kaliua kwenda Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya naomba niunge mkono hoja, lakini niaba ya wananchi wa Kaliua nimalizie kwa kusema kwamba tunashukuru kwa kutokutubomolea nyumba zetu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwezi.

Waheshimiwa Wabunge, tuna taarifa ya wageni waliopo Bungeni ambao hawakutangazwa, kwanza tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge na tunao wageni 42 wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi ambao ni wasaidizi wa Mbunge, Sekretarieti ya Wilaya, watumishi wa Chama na Madiwani kutoka Ileje, Mkoa wa Songwe, kama mpo msimame na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Maafisa Elimu Kata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 30 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Iyula Malaika kutoka Manispaa ya Morogoro. Wanafunzi kutoka shule ya Morogoro kama wapo, sawa karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 53 wa Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir na Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni viongozi na watumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*. Kama wapo wasimame na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi la pili ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 50 wa Chuo cha Biashara *(CBE)* cha Jijini Dodoma, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu. Kama mpo msimame na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 65 na walimu sita wa Shule ya Msingi *St. Gaspar* ya Jijini Dodoma, kama mpo msimame na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 80 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi *Holy Face* ya Jijini Dodoma, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunaendelea, nilishamtaja Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, atafuatia Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata na Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kuweza kuchangia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu katika hotuba yake ya kwanza alisema kuwa atahakikisha kwamba miradi yote inayoendelea/iliyoachwa na marehemu itatekelezeka. Kweli miradi iliyoachwa katika Mkoa wa Dar es Salaam imetekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Daraja la *VETA* lilikuwa halieleweki wala hatujui kwamba lingekwenda vipi, leo hii daraja lile liko katika asilimia kubwa ya kuisha. Daraja la Uhasibu, ujenzi wa barabara kutoka Bendera Tatu mpaka Gerezani, kile kipande kwa kweli kimekwisha, huwezi kudhani kwamba uko Tanzania, utafikiri uko kwenye nchi nyingine yoyote, kumbe tuko Tanzania tena katika Wilaya ya Temeke. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sasa napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu mdogo wangu Aisha anafanya kazi nzuri na mtoto wangu Mheshimiwa Bashungwa pamoja na Naibu wake. Hawa kweli ni viongozi wakarimu, wanaosikiliza shida za wananchi wao na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawalipa mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwapongeza sasa nije kwenye mchango wangu ambao utajikita katika hotuba ya bajeti ya Waziri ukurasa wa 10, 15 na 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na ukurasa wa 10 - ujenzi wa barabara; upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha na Daraja la Kibamba, Daraja la Kiluvya na Daraja la Mpiji, ujenzi wa Barabara ya Makongo – Goba, upanuzi wa Barabara ya Morocco, upanuzi wa Barabara ya Tungi – Kibada, upanuzi wa Daraja la Gerezani na barabara za maingiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali, miradi hii imetekelezeka kwa asilimia kubwa japokuwa kuna changamoto. Upanuzi wa Barabara ya Morocco, barabara ile mvua inaponyesha ghafla inakuwa bahari, hakupitiki, hakuendeki na msongamano unakuwa mkubwa. Pale wanatakiwa

wakafanye tafiti ili kujua ni tatizo gani linalosababisha yale maji yajae kwa kiasi kile. Waangalie kwa upande mwingine namna ya wanavyoweza kufanya katika kulirekebisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio, lakini ziko changamoto. Niwapongeze sana kwa ile *El Nino* pamoja na kimbunga. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri wamefanya kazi kubwa sana. Hakukuwa na mawasiliano kati ya Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Dar es Salaam, yalikuwa yamekata kabisa. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na alionja *taste* ya wali ule wa Pwani ya Kilwa, aliona jinsi mama zake tunavyoandaa vyakula kule. Ninamshukuru sana kwa hilo, alijitoa kwa hali na mali. Kwa kweli Serikali ilifanya kazi kubwa, kulikuwa hakuna jinsi, hali ile ilikuwa ni mbaya. Yale mambo ni ya Mungu si ya binadamu, kulikuwa hakuna njia, ni lazima tufanye vile, lakini wananchi walifarijika kwa jinsi alivyolichukulia kwa upekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitaanza na changamoto, tuna changamoto kubwa kwa Barabara ya Kilwa ambapo ukifika maeneo ya Mbagala kuna msongamano wa kutisha, yaani ile barabara imezongwa, yaani kuanzia kipande cha Mbagala Rangi Tatu hakuna pa kupita. Kila siku tunaambiwa kuwa kuna upanuzi wa barabara ile au itajengwa kwa njia nne, lakini kuanzia Mbagala Rangi Tatu, Kokoto mpaka Kongowe muda umekuwa mrefu sana. Wananchi wamefanyiwa tathmini kwa muda mrefu hawajalipwa na hata huo ujenzi wenyewe bado, lakini ukiingia kwenye vitabu huu ni mwaka wa tatu sasa kutajwa Daraja la Mzinga na Barabara ya Kilwa. Mheshimiwa Waziri akifika hapa wakati anahitimisha naomba aje aniambie ni lini barabara ile itaanza kujengwa, ninataka *commitment* ya Serikali sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nieleze kuhusu Barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwi Songani. Hii barabara ni ya kiuchumi, Kigamboni tumeipa ni eneo la kiuchumi ambalo lina viwanda, lakini barabara hii imeguswa tu kidogo, imejengwa sijui kilometa moja tu na hakuna mwendelezo. Mvua hizi barabara ile ilikuwa haipitiki. Wenye viwanda kule Kimbiji wanaomba sana muwasaidie ili ile barabara ipitike, lakini na wananchi nao

wanapata shida ya usafiri, wanapanda bodaboda na magari kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa pamoja na juhudi zao za kuandaa kutusaidia kwa muda, lakini tunaomba sasa barabara ile ya Kibada – Kisarawe II – Mwasonga – Pemba Mnazi, lakini na Tundwi Songani. Wananchi wa Tundwi Songani wanahisi wao kama wako kisiwani, wanahisi wao kama hawana watu wa kuwasemea. Sasa mimi leo naongea hapa kama mkazi wa Dar es Salaam na Mbunge wa Dar es Salaam, nataka anipe *commitment* leo hii, aniambie Barabara ya Kibada – Kisarawe II – Mwasonga – Tundwi Songani ni lini itaanza kujengwa na kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie barabara ya kutoka Kongowe mpaka Mji Mwema, barabara ile ni ya muda mrefu, imechakaa sana na imekuwa finyu. Niombe Serikali waangalie jinsi ya kuiongeza barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwneyekiti, pia barabara ya kutoka Mji Mwema – Somangira – Kimbiji – Pemba Mnazi, barabara ile isipokwisha vile viwanja vilivyokatwa kule Pemba Mnazi wananchi wa kule watazidi kukaa mji ule hautaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Waheshimiwa Wabunge ambao wana viwanja kule Pemba Mnazi wapo, lakini wanashindwa kufika. Wakiangalia wanaona kama wanapelekwa porini, lakini kumbe si porini, upori unakuja kwa sababu ya kukosa barabara yenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iwaangalie wale wananchi, wananchi wale wako kisiwani sasa kwa sababu Barabara ya Kibada kwenda *Kisarawe Two*, kwenda Mwasonga mpaka Pemba Mnazi haipitiki na barabara ya Mji Mwema kupita Somangira kwenda Kimbiji haipitiki. Sasa watu hao wataishi vipi? Niiombe Serikali waziangalie barabara hizi kwa jicho la kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hizo yapo mafanikio, wote tumeona kuna mafanikio ya zile barabara za mwendokasi. Barabara ya mwendokasi kutoka Mbagala mpaka Gerezani imekamilika, lakini barabara ile imewekwa mawe na vigogo ili watu wasipite. Ikumbukwe kwamba kuna wagonjwa wanaoenda na *ambulance*, sasa tufike sehemu ukifika Rangi Tatu huku hakuendeki, huku hakuendeki, basi angalau yale magogo waliyoyaweka na yale mawe wapishe angalau *ambulance* ipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaotoka Jimbo la Mkuranga wanatumia barabara ile kwenda Muhimbili, wanaotoka Mikoa ya Kusini wanatumia barabara ile kwenda Muhimbili kupeleka wagonjwa. Hivyo, barabara ile inapokuwa na changamoto kubwa inakuwa shida, hata wagonjwa wanaweza wakafa njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hizo, pia niombe barabara ya kutoka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, hitimisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote. Waendelee hivyo na Mwenyezi Mungu atawabariki, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge wakati natangaza wageni, miongoni mwa wageni 42 wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi, yupo Ndugu Diana Ngabo ambaye ni Katibu wa Umoja wa Vijana CCM Ileje. Naomba usimame na karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa tunaye Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata atafuatiwa Mheshimiwa

Asia Abdukarimu Halamga na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ajiandae.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa na Naibu wake, kaka yangu Mheshimiwa Godfrey Kasekenya kwa kazi nzuri waliyoionesha katika kipindi kigumu cha maafa ambacho kimepita. Kwa kweli hakika upele umempata mkunaji. Mheshimiwa Rais hakukosea kuwaunganisha majembe haya. Mimi nawaombea Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki ili muendelee kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara ya ujenzi wote akiwemo Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Rukwa Dada yangu Mgeni Mwanga. Ni mama shupavu ambaye katika kipindi cha shida kwa kweli ameonesha uwezo wake na umama. Amefanya kazi nuri katika Mkoa wetu wa Rukwa, kwa kweli alihakikisha barabara zinapitika, barabara zilikuwa zimeachana hasa katika Bonde la Rukwa. Lakini mama huyu amepambana akishirikiana na Mawaziri hawa akiwemo Bashungwa na Kasekenya, wamekuwa wakipishana, akitoka Waziri Bashungwa anakuja Naibu Waziri Kasekenya. Kwa kweli mmeafanya kazi nzuri hongereni sana, mmetukimbilia wakati wa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wangu wanawake wa Mkoa wa Rukwa, wale wote waliopata maafa poleni sana Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye suala la uwanja wa ndege, katika Mkoa wetu wa Rukwa tumepata bilioni 76 za

uwanja wa ndege. Tumezipokea na uwanja unaendelea kujengwa na sasa imefikia 40%, tunaomba uwanja huu uishe haraka ili hizo 60% zilizobaki basi zifanye haraka ili wananchi wa Mkoa wa Rukwa waweze kufurahia matunda ya Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikua na Mradi wa barabara kupitia *TACTIC*, sasa kutokana na upanuzi wa uwanja wa ndege kuna kilometa 1.3. Sasa tunaomba mamlaka itupatie mbadala wa barabara ambayo wananchi watakwenda kuitumia ambayo itabadili ile kilometa 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuishukuru sana sana Serikali Sikivu ya Chama cha Mapinduzi, kipindi kilichopita nilisimama hapa kuomba kutolewa matuta ya barabara iliyotoka Songwe mpaka Sumbawanga. Nashukuru sana Serikali imesikia kilio cha wana Rukwa imeweza kuyatoa matuta yote, sasa hivi Mkoa wa Rukwa ni Mji mzuri, naomba sasa Serikali iweze kuweka mataa barabarani kutoka Songwe mpaka Sumbawanga ni giza, barabara ni nzuri lakini giza limetawala. Kwa hiyo Wizara iweze kuweka taa za mataa kama ilivyo barabara ya kutoka Katavi Mpaka Tabora, barabara inapendeza ina mataa na ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba, barabara ile inatunzwa vizuri na watendaji wa *TANROADS* akiwemo *Engineer* Selemani Bishanga ambaye ni *Engineer* wa Mkoa wa Songwe wakishirikiana na *Engineer* Mgeni Mwanga wanazitunza vizuri sana hizi barabara. Mimi naomba tuwapongeze, na Mheshimiwa Waziri ukipata wakati mwingine unawapongeza na unawatia moyo hawa watendaji, wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye suala la barabara za Mkoa wa Rukwa, barabara ya kutoka Mfinga – Muze – Ilemba – Kilyamatundu mpaka Mlowo, barabara hii kwanza kabisa niipongeze sana Serikali wakati wa maafa imetuletea bilioni sita za dharura. Hongera sana Serikali mnatukimbilia sana wakati wa shida, Mungu awabariki, fedha hizi zimeweza kusaidia

barabara hii inajengwa lakini niombe, barabara hii ni ya kiuchumi, mazao mengi ya kimkakati yanatoka Bonde la Rukwa. Tunaomba sana barabara hii iweze kukamilika haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee suala la nyumba za *TBA*, hapa Dodoma kuna nyumba za *TBA* zimejengwa na nyingine zinaendelea kujengwa. Lakini nyumba za *TBA* zinakuwa zimechakaa sana, tunaomba Wizara iweze kuzikatabati na kujenga nyingine kwa ajili ya kuingiza kipato kwenye suala zima la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee suala la barabara za Dodoma. Hii Dodoma ni jiji ambalo linakwenda kuwa kubwa sana. tunaomba sasa muweze kuongeza Barabara, ukitoka hapo nje tu unakuta foleni kubwa na ndefu. Ninaomba Wizara iangalie suala la kuongeza barabara katika Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninaunga mkono hoja na Wabunge wenzangu hii trilioni 1.5 tuweze kuipitisha kwa kishindo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana,Mheshimiwa Asia Abdukarim Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mheshimiwa Armandus Julius Chinguile ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara hii muhimu kabisa Wizara ya Ujenzi katika nchi yetu kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba yale matatizo makubwa ambayo tumeyapata kwenye nchi yetu kulingana na majanga ya *El Nino* kutokea mwezi wa tisa mwaka 2022, tumeweza kukabiliana nayo na ile shida kubwa imeondoka kwenye nchi yetu, jambo ambalo hatukuweza kulitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa tunaendelea kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. kile kipindi cha maafa kwetu sisi tunaotoka Wilaya ya Hanang' ilitolewa zaidi ya bilioni 1.5 kwa ajili ya kuja kuokoa mji wetu na kwa namna hii nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Innocent Bashungwa Mbunge wa Jimbo la Karagwe, hakika wananchi wako hawakukosea kukuchagua na ninataka kuwahakikishia wananchi wako kuwa, wasikosee tena wafanye kama walivyofanya mwaka 2020. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuwa ni mwema kwa watu wa Hanang', umekuwa ni mwema kwa Watanzania, mafuriko katika nchi yetu yametokea katika mikoa mbalimbali lakini kila sehemu tumekuona kwa bodaboda, Mama ntilie, umehakikisha kwa jitihada zako za kibinadamu pamoja na kumuomba Mungu kuhakikisha kwamba unasimamia vizuri zile fedha za dharura ambazo, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amezitoa. Lakini bila kusahau Naibu wako Waziri, Baba yangu Kasekenya, Katibu wako Mkuu ndugu yetu Aisha, Mwana Mama shupavu kabisa ambaye ameanza kutenda haki na amefanya kazi kubwa sana bila kuwaangusha wanawake na bila kuwasahau Naibu Katibu Mkuu wako na timu yako nzima ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Meneja wetu wa Mkoa, hakika katika kipindi kile cha majanga siyo tu Hanang' ndani ya Mkoa mzima tulipata changamoto hizo za *El Nino* lakini Meneja wetu Doto Masele hakika ni mchapakazi, mtu bingwa, tunakushukuru sana. Tunajua ni sehemu ya kazi yako na majukumu yako lakini sisi watu wa Manyara tuna kila sababu ya kukushukuru kwa sababu umefanya zaidi ya unavyotakiwa kufanya katika wajibu wako wa siku zote wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga fedha katika bajeti na kutuletea Mkoa wa Manyara ili kuhakikisha kwamba Mkoa wetu unafikika na unaweza kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, kuna kila sababu na haja ya kuongeza fedha Mkoa wa Manyara. Tumetengewa kiasi cha shilingi bilioni 11 ambayo ni sawa na aslimia 13 tu ndani ya Mkoa wetu wa Manyara katika utatuzi wa changamoto za barabara, haitoshi, haitoshi, haitoshi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuiomba sana Serikali kwa sababu Mkoa wetu wa Manyara una jumla ya mtandao wa barabara za changarawe pamoja na lami 1657. Hata hivyo, ukizingatia lami ambayo inapita kwenye Mkoa wetu katika mtandao wa barabara ni kilometa 207. Lakini barabara halisi, lami ambayo iko ndani ya Mooa wa Manyara ni kilometa 52 peke yake na hasa ukizingatia Mkoa wetu wa Manyara ni Mkoa wa tatu kwa ukubwa katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kukuomba sana Mheshimiwa Waziri watu wa Manyara tunakuheshimu na tunakupenda. Toka ukiwa TAMISEMI umekuwa ni sehemu ya kuja Manyara na unaijua sana jiografia, kilometa hizi 52 kwa kweli hazitoshi ndani ya Mkoa wetu. Tukushukuru kwa juzi ulivyokuja na kutupitishia Kilometa saba za kutoka Dareda *Center* kwenda Dareda *Mission* ambazo zinasababisha mkoa wetu kuwa na kilometa 59 za lami. Tunakushukuru sana kwa hili lakini tukuombe sana bado mna kazi kubwa ya kuangalia Mkoa wa Manyara hasa ukizingatia jiografia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe sana sasa Serikali kwa kuangalia barabara hizi za ndani ya mkoa. Tuombe ifunguliwe barabara ya Singe – Galapo - Kiteto mpaka Simanjiro ili kutengeneza mkoa wetu kuweza kuongezewa kiwango hiki kikubwa cha Barabara tuone hii asilimia 59 ya lami inakwenda kuongezeka kulingana na jiografia ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuombe barabara ya Basotu kwenda Mbulu, hii ikifunguliwa mtakuwa mmetusaidia sana, lakini tuishukuru Serikali kwa kutupatia fedha barabara ya Nangwa kuja Gisambalang kutokea Kondoa, hakika tunauona huu ni mchango

mkubwa na tunaomba sasa ule ujenzi uanze ili ile dhima ya Mheshimiwa Rais ya kuendelea kuufungua Mkoa wa Manyara tuendelee kuiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee tuiombe sana Serikali, Mradi wa *EPC+F* ni Mradi ambao ulikuwa mkubwa wenye matumaini makubwa katika mkoa wetu na mikoa mingine ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Barabara ile ingeweza kufungua kati ya Mkoa wa Manyara na Tanga, Mkoa wa Manyara na Morogoro na ingeweza kufungua Dodoma, Arusha pamoja na Singida. Pia, ingeweza kutufungulia barabara za ndani Kiteto, Simanjiro mpaka kuja kutokezea Kondoa. Hakika hii barabara ilikuwa na tija sana na ule mradi uliuwa una mpango mzuri, tuombe Serikali ikazie na ione namna bora ambayo itakuja sasa ili ile nia na dhamira njema ya Serikali iweze kufika mwisho na wananchi waweze kupata barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa namna ambavyo mmeendelea kuwabeba wakandarasi wanawake na hatimaye kwenye bajeti hii tunaona mtawapa zaidi ya kilometa 20 za lami. Huu ni uwekezaji mkubwa kwa wakina mama na ninawaomba sana wakina mama watakaopata hizo fursa wahakikishe wanafanya kikamilifu ili kuendelea kuweka dhamira njema ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumuinua mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze wizara kwa sababu mmekuja na mikakati mizuri kwa upande wa vijana ukiangalia ukurasa wa 60 wa hotuba ya bajeti yako, *page* nzima umeongelea vijana. Tunaiona mikakati ya kufanya mikutano zaidi ya mitano ya kukutana na wanafunzi wa shule za msingi pamoja na sekondari ili kuweza kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi. Huu ni uwekezaji mkubwa lakini bado tumeona mmeendelea kuwa na mpango wa kuwasaidia vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa sababu ya muda ningeendelea kuchangia lakini Mheshimiwa Waziri pamoja timu yako hongera sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, atafuatia Mheshimiwa Armandus Julius Chinguile na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya ujenzi. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Bashungwa namna ambavyo anafanya kazi kubwa na nzuri sana, anaitendea haki Wizara yake. Mheshimiwa Waziri Bashungwa endelea na moyo wako huo unaokutuma kufanya kazi za Watanzania. Sina mashaka na wewe unafanya kazi nzuri sana Mwenyezi Mungu aendelee kukusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kaka yangu Kasekenya, unafanya kzi nzuri sana. Yaani wewe umekuwa unaifahamu Tanzania karibu yote. Maana hata maswali unayojibu hapa unajibu kwa uhakika kabisa na kujiamini. Pongezi nyingi sana kwako kaka yangu Kasekenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze Wizara yote kwa ujumla wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya hawa viongozi wa Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mkuu wa Mkoa wangu wa Mbeya kaka yangu Juma Zuberi Homera, yeye pamoja na Kamati ya ulinzi na usalama anafanya kazi nzuri ndiyo maana Mkoa wetu kwa sasa uko shwari kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani Mbeya tuna Meneja wa *TANROADS Engineer* Matari Masige, huyu *engineer* anafanya kazi nzuri sana pale Mkoani kwetu Mbeya. Yeye pamoja na watumishi wote wa *TANROADS* wa Mkoa wa Mbeya, mara tu wakisikia kwamba kingo ya barabara au kwenye Daraja imebanduka, imechomoka au gari imegonga, anaposikia yeye na timu yake

wanakwenda haraka sana kurudishia kingo zile kwa ajili ya usalama wa Watanzania wanaopita na magari. Nakupongeza sana Mheshimiwa Masige, kazi yako na timu yako ni nzuri sana. endelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naamini Mtendaji Mkuu wa Taifa wa *TANROADS* anasimamia vizuri sana hawa Ma-*engineer* wa mikoa maana nimeona Wabunge wengi sana wanaposimama hapa wanawapongeza mameneja wao wa Mikoa wa *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, barabara ya kwetu Mkoani Mbeya tunaishukuru sana Serikali kwa kumleta Mkandarasi na kuanza kazi pale. Wananchi wa Mkoa wa Mbeya tuna imani na matumaini makubwa sana kwamba, barabara ile itakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa kweli mara baada ya kusainiwa barabara ile ambayo Mkandarasi alisaini 14 Februari, 2023 mkataba ule unaonesha barabara ile ikamilike 14 Aprili, 2025. Barabara ile nimeona hapa mmeeleza kwamba asilimia 14 imekamilika. Hofu na mashaka ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya ni kwamba, ile barabara hatuna uhakika kama itakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa yule mkandarasi fedha ambazo aliomba za awamu ya kwanza kiasi cha shilingi bilioni 13.6 alikabidhiwa kwa wakati. Awamu ya pili aliomba bilioni 6.8 hajapewa, awamu ya tatu aliomba bilioni 4.3 alipewa bilioni nne pekee, milioni 300 hajapewa, awamu ya nne ameomba fedha bilioni 2.8 hajapewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mashaka sana, sasa mkandarasi anahitaji fedha, hapewi kwa wakati ile barabara inakwenda kwa kusuasua na ile barabara ni ya muhimu sana. Watanzania kwa maana ya wananchi wanaoishi Mkoa wa Mbeya ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara Wilaya zote iwe Rungwe, Kyera, Mbalali, Mbeya Vijijini wote wanaitegemea barabara ile. Lakini mpaka sasa ile barabara inakwenda kwa kusuasua. Kama ni asilimia 14, sasa ni miezi 16 imepita na barabara ile haileti matumaini kwamba hiyo miezi kumi iliyobaki itakamilika? Kwa sababu kama ni asilimia 14 bado asilimia 86 ili barabara ile ikamilike. Je, ile barabara itakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri, unapokuja hapa naomba sana, kwa sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema kwamba barabara ile inatakiwa ikamilike na barabara ile kwa kuanzia kutoka Uyole mpaka Ifisi ilitakiwa itumike kwa kilometa 23. Lakini Mheshimiwa Rais kwa mapenzi yake mema akasema kwa kuanzia muanzie na kilometa 29, kama ni kilometa 29, mpaka sasa hivi hapaeleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachoelewa na Watanzania, atakachosema Mheshimiwa Rais hayo ni maagizo inatakiwa utekelezaji. Sasa ni kwa nini hampeleki fedha kwa wakati? Mpaka sasa hivi mkandarasi yule anadai shilingi bilioni 9.9 ambapo mngekuwa mmempa, barabara ingekuwa inakwenda kwa kasi, sasa inakwenda taratibu inasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ni ya muhimu sana, ukizingatia kule Mkoani Mbeya kiuchumi ukienda kwa maana ya Nyanda za Juu Kusini ile barabara pale Mkoa wa Mbeya ni kitovu cha wafanyabiashara kwa Nyanda za Juu Kusini lakini haitiliwi maanani hofu ya Wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanataka kujua ile Barabara kwenye hii miezi kumi itakamilika? Katika fedha kwa sababu fedha za ujenzi ule ni shilingi bilioni 138 mpaka sasa hivi ni shilingi bilioni 17 tu zilizotolewa. Je, hiyo barabara itakamilika? Tuna mashaka makubwa sana sijajua mnafikiria kitu gani na tunalia kila siku juu ya ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ya kutoka Uyole kwenda Ifisi ni barabara muhimu sana iko tu moja hatuna *service road* pembeni ni pamoja hapohapo makontena yanapita hapo, *petrol tank* hapohapo, magari ya mizigo hapohapo, mabasi

makubwa hapo, daladala hapo baiskeli, bajaji, bodaboda. Sasa kama kuna mgo njwa anatoka kwenye wilaya nyingine zile za Rungwe, Kyela, Mbarali au Mbeya Vijijini anapitapitaje sasa kwa sababu pamebanana ili wamuwahishe mgonjwa rufaa ukizingatia hospitali ya rufaa iko mbali kabisa kule, wanamfikishaje kwa haraka? Kusema apae haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali na Wizara ya Ujenzi naomba itazameni kwa makini sana ile barabara. Ile barabara yenyewe iko Mbeya Jiji, Jiji lenyewe ndio la Dkt. Tulia Ackson ambaye ndiye Spika wetu hapa. Dkt. Tulia Ackson kwa mapenzi mema Mheshimiwa Rais akampa ruhusa ya kwenda kugombea kuwa Rais wa Mabunge ya Dunia kule, amekuwa Rais wa Mabunge ya Dunia kwenye njia za watu kule akifika kule duniani tumeona anapita na ving'ora kwa usalama kabisa wanamtembeza yeye kwenye barabara yake anapita wapi? Wakimtembelea atapita wapi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana sana Serikali tuna kilio kikubwa sana Mbeya …

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** ...ni kweli kabisa mawasiliano Mbeya ni shida maendeleo yamekwama unapokwenda mjini lazima utumie masaa mawili unavyorudi tena masaa mawili masaa manne yanapotea huko barabarani…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** ...wakati tunajua kabisa wakati ni mali *time is money*. Tunaomba sana Mbeya jamani barabara ile tuna kilio kikubwa sana Mkoa wa Mbeya tunaomba mtupe heshima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo. Anafuatia Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, atafuatiwa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na Mheshimiwa Hamis Tabasam, ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu awali ya yote kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi na wilaya zake ni kati ya maeneo ambayo yameathirika sana na *El Nino* lakini pia kikaja Kimbunga Hidaya na nyakati zote Mheshimiwa Rais alituma wasaidizi wake akiwemo Mheshimiwa Waziri na kuja kwenye maeneo hayo husika. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu Waziri Katibu Mkuu wa Wizara na wataalamu wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Waziri ni msikivu lakini Waziri huyu anajali sana, Waziri huyu simu yake hata ukipiga saa nane ya usiku anapokea, anakusikiliza mnashauriana, mnatafuta ufumbuzi wa jambo ambalo linakukabili Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana lakini tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pale aliposhindwa kuingia wakati ule Wilaya ya Nachingwea na Liwale vikiwa kisiwa Mheshimiwa Waziri kuna chochoro zingine alipita zilikuwa haziwezekani kupita kwa nafasi yake kama Waziri lakini alisema Mheshimiwa Mbunge nimekuja kufanya kazi hapa ya wananchi twende *site* tulipita kwenye maeneo hayo Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kabla ya hayo nilifikiri kwamba kwa sababu kulikuwa na mambo ambayo nilikuwa na kiu nayo nikasema sasa shilingi ya Waziri nitaondoka nayo kurudi nayo kule Nachingwea lakini Mheshimiwa Waziri kwa wema huu uliotufanyia lakini kwa namna ulivyotujali tukiwa na shida siondoki na shilingi yako kwenda nayo kule Nachingwea badala yake tutaendelea kuomba utusaidie hata yale mambo mengine ili yaweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya Masasi - Nachingwea mpaka Liwale kilometa 175. Barabara hii ilishawekwa kwenye mpango wa kujengwa kuanzia 2021/2022, 2022/2023 na baadaye ikaingizwa kwenye Mfumo wa *EPC+F* mwaka jana na tayari mkataba ulisainiwa tarehe 16 mwezi wa sita, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo ambayo yamecheleweshа sana maendeleo kwenye Mikoa ya Kusini ni pamoja na mawasiliano na miundombinu ya barabara. Baada ya kusaini ule mkataba ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami Wananchi wa Mikoa wa kusini kwa maana ya Lindi lakini barabara hii inanufaisha majimbo manne Jimbo la Nachingwea, Jimbo la Ndanda, Jimbo la Masasi na Jimbo la Liwale. Tumekaa mkao wa kusubiri na huku tukiendelea kumwombea dua njema Mheshimiwa Rais kwa wema alioufanya kuelekea hata kusaini huo mkataba ni hatua kubwa na nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu wananchi sasa wamebaki hawaelewi chochote kinachoendelea kuhusu ujenzi wa barabara hii, sasa inakimbilia mwaka na Naibu Waziri hapa amejibu kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe kwamba mradi ule utatekelezeka kabla ya bajeti hii kuisha ambayo kimsingi tumebakiwa na mwezi mmoja kipindi cha bajeti hii kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake aweze kutoa ufafanuzi ambao utawafanya wananchi wa majimbo yale manne kwa

maana ya Nachingwea, Ndanda Masasi na Liwale waweze kujua nini kinaendelea. Tunajua nia njema ya Mheshimiwa Rais na nimeona kwenye hotuba yako hapa ya bajeti Mheshimiwa Waziri lakini mimi kama Mbunge najua wananchi wanatamani kujua zaidi Serikali yao ina nini kuhusu ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko barabara nyingine ya kutoka Nanganga kwenda Nachingwea kilometa 43. Mheshimiwa Waziri wakati uko pale Nachingwea tulizungumza na hili mimi nikuombe sana tayari upembuzi yakinifu unaendelea basi baada ya kumaliza ili na sisi tuende mkoani tukiwa na uhakika wa usafiri utusaidie kuhakikisha hii barabara kwa kipande kile kilichobakia kiweze kujengwa na tuweze kufika mkoani vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili niishukuru sana Serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka pale Nanganga, Ruangwa kuelekea Nachingwea. Tunaishukuru sana Serikali kazi hii kubwa ni nzuri na sisi kama Wana-Lindi na Wana-Nachingwea tunaendelea kuunga mkono juhudi hizi za Mheshimiwa Rais na tunapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko barabara nyingine ya kutoka Nachingwea - Kilimarondo mpaka kwenye Mto Rumesule pale. Kuna Mto Rumesule, Mto Rumesule unaunganisha kati ya Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Ruvuma. Nikuombe Waziri hapa yaani kilometa 90 kutoka Nachingwea kwenda Kilimarondo zinamilikiwa na *TANROADS* halafu kuna kilometa 16 zinamilikiwa na *TARURA* upande wa Ruvuma wanamiliki *TANROADS* na hata lile daraja limeshafanyiwa usanifu waliofanya ni *TANROADS* sisi kwenye vikao vyetu vya mkoa tulishamaliza jambo hilo na tuombe jambo hilo ulichukue ili barabara yote iweze kuhudumiwa na *TANROADS* tuweze kupata sasa uhakika wa kuendelea kujengwa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kibiti - Lindi wenzangu wameizungumzia. Mheshimiwa Waziri kwa bahati nzuri umepita sana hiyo barabara. Hiyo barabara ina mashimo makubwa na sasa imekuwa ni adha na hiki Kimbunga Hidaya kimekuja

kutuonesha maeneo mengine ambayo tayari yalishakuwa mabovu. Hii barabara tumeipigia kelele kwa muda mrefu sana mwone namna ambavyo Wizara mtaendelea kuona namna ya kukarabati hii barabara na Mheshimiwa Waziri kwa namna ilivyo kwa sasa kuna maeneo ambayo hayafai kuweka viraka tena yanafaa kubadilisha kabisa kwa sababu yameharibika. Sehemu ambayo ungeweza kutembea kilometa kwa muda fulani lakini utakwenda kwa mwendo mdogo kiasi ambacho shughuli zingine za wananchi zinasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* mimi niendelee kumtakia heri Mheshimiwa Waziri na timu yake kazi hii wanayoifanya Watanzania tunaiona lakini utakapokuja ku-*windup* bado niendelee kukuomba tena sema neno kuhusu Barabara ya Masasi - Nachingwea - Liwale ili wananchi wa maeneo hayo waweze kutulia mioyo yao ili wajue kabisa kwamba Mama, Dkt. Samia Suluhu Hassan yuko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana pia kwa kuzingatia muda, nakushukuru. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Tabasam.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Ujenzi. Kwanza naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana ambayo ameendelea kuifanya katika nchi hii hongera sana Mama tuko nyuma yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wetu wa ujenzi Innocent Bashungwa kwa kweli kama jina lako lilivyo Innocent uko vizuri na kila mtu amesema kazi nzuri unazozifanya endelea kumtanguliza Mungu pia katika kazi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Naibu Waziri wa ujenzi *Engineer* Kasekenya, kwa kweli unafanya kazi nzuri sana na unatujibu maswali yetu vizuri sana kila siku hapa ahsante sana. Pia niendelee kumpongeza Katibu Mkuu wetu *Engineer* Balozi Aisha hongera sana unatuwakilisha vizuri sana wanawake na uko jikoni katika Wizara hii ya Ujenzi na watendaji wote pia ninawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitakuwa sijamtendea haki nisipompongeza *Engineer* Wetu wa Mkoa wa T*ANROADS* Iringa, *Engineer* Msangi hana baya, anafanya kazi nzuri sana na ana ushirikiano mzuri sana endelea kushirikiana na sisi Wabunge wote hongera sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali iwapatie Wizara hii pesa ya kutosha kama ambavyo Wabunge wengi wamesema pesa hii waliyotoa haitoshi ongezeni ili barabara zetu ziweze kujengwa kwa kiwango lakini pia ili wakandarasi wetu pia waweze kulipwa. Pia ili wanaodai fidia waweze kulipwa kwa sababu barabara ni uchumi wapeni pesa ya kutosha Wizara ya Ujenzi ifanye kazi katika barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Barabara ya Dodoma - Mtera - Nyang'oro mpaka Iringa hii barabara haijajengwa kwa kiwango, hii barabara ina makorogesheni mengi sana mimi naomba Serikali iangalie Mheshimiwa Waziri hebu pita; twende tu hata kesho baada ya hii Wizara ukaangalie hii barabara ilivyokuwa mbaya, magari makubwa yanapita kwenye hii barabara lakini viraka ni vingi sana ukikwepa unaingia kwenye korogesheni. Kwa hiyo naomba hebu iangalieni hii barabara ni ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukienda kwenye kona zile za Nyang'oro maporomoko wakati wa mvua kila wakati Meneja wetu analala pale. Naomba tena Mkoa wa Iringa wapewe pesa ya kutosha ukarabati kwa sababu pia inakuwa ina makorogesheni lakini pia maporomoko ifanyiwe upembuzi yakinifu ili tuone tunasaidiaje ile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mgololo - Mafinga mkataba ulisainiwa toka mwaka 2022/2023 hii barabara majimbo yote matatu ya Mufindi yanapitiwa, lakini hii barabara ni ya kiuchumi. Malori yanakuwa yako pale muda mrefu nini lini sasa itajengwa? Tunawaombeni utakapojibu hebu utujibu hii barabara lini itaanza ujenzi kwa sababu ni barabara ambayo ni ya kiuchumi na Marais wote wametoa ahadi katika hii barabara. Pia barabara ya Nyororo - Mtwango tunashukuru imeanza kujengwa lakini tunaomba sasa muifikishe mpaka Igowole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza kwa upanuzi wa Barabara ya Kitonga. Mlima Kitonga tumeuliza sana maswali pale na barabara ile ilikuwa inakwamisha sana magari. Ninawaombeni jamani mmeanza kujenga njia ile moja mngefanya hata mbili ili msiendelee kurudia mara kwa mara kwa sababu ile barabara ni barabara inakwamisha mno magari na magari makubwa kuna ajali kila wakati. Tunawaombeni muongeza pesa ya kutosha ili angalau tuweke hata barabara nne katika ule Mlima Kitonga. Vilevile endeleeni kufanya upembuzi yakinifu kwa ile barabara mbadala ili tukipata matatizo. Lile eneo toka Mahenge – Udekwa - Wotalisoli, Mlafu inatokea Ilula itaweza kutusaidia hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ile ya Ipogolo - Kilolo. Hii barabara tunakupongeza Mheshimiwa Waziri ulikuja ukasaini na hii barabara pia inapitiwa na majimbo matatu lakini tunakuomba kama nilivyokuomba siku ile kile kipande ambacho hakijawekewa lami kingewekewa kwa sababu ndiyo kinakwamisha magari mengi, kile kinachotoka Kilolo pale kibaoni mpaka Kidabaga kiwekewe lami ili hii lami inaweza ikaungana na ya pale Ng'ang'ange kwenda mpaka kule Boma la Ng'ombe. Pia kuna hii barabara ikitokea pale Kidabaga iende Idete ndio kwenye shida sana watu wanapata shida wanakwama tunaomba sana Mheshimiwa Waziri ukija tena nenda kaitembelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, pia kuna barabara muhimu sana pale Kilolo, inatoka Kilolo kwenda Kising'a inakwenda Mkalanga, Wotalisoli, Mlafu mpaka Ilula, wananchi wanapata

shida kwenda mjini wakati hii barabara ikiwa inapitika japo msiweke lami lakini ipitike watu waende Makao Makuu ya Kilolo waende kwenye Ofisi za Kilolo wanapata shida kupita mjini, ninawaombeni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii *bypass* ya Barabara ya Tumaini. Ninakuomba magari makubwa kupita katikati ya mji ni mateso makubwa itatokea ajali kubwa lakini wafanyabiashara wanafanya biashara kwa shida mno magari yanafungwa wanalipishwa pesa lakini pia wafanyabiashara hawafanyi biashara zao vizuri kuna siku ajali itatokea pale Iringa Mjini jamani nawaombeni hii barabara ya *bypass* iishe sasa, iishe Mheshimiwa Waziri uje utuambie tunapata mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kiwanja cha Iringa. Hiki kiwanja kimeanza kujengwa siku nyingi sana, sasa ni lini kitaisha? Tunamshukuru Mheshimiwa Rais alikuja kwenye hiki kiwanja akazindua tukajua sasa kitakwisha lakini bado mpaka leo zaidi ya miaka mitano sita, saba bado lakini kinachoniuma mimi kuna Shule ile ya Nduli shule ya msingi watoto wanateseka miaka saba sasa hivi wanateseka Diwani wa pale ameugua mpaka afya ya akili kwa sababu haikarabatiwi. Ile shule inatakiwa ihamishwe watoto ufaulu wao umekuwa ni mbaya mno kwa sababu wanaishi kwenye mateso, vyoo havikarabatiwi, shule haikarabatiwi, walimu wanapata shida makelele mengi. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri hii shule iondoke iende ikajengwe kunakotakiwa kwa sababu tayari ilitakiwa ihamishwe toka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie Barabara ya Msembe inayokwenda *Ruaha National Park*. Hii barabara pia muda mrefu sana sana tumekuwa tukiomba ikarabatiwe hii itatuongezea uchumi sisi wananchi wa Mkoa wa Iringa lakini na Taifa zima tunakuomba ni muda mrefu sana sana lakini mwisho wakandarasi walipwe pesa zao ninakuomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niunge mkono hoja hii ya ujenzi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hamis Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini leo kidogo naomba nianze kwa Dua kumwombea sana Mheshimiwa Rais; "*Bismillah Rahman Rahim Rabbanna ahfilana wallii ikhwanina ladzina sabaquna bil iman, walatajiru fil ikurubina illa Al ladhina amanu rabbanna innaka raufur Rahim.*" Mwenyezi Mungu umjalie sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Kwa nini nimeanza na dua hii, ni kwamba kelele zilikuwa nyingi sana siku zinavyozidi kwenda kelele zinapungua katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi na mwaka jana barabara zilitengenezwa kwa kiwango cha hali ya juu tokea nchi hii imepata uhuru na tulikuja hapa sisi mwaka juzi kwa kuchukua mgawanyo kwamba *TANROADS* wapate pesa zao na *TARURA* wapate pesa zao. Kule *TARURA* walibakiza 30% zilizokuwepo za mwanzo halafu *TANROADS* wakawa wana pesa zao kule 70% kwenye pesa za Mfuko wa *Road Fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu kwa ilivyokuwa mafuriko yametokea ya kila namna, mara sijui kuna Hidaya, sijui kuna Farida. Kwa hiyo ikatokea hali ya sintofahamu katika nchi hii. Haijawahi kutokea mvua ya namna hii na mvua hii mimi nimepita katika maeneo kule nilikuwa nimetembelea maeneo ya Tabora sehemu za Tura kule, Maguliati sijui Loya watu wanasema kwamba tena hawana habari kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani nyinyi huku mnavyohangaika na barabara wale hawana habari wanasema tena wanazungumza kwa Kisukuma kwa huyu Mama alikuwa wapi mvua za namna hii tunapata mpunga wa ajabu mwaka huu. Sasa yaani wao wanaombea mvua izidi sisi huku tunatafuta

barabara Wabunge Bungeni yaani hawana habari na nyinyi. Kwa hiyo kuna watu yaani hii mvua wao wanaitaka wanataka huyu mama aendelee kuomba alikoenda kuomba mvua hii yaani ni maajabu makubwa sana, halafu humu ndani Wabunge tunahangaika sasa na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu nataka nianze kuchangia, *Bismillah*. Kwanza nataka nikutoe hofu Mheshimiwa Waziri Bashungwa ni kwamba kwa mimi hivi ambavyo Mwenyezi Mungu akijalia mwaka huu Mwezi wa Kumi na Mbili nakwenda kupokea daraja. Tukiwa hai tunakwenda kupokea Daraja la Kigongo – Busisi kilometa 3.3. Ndugu yangu shilingi bilioni 730, kwanza naangalia unaingia kwenye historia ya dhahabu Mjomba wangu Bashungwa wanapokea daraja hili na Mama anakabidhi daraja hili ambalo lina uwezo wa kukaa miaka 100 zaidi ya Marais kumi watakuja kuliangalia daraja hili, mpigieni makofi Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ambao hamjafika Sengerema nawaombeni mkaribie mje kuona huu muujiza uliotokea Sengerema kule. Kwanza najiuliza sana wakati Mheshimiwa Dkt. Magufuli anawaza habari hii ya kujenga daraja ndani ya ziwa mimi niliona kama hadithi, amefariki Mheshimiwa Dkt. Magufuli daraja lina 24%. Leo tunavyozungumza daraja lina 89% bado 11% tu daraja likamilike. Tunatengeneza muujiza mwingine ndani ya Tanzania. Ndugu zanguni kelele mpaka sasa hivi watu wananiuliza Mheshimiwa Tabasam mbona umekaa kimya kwani unafikiri haya yanayofanyika Sengerema hamuyaoni? Nitakuwa mtu gani mimi ambaye sina shukrani? Mtu gani ambaye sina shukrani? haiwezekani. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza ni kwamba daraja lile sasa hivi wanaanza kuunda barabara ya lami upande wa Misungwi kuja pale Sarajani na upande wa Sengerema kwenda Darajani. Tunachosubiri hapa Mheshimiwa Bashungwa kwenye *design* yako hii ambayo inaendelea pale tunakuomba daraja hili lilindwe kwa mizani. Hatuona mpango wa ujenzi wa mizani, magari yanayoingia darajani tusije tukaharibu daraja letu

sisi. Huu ni urithi tunapata sisi wana Sengerema ambao wakina Tabasam tutakuwa hatupo lakini tutakuwa kwenye historia kwamba Mheshimiwa Tabasam alikuwa Mbunge daraja limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachomshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako ya Wizara ni kwamba *design* ya lami lile daraja linakuja kupokelewa na lami yingine kutokea Busisi kwenda Ngoma kwenda Nyang'hwale tayari mkandarasi yuko kule anaendelea na usanifu na Wana-Sengerema jamani nawaombeni mmpe ushirikiano. Pia kuna lami ya kutokea Sengerema kwenda Ngoma kuna lami ya kutokea Kamanga inaendelea kilometa tatu na kilometa saba zingine Mheshimiwa Waziri umetupa tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema vivuko vyetu vyote vinavyoendelea kujengwa nilikuwa na Mheshimiwa Naibu Waziri tumekwenda na wewe kwenye kikao Mheshimiwa Waziri pamoja na Katibu Mkuu na timu yake Mkandarasi Songoro tayari jamani tunaombeni Serikali imekubali kumlipa pesa Waziri wa Fedha kanihakikishia kwamba analipwa pesa zake mwezi huu kabla haujaisha na bado siku mbili. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri tunakupitishia bajeti yako tumlipe Kandarasi Songoro vivuko vyetu viweze kufanya kazi. Nakushukuru kwa *design* ya vivuko hivi vivuko viko salama upande wa ndugu yangu Mheshimiwa Eric Shigongo tayari kivuko kiko salama kule hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Waziri tutakwenda kukabidhi kivuko hicho lakini kuna Kivuko cha Buyagu Mbalika sasa hivi kiko 60% na magati sasa hivi yameshaanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gati la Buyagu - Mbalika tayari mkandarasi ameshapatikana na ameshasaini mkataba. Kuna gati lingine la ndugu yangu Mheshimiwa Mabula pale Luchelele, kuna gati linatengenezwa Luchelele pamoja na Ilunda, kwa hiyo tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni barabara yetu sisi ya Sengerema - Nyehunge tuko kwako na Mheshimiwa Eric Shigongo

tumezungumza na Katibu Mkuu pamoja na Mtendaji wa *TANROADS* mnamchukua mkandarasi wa pili *CCIC* kwenda kutengeneza barabara tunawapongezeni sana, kwa sababu huyu bwana ndiye anayejenga daraja na vifaa vyake viko pale na kokoto anazo palepale. Kwa hiyo hii barabara itakwisha kwa muda wake, hatuna wasiwasi kabisa na jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza sana kwa barabara zetu zilizopanda hadhi Sengerema kwenda Chifufu kilometa 43 tayari mkandarasi ameshapatikana kuna shilingi milioni 500, Nyitundu kwenda Nyamatongo Karumo shilingi milioni 500 iko pale na mkandarasi yuko *site*. Barabara nyingine inayopita kwa mama yako mzazi kutoka Ikoni kuja Sima moja kwa moja kwenda mpaka Buyagu kwenye *ferry* na yenyewe tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo uko vizuri Mheshimiwa Waziri hawa wanaozungumza kwamba wanataka kukamata shilingi wanataka kwenda kukuonea tu lakini ninachotaka kukuambia atakayekamata shilingi Mungu anamwona. Ahsante sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge tupitishe bajeti hii bila mgomo wa aina yoyote, mtatutia simanzi sisi akina Mheshimiwa Tabasam ambao tunaona miradi inaendelea hali ni ngumu sana Mama yetu tumwombee kwa Mungu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata fursa ya kuchangia kwa niaba yetu na kwa niaba ya wananchi na nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Ujenzi kwa usikivu na ufuatiliaji wa ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo mawili hivi.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge tunataarifiwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi zake inatualika kwenye maonesho katika viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 30 Mei mpaka tarehe 03 Juni mwaka 2024. Lengo la maonesho hayo ni kuonesha majukumu yanayotekelezwa na Wizara hiyo kuhusu uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji wa utalii. Waheshimiwa Wabunge wote tunakaribishwa kutembelea maonesho hayo.

Pili waheshimiwa Wabunge mliokuwa mnafuatilia orodha ambazo zimetumwa *Caucus* zetu za vyama utaratibu umeboreshwa na uchangiaji unaanza na aliyechangia mara sifuri anafuata aliyechangia mara moja, anakuja aliyechangia mara mbili, mara tatu, mara nne, mara tano. Kwa hiyo mkiona *order* imevurugika kwenye vishikwambi vyetu tulivyopewa taarifa basi utaratibu ni huo kwa hiyo naomba tuuzingatie.

Kwa utaratibu huo basi watakaoanza kuchangia mchana nitawatamka wale watano wa mwanzo; tutaanza na Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuata Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, wengine watasomwa wakati ukifika.

Upande wa CHADEMA tuna mchangiaji mmoja ambaye atakuwa Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala naye amechangia mara nne, kwa hiyo baada ya kumaliza wale walichangia mara tatu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunasitisha Kikao cha Bunge mpaka saa 11.00 alasiri.

*(Saa 7.09 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. MONICA MWANGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja iliyopo mezani ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na mambo machache, jambo la kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya, ninampongeza Waziri wetu Mheshimiwa Innocent Bashungwa, nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Watendaji na Naibu Waziri pia kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwenye Wizara hii. Mzigo akiubeba mwenzako ni rahisi kuona ni mwepesi lakini kazi ambayo wanaifanya wenzetu wa Wizara ya Ujenzi ni kazi kubwa sana na sisi wananchi wa Makete tunaitambua.

Mheshimiwa Spika, toka jana nasikiliza michango mingi hapa ndani, Waheshimiwa Wabunge wanatambua *efforts* za Mheshimiwa Waziri kwenye ujenzi na kupambana na mambo ya barabara kwenye nchi yetu, kwa hiyo, mimi Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana, kwanza ni mtu ambaye ni msikivu na pili ni darasa kwa sisi vijana tunajifunza jinsi gani ambavyo inatakiwa tu-*behave* na jinsi gani ya kufanya kazi za watu. Kubwa zaidi ni jinsi ambavyo una-*attend* kwenye matukio kwa wakati, mimi niseme

wazi ulikuja Makete mdogo wako nilipokwambia kwamba Makete kuna changamoto ya barabara kutoka Makete kwenda Mbeya, ulifika *site* na wananchi wa Makete wamenituma, Mwenyekiti wangu wa Chama, Katibu *DC* na Mkurugenzi wamenituma kukushukuru sana kwa kufika Makete, kufika kwako Makete kumekuwa ni muarobaini kwa barabara ile angalau wananchi sasa wameona jitihada.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Makete tulikuwa tukisimama kwenye hili Bunge siku zote ni barabara kutoka Makete kuelekea Mbeya ilikuwa ndiyo kaulimbiu yetu. Pili, hata kwenye uchaguzi yeyote anayetafuta nafasi yoyote kwa Jimbo la Makete alikuwa anatumia barabara ya kutoka Makete kwenda Mbeya. Leo nasimama hapa siyo kwa sababu nyingine yoyote ni kuishukuru Serikali kwa sababu mkandarasi yuko *site* anaendelea na kufanya kazi. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yangu iliyopita wakati Mheshimiwa Mbarawa ni Waziri nilisema: "Hatutachanguliwa kwa uzuri wa suti au uzuri wa tai tunazozivaa lakini tutachaguliwa kama miradi ya maendeleo inaenda kwa wananchi".

Mheshimiwa Spika, leo hii wananchi wa Makete wanasema ahsante sana kwa sababu wanamuona mkandarasi yuko *site* anaendelea na kazi. Jambo moja pekee ambalo wananchi wa Makete wanaliomba ni mkandarasi alipwe fedha, amefika *site* lakini *speed* yake siyo kubwa sana kwa sababu kuna changamoto ya fedha, hajalipwa. Mnasema *advance payment,* mkandarasi wetu hajapewa fedha kwa sababu ya changamoto ambazo mnazipitia. Nakuomba Mheshimiwa Waziri chukueni hatua ya kumlipa mkandarasi huyu kwa sababu ulipokuja kule uliona kuna vifaa vingine pia ameshindwa ku-*mobilize* kutokana na uhaba wa fedha. Sasa nakuomba ili wananchi wa Makete tunapoelekea huko mbele tuwe na nguvu kubwa zaidi ya kuiunga mkono Serikali ni kuona mkandarasi huyu anaendelea, ni kilomita 36 ambazo amezianza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya kutoka Makete kwenda Mbeya ni barabara ya kiuchumi, ndiyo *oxygen* ya Wilaya yetu. Kama ni *oxygen* ya Wilaya yetu kuna *lot* mbili bado, imetangazwa

hiyo *lot* ya kwanza katika kilometa 96 za barabara yote, *lot* moja tu ya kilometa 36 imetangazwa bado *lot* mbili. Mheshimiwa Waziri tunakuomba kama kuna mchakato unatakiwa uanze ni kutangaza *lot* mbili, *lot* ya kwanza kutoka Makete kupita Bulongwa kwenda hadi pale Ipelele na nyingine ya kutoka Kikondo kufika Mbeya ni kilomita chache chache ambazo zimebaki, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri ulichukulie hatua barabara hii sisi ndiyo *oxygen*.

Mheshimiwa Spika, kutoka Makete kwenda Njombe ni mbali kuliko kutoka Makete kwenda Mbeya kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia, ni sehemu ya karibu zaidi na sisi tumeiuchagua ile kwa sababu pia shughuli kubwa za kibiashara na kiuchumi tunazifanyia pale. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, barabara hii ndiyo *oxygen* ya Wilaya yetu ya Makete.

Mheshimiwa Spika, niliporudi Makete wananchi wanasema kwa jinsi ambavyo barabara zimeharibika nchini matarajio yao ni kuona Wizara ya Fedha wanaiangalia Wizara ya Ujenzi kwa jicho la karibu sana. Mheshimiwa Waziri kwa fedha ulizotengewa kwenye bajeti hii nikuambie wazi tutaendelea kukulaumu. Tutakulaumu kwa sababu fedha hizi ni kidogo sana, haziwezi kukusaidia.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara ya Fedha waiangalie Wizara ya Ujenzi kwa jicho la karibu, miundombinu ya barabara, wananchi ukitaja *TARURA* ni nadra sana kukuelewa *kuhusu TARURA,* lakini ni nadra sana kukuelewa kuhusu *TANROADS* na barabara nyingine. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri na naliomba Bunge tuongeze fedha kwenye Wizara ya Ujenzi. Kama kuna *source* zozote tunaweza tukazichukua sehemu Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuomba kama kuna jinsi ya kum-*support* Innocent Bashungwa Waziri wa Ujenzi, kupata fedha za kutosha ili aweze kujenga barabara na kurekebisa barabara zilizoharibika ni vema tukamuongezea fedha kwenye bajeti yake. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuzungumza uchumi wa nchi kama hujazungumzia barabara, huwezi kuzungumzia afya za

watu kama hujazungumzia barabara, huwezi kuzungumzia kilimo cha nchi kama hujazungumzia barabara, huwezi kuzungumzia biashara za ndani na za nje kama hujazungumzia Barabara, barabara ndiyo uti wa mgongo wa Taifa lolote lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tumepitia katika kadhia ya barabara kuharibika sana, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunajua unafanya kazi nzuri sana lakini Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Bashugwa aongezewe fedha ili Wizara hii iweze kuleta tija na kufanya marekebisho. Tutakuwa tumejenga vituo vya afya vingi sana lakini wagonjwa hawatafika kwenye vituo vya afya kutokana na changamoto za Barabara, tunaweza tukawa na changamoto za vifaa kupanda bei kutokaana na barabara kuwa mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu ya kuendelea kuwashawishi pia Wabunge wenzangu tuweke *joint* kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ili aweze kupata fedha za kuongezewa ili barabara ziweze kujengwa kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sina mambo mengi lakini sisi kama wananchi wa Makete tunapongeza sana tunae Mkurugenzi wa *TANROADS* mzuri sana Mkoa wa Njombe, Mama yetu Shallua, anafanya kazi nzuri sana, anatuunga mkono Wabunge na anatushirikisha kwenye changamoto zote na anafika kwa wakati, kwa kweli nisipompa maua yake nitakuwa sijamtendea haki. Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe anatu-*support* sana na pale ambapo kuna changamoto anatusaidia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa mezani kwako kuna barabara ya kutoka Lupila kuelekea Kipengele. Mheshimiwa Waziri ulipokuwa TAMISEMI ulifika Makete ile barabara tuliileta mezani kwako uipandishe kwenda *TANROADS,* wana-Lupila na wananchi wa Makete wanakuomba barabara ile ipelekwe *TANROADS* angalau iwe kwa kiwango cha changarawe Mheshimiwa Waziri ili iweze kupitika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kengele ya pili imeshagongwa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa John Danielson Pallangyo ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa Jumapili nilikuwa na mkutano wa hadhara kwenye Kata Weruweru na wananchi wa Kata ya Weruweru wakanambia Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa alizofanya Mheshimiwa Rais, kila ukisimama hata kama ni kuuliza swali anza kwanza kumshukuru Rais. Kwa hiyo, nami natumia *formula* hiyo kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa miradi mingi aliyofanya ndani ya nchi yetu lakini kwa Jimbo la Hai ni miradi kedekede aliyotuletea ambayo kihistoria haijawahi kutokea, tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri najua una 'zigo zito hili hapa' na ni lazima liende kwa sababu ni la kwako. Kwa hiyo, ninakupongeza kwa kazi unazozifanya wewe na Naibu Waziri, Katibu Mkuu pia na Meneja wangu Ndugu Kyando wa Mkoa wa Kilimanjaro. Huyu Mama anafanya kazi nzuri sana, kama ni kumpandisha cheo mpandishe cheo na mshahara uongezeke lakini abaki palepale Kilimanjaro, anatusikiliza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri alitusaidia fedha tukajenga daraja lile la Msomali, lilikuwa linasumbua sana. Niseme kwamba naomba sana mfanye utafiti chanzo cha yale maji yanatokea wapi kwa sababu hata haya mafuriko yaliyokuja juzi yalivuka tena daraja. Kwa hiyo, maana yake kazi inapaswa kufanyika pale. Nakushukuru kwa fedha

ulizotuletea, tunajenga daraja la Makoa na kazi inaendelea vizuri haijasimama na haijayumba. Ninakushukuru pia kwa ajili ya fedha ambazo umeshatuletea na mkandarasi amepatikana kwa ajili ya ujenzi wa daraja lile la Kikafu kwa maana ya barabara ya Kalari kwenda Uswaa.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba lile daraja la zamani lisivunjwe kwanza, yaani lisivunjwe kwa sababu hakuna *diversion road* isije ikawa kama vile la Makoa, lijengwe pembeni na hili liendelee kuwepo. Nakuomba maombi machache kabisa kwenye eneo langu, nakuomba ile barabara ya kwa Sadala – Kwale, kilomita 15 tu na nimeambiwa imeshawekwa *feasibility study,* iwekwe *feasibility study* na hii barabara ipatikane, kwa sababu ndiyo barabara inayokuletea chakula kule nyumbani kwako. Hii ndiyo inaleta chakula pale kwenye Soko la kwa Sadala. Ni sambamba na ile ya kwa Sadala kwenda Longoi, hii na yenyewe ni kilomita 17 tu lakini imepangiwa bajeti kwenye Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninakuomba pia hii barabara ya Machame kwenda Kyalia tusaidie taa, kuna taa mlifungua pale *KIA,* mngetupa zikawekwa kwenye hii barabara ili ifanane na barabara nyingine. Pamoja na pale Bomang'ombe, tumepata barabara zile *TANROADS* zote zina taa lakini barabara kuu haina taa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nakuomba sana, tuna barabara ya Bomang'ombe – Chekimaji – *TPC, TARURA* wametuwekea kilomita tatu lakini hii ya barabara najua ni ya *TARURA,* ninyi *TANROADS* ni walaji wakubwa kwa sababu hii barabara ina hadhi ya Kimkoa, hii barabara lile daraja likiharibika ndilo inayotumika. Naomba angalieni namna ya kukaa na *TANROADS* muwaongezee nguvu ili hii barabara ijengwe kwa kiwango cha lami na ikamilike.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine hili Mheshimiwa Waziri unisikilize vizuri. Tuna madeni ya fidia tunawadai, barabara ya mashine *tools* kwenda Kyalia tangu mwaka 2007 wananchi

walianza kuwekewa *X* kwa awamu mbalimbali, hawajalipwa na hawajaambiwa barabara endeleeni na matumizi. Tunaomba sentensi moja, pamoja na kesi zilizopita barabara tuendelee kutumia au mtatulipa fidia? Unapohitimisha nakuomba sana utoe sentensi kwenye barabara hii kwa sababu watu wamebaki hawaelewi kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, iko fidia nyingine ya daraja la Kikafu, mlifanya tathmini wananchi wanaendelea kukaa pale hawajui watalipwa lini. Nakuomba unapokuja kuhitimisha utuambie lini unalipa fidia kwani wananchi walishaacha kujenga, wameacha kuendeleza mashamba yao na wako *stranded* kwa sababu hawajapewa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tulipitisha kwenye *RCC* kikao cha mwisho ambacho kinakuja kwako kupandisha hadhi barabara. Zikiwa ni barabara zile za vijiji kwenda *TARURA* na zile nyingine zilizokuwa *TARURA* kwenda *TANROADS,* naomba utakapokuja kuhitimisha utupe majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nikushauri kuwa mfuko wa barabara umeweza kukarabati barabara kwa asilimia 40.8 tu, lakini nilikuwa natazama mkakati uliouweka pale kwamba ni nini kifanyike ili kufanya mfuko huu uwe na nguvu. Mmesema mnaenda kubadilisha sheria, mimi sioni kama mkakati huu utatufikisha mahali, lakini nimejiuliza kwa nini tunatengeneza sana barabara? Matengenezo ya barabara yaliyofanyika ni kilomita 34,383.67 na zile barabara maalum, matengenezo maalum, mmefanya zaidi ya kilomita 3,600. Kwa nini tunafanya matengenezo mengi? Jibu ni rahisi, barabara zinajengwa *below standard* ndiyo maana kuna matengenezo mengi.

Mheshimiwa Spika, inawezekana Mheshimiwa Waziri kuna mahali unapigiwa kona hapa, kwamba hizi barabara ni miradi ya watu wanaipenda, kwa sababu pesa za matengenezo ni nyingi sana hizi. Nimesoma hotuba yako ukurasa wa 129, mngeweka mkakati ni kudhibiti, barabara zitengenezwe kwa kiwango kinachotakiwa ili zidumu muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naona aibu sana nikikuta watu wa *TANROADS* wameweka vitoroli barabarani wanaziba shimo la barabara, hii ni aibu! Kwa nini tusitengeneze barabara zetu kwa ubora ili tupunguze gharama hii? Naomba kwenye hotuba yako ukaongeze neno linguine la kuhakikisha barabara zinajengwa kwa kiwango kinachostahili ili kupunguza gharama hizi za matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimeona kuna tatizo, nauliza *TBA* kwa nini tunawapa ruzuku ya Serikali wakati wanafanya kazi kama wakandarasi wengine? Basi kama *TBA* mnawapa ruzuku naomba na wakandarasi hawa watanzania ambao mnataka kuwainua, kwanza, mnawacheleweshea malipo yao, wajengeeni uwezo, wapeni ruzuku kwa kuwapa vifaa kwa bei nafuu ili wawe na uwezo wa kufanya hizi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wafanyabiashara wanaoitwa wakandarasi unaosema unaenda kuwainua na umewatengea pesa nyingi, wengi sasa hivi wana magonjwa, wengi wamekuwa *frustrated,* kwa nini? wanawadai hela nyingi, mimi nina mmoja nilikuwa naongea na KM wako hapa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili imeshagongwa, ahsante sana.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa John Danielson Pallangyo Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii na nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya, pamoja na changamoto mbalimbali lakini kwa muda huu mfupi aliokaa madarakani kazi kubwa sana imefanyika kuimarisha miundombinu yetu. Nisiwe mchoyo wa fadhila kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu nzima, kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana pamoja na changamoto kubwa wanazozipitia lakini wanafanya kazi kubwa sana, mnastahili pongezi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza meneja wangu wa *TANROADS* Mkoa Mhandisi Ambrose, ni moja kati ya watendaji wahandisi wanaoifanya kazi kubwa sana. Amekuwa anatupa ushirikiano, mimi binafsi amekuwa ananipa ushirikiano mkubwa sana, kwa kweli anastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda huu mfupi nita-*concentrate* kwenye Jimbo langu la Ukerewe. Moja ni kutoa shukrani. Tunayo barabara yetu ambayo ni sehemu ya barabara ya Bunda - Kisorya – Nansio, kwa muda mrefu sana ilikuwa ni tatizo kubwa lakini kwa namna ya pekee ndiyo maana nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, fupa ambalo limewashinda viongopzi wengi yeye safari hii ameliweza na hatimaye sasa barabara ile kilomita 12 inaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Nampongeza sana lakini nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili naomba tu kushauri Mheshimiwa Waziri, wakati mkandarasi kafika *site,* basi alipwe pesa yake ya awali ili asikwame katika eneo lolote lile. Nashauri vilevile ubora wa kazi ile uwe ni wa kiwango cha juu, ina maana kuwe na usimamizi mkubwa, ingawa sina mashaka sana na Meneja wangu wa *TANROADS* Mkoa kama nilivyosema, kwa hiyo nasisitiza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa hatua iliyofikiwa sasa ya kuanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kisorya – Rugezi, ni hatua nzuri sana. Daraja lile ni muhimu sana kwa wananchi wa Ukerewe na hata Bunda kwa sababu ni kiunganishi kikubwa na ndiyo misingi wa uchumi wa maisha ya watu wa Ukerewe. Kuwepo kwa daraja lile kutaimarisha sana mawasiliano na uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Kwa hiyo, nashukuru na napongeza na ingependeza sana kama vifaa vilivyoko Kigongo Busisi baada ya mradi ule kukamilika vikahamia pale ili kupiga ile kazi, ikafanyika mara moja na maisha yakaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni juu ya vivuko. Ukerewe ndiyo wateja wakubwa wa Wizara hii kwenye eno la *TEMESA* kwa upande wa vivuko. Nashukuru Kivuko cha Bukondo – Bwiru kinaendelea vizuri lakini pia Kivuko cha Kisorya - Rugezi. Naomba tu yale madai anayodai mkandarasi wetu Songoro *Marine* alipwe ili akamilishe kazi ile vivuko vile viende kutoa huduma kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ilani yetu ya uchaguzi Ibara ya 57 (j) ambayo inaongelea vivuko; kwenye Ilani ya 2020/2025 tuliahidi wananchi kuanza kutengeneza vivuko nane. Katika vile vivuko nane tulivyoahidi, mojawapo ni kivuko cha Irugwa kwenda Murutanga na Kakukuru kwenda Ghana. Bado vivuko hivi havijaanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kisiwa cha Irugwa wanaishi maisha magumu sana. Wanapotaka kusafiri kuja Ukerewe inabidi wapite Jimbo la Musoma Vijijini, wapite Jimbo la Musoma, wapite Bunda, wapite Mwibara ndiyo warudi kuja kupata huduma Ukerewe. Kwa hiyo, ni muhimu sana kivuko hiki kikatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, wananchi wa visiwa vya Ghana, Kamasi na vinginevyo, visiwa vyote karibu saba, kutoka Kakukuru wanapata wakati mgumu sana kusafiri kwenye eneo lile. Ndiyo maana vivuko hivi ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu na kama ilivyoelekeza Ilani, Mheshimiwa Waziri, mimi ningeomba kushauri. Kwa sababu kivuko cha *Mv Ukara* namba moja tayari kimeenda matengenezo na kwa mujibu wa hotuba yako, kimefikia asilimia 10. Vilevile, Kivuko cha *Mv Nyerere* nacho kiko matengenezo kinakaribia kukamilika. Mheshimiwa Waziri, ushauri wangu, vivuko hivi vikikamilika virudishwe Ukerewe ili kimoja kiweze kufanya kazi kati ya Irugwa kuja Murutanga na kingine kifanye kazi kati ya Kakukuru kwenda Ghana. Tutaokoa sana maisha ya watu wetu na vilevile kuimarisha uchumi wa wananchi wa Ukerewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kufanya hivyo mazingira yetu yatakuwa magumu sana. Ninaamini, Mheshimiwa Waziri sina mashaka na wewe kwa sababu kama nilivyosema, vivuko hivi vilikuwa vinafanya kazi Ukerewe, vimeenda matengenezo. Nishauri sana na niombe vikikamilika kutengenezwa virudi Ukerewe. Kimoja kifanye kazi kati ya Murutanga kwenda Irugwa na kingine kutoka Kakukuru kwenda Ghana kama nilivyoshauri. Litakuwa limefanyika jambo kubwa na la maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu, Mheshimiwa Waziri, tulizungumza juu ya barabara ya kutoka Bulamba kwenda Murutunguru – Bukonyo – Masonga kilometa 28. Ni barabara muhimu sana, ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa wananchi wa Ukerewe. Pamoja na kwamba wanapitia changamoto kubwa sana za kifedha lakini niombe tafadhali, hata kama ni kwa awamu, kwa sababu tunatumia pesa nyingi sana kutengeneza barabara ile kila wakati na ikitengenezwa muda mfupi baadaye inaharibika tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu, kama itawezekana tutafute rasilimali fedha ili tuwe tunaitengeneza hata kwa awamu ili mwisho wa siku barabara ile iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami na kuepusha gharama kubwa ambazo tunazitumia kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu awabariki sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa hii nafasi nichangie kwenye hii hotuba ya Wizara ya Ujenzi; Wizara ambayo ina kazi nzito ya kubadilisha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitangulie pia kumshukuru Mungu kwa kunisimamisha hapa leo lakini nimshukuru na kumpongeza sana Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameendelea kuongoza nchi hii kwa umahiri mkubwa ili atufikishe *next level*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kipekee nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya, Katibu Mkuu Balozi *Engineer* Aisha Amour pamoja na watumishi wote wanaofanya kazi Wizara hii pamoja na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia *TANROADS* pamoja na barabara zingine, inasimamia barabara zenye urefu wa kilometa 24,889 za mikoa. Katika hizo, kilometa 26 ni barabara ya Mbuguni kutokea Tengeru kwenda Mererani. Barabara hii nimekuwa naipigia kelele kwa muda mrefu sasa takriban miaka miwili na Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya amekuwa ananiahidi itajengwa, itajengwa, nikimuuliza vipi? Ananiambia inafanyiwa usanifu, upembuzi yakinifu, kila leo, usanifu, upembuzi yakinifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimepitia majedwali haya sijaona chochote kinachogusa

Arumeru Mashariki. Nikitoka hapa nina *pressure* sijalala usingizi, nawaza nakuja kuondoa shilingi kwenye bajeti yako na wewe ni kijana wangu. Ni mtu mzuri, mwema, mpole, *Innocent* kama jina lako linavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuja kupata ahueni kidogo leo nilivyokuta kwamba bado inafanyiwa upembuzi yakinifu. Sasa niombe, kwa sababu kuna wenzetu walisema kwamba kipindi kile cha Serikali kutafakari mjadala wa bajeti zote za Wizara, tuangalie namna gani tunaweza tukawaongezea hela. Kwa hiyo, hili lichukue, barabara ya Mbuguni, kuanzia Tengeru hadi Mererani, ni barabara muhimu sana maana inakwenda kwenye machimbo ya Tanzanite. Ni fedha nyingi zinatoka pale kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii lakini zaidi inaunganisha mikoa miwili, Manyara na Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana isikosekane kwenye bajeti ya mwaka huu. Mheshimiwa Waziri ukumbuke kwamba siasa sasa hivi za majimboni ni barabara. Kila ukizunguka ni barabara, kila ukipita hapa barabara. Kwa hiyo, tafadhali nakuomba sana hiyo barabara isikosekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi tena, kuna ahadi za viongozi wakuu kule jimboni kwangu ambazo hazijatekelezwa. Kuna barabara inatokea Usa River kwenda Oldonyosambu kwa kupitia *Arusha National Park*. Imejengwa mpaka pale kwenye lango la kuingia *ANAPA*, inapaswa iendelee Ngarenanyuki iende mpaka Oldonyosambu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. Magufuli, ya kutokea Malula mpaka Ngarenanyuki inaungana na hiyo barabara. Naomba uichukue hiyo barabara ya King'Ori kutoka Malula kwenda Ngarenanyuki mpaka Oldonyosambu ili nayo ijengwe kwa kiwango cha lami maana ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ni ahadi ya viongozi wakuu wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna ahadi ya kilometa tano pale Usa River ilitolewa mwaka 2015, zijengwe kwa kiwango cha lami. Nimesubiri niambiwe sasa mnaanza, sijasikia. Nakuomba nalo ulichukue, kilometa tano Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli alisema pale Usa River kwamba atatoa kilometa tano za lami kwa ajili ya mji wa Usa River, naomba nazo uzichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza imelia eeh?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, bado.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, bado. Nadhani ni hayo niliyokuwa nataka niyaseme kwa ajili ya jimbo langu. Barabara ya Mbuguni, barabara ya King'Ori – Malula – Oldonyosambu na kilometa tano za mji wa Usa River. Pia, kuna kilometa tano za barabara ya Kikatiti kwenda Sakila alitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameingia sasa hivi, mwaka jana tukiwa kwenye …nayo ichukue pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa mbona unamsemelea? Mheshimiwa Mbunge ngoja kwanza, ameingia sasa hivi akitokea wapi? *(Makofi, Kicheko)*

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, yuko hapa ndiyo kaingia.

**SPIKA:** Hapana yupo Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo Bungeni.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru sana. Basi na hilo ulichukue Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kuendelea kuwemo katika Bunge hili kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia nichukue nafasi hii kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa hasa kwenye Kata ya Murongo, Bugomora na Kibare kwa adha ambayo wameipata kutokana na wadhibiti wa magendo ya kahawa. Tayari nimeshawasiliana na Mkuu wa Wilaya na tumeshakubaliana wadhibiti wa magendo waende kwenye mipaka waondoe hii adha ambayo wanaipata wananchi. Ninampongeza sana Mkuu wa Wilaya ameshachukua hatua mbalimbali kwa hiyo ninaamini tabia ya kuwavamia wananchi kwenye nyumba zao haitaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia. Kwanza; nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya maeneo mbalimbali. Kwa kweli kwa upande wa ujenzi amefanya mageuzi makubwa, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze sana pacha wangu Mheshimiwa Bashungwa pamoja na timu yake, mnafanya kazi kubwa nzuri sana. Kwa kweli, tumemuona maeneo mbalimbali, kwenye madaraja, mafuriko, mpaka watu wengine wakawa wanasema siku hizi Mheshimiwa Bashungwa amekuwa mkandarasi na ni *Engineer* kabisa. Tunampongeza sana anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara zangu ambazo ni barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo. Barabara hii ni barabara ambayo inaunganisha Wilaya ya Karagwe ambako

unatoka Mheshimiwa Bashungwa lakini pia Wilaya ya Kyerwa. Ni barabara ambayo ni ahadi ya miaka mingi tangu kipindi cha Hayati Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa na mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Amesharuhusu barabara hii ya Murushaka – Murongo kilometa 50, ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Mkandarasi ameshaonyeshwa barabara, kilichobaki ni kupewa *advance* ili barabara hii ianze. Sasa nikuombe sana Mheshimiwa Bashungwa, barabara hii ni muhimu sana, mlipeni mkandarasi ili aanze barabara hii ili tuondoe yale maneno ya watu ambao hawatutakii mema wanaosema yule mkandarasi aliyepelekwa alikuwa ni Mchina aliyetoka *syndicate* kwa hiyo tulikuwa tunawazuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee tena barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo, hii ni barabara ambayo inaunganisha wilaya zetu za Karagwe na Kyerwa na ni barabara ambayo ni muhimu sana. Ninaomba sana Mheshimiwa Bashungwa, baada ya tatizo lililojitokeza baada ya kupata mkandarasi wa kwanza, sasa muitangaze upya. Niombe sana barabara hii iweze kujengwa, iweze kutangazwa na mkandarasi apatikane ili akabidhiwe barabara hii, kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ninazisemea kwa muda mrefu kwa sababu ya umuhimu wake. Wilaya za Kyerwa na Karagwe ndizo wilaya ambazo zinalima kahawa nyingi sana. Pamoja na wilaya nyingine, hizi ni wilaya ambazo tuna uzalishaji mkubwa wa kahawa na tunaliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Kwa hiyo, ninaamini tutakapokuwa tumetengeneza barabara hizi, tunaenda kuinua uchumi wa wana-Karagwe na pia uchumi wa wana-Kyerwa na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana barabara hizi tuziangalie ili ziweze kutengenezwa. Jambo lingine ambalo nilisemee; Mheshimiwa Bashungwa nikupongeze sana, umeanza kuinua na umekuwa uki-*promote* sana wakandarasi wazawa. Hili

jambo ni zuri sana lakini niombe sana pamoja na kuwainua hawa wakandarasi niombe Mheshimiwa Bashungwa, mjali na malipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wakandarasi wamekuwa wanakopa hela benki lakini wanapopewa kazi wanacheleweshewa malipo na mwisho wa siku wanaishia kufilisika. Kwa hiyo, niombe sana, pamoja na kuwa-*promote* tuhakikishe hawa wakandarasi wanalipwa kwa wakati ili tuwainue kifedha waweze kuendelea kufanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi leo niliona niongelee barabara zangu pamoja na hilo la wakandarasi. Mheshimiwa Bashungwa tunaendelea kukuombea, unafanya kazi nzuri sana na Mungu akufanikishe, akulinde na yale maono yote uliyonayo yaweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza miradi ya kimkakati ya kitaifa kwenye Wizara hii. Kipekee, kwa kazi inayoendelea na hakuna kilichosimama kwa barabara ya Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi, kilometa 160. Mkandarasi yuko kazini na ujenzi unaanza, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi tutamlipa kwa imani tuliyonayo kwake na kura zitatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuanza kumpongeza, tofauti na tulivyo wengi, nimpongeze sana Balozi Dkt. Aisha Amour, Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri na yeye ni mwana-Mtwara anajua changamoto za huko. Nimpongeze pia

Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri. Naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi pia kwa zile kilometa 35 za Mangamba – Madimba – Msimbati, taratibu za kupata mkandarasi zinaendelea, tunaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa zile kilometa 200.51 za Mtwara – Mingoyo – Masasi. Tunaambiwa taratibu za manunuzi zinaendelea na hii ilikuwa bajeti ya 2023/2024. Tuna uhakika kabisa hata kama zimebaki siku chache lakini taratibu zinaendelea, tuna imani kwamba hii barabara itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nishauri; kwa sasa hii barabara ndiyo inapita malori yote yanayotoka Liganga na Mchuchuma kwa hiyo mzigo ni mkubwa. Tunaomba itakapojengwa ijengwe kwa kiwango cha juu ili isije ikawa kama ile barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mtwara ambayo imekwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa sasa hatuna mategemeo ya kupata treni ile ya Kusini kwa sababu bajeti imepita na haipo, kwa hiyo tunategemea hii barabara kwa mambo yote. Kwa hiyo, tunaomba sana hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo naomba kushauri kwenye maeneo mawili, la kwanza; barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Mtwara tunajua haikujengwa kwa kiwango cha juu na ndiyo maana imepondeka pondeka. Kila baada ya mita 100 kuna kiraka na hii barabara kwa sasa hali yake ni mbaya. Tunajua awamu iliyopita Hayati Mheshimiwa Magufuli aliagiza itengenezwe lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi haijatengenezwa. Tunaomba sana, Kimbunga Hidaya kimekwenda tu kuongezea madhara lakini tunafahamu barabara hii iko hoi. Sisi kule hatuna meli kwa hiyo tunategemea barabara hii peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa inafanya gharama za maisha kwa wananchi wa Lindi, Mtwara na maeneo hayo hata Pwani

yawe magumu kwa sababu hata mizigo ya mabegi inatozwa kwenye mabasi, sembuse mizigo ile inayokwenda madukani. Kwa hiyo, tunaomba hii barabara ijengwe kwa kiwango cha lami maana sidhani kama itakuwa ni ukarabati kwa sababu imeharibika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili; ni huyu anayeitwa *EPC+F*. Hapa ndani tumeuliza maswali ya msingi na maswali ya nyongeza zaidi ya 15, tukipata majibu kwamba ujenzi unakwenda kuanza lakini cha kusikitisha ni kwamba kwenye bajeti hii hakuna japo tuliambiwa ujenzi utaanza na utiaji saini ulifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri, sasa tunapojenga barabara mimi nilikuwa nadhani kuna mambo matatu ya kuzingatia. Jambo la kwanza ni sababu za kiuchumi, pili ni sababu za kiusalama na tatu ni za sababu za kijamii. Kwa hiyo, Wizara iweke vipaumbele na izingatie. Kwa nini tumeingiza mikoa 13 kwenye *EPC+F*, tumeingiza majimbo 32 kwenye *EPC+F*, Wabunge wameenda kujinadi kule hizi barabara zitajengwa na imeshindikana?

Mheshimiwa Spika, sasa kama imeshindikana tutafute utaratibu mwingine. Jambo la kwanza ni kuboresha mfuko wa barabara kwa kutafuta vyanzo vingine ili ikafanye hiyo kazi kwa sababu sasa hivi uwezo wake ni shilingi bilioni 600 lakini mahitaji ni shilingi trilioni mbili; haiwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bajeti ya mwaka huu shilingi trilioni 1.7 tunaona shilingi bilioni 900 inakwenda kulipa madeni, shilingi bilioni 700 *plus* inayobaki haiwezi kukamilisha zile shilingi trilioni 2 zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili; huu utaratibu umeshindikana, hii *module* imeshindikana basi tutafute labda *PPP,* pengine inawezesha. Hatusemi wananchi watachangia lakini Serikali ichangie, itafute mwekezaji halafu Serikali itaona kama ni huduma basi Serikali itakuwa imebeba mzigo na wananchi watakuwa wamepata hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kule kwetu, Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale, hizo 175, hali ni mbaya, hali ni mbaya, hali ni mbaya. Kwa hizi mvua za *El Nino*, madaraja yaliondolewa, Daraja la Mto Lukuledi liliondolewa, lakini kule Liwale Mheshimiwa Bashungwa amekwenda na amejionea, hivyo kweli anaweza akasema hali ni nzuri ama hali ni ya kuridhisha? Kwa hiyo, ni muhimu kufanya jambo, hata akatupa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule zamani kulikuwa na utaratibu, maeneo ambayo yalikuwa hayapitiki kabisa tumekuta kuna zege, watu wamejenga, lakini kama si zege akajenga madaraja, tukaanza kidogo kidogo. Ninavyoona kwa sasa *EPC+F* kwa utaratibu wa bajeti uliokuwa nayo hautaweza na wala hauwezekani, hiki ni kizungumkuti. Serikali itafute utaratibu mwingine wa *PPP* wa kujenga barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni kuhusu ulipaji wa fidia. Naomba maeneo yote hayo yalipwe fidia ili wananchi wawe na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi, lakini pia naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu. Ninaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na wasaidizi wake wote akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi na wasaidizi wake wote, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba kwenda moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, brabara ni uchumi. Mazao yote, bidhaa zote na mambo yote mengi ambayo yanakuza uchumi wa nchi hii yanategemea sana uwepo wa barabara, barabara ambazo ni nzuri na zilizoimarika. Ametoka kuongea hapa Mheshimiwa Hokororo, kwa kiasi kikubwa ameni-*pre-empty*.

Mheshimiwa Spika, ukianza na Barabara ya Kibiti – Lindi, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, walijitoa sana, kwa sababu mawasiliano yalikatika ya kwenda Lindi na Mtwara. Tumemuona Mheshimiwa Bashungwa alikuwa anashinda kule, anakula kule, anatembea na wananchi wa kule. Hayo wakati yanatokea, najua ni madhara ambayo yametokea kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi kwa sababu ya uwepo wa kimbunga kile, hatuna jinsi, lakini yalipandisha kwa kiasi kikubwa sana maisha ya wananchi wetu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoka Dar es Salaam kwenda Newala bei ya kawaida ya basi ni shilingi 35,000, lakini watu walikuwa wanalazimika kuzunguka Newala – Songea – Dar es Salaam kwa nauli ya shilingi 120,000 kwenda tu. Kwa hiyo, utaona namna ambavyo mzigo ulikuwa mkubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa jitihada za Serikali, kwa dharura ambayo wameifanya sasa hivi barabara ile inapitika, lakini tuendelee kuomba Mungu kwa sababu kilichofanyika pale ni matengenezo ya dharura. Ikitokea leo kikaja kimbunga chenye jina lingine ile barabara inaondoka tena na mawasiliano yanakatika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimeangalia kwenye bajeti, taarifa ya Mheshimiwa Waziri inasema kuwa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu za kuanzia Kongowe – Malendego – Nakungurukuru – Mbwenkuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba hii iwe ni hatua ya dharura, kwa hiyo, lazima kuwe na *short term plan* na *long term plan*. *Short term plan* iwe ni hii ya kutafuta fedha kwa ajili ya

ukarabati, lakini ile barabara haikarabatiki, ile barabara inatakiwa kujengwa upya kwa sababu sehemu zote zimeoza. Waliotangulia kusema wamesema, ina viraka kila sehemu. Kwa hiyo, ilikuwa ni kufanya tu ukarabati, lakini sasa tuijenge iwe imara. Tutakapokwenda kujenga tuwatafute wakandarasi ambao wana uwezo ili waijenge barabara ile kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kipande ambacho kimeharibika mno ni kutoka Somanga – Nangurukuru – Lindi, ndiko ambako madaraja yalitoka. Ile barabara ilijengwa kwa wakati mmoja kutoka huku Kongowe – Lindi. Kwa hiyo, ukiangalia kuna sehemu ambazo ziliimarika na sehemu nyingine ambazo hazikuimarika. Ninaomba tutafute wakandarasi wenye uwezo, watakaoijenga barabara kwa uimara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda sasa Barabara ya Mtama – Mkwiti – Newala, kilometa 74. Kwa mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 ilitengewa bajeti ya shilingi 145,000,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Nimesikitika kidogo kuona kwamba barabara hii mpaka leo kwenye taarifa ya leo ya Mheshimiwa Waziri inasema kuwa wapo kwenye hatua ya taratibu za manunuzi na kumpata mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumebakiza siku tu kadhaa ili mwezi uishe, lakini ndiyo kwanza taratibu zinafanyika, yaani nimechoka kidogo. Ninaiomba Serikali, wananchi wa Newala wanategemea barabara hii ambayo ndiyo wanapita kwenda Mtama na Dar es Salaam kila siku kwa ajili ya kuchukua bidhaa mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maisha yao. Tulishawapa matumaini kuwa barabara inakwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu ili iende kwa *stage* nyingine ya ujenzi kwa ajili ya lami, lakini leo ndipo taratibu zinaanza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni taratibu inawezekana hata bajeti hii ikaisha ilhali taratibu hazijakamilika. Ninaiomba Serikali, ninaiomba sana, wananchi wa Kusini wamekaa muda mrefu na barabara mbovu. Leo tumeshaweka kwenye vitabu,

basi tunaomba fedha zipatikane ili wananchi wale wanasuke na shida za kila siku za ubovu wa barabara ambazo wanakabiliana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kutoka Mtama kwenda Newala sasa hivi wanaopeleka mabasi kule hawapeleki mabasi mazuri. Ukiwa unafika Newala ukitokea Mtama leo hii ni lazima ukaoge ili kuondoa vumbi ndipo uendelee na mambo mengine. Tumekwishatoka huko, sasa hivi tuko karne ya 21. Ninaomba Serikali itufanyie hima ili tuondokane na hii kadhia ya kwenda kuoga halafu ndipo uendelee na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitoka maeneo mengine sasa hivi, mtu anaondoka, anafika anaendelea na shughuli zake, Newala hicho kitu hakipo. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali, tumechelewa na tunakubali kwamba tumechelewa, lakini sasa muda umefika, tukomboeni na sisi ili tunapofika mjini, wasitushangae, maana unatoka pale, unafika mjini umekuwa mweupe wa vumbi kama unaenda kucheza ngoma, hapana. Naona huo muda umeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nasisitiza Barabara ya Mnivata – Newala – Masasi…

*(Hapa kengele ililia muashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, kengele imekwisha…

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, ahsante sana nna naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi

Mungu kwa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, pili namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya hususani katika Wilaya na Jimbo la Kilolo. Mheshimiwa Waziri atakumbuka kuwa alikuja mwaka jana, akasaini mkataba wa ujenzi wa barabara kilometa 33 kutoka Ipogolo - Iringa Mjini – Kilolo. Furaha yetu Wana-Kilolo ni kwamba barabara ile sasa inajengwa tena inajengwa kwa kasi kubwa sana. Hii ni historia kwa Wana-Kilolo, na ndiyo maana Wana-Kilolo wanaona juhudi za Mheshimiwa Rais na pia wanaona juhudi za Wizara, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumushi wote, pia juhudi za watumishi wa *TANROADS* Mkoa wa Iringa, tunashukuru sana barabara inajengwa na inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa amekuja Kilolo, nilimwomba na ninajua kwamba barabara kilometa 33 inaishia Kilolo, lakini barabara ile ni ya kutoka Ipogolo – Iringa Mjini – Idete. Nikamwomba kwamba kwenye hii barabara yapo maeneo korofi ambayo jumla yake ni kilometa sita. Kilometa sita ni zile ambazo kila msimu wa mvua unapoanza hayo maeneo ni lazima tupate *disaster,* yaani hayawezi kupitika.

Mheshimiwa Spika, mimi najua kwamba bajeti yetu hatuwezi kila mtu kuomba barabara ndefu. Unapokula lazima ujue na wenzako wapo. Mimi namwomba kilometa sita za maeneo korofi *either* iwekwe zege au iwekwe lami kwenye yale maeneo kwa sababu ndiyo maeneo yanayosababisha kukatika kwa mawasiliano kipindi cha mvua. Halafu hayo maeneo mengine yakishindiliwa vizuri na kokoto ndipo tunapoweza sasa kuendelea kujenga taratibu. Kwa sababu barabara yote kutoka Kilolo – Idete imekwishafanyiwa usanifu na kwa hiyo, inaweza ikajengwa wakati wowote. Kama fedha hakuna basi iwe kwa maeneo korofi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mlima Msonza, nilimwomba wakati ule, nikamwambia ni kilometa mbili, tumepewa meta 200.

Sasa meta 200 kwa kilometa mbili kwa kweli bado lile eneo linabaki kuwa korofi. Hata kwenye banda pale niliwaambia wale watu wa *TANROADS* Mkoa, nikawaambia, tungeweza kupata kilometa mbili, tukaumaliza ule Mlima Msonza tunakuwa tumetatua tatizo, halafu tukapata kilometa nne kwenye Mlima unaoitwa Mizani. Mlima ule unaitwa mizani kwa sababu lazima washushe mzigo ndipo waanze kupanda kwa sababu ule mlima hauwezi ukapanda na mzigo mkubwa kutokana na ubovu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukapata hizo kilometa nne tukaweka pale Mlima Mizani tunakuwa tumepunguza tatizo kwenye ile barabara na kwa hiyo, kipindi cha mvua, sitawasumbua sana. Hilo ndilo jambo bado halijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo hii barabara inaishia pale Idete, ikitoka pale Idete inakwenda kilometa 18 inafika Mlimba. Hii ina daraja moja tu la Mto Mngeta na *TARURA* tumeshaichonga ile barabara. Kwa hiyo, kwanza haiwezi kubaki kule na tayari *RCC* tulikwishasema kwamba barabara ikiishia Idete na inaunganisha Mlimba, maana yake hiyo ni barabara inaunganisha mikoa. Kwa hiyo, kile kipande cha kilometa 18 inabidi kihamie *TANROADS* ili *TANROADS* waendelee na ile barabara kwa sababu imekwishachanwa na *TARURA* na ikishachanwa daraja la pale Mlimba linatakiwa lijengwe.

Mheshimiwa Spika, ninajua na Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba anajua, ili yeye aweze kuunganisha pale kwa maana kwamba hiyo itakuwa ni *alternative* ya watu wanaotoka Iringa kwenda Morogoro kupitia Ifakara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tunaomba liangaliwe kwa mtindo huo kwa sababu linaweza kusaidia sana kwenye ile kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine tunashukuru sana kwa kazi inayoendelea pale Mlima Kitonga. Mheshimiwa Waziri hilo ni mojawapo ya vitu vinavyoashiria usikivu wenu na jinsi ambavyo mnaelewa kwa sababu kwa ujenzi wa Mlima Kitonga na upanuzi wa ile barabara maana yake ni kwamba uchumi wa nchi yetu

utafunguka kwa sababu foleni za pale zilikuwa zinaathiri kwa kiwango kikubwa sana. Namna ambavyo barabara ile ilivyo ilikuwa wakifika pale chini ni lazima wasubiriane au kusababisha ajali mbalimbali kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, maombi yetu ni kwamba barabara ile iendelee kujengwa kwa kasi kubwa na fedha itolewe ili kwamba kusisimame, maana ni barabara ambayo kama itasimama hata kidogo tu, tayari wamekwishatindua na pale kunaweza kukasababisha kero zaidi. Kwa hiyo, tunaomba katika utoaji wa fedha, Mlima Kitonga pazingatiwe kwa sababu pakisimama kidogo panaweza pakaathiri nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana ambacho kinaweza kusababisha changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba ninashukukuru kwamba barabara ya kutoka Ilula inayopita Mkalanga kwenda Kilolo, ambayo ndiyo barabara kubwa ya ndani ya Kilolo ya *TANROADS,* ile barabara kwa kweli matunzo yake ni mazuri kwa kiwango cha changarawe na ina maeneo machache ambayo ni korofi. Kama ilivyo kwenye barabara nyingine, mimi hofu yangu ni kwamba inapofika kipindi cha mvua na yale maeneo korofi tunayafahamu, lakini hatuchukui hatua ya kuyapiga kiwango cha zege kama ilivyo pale Mlima Kitonga au kwa lami kama tunaweza.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi ndio usafirishaji wa mazao unakuwa mgumu. Barabara hii Mheshimiwa Waziri Mkuu bahati nzuri yeye mwenyewe yupo tangu wakati huo, alipita pale Ilula na aliahidi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, basi sasa kwa kuwa aliahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu ianze kidogo kidogo, hata kilometa tano/tano, hata tatu/tatu. Sisi tutawaonesha maeneo ambayo yanatakiwa kujengwa ili kuzuia kusitisha shughuli za maendeleo kwenye lile eneo kwa sababu ni ahadi ya viongozi na ninyi mnafahamu ahadi za viongozi zinatakiwa zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maeneo ambayo kwa ninavyoona, kama watayafanyia kazi basi yanaweza yakasababisha mabadiliko ya kiuchumi kwenye yale maeneo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba ile ahadi ya kilometa mbili, ambapo tumepata meta 200, kwa kweli meta 200 ni chache, Mheshimiwa Waziri aongeze tu, basi iwe kilometa moja kwa sababu sasa meta 200 ni padogo, ni viwanja viwili tu vya mpira, padogo tu. Kwa hiyo, nakuomba sana uwaagize wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi najua akiwaagiza yeye mkoani pale, watajua wenyewe hiyo hela wanatafuta wapi, wakaweke angalau kilometa moja pale Mlima Kitonga ili angalau na mimi nikirudi, niwaambie Mheshimiwa Rais mnaona ametupenda, tumeongezewa hii kilometa moja, kwa sababu wananisikia naongea, basi wajue kuongea kwangu humu ndani huwa kunaleta maana kwa sababu sasa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana…

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** …kama nitashindwa hata kupata kilometa moja, nitakuwa na sababu gani nisimame kuongea? Kwa hiyo, mimi naamini mimi kwamba hiyo angalau itanifanya niondoke nikiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenitunuku uhai hadi leo nikapata fursa kuchangia hapa kwenye bajeti hii muhimu kwa Taifa letu. Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mara ya kwanza anakwenda kutengeneza historia ndani ya Mkoa wa Morogoro, ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ni Waziri makini, msikivu, mchapakazi na mwenye kujituma kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, mimi huwa sisifii hovyo hovyo, ukiona ninasifia maana yake kuna kazi inafanyika, kwa kweli ni mtu rahimu, kama jina lake lilivyo *Innocent*. Vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu pia na Mhandisi ndugu yangu Razack, Mhandisi wa *TANROADS* Mkoa wa Morogoro na msaidizi wake Patrick, wanafanya kazi nzuri kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na shukurani, ninaomba kueleza kwa nini nina kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais. Kwa mara ya kwanza na jambo hili mtashangaa sana, Mkoa wa Morogoro ni mkoa mkongwe, siyo mkoa mpya, lakini mpaka leo ni mkoa ambao ulikuwa hauwezi, haujaunganishwa kwa kiwango cha lami na Mkoa wa Ruvuma, haujaunganishwa kwa kiwango cha lami na Mkoa wa Lindi, haujaunganishwa kwa kiwango cha lami na Mkoa wa Njombe hadi leo na Mkoa wa…, siyo Mkoa wa Songwe kwa maana mkoa mpya, Mkoa wa Morogoro ni mkoa ambao ni mkongwe, bado ulikuwa haujanganishwa na mikoa yote mitatu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini ninasema Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kutengeneza historia, kwa mara ya kwanza nimeanza kujenga hoja hapa Bungeni na Mheshimiwa Spika utakuwa shahidi, nikizungumza kwa habari ya Barabara ya Morogoro – *Njombe Border*, nikieleza umuhimu wa barabara hii, nikasema barabara hii inakwenda kuunganisha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na ni barabara muhimu sana na ni barabara ya kimkakati katika uchumi wa Taifa letu na sasa Mheshimiwa Rais amesikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hapa, kwa mujibu wa Ilani, Ilani ilisema barabara hii itajengwa kilometa 50, lakini Mheshimiwa Rais ameruhusu barabara hii ya Morogoro – *Njombe Border* mpaka pale Madeke yenye urefu wa kilometa 223, ameruhusu ianze

kujengwa kwa kiwango cha lami kilometa 100. Kwa nini nisishukuru hapo? Yaani amepitiliza hata ahadi ya Ilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema tu kwa dhati kwamba nitasikitika sana kama kuna Waheshimiwa Wabunge ambao hawataunga mkono bajeti hii na hasa wale ambao hawajabahatika kuwa na viwanja vya ndege na wale ambao hawana hata ndoto za kuwa na viwanja vya ndege, kwa sababu zaidi ya 90% ya Watanzania kama siyo 100%, wanategemea barabara. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa kauli moja, tuunge mkono bajeti hii ili ipite kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama haitoshi, kilometa 100 tayari zina wakandarasi wawili, *Lot 1* kutoka Ifakara – Mbingu eneo la Igima pale Miale kilometa 62.5 mkandarasi yuko *site* anasubiri tu apewe fedha anazodai kwenye malipo ya awali shilingi 9,000,000,000. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ananisikia hapa, ninaamini hawezi kuruhusu mdogo wake nikose kurudi tena hapa Bungeni kwa sababu ya barabara, atalipa tu hiyo *advance payment* mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kutoka Mbingu – Chita JKT kilometa 37 na nusu kukamilisha kilometa 100, lakini kutoka pale Kihansi kwenda Madeke, napakana na ndugu yangu Mheshimiwa Swalle pale Lupembe, tayari kuna Benki ya Maendeleo ya Afrika wanafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii, nayo nina matumaini makubwa kuwa itajengwa. Kwa hiyo, nasema tu kwa dhati kwamba nina kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nieleze hapa kuhusu bajeti. Bajeti hii tunayokwenda kupitisha hapa ni *1.7 billion,* lakini nikawa najiuliza maswali, deni peke yake, watu wanasema ni shilingi 929,000,000,000, hili deni ni madeni ya nje, deni la ndani ni shilingi 257,000,000,000, uki-*plus* unapata *one trillion point something,* lakini bajeti ni shilingi bilioni 1.7. Maana yake ni kwamba kama

Mheshimiwa Waziri atatumia fedha hizi akalipe madeni, hatuna bajeti ya mwaka huu wa fedha na hivyo hakuna kinachokwenda kufanyika, hamna hela inayobaki.

Mheshimiwa Spika, sasa rai yangu na ombi langu Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa ni muhimu sasa ikae na Kamati yako tukufu ya bajeti wafanye mapitio au Waziri wa Fedha atusaidie kutafuta fedha zingine nje ya bajeti hii tulipe madeni. Tukilipa madeni kwa fedha zingine nje ya bajeti ninahakika Mheshimiwa Waziri atafanya kazi nzuri sana ya kutukuka na barabara zetu zitapitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimeona jana la anakusurubu *he is very innocent* kwa sababu katika hali ya kawaida wewe angalie bajeti ya *five point seven billion,* anaenda kufanya nini? Deni *trillion* moja *plus, s*asa rai yangu Bunge lako Tukufu na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Kamati yako Tukufu ya Bajeti iende ikafanye mapitio au kama kuna njia yeyote ile ya kupata fedha za kulipa deni hili ambalo *TANROADS* wanadaiwa ili kunusuru hizi fedha zikafanye kazi inayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nieleze kuhusu maombi, wananchi wa Mrimba wanaomba vitu vidogo sana kama ifuatavyo; kitu cha kwanza wananchi wa Mrimba wanasema kwa kuwa tulichelewa sana mikoa mingine wanahangaika na kuunganisha wilaya, sisi Mrimba tunahangaika na kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Njombe, Serikali itupe kipaumbele hasa kwenye malipo ya Wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, maombi yao kupitia Wizara ya Fedha Mkandarasi huyu ambaye anadai bilioni tisa malipo ya awali alipwe mara moja kwani amekaa *site* huu mwezi wa tano hajaanza kazi anasubiri fedha hizo na hii hasara yake ni nini? Mwisho wa siku atakuja kudai riba na taarifa zinaonyesha kila mwaka madeni yanayotokana na riba ni bilioni 73. Sasa niombe Mkandarasi huyu alipwe mapema ili aanze kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi la pili kwa wananchi wa Mrimba wanasema Waziri wa Ujenzi ni muhimu Mkandarasi huyo aliyesaini Mkataba *Lot two* hii ya awamu ya pili kilomita 37 na nusu akabidhiwe *site*. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria mara tu Mkandarasi atakaposaini mkataba yeye anahesabu yuko *site*. Kwa hiyo, ukimwacha mtaani miezi sita hajakabidhiwa eneo la kazi maana yake anahesabu yupo *site*. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kaka yangu kama ulivyo na una uungwana wako tukimaliza bajeti hii ya kwako ebu twende pale tukakabidhi *site* aendelee na majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine la mwisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele imeshagonga…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, wanaomba kuunganisha Barabara ya Morogoro na Iringa kupitia Kihansi mpaka hapa kwa ndugu yangu Chumi – Mafinga. *With all I due respective* Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia na mimi hii Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa afya njema, kuendelea kuwasemea wananchi wangu wa Jimbo la Rorya Mkoa wa Mara lakini pili niseme neno moja kwamba leo nasimama hapa kuchangia juu ya Barabara ya Mika – Utege – Shirati – Kirongwe ni kwa mara ya nne. Lakini tumekwisha uliza maswali, mimi binafsi toka nimeingia Bungeni nimeuliza maswali ya nyongeza kama mara nane kwa namna tofauti tofauti lakini nje ya hapo nimeuliza maswali ya msingi kuhusiana na barabara hii kama mara nne, barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imekuwa ikitajwa kwenye Ilani toka mwaka 1995 kwenda mwaka 2000 ikatajwa 2000 kwenda 2010 Mheshimiwa Rais wakati huo akiwa Jakaya Mrisho Kikwete, lakini pia ikatajwa baada ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa maana ya 2015 kwenda 2020.

Mheshimiwa Spika, kipekee kwa niaba ya Wananchi wa Rorya nimesimama hapa kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kutoka moyoni kwa kazi kubwa nzuri aliyotufanyia Mheshimiwa Rais. Tazama barabara hii imetajwa kwa zaidi ya miaka 20 na kuendelea lakini mimi Mbunge nimesimama ukiacha siku ya leo ni zaidi ya mara kumi tano naizungumzia barabara hii. Rais huyu huyu Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kuwiwa na kuona umuhimu wa barabara hii, akaridhia barabara hii ya Mika – Shirati – Kirongwe kilometa 56 na leo kilometa 27 zinakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami na akaridhia kuiweka kwenye bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesimama hapa kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa kuona utashi huo wa kisiasa na kuona namna ya kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sembuse tofauti na Mheshimiwa Rais, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri pongezi unazoziona kwa Waheshimiwa Wabunge hapa ni kwa sababu unajua namna ya kuishi na wao, unajua namna ya kuzungumza nao, unajua lugha ya kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge hata kama hauna fedha. Lakini bado umekuwa miongoni mwetu kuzungumza na kututia moyo kiukweli ndiyo maana unaona pongezi nyingi tunakupa pamoja na kwamba tunajua hauna fedha siyo makosa yako. Lakini kwa namna unavyojishusha na kuzungumza na Wabunge, kwa namna unavyoshughulika na changamoto Mwenyezi Mungu aendelee kukutia moyo sisi tunakuombea sana uendelee kufanya kazi nzuri na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kukuweka kwenye Wizara hii. Sisi, kama Wabunge vijana tunajivunia sana kuona kijana mwenzetu ukifanya kazi kubwa

nzuri na tutakuwa nyuma yako wakati wote, wakati wote utakapohitaji tutakusemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue nafasi hii kumpongeza sana Naibu Waziri kwa namna ambavyo alikuwa akisimama hapo mbele anajibu maswali ya Wabunge. Barabara zote unazoona zinazungumzwa humu Naibu Waziri amekuwa akizungumza kwa kutitia moyo, hata pale anapoona kwamba barabara hii imeulizwa hakuna fedha lakini amekuwa akitufariji, faraja zile za Mheshimiwa Naibu Waziri lazima tuendelee kumshukuru sana na yeye tumtie moyo kwa namna ambavyo ameendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu wa tatu nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara hii Balozi Aisha Amour kwa namna ambavyo na sisi Wabunge tunavyokimbia kwenda Wizarani anatupokea, anatufariji na kutupa matumaini ambayo kimsingi tunaamini haya yote si makosa yao, kama Wabunge wenzangu walivyosema tatizo ni fedha. Kwa hiyo, hawa wenzetu wanatufariji kwa namna ambavyo nje ya uwezo wao kwa sababu hakuna namna ambavyo wanaweza wakafanya zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho nichukue nafasi hii ya kipekee kabisa kumpongeza sana Meneja wetu wa Mkoa wa *TANROADS,* Meneja wetu Mkoa wa Mara, Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mara, ndugu yangu Vedastus Maribe. Huyu ni mtu ambaye kila muda ukimpigia simu sisi Wabunge wa Majimbo ya Mkoa wa Mara kila muda ukimpigia simu anapatikana, kila ukimpa changamoto anapatikana.

Mheshimiwa Spika, leo tunavyozungumza hakuna barabara ambayo inahitaji *maintenance* kwa Wilaya ya Rorya ambayo haipitiki. Barabara inaweza isipitike upande wa *TARURA* lakini *TANROADS* Meneja huyu amekuwa akifanya kazi zake kwa ufanisi sana, tumpe maua yake na nikuombe Mheshimiwa Waziri usije ukatuhamishia Meneja huyu sisi tunamuhitaji sana kwa sababu kiukweli anatufaa sana sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu nilitaka niseme jambo moja na hili Waziri wa Fedha atusikilize vizuri sana. Siasa ya Mkoa wa Mara ni barabara pamoja na maji, ukituuliza vipaumbele sisi Wabunge tutakwambia moja ni barabara mbili ni maji lakini Sekta ya Maji tuiche kwa sababu leo tunazungumzia barabara. Barabara ndiyo inabeba siasa yetu ya Mkoa wa Mara, kipaumbele kikubwa cha siasa Mkoa wa Mara ni barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini utaona hapa kwenye bajeti yetu hii, barabara karibia wilaya zote sita zimesimama. Ukimsikiliza Mbunge wa Tarime Vijijini anakwambia barabara aliyopewa fedha ya kwenda Mogabiri kwenda Nyamongo ambayo ni kilomita 25 Mkandarasi yuko *site* imesimama kwa nini? Hakuna fedha, Mkandarasi hajalipwa. Ukiuliza barabara inayotokea Nyamongo kwenda Mugumu kwa maana ya Serengeti imesimama kwa nini? Mkandarasi anadai zaidi ya bilioni ngapi? Hajalipwa imesimama na haifanyiwi kazi, ukiuliza Musoma Vijijini hivyo hivyo, ukiuliza Bunda umesikia Mbunge wa Ukerewe hapa amezungumza barabara inayomuunganisha Bunda na Ukerewe imesimama kwa nini? Wakandarasi hawana fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme haya yote hatupaswi kumrudishia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, tumuombe Waziri wa Fedha alione hili barabara zote zinazotuunganisha ndani ya Mkoa, barabara ya *TANROADS* ndiyo barabara zenyewe za msingi za *TANROADS* hakuna barabara zingine. Kitendo cha barabara hizi kusimama kwa muda mrefu bila Wakandarasi kuonekana *site* maana yake unatusimamishia Mkoa, tunashindwa jambo la kusema, kwa nini? Wakandarasi hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha mlione hili mtakapokuwa mmekaa. Tumuongezee fedha Waziri wa Ujenzi ili alipe Wakandarasi hawa warudi *site* wakatengeneze barabara hii. Dhamira na madhumuni ya Mheshimiwa Rais ni mazuri sana kwa hiyo, nyinyi mkae tuone namna ambavyo tunaweza tukafanya kutatua changamoto ya hizi barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nichukue nafasi kumshukuru sana, sana sana Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais. Barabara ya Kuruya ya kwenda Kinesi upembuzi yakinifu nimekuwa nikizungumza hapa ndani lini utafanyika? Nimeona mtenge fedha upembuzi yakinifu unakwenda kufanyika na naamini mwakani itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa kuliko yote nimeambiwa mmetupa zaidi ya milioni 600 kwa ajili ya kujengwa *box* karavati kwenye Mto Tobwe ambayo inatuunganisha kwa maana kwamba kutoka Masonga kwenda Sirari. Pale ule Mto mvua ilikuwa ikinyesha Mheshimiwa Waziri, hakuna mwananchi alikuwa anavuka kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine, leo Meneja ananiambia mmetupa milioni 600 kutoka kwenye fedha za dharula na ujenzi umeanza, nikushukuru sana kwa kazi kubwa nzuri unayofanya.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho ni ujenzi wa maegesho. Nimuombe sana mtu wa *TEMESA,* Mheshimiwa Waziri nimeona mmejenga maegesho pale upande wa pili wa kivuko huko Musoma Mjini. Lakini mtambue wale wannchi wanatoka Rorya – Kinesi wanavuka kuja Musoma Mjini ni sawa ujenge egesho Kigamboni halafu uache kujenga upande wa pili huku wa Mjini, unajenga sehemu ya wananchi kumpuzikia kivuli upande wa Kigamboni halafu upande wa Mjini hujengi haina maana. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri uone hili kwa kuwa tumejenga upande wa Musoma – Kinesi kule pia uwajengee egesho kwa ajili ya kivuli pamoja na wakati wa mvua. Kwa sababu haiwezekani ukaenda upande mmoja mtu anafika anaumia kwamba kuna mvua ananyeshewa, akienda upande wa pili anapata uwafadhali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe hili watu wa *TEMESA* na ninaomba Mheshimiwa Waziri ulichukue hili uone namna ya kuwasaidia wananchi wetu wa Rorya.

Mheshimiwa Spika, kwa leo sikuwa na mengi sana, niliona ni muhimu tum-*support* sana Mheshimiwa Waziri na tumuombee

Mheshimiwa Waziri wa Fedha amuongeze fedha ili haya yote tunayoyasema yaweze kufanyika, tunashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipatia fursa ya kuchangia bajeti hii ya ndugu yangu Bashungwa, Mheshimiwa Bashungwa. Nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kuliongoza Taifa letu, uongozi mzima wa Serikali yetu Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na viongozi wote wakuu wa Taifa hili. Pia niwapongeze Wizara kwa kweli wanafanya kazi kubwa chini ya uongozi wa Waziri ndugu yetu Mheshimiwa Bashungwa, Naibu wake Watendaji Wakuu wote wa Wizara kwa kweli mnastahili pongezi na pongezi za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye Jimbo la Muleba, pamoja na kazi kubwa inayofanyika kitaifa tunaiona na tunaipongeza Serikali, madaraja makubwa yanajengwa na miradi mikubwa mikubwa inaendelea kujengwa chini ya usimamizi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake wamefika Muleba, wamekagua kazi zinazoendelea ambazo zinasimamiwa na kupewa pesa na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Muleba tuna barabara yetu ya Muhutwe – Kamachumu – Buganguzi – Inshamba kwenda Muleba. Mheshimiwa Waziri unaifahamu sana wote wawili mnaitembelea hiyo barabara kazi inaendelea, kimebaki kipande cha kilometa 9.7. Mheshimiwa Waziri nimeangalia kwenye bajeti sijaona popote ambako mmeweka kuikamilisha, najua kuna kazi inaendelea ya kilomita moja tunawashukuru wanasema

asiyeshukuru kwa dogo hata kubwa hatapata, nakushukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ningeomba sasa Mheshimiwa Waziri hii barabara imekuwa ikijengwa kwa kilomita tatu, mbili na wewe mwenyewe ulipokuja kuitembelea ulisema ni kipindi kirefu imejengwa na kilometa 54, nakuomba sasa iwe ni mwisho kabla hatujamaliza kipindi hiki bajeti hii Mheshimiwa Waziri angalia tunaweza tukaja angalau tuweze kumaliza hii barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna madaraja makubwa mawili tumejenga hii barabara Muhutwe – Kamachumu – Nshamba hadi Muleba lakini tumeacha madaraja mawili, tuna daraja la Kamishango na daraja Kyabakoba. Ningeomba Serikali kupitia bajeti hii mmekuwa mkifanya upembuzi yakinifu na usanifu, sasa nimepata taarifa kwamba mmeishamaliza, niombe haya madaraja ambayo yamebaki kati kati najua yana gharama kubwa tukayajenga. Lakini naombi moja, wakati tunajenga hii barabara hatukuwa na njia ya kuendelea na shughuli za kibiashara katika hiyo Barabara, naomba wakati wa tunajenga tutafute njia rahisi ambayo itawarahisishia wananchi wa maeneo hayo waweze kuendelea na shughuli zao wakati ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwamba haya madaraja tujenge kama tulivyojenga daraja la Ruvu, lile liliopo tuliache tujenge daraja jingine pembeni ili shughuli za kibinadamu na shughuli za kibiashara ziendelee. Mheshimiwa Waziri unafahamu Wilaya ya Muleba lile daraja linakwenda Nshamba na ukiacha Nshamba ndiyo sehemu ya uchumi na wafanyabiashara wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna barabara nyingine ambazo zinatusaidia unavyojua Mkoa wa Kagera ni Mkoa wa uzalishaji kahawa na hizi barabara zinatusaidia kuhakikisha kuwa zinatoa kahawa kwenye mashamba na kulileta kwenye masoko na kuleta wilayani. Tuna barabara ya Rutenge – Izimbya hadi Kishojo nadhani Mheshimiwa Waziri unaifahamu kwa sababu na hii

barabara ndiyo inakuja kuinga hata Karagwe na hii barabara tunakuomba Mheshimiwa Waziri iangalieni tukaijenge itarahisisha mawasiliano lakini pia itakuza uchumi wa hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna barabara nyingine Mheshimiwa Waziri anaifahamu ya Kasindaga – Kyebitembe – Karambi – Kimeya hadi Lunazi ni barabara kongwe ya *TANROADS*. Lakini tumeisahau Mheshimiwa Waziri, angalau tuitengee tuanze kuijenga kwa kilomita moja, kilomita mbili ili baada ya muda na yenyewe iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna barabara nyingine ya Rutenge kwenda Mushabago ni barabara ya *TANROADS* hii lakini mara nyingi tu huwaga tunaisahau, tuwe tunaitengea fungu la kuitengeneza ili shughuli za kiuchumi na za kibinadamu ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, la mwisho Mkoa wa Kagera bado uko kwenye giza Mheshimiwa Waziri. Tukitoka kwenda Mikoa mingine nje ya Kagera tunaona taa nyingi lakini Kagera bado tuko kwenye giza. Nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yako Miji yote ambayo kwenye Mkoa wetu hasa kwenye Jimbo langu la Muleba Kusini, Muleba pale kwa kweli mlituwekea taa kidogo, Lakini nikiangalia kwenye *commitment* yenu mna kilometa 1.1 naomba sasa kwenye bajeti hii Muleba ikawekwe taa lakini na Miji yote ambayo inaibukia hii barabara yote kutoka Kasindaga mpaka Bukoba kuna *center* nyingi sana kubwa lakini tusisahau na Kamachumu pale. Tunaomba Mheshimiwa Waziri tuweke taa za barabarani tutoke kwenye giza sasa Muleba na Kagera iwake imeremete ili ivutie Watalii na ivutie wakazi wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nipende kuomba kwamba tuongeze bajeti ya Wizara, bajeti tuliyonayo ni ndogo, ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya lakini sasa hivi nishukuru kuwa mzima na nimesimama nataka kuichaingia Wizara hii ya Ujenzi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda sana kumshukuru Waziri wangu, Waziri Bashungwa pamoja na Naibu wake Kasekenya. Kwa kweli, hawa wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi kubwa tena nzuri na jitihada tunaziona sisi sote katika Wizara yake, maana tunatembelea maeneo mbalimbali katika Wizara hii. Lakini pia nimshukuru na Mwenyekiti wangu huyu wa Kamati, Mheshimiwa Selemani Kakoso kwa kutulea katika Kamati ile mpaka leo hii mimi naweza kusimama hapa sasa hivi na nikaweza kuchangia, namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuendelea kuna suala hili kidogo nataka kuliwekea sawa kwamba kwa kuwa, mkakati wa kuwawezesha Wakandarasi wanawake na vijana. Mimi hili neno nilivyoliona katika mkakati wao mimi nilishukuru sana hili suala kwa sababu wanawake watapokuwa wao Wakandarasi pamoja na vijana wakawawezesha, wakajua kwamba hapa sasa hivi sisi tupo tunafanya kazi basi sisi wanawake tunafanya kazi kubwa sana kuliko wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana nao hali kadhalika kwa sasa hivi wanafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, hili suala mimi naomba hawa wanawake pamoja na vijana wapewe kipaumbele waweze kufanya kazi zao katika ukandarasi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuongezea nazungumzia kuhusu ubora wa madaraja. Madaraja na ubora haya ndiyo tunayoyataka kwa sababu mimi nimetembelea katika barabara zetu tunazopitia nilishashuhudia kuna madaraja mengi sana yalikuwa yanakatika hasa kipindi hicho cha mvua mimi mwenyewe nilishashuhudia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wakandarasi wanaojenga madaraja wayajenge madaraja

yenye kiwango, madaraja yenye kiwango ambayo yanaweza angalau yakadumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wanaweza kuifanyia hasara Serikali wakawa wanajenga madaraja ambayo hayana kiwango matokeo yake tunafika karibu ya madaraja magari yanasimamishwa mabasi tunaambiwa kule daraja limekatika kwa hiyo, Serikali pale imeishapata hasara.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nizungumzie na hili kwamba mimi hapa nitasema sasa hivi ni mkazi wa Dodoma, Manispaa yangu ya Makulu ninakokaa mimi Mkalama. Nimshukuru Naibu Waziri wangu Biteko, kwa kazi kubwa anayoifanya katika barabara za Mkalama. Hivi sasa hivi kazisimamia madaraja yanafanya kazi na kesho kutwa karibu tutatembelea nini mgongo wa ngisi, maana ile barabara watazitia lami. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Biteko, afanye kazi kubwa ili tuweze kupita pale. Yule Mwenyezi Mungu katuletea kule aje akae ili na sisi Wanawake wa Mkalama tufaidike katika barabara zile pamoja na Wananchi wote wa Mkalama. Tunamshukuru sana sana sana na nikisema haya nikakosa kumshukuru basi mimi nitakuwa sina fadhila maana hili suala mimi nilimwomba na akaniambia Mheshimiwa taratibu, tutakwenda na tutafika. Ni kweli sasa hivi tumefika na tunamshukuru sana na naunga mkono hoja 100%, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuniona na mimi kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani kwa Serikali kwa nia ile ya kutujengea barabara ya kutoka Kitai – Amani

Makolo – Rwanda – Litui. Kwa nini nasema kwa nia? Barabara hii tayari kilometa 35 mkandarasi yupo *site* na kwa maelezo ya kwenye hotuba tayari kilometa 54 za kuanza Rwanda – Litui tayari mkataba umesainiwa, lakini kwa bahati mbaya hizi kilometa 35 tulikuwa tunatarajia barabara ikamilike tarehe 18 ya Mwezi wa Kumi na Mbili, mwaka jana. Hadi leo hata siyo kilometa, hata kipande kidogo tu cha lami hakuna.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hapa kwa masikitiko makubwa. Tulienda na Mheshimiwa Waziri, aliona utendaji katika barabara hii na alitoa maelekezo pale kadhaa lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri hadi leo hamna kinachoendelea katika ile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ipo *busy* kweli kweli. Barabara hii ndiyo inayopitisha makaa ya mawe kutoka Rwanda Mgodini, pia kutoka pale Amani Makolo ambapo pana *dry port*. Kwa hiyo, magari kwa siku ni zaidi ya 1,000 yanapita hii barabara. Ni huzuni sana wananchi wanaokaa Amani Makolo, Paradiso na Rwanda kuanzia huu Mwezi wa Tano, Sita, Saba mpaka wa Kumi na Moja kabla ya mvua kunyesha, huwezi kuzitambua nyumba zao. Huwezi kutambua nyuso zao wanavyotembea. Ni watu waliooga vumbi, nyumba zilivyooga vumbi, kwa hiyo, ni hatari kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunazungumza mara kadhaa na wananchi hawa kuwatia moyo kwamba, hii barabara inaenda kukamilika na sasa wataondokana na adha hii ya vumbi. Mwezi wa Kumi na Mbili ilikuwa ndiyo mwisho angalau wananchi hawa wafurahie, lakini mpaka leo hakuna hata doti moja ya lami kwenye hizi kilometa 35. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tumekubaliana hatutakubali kula vumbi tena mwaka huu, hatutakubali kwa sababu tumekula vumbi kwa miaka yote makaa ya mawe yanachotwa pale. Hatuwezi kuendelea kula vumbi hizo. Tutasimamisha mgodi mpaka tupate barabara ya lami pale Amani Makolo mpaka Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wakati fulani wale wananchi walikuwa wanalaumu kwamba, Mbunge hasemi. Nimempeleka Waziri wakagundua tatizo siyo la Mbunge, tatizo lipo kwa mkandarasi. Waziri akatoa maelekezo pale sasa wanauliza mbona maelekeo yale ya Waziri hakuna linalotekelezwa hata moja? Kwa sababu Waziri alisema tunafukuza mkandarasi na mhandisi mshauri, bado wapo wanafanya kazi. Kwa nini waendelee kufanya kazi? Kazi yenyewe hawafanyi wame-*park* tu magari pale hamna kazi inayoendelea. Kwa hiyo tumekubaliana safari hii hakuna makaa ya mawe kutoka pale kama hatuoni barabara ya lami pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninalotaka kulizungumzia ni eneo la barabara hizi ambazo zipo siyo za lami ni za changarawe. Zipo barabara kipindi hiki cha mvua zimetutatiza sana. Barabara ya kutoka Peramiho kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama kuja Litumbandyosi hadi Paradiso kuna maeneo ya Mlima Sanga pamoja na maeneo yenye mito, yalifunga barabara ile kwa muda wa miezi miwili. Wananchi walikuwa wanatembea zaidi ya kilomEta 100 kufuata huduma kwa mguu. Kwa hiyo, niombe kwamba kwenye maeneo yenye mito kama hayo nimeona baadhi ya maeneo mmeanza utaratibu wa kuweka reli. Basi niombe na barabara hii ya kutoka Paradiso – Kingole – Peramiho tuwekewe reli angalau hawa wananchi watumie barabara hii kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, pia vivyo hivyo niongelee suala la Ahadi za Viongozi. Sisi tuna ahadi pale, Mheshimiwa Rais alifika Mwaka 2020. Barabara ya kutoka Kigonsera kwenda hadi Matiri, pia barabara ya kutoka Mbinga kwenda hadi Litembo. Nimeuliza maswali hapa nashukuru kwamba, Serikali imeahidi kwamba sasa hivi ilikuwa na nia ya kufungua njia hii lakini imeshafunguliwa ambako wanaongelea kufunguliwa ni kutoka Matiri kuelekea Mbaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niombe hii ahadi ni ya Rais na wananchi wale kila siku wanakumbusha. Pia kwa kutoka Mbinga kwenda Litembo mwaka jana mliahidi uthamini unafanyika.

Tufanye ule uthamini ile barabara, hata tukakosa hii ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi kutokea Ndengu kwenda Mbuji hadi Litembo itakuwa suluhisho au itakuwa majibu ya barabara hii ambayo Rais aliahidi, ni kilometa 22 tu. Niombe sana kwa sababu pale pia kuna ombi la Mhashamu Askofu John Ndimbo la kumwomba Makamu wa Rais wakati anaenda kufungua Chuo cha Afya kule kwamba ile barabara itekelezwe. Kule Litembo ndipo kuna hospitali ambako wananchi wa Jimbo la Mbinga Vijijini wanatumia kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwsiho nililotaka kushauri ni namna tunavyoweka matuta barabarani. Zipo barabara unapita kwa uzuri sana kwamba, unaweza ukawa hata kwenye *speed* ya 50 unapanda lile tuta vizuri, unashuka, lakini zipo barabara hata ukiwa kwenye *speed* ya sifuri (gari linaseleleka tu hivi) ukifika kule chini lazima gari lilie *boom!* Mkito mkubwa. Sasa, ombi langu Mheshimiwa Waziri hivi hatuwezi kuwa na viwango vya usawa. Ukipita barabara ya kutoka Makambako kuja Iringa hapa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** … matuta yake ni mazuri sana. Hivi hatuwezi kuwa na matuta ya namna ile nchi nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kupata nafasi ya kuongea Bungeni leo. Pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi ambayo ameruhusu Bunge liendelee kuwepo, ili tutoe michango yetu kwa kadiri Mungu anavyopenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Innocent Bashungwa kwa nia njema anayoionesha kwa sababu naona miradi mingi imeendelea kusainiwa na kutekelezwa japokuwa kuna changamoto kadhaa ambazo zinaendelea kusemwa ndani ya Bunge hili. Pia nimpongeze Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya kwa kumsaidia Waziri kwa kiwango kikubwa hadi hapa tulipofikia sasa. Nampongeza sana Katibu Mkuu Balozi Aisha, kwa uratibu mzuri wa kazi ambazo tunaona zinaendelea na wataalamu wote katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, taarifa hii inaonesha wazi kwamba tangu ameingia madarakani tulikuwa na kilometa za lami 10,830.2 na sasa tuna 12,024.7 maana yake kuna ongezeko la 1,198.5. Kwa hiyo, kama kuna ongezeko maana yake kuna kazi kubwa inafanyika na kwenye awamu hii kazi hii imeshaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii inayoonekana kwenye maeneo yetu na hata hii nia njema inayoonekana. Katika hili inaonekana wazi miradi 25 imekamilika, ikaja na kilometa hizi 1,198 lakini bado kuna miradi 74 ambayo ipo katika hatua mbalimbali tunaamini hii ina kilometa 3,774 itakapokamilika basi hazitakuwa tena 1,100 na kitu, itakuwa 5,000. Ninaamini hizi nazo ziendelee kukamilishwa ili Mheshimiwa Rais nia yake njema ya kuhakikisha kwamba lami inapatikana nchi hii iendelee kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa Jimboni kwangu Busanda; nimpongeze Mheshimiwa Waziri, nilikuwa nasoma bajeti ya mwaka huu kwamba kuna nia njema inaonekana kwenye bajeti. Kwenye bajeti ya mwaka huu barabara ambayo tumekuwa tunaisema kila siku ya kutoka Geita kwenda Kahama sasa inaonekana ina nia njema ya kuanza kushughulikiwa na kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipande ambacho kinatoka Kahama kuja Bulyanhulu pale *Kakola Junction* tayari kina fedha ambayo inaonekana takribani shilingi bilioni 14 zinaanza kufanya kazi. Pia

kuna kipande cha kutoka Bulyanhulu kuja Geita ambacho tayari kimekwishatangazwa na sasa tunaamini kwamba wanakwenda kusaini mkataba kwa ajili ya kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu katika eneo hilo basi haya tunayoyasikia kwamba imetangazwa na imesainiwa mwaka mzima na hamna kilichofanyika isiwe sehemu ya barabara hii ambayo tunaisema sasa. Vilevile bado nimeona kuna Barabara ya kutoka Katoro – Nyikonga – Ushirombo pia kwenye *page* 228 inaonesha kutengewa fedha kidogo kwenye hizo kilometa 22.5 kwa ajili ya kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana kwamba, tunapokwenda kwenye hatua hizo za upembuzi yakinifu kwenye barabara hii ya kutoka Katoro – Nyikonga – Ushirombo ina miaka mingi na upembuzi huu sasa nafikiri hata inapoenda kuanza kushughulikiwa ni lazima irudiwe tena kwa sababu itakuwa ule upembuzi yakinifu sasa hauwezi kuwa *up to date*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana haya ambayo yameandikwa hapa yaweze kufanyiwa kazi na sisi Busanda sasa tuone. Sisi ni wachimbaji wa madini tunazihitaji barabara hizi zipite kwenye migodi yetu ili tuweze kufanya kazi yetu vizuri na kuongeza uchangiaji wa Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kila aliyesiamama hapa anaonesha ipo miradi yetu ya *EPC+F* imekwama. Kila anayesimama anaonesha tukilipa deni la karibu bilioni 929 ukiongeza na riba inakwenda kwenye trilioni moja maana yake hii trilioni moja ambayo ni ya ndani hapa ikitolewa tutabaki na bilioni 10. Bilioni 10 hatuwezi kufanya kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapata mawazo kwamba inawezekana tunatakiwa tuishauri Serikali iangalie vyanzo vyake vya upatikanaji wa fedha kwa sababu kama kila mmoja anayezungumza miradi imekwama maana yake ipo nia njema ya Wizara na ya Mheshimiwa Rais lakini mapato yetu hayatoshi kufanya miradi hii. Nimesikia ndugu yangu mmoja amesema

kwamba mpaka wanataka wazuie na barabara. Sasa kama mapato hayapo wakizuia barabara maana yake mapato yatakuwa hayapatikani kabisa. Kwa hiyo, niseme wazi kwamba tunatakiwa sasa tuangalie kuna mahali fulani ambapo kwenye makusanyo yetu hapako vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nina mashaka na nidhamu ya matumizi yetu kwenye bajeti hizi, kwa sababu kila tunapopata Ripoti ya *CAG* tunaona kama kuna malalamiko hivi. Hebu tusimamie nidhamu ya matumizi ya bajeti na tusimamie vilevile kuongeza vyanzo vya mapato ili mapato yapatikane tuweze kutumia. Tofauti na hiyo tutaendelea kutangaza barabara kila mwaka, tutampongeza Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Rais, ukija mwaka mwingine tunasema hazikufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili hili tusione ni lazima twende tuhakikishe kwamba, tuna bajeti ya kutosha. Kama kuna pesa inatakiwa ipatikane kwenye kilimo ipatikane, pesa ya kwenye madini ipatikane, isimamiwe vizuri kuhakikisha kwamba tunaenda kufanya miradi hii ambayo na kwa hali halisi tunashindwa kutekeleza kwa sababu ya vyanzo vyetu vya mapato havitoshi kufanya kila mradi uliokwishasainiwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo naomba niunge mkono hoja nikiamini kwamba, hizi barabara nilizotaja za Busanda zitakwenda kufanyiwa kazi na watu wataanza kupata maendeleo yao, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mungu muumba ardhi na nchi kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu mpendwa mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha Taifa letu linaendelea kupata maendeleo. Kazi kubwa alizozifanya ni pamoja na kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuunganika na nchi za jirani kwa kuwa na mtandao mkubwa kwa takribani 200,000; tunao mtandao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niipongeze sana Wizara pamoja na watendaji wake wote chini ya uongozi wa dada yangu *Engineer* Aisha kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha kama Taifa tunaungana mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya na mataifa ya jirani. Kipekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri rafiki yangu na kaka Mheshimiwa yangu Bashungwa na Naibu wake. Kiukweli kabisa bila kupepesa maneno na sisi wanasiasa wakati mwingine tunapaswa kuwa *realistic*, tuwe wakweli wa nafsi setu. Kwenye suala zima la miradi yetu hii leo tunayoipigia kelele sana, kutokufanyika kwa wakati, kutokumalizika kwa wakati na wakandarasi kutokulipwa kwa kweli Mheshimiwa Bashungwa *is innocent. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tulimwita Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha alikuja kwenye Kamati yetu na akatueleza changamoto zilizopo zinazopelekea fedha zisiende kwenye ujenzi na kiuhalisia kama Taifa tutafikia wakati vilevile unaweza ukasema hata huyo Waziri wa Fedha unayesema unaweza usimlaumu lakini ni katika kuhakikisha bado kama Taifa tunapigana na tunaendelea kukua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba niseme kwamba kama Taifa tumekuwa na wakandarasi nchini ambao wakandarasi wetu hao takribani 16,020 ndio ambao wametuwezesha miaka yote kuwa na mtandao huu wa barabara ambao tunao. Wakandarasi hawa nafikiri leo nyinyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mashahidi, mara nyingi mmekuwa mkilaumu kwamba wakandarasi wanafanya kazi kwa fedha nyingi, lakini sababu kubwa hata wewe ukiwa mfanyabiashara lazima faida uiweke kidogo kubwa ukisubiria zile fedha zako muda wote ambao

utakuwa hujalipwa. Ile *profit margin* lazima utaiongeza kidogo. Kwa hiyo, suala la wakandarasi wetu kuwa ghali linasababishwa pia na ukosefu wa fedha zinazotakiwa kulipwa kwenye miradi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo leo mmekuwa mashahidi mmewatetea wakandarasi kwamba hawalipwi na hatimaye tunazalisha riba kubwa. Vilevile, siyo wakandarasi tu hata wahandisi washauri na wenyewe kadiri mradi unavyoongezeka muda vilevile fedha inaongezeka. Kwa hiyo, hii ni changamoto ya kucheleweshewa miradi kama Taifa ni wakati sahihi namna ya kuangalia tutavyokwenda vizuri na kuweza kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kusema kiuhalisia Mheshimiwa Bashungwa *is innocent,* hakuna sababu ya kushika shilingi yake ndugu zangu wala hakuna sababu ya kutokupitisha bajeti hii. Wote ni Watanzania na wote ni wananchi lazima tuwe *realistic* tunafahamu hali halisi, wala Mama Samia na yeye unaweza ukasema vilevile *is innocent*. Lazima tukubali tumekuwa na miradi mikubwa mingi ambayo imefika wakati lazima imalizike, ni *point of no return.* Kwa hiyo, tukubaline na uhalisia, tujipange kama Taifa tuweze kusonga mbele. Ukiangalia pia hata aliyeondoka hatuwezi kusema hakuwa sahihi kwa sababu tunafahamu umuhimu wa miundombinu yetu kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, ndugu zangu sisi *politicians* wakati mwingine *we have to be realistic* kwa manufaa mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Mwakibete amezungumza vizuri sana ni wakati sahihi vilevile tuone namna ya kuwa na Benki za Wakandarasi nchini kama vile *China Construction Bank* zipo, kwa sababu ukiangalia mkandarasi mmoja anaweza akawa na ile *annual turnover* (ule mzunguko wa mwaka) wa takribani kama bilioni mbili au tatu. Ukichukua hiyo 40% tu ya wakandarasi waliokuwepo wakiwa wanapita kwenye benki fulani moja, maana yake hiyo benki ina uwezo wa kujizungusha vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tuone namna ya kutengeneza utaratibu huu kwa manufaa mapana, siyo kwa wakandarasi bali kwa Taifa letu, kwa sababu wanaajiri vijana wengi na vijana wengi wanaotoka vyuoni wanapata ajira kupitia wakandarasi. Ni huu umuhimu wa *private sector* katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tangu mwaka 2013 – 2023, zaidi ya shilingi trilioni 61.6 zimetumika katika miradi ya ujenzi ndani ya miaka 10 lakini tumekuwa na hizo kilometa za lami tulizokuwa nazo. Kwa hiyo, ni wazi kwamba kupitia sekta ya ujenzi ni sekta ambayo kama Taifa tukiwekeza vizuri tunaweza kupiga hatua kwa sababu mzunguko wake ni mkubwa na bado kama Taifa tunahitaji kupanua miundombinu yetu kwa mustakabali mpana wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumekuwa na shida ya Wahandishi wa Udongo *(Geotechnical Engineers)* na kwa kuwa Wizara hii ndiyo Wizara Mama ya Wahandisi na Bodi ya Wahandisi iko chini ya Wizara hii, ninaiomba sana Serikali ione namna ya kuhakikisha wanafanya jitihada za maksudi kuhakiksha tunaongeza Wahandisi wa Udongo *(Geotechnical Engineers)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafikiri utakuwa umeona kule Kigoma barabara ilivyokuwa imekatika na kule Pwani barabara ilivyokuwa imekatika, kama tutakuwa na *Geo Technical Engineers* wa kutosha nchini lile tatizo mimi nina uhakika lingeweza kuepukika, kwa sababu teknolojia zipo za kuhakikisha tunaboresha *layer* ya chini ya udongo, ile *sub-grade layer* ili kuhakikisha wakati wote inakuwa na nguvu inayohitajika kuhakikisha hayatokei matatizo kama yale katika barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Bagamoyo – Msata ilipojengwa, changamoto kama ile iliwahi kutokea, *cracks* kwenye barabara zile na ipo nja sahihi ambayo ilitumika kuboresha kuboresha barabara ya Bagamoyo – Msata na mpaka leo tunaiona ipo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninamaliza kwa kusema kwamba, tuone haja ya kuhakikisha tunaongeza nguvu, Wahandisi wengi wa Udongo wanatoka nchi za nje, wanaofanya kazi Tanzania, wanalipwa shilingi milioni 10 kwenye miradi, Watanzania tunaweza pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na mimi kwa kunipatia muda niweze kusema machache kwenye Wizara hii. Mimi ninaomba nianze kwenye ukurasa wa 35, barabara za *EPC + F*.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ziko nyingi hapa lakini ninaomba niisemee barabara hii ya kutoka Olboroti – Mrijo mpaka Kwamtoro, kuunganisha na Singida. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa anatuambia Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimeingia Bungeni hapa mwaka 2015. Bajeti ya kwanza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi niliichangia mwaka 2016. Tangu mwaka 2016 ninachangia bajeti hii, ninauliza maswali ya msingi. Ahadi ni kila leo kwamba barabara hii itajengwa, barabara hii itajengwa. Mwaka jana tukaambiwa barabara hii sasa inakwenda kujengwa kutoka kwenye Serikali

Kuu kwenye mapato yetu, tunaenda kupata fedha za kwenda kuijenga hii barabara yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022 walituambia wanaanza kujenga kipande kipande kuanzia Kibirashi. Tukaambiwa safari hii barabara hii inaenda kujengwa yote kwa mfumo wa *EPC*. Kibaya zaidi mwaka jana tumesaini mikataba kwa ajili ya ujenzi wa hizi Barabara, lakini leo kwenye andiko la Waziri anatuambia kwamba wao bado wako kwenye mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninajiuliza, haya mazungumzo mpaka tunafikia kusaini mikataba, ina maana tulianza kusaini mikataba kabla ya mazungumzo? Ni kweli Serikali tulikuwa hatujui nini tunachokifanya? Kwa sababu mpaka tunafikia hatua ya kusaini, tumeshakubaliana na hawa watu tumejua gharama ni kiasi gani, watafanyaje kazi, kusaini ni kitendo cha mwisho kwamba umesharidhia kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, leo inakuaje Serikali mnarudi kinyumenyume mnatuambia kwamba mko kwenye mazungumzo, tena mapya? Kama hamjengi hizi barabara tuambieni. Wilaya ya Chemba tuna kama 26, ni Kata tatu tu ndiyo zinazopitiwa na lami, Kata 23 hazina lami! Wilaya ile ndiyo inayolima leo, wakulima wake wanasota wanahenya kwa kuuza mazao yao kwa bei ya chini kwa sababu hawana barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wakinamama wanajifungulia barabarani kwa sababu hawana barabara ya kuwafikisha hospitalini. Watu wanakufa kwenye madaraja, maporomoko huko, mitaro iko ya ajabu kwa sababu hakuna Barabara, watoto wanafia kwenye maji wakivuka vivuko. Mheshimiwa Bashungwa umeenda ukafika na ukatupatia ahadi ukatuambia unapeleka hela kwa ajili ya kujenga lile daraja la Kelema, leo unakuja kutuambia *story* hapa! Kwani mnatuchukuliaje? Yaani mnatuonaje kwa mfano? Kwamba kuna watu *special* sana katika Taifa hili na wengine hatustahili kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani watu wa Wilaya ya Chemba leo kuanzia mwezi wa 12 mpaka mwezi wa tano wao wanahangaika na maporomoko ya maji, wanakesha barabarani magari yamekwama. Kiangazi hiki leo wanahangaika tena na hii mitaro, ni kupanda na kushuka, rasta za kutosha, wakifika wanasafiri wanakotoka, hata wakija tu hapa Mjini mpaka wakifika hapa wamepauka kama nyani. Ni kwa nini mnatuchukulia sisi watu wa Wilaya ile kwa namna hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninataka tu kumwambia dada yangu ambaye anachangia vizuri na ninamwelewa sana lakini ninataka kumhakikishia kwamba hakuna mtu mwenye utu na mchapakazi na *humble* kama Waziri wa Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie tu, hapa juzi mmetuuliza swali la kipindupindu, *the corner stone* ya kusababisha ni pamoja na mafuriko, majanga ya *El Nino* na leo hakuna kipindupindu na magonjwa, ni kwa sababu saa zote Mheshimiwa Bashungwa yuko *site* na anahakikisha nchi inafunguka. Mimi ninachokuomba tumvumilie, mimi nina hakika hayo unayoyasema yatafanyika kwa aina ya mtu tulienae hapo mbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa. Wema, u-*innocent* wake na jina lake ni kwake yeye Mheshimiwa Dkt. Mollel, siyo kwa wananchi wa Wilaya ya Chemba na Mkoa wa Dodoma. Watoto wanaokufa, juzi mvua za mwezi wa pili, kwenye Daraja la Songolo watoto watatu wamesombwa na maji, wewe unaniambia kwamba yeye ni mtu mwema? Ingekuwa ni

mtoto wako Mheshimiwa Mollel kafa pale, kwa nini mnachukulia hivi vitu *simple* kiasi hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani ni kwa sababu gani haya mambo yanatendeka kwa watu wengine, kwa nini? Mheshimiwa Waziri umefika umeona na ulishuhudia, wamama wa Wilaya ya Chemba Kata ya Mondo, Kijiji cha Kelemasimba walipiga magoti na kukushika kichwa na kukuvisha ushanga, wakakuomba uwasaidie daraja lile linalowauwa wakina mama na watoto wao wanakwenda shule, mpaka leo hujafanya jambo! Ukija hapa wameniambia wanatamani kusikia, ni lini fedha ulizoziahidi zinakwenda kujenga lile daraja? Lakini wananchi wa Chemba wameniomba nije nikukumbushe kwamba, ulizungumzia pia suala zima la barabara hii ya kutoka Kibirachi, wanataka kujua barabara hii inajengwa ama haijengwi ili wajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, barabara hii pia imewarudisha nyuma wananchi wa Wilaya ya Chemba zaidi ya Kata 13 ambao wanapitiwa na mradi huu. Mliwawekea X leo ni mwaka wa 29 hamjawalipa fidia hamjafanya chochote na mmewazuia kuendeleza maeneo yao. Wako pale kimya hawana chochote wanachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaomba kujua leo kupitia sauti yangu, ni lini mnakwenda kuwalipa fidia? Kama hamuwalipi wamesema wanataka tamko la Serikali. Waambieni waendeleze maeneo yao ili waachane na hadithi hizi za kwenda kuwajengea barabara ambayo ni hadithi za abunuwasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, Ludewa haijafikiwa hadi makao makuu ya Wilaya kwa kiwango cha lami. Tunaomba sehemu ya Mawengi Ludewa ifanyiwe kazi mapema.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mkiu-Liganga na ile ya Liganga kwenda Mchuchuma ziwekwe kwenye mjadala wa uwekezaji wa Liganga na Mchuchuma na mwekezaji atoe fedha ili barabara hizi zijengwe haraka ili kurahisisha shughuli za uchukuzi na usafirishaji.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa (Mb) kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA),* Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* na taasisi nyingine chini ya Wizara hii kwa namna wanafanya kazi. Aidha, nimeshindwa kujizuia kumpongeza kwa dhati Mtendaji Mkuu wa *TARURA,* Mhandisi Victor H. Seff, Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Simiyu, Mhandisi Boniface Mkumbo, Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Simiyu, Mhandisi Gaston Pascal na Meneja wa Wilaya ya Meatu, Mhandisi Elieza Mayengo kwa namna wanavyosimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja katika Jimbo la Kisesa na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kiujumla na nianze na miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja yaliyokamilika miaka ya nyuma kurejewa kwenye hotuba ya Waziri ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Ibara ya 18 na baadhi ya Ibara zingine imeorodhesha miradi mingi ya barabara na madaraja yaliyokamilika miaka ya nyuma na kuanza kutumika na hivyo siyo sehemu ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/2024 na mipango ya bajeti ya 2024/2025. Nini sababu za Waziri kurejea miradi iliyokamilika tangu mwaka 2021 kwenye hotuba ya bajeti yake?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Bariadi-Kisesa-Mwandoya –Ngh’oboko kilometa 102; barabara hii kwa muda mrefu imekuwa ikiripotiwa iko kwenye

hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na tulitegemea leo tutaambiwa hatua ya awali imekamilika na ujenzi umeanza, lakini cha kusikitisha hotuba ya Waziri Ibara ya 131(c)(viii) ukurasa wa 73 inaeleza kuwa Serikali ipo katika taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ipo kwenye ahadi zilizotolewa na viongozi wakuu wa kitaifa na katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020. Waziri atuambie, je, ni nini kinachosababisha Serikali kuwapiga danadana wananchi wa Jimbo la Kisesa na Mkoa wa Simiyu kuhusu barabara yao hiyo ya lami?

Mheshimiwa Spika, miradi mingi imeorodheshwa ikiwa haina kasma ya Bajeti, kwa mfano Barabara ya Kolandoto-Lalago-Sanga Itinje-Ng'ohobokoMwanhuzi kilometa 122 na miradi mingi ya barabara na madaraja imeorodheshwa na Serikali, lakini haijatengewa fedha hali inayopelekea matumaini hewa kwa wananchi. Utaratibu mzuri wa mipango miradi inayoorodheshwa ni ile iliyopangiwa fedha katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege; hotuba ya Waziri Ibara ya 20 ukurasa wa 19 anaripoti viwanja vya ndege ambavyo vilishajengwa miaka mingi iliyopita na kuanza kutumika. Nini sababu ya Waziri kurejea kutaja majina ya viwanja hivyo?

Kuhusu barabara za michepuo hotuba ya Waziri imeonesha orodha ndefu ya miradi ya ujenzi wa barabara za michepuo zinazofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili baadaye zijengwe kwa lengo la kupunguza msongamano katika miji mbalimbali nchini. Nimepitia miradi hiyo mingi haina ulazima kwa sasa na Serikali isiondoke kwenye jukumu la msingi la kupeleka barabara za lami maeneo mengine ambayo hayajafikiwa, haiwezekani tukaanza kuweka vipaumbele vya barabara za michepuo na kuwaacha Watanzania wengine wakiwa na shida ya barabara za lami kwa miaka mingi. Waziri wa Ujenzi awe

makini na mipango ya aina hii ambayo inaweza kuwa ni sehemu ya kufuja fedha za umma na kufanya upendeleo katika ugawaji wa raslimali za nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zilizoombwa; fedha za maendeleo zinazoombwa ni shilingi trilioni 1.628 ikiwa ni ongezeko la 14.88% ya bajeti ya mwaka 2023/2024 ambapo pia ongezeko hilo ni fedha za kutoka nje. Miradi mingi imetajwa katika hotuba ya Waziri lakini haina kasma ya fedha na miradi mingi ni ahadi za muda mrefu, Kamati kwa kuliona hilo imeomba bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo iongezwe hadi kufikia shilingi trilioni tano ili kuwezesha ujenzi wa viwanja vya ndege, barabara na madaraja kote nchini, lakini pia kuna miradi hewa ya *EPC+F*.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tuungane na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini tuikatae bajeti hii na tuirudishe Serikalini ikafumuliwe na kuandaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba ya ujenzi wa barabara kwa utaratibu wa *EPC+F;* tarehe 16 Juni, 2023 Serikali ilisaini mikataba saba ya ujenzi wa miradi saba ya barabara zenye jumla ya kilometa 2,035 kwa gharama ya shilingi trilioni 3.75 kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F)* na kama pia ilivyoelezwa katika hotuba ya Waziri miradi hiyo ni kama ifuatavyo; Mafinga-Mtwango-Mgololo (kilometa 81); Igawa-Songwe-Tunduma (kilometa 218); Uyole-Songwe (kilometa 48.9); Masasi-Nachingwea-Liwale (kilometa 175); Arusha-Kibaya-Kongwa JCT (kilometa 453.42); Ifakara-Lupiro-Malinyi-Kilosa,Kwampepo-Londo-Lumecha/Songea (kilometa 435); Karatu – Mbulu - Haydom-SibitiRiver-Lalago-Maswa(Simiyu) (kilometa 339); na Handeni-Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti - Mrijochini-Chambalo- Chemba - Kwa Mtoro - Singida (kilometa 374.24).

Mheshimiwa Spika, tangu kusainiwa kwa mikataba hii leo ni takribani mwaka mzima umepita ujenzi haujaanza, aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa

na Waziri wa Ujenzi wa sasa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa walikuwa wakieleza kuwa wakandarasi bado wanafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na baadaye maelezo yakabadilika kuwa Serikali inatafuta fedha za kuwalipa wakandarasi malipo ya awali 10% ya thamani ya mradi kiasi cha shilingi bilioni 375.51 ndiyo kazi iweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, awali siku ya kusaini mkataba huu ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tulishiriki tukio hilo nilipinga wasilisho la Waziri la kuitambulisha miradi hiyo kwa kuwa hapakuwa na maelezo ya kina. Miradi hiyo inatekelezwa kwa utaratibu upi kwani masharti na vigezo vya mikataba hiyo havikuwekwa wazi, ilikuwa ni siri kati ya Waziri na wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, siku ya kusaini mikataba na ndani ya Bunge nilihoji nini faida ya kutumia *EPC+F* badala ya utaratibu wa kawaida wa Serikali kuajiri na kulipa wakandarasi, wakandarasi wa *EPC+F* watalipwa kwa utaratibu gani baada ya miradi kukamilika au kwa kipindi gani? Na kwa kuwa huu ni mkopo kwa nini tunapanua dirisha la ukopaji fedha nje ya utaratibu uliowekwa? Ulinzi wa ajira za vijana nchini utalindwaje katika miradi ya aina hii? Na kwa kuwa miradi hii wakandarasi watatumia fedha zao, nafasi ya *CAG* na Bunge itakuwaje katika utekelezaji wa miradi hiyo? Kwa kiufupi maswali haya hayakupata majawabu hadi leo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2022/2023 imethibitika kuwa mikataba hii ilisainiwa bila kuwa na ufadhili wa uhakika wa miradi hiyo na wakandarasi wameshindwa kuwasilisha dhamana ya benki ya utendaji kazi yenye thamani ya shilingi bilioni 375.51 kama matakwa ya mkataba na ndiyo sababu ya miradi hii kushindwa kuanza hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, hawa wakandarasi walipatikanaje hadi wakasaini mikataba wakiwa hawana sifa na uwezo wa kifedha? Mkataba wa *EPC+F* uliwezaje kusainiwa bila kujiridhisha na masuala ya msingi ikiwemo ufadhili wa fedha za mradi? Hapa

kuna kila dalili ya harufu ya rushwa na Taifa letu kuingizwa kwenye nikataba ya kinyonyaji.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amekuwa akitumia nguvu kubwa kulipotosha Bunge na umma wa Watanzania kwa makusudi kuhusu faida za miradi ya *EPC+F* na akituita baadhi ya Wabunge tuliohoji mikataba hii kuwa ni wapotoshaji na tuna nia mbaya. Pia Waziri Mbarawa alikiri kwamba hata alipowashirikisha *TANROADS* walipinga utaratibu wa *EPC+F,* lakini yeye akatumia madaraka yake kulazimisha utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia gharama kubwa kuandaa miradi hewa na kupeleka ahadi hewa kwa wananchi wa maeneo yaliyotajwa na mbaya zaidi wananchi wa mikoa inayopitiwa na miradi saba ya barabara wameondolewa kwenye mipango na bajeti ya mwaka 2023/2024 na 2024/2025 kwa kuwa barabara zao zitajengwa kupitia utaratibu wa *EPC+F*.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inakiri kwamba hakuna kinachoendelea katika miradi ya *EPC+F,* hotuba ya Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Innocent Bashungwa katika Ibara ya 40 ukurasa wa 36 anakiri kuwa miradi hiyo haina chanzo cha fedha na bado haijaanza na kwamba Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za kutekeleza miradi hiyo. Miradi tuliyoambiwa ina ufadhili wa moja kwa moja yaani mkandarasi anayejenga atatumia fedha zake na baadaye kuidai Serikali, leo tunaambiwa anatafutwa mfadhili wa kugharamia miradi hiyo. Hii inaleta sintofahamu na mkanganyiko mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa utapeli huu wa kuajiri wakandarasi wasio na uwezo wa kutekeleza miradi ya *EPC+F,* kupeleka ahadi hewa kwa wananchi na kutumia fedha za umma nje ya utaratibu uliowekwa, Waziri Mbarawa aliendelea kulihadaa Bunge kuwa uchelewaji wa kuanza miradi umesababishwa na wakandarasi kufanya *detailed design* na kwamba wanasubiri malipo ya awali ya 10% kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ni Tanzania pekee Waziri aliyeyafanya haya Profesa Mbarawa anaweza kuwa kwenye ofisi za umma mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, nashauri mikataba yote ya *EPC+F* ivunjwe na miradi hiyo ifutwe kwenye vitabu vya Serikali. Pia bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2024/2025 irudishwe na ifumuliwe upya ili kuwezesha majimbo, wilaya na mikoa iliyokuwa imeingizwa kwenye miradi hewa ya *EPC+F* ipangiwe upya fedha katika ugawanaji wa keki ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Waziri Profesa Mbarawa ameichonganisha Serikali na Mheshimiwa Rais mbele ya wananchi, amekichonganisha Chama Cha Mapinduzi na wananchi kwa ahadi hewa ya ujenzi wa barabara kilometa 2,035, na kwa kuwa kuna dalili na harufu ya rushwa, vyombo vya uchunguzi TAKUKURU, *DCI* na *DPP* wachukue hatua kwa Profesa Mbarawa na wote waliohusika kwenye kashfa hii, kwa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi na kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya barabara na madaraja ya *PPP;* maelezo yaliyotolewa katika hotuba ya Waziri katika Ibara ya 215 ya hotuba kuhusu utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara *(express way)* kwa utaratibu wa *PPP* ni maelezo hayo hayo yaliyotolewa mwaka jana na Profesa Makame Mbarawa aliyekuwa Waziri wa Ujenzi ambapo iliahidi kuwa mikataba ingekuwa imesainiwa kufikia Juni, 2023 na kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukihoji sana suala hili hapa Bungeni lakini hatupati majibu kutoka Serikalini, binafsi nimehoji kwa kusema na kwa michango ya maandishi ya mara kwa mara bila majibu, Serikali inawezaje kuanzisha mchakato unaohusu kutwaa au kutumia ardhi ya umma bila kibali cha Bunge, hifadhi ya barabara tuliyonayo ni mali ya umma kwa matumizi ya umma, Wizara ya Ujenzi haina mamlaka ya kukabidhi maeneo ya hifadhi za barabara kwa mwekezaji wa sekta binafsi bila kibali cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuna mkanganyiko mkubwa wa mipango ya Serikali na pengine huoni kama kuna nia njema kwani huwezi kuja na mradi wa ujenzi wa barabara ya kulipia kutoka Kibaha-Chalinze-Morogoro-Dodoma *(express way)* yenye urefu wa kilometa 531.8 kwa utaratibu wa *PPP* huku kuna mradi mkubwa wa *SGR* ambao uko hatua za mwisho kukamilika na utaanza kutoa huduma Julai, 2024. Mradi huu unatarajiwa kupunguza msongamano wa magari barabarani kwa zaidi ya 60%. Hii ni mipango mibovu na matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa nchi zilizojenga barabara za kulipia huacha kwa makusudi kukarabati njia mbadala ili wananchi walazimike kupita katika barabara za kulipia, lakini pia makampuni ya ubia yamekuwa yakiweka bei kubwa za tozo na kusababisha gharama za usafiri na usafirishaji kuwa juu na hivyo kuchochea mfumuko wa bei za bidhaa na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, kama nchi tumejipangaje kabla ya kuiendea miradi ya namna hii? Ikumbukwe kuwa barabara hii inatoka kwenye lango kuu la uchumi wa nchi yetu yaani Bandari ya Dar es Salaam kwenda kwenye mikoa na mataifa mbalimbali ya nchi jirani. Mchakato unaoendelea wa kumpata mkandarasi ni kinyume cha Sheria ya Ardhi na Sheria ya Rasilimali inayotaka hatua zote kuwa wazi na Bunge kujulishwa.

Mheshimiwa Spika, leo Waziri atuambie ukweli juu ya faida ya mradi huu, nchi yetu imejenga na imeunganisha mikoa yote kwa barabara za kiwango cha lami, tumejenga mtandao mkubwa wa *SGR*, leo hatuna fedha za kujenga njia nne kutoka Kibaha-Chalinze-Morogoro hadi Dodoma? Au kuna jambo lililojificha nyuma ya pazia kwenye miradi hii ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, tulishaanza safari ya upanuzi wa barabara ya kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo ujenzi wa barabara wa njia nane umeshakamilika kutoka Kimara hadi Kibaha na hivyo tunaweza kuendelea kutenga bajeti kwa awamu

hadi Chalinze na baadaye Morogoro na Dodoma ikizingatiwa kuwa miradi mingi ya kimkakati iliyokuwa inachukua fedha nyingi inakamilika ya Bwawa la Nyerere, Daraja la JPM (Kigongo Busisi) na *SGR*. Tume ya Mipango iko wapi hadi mipango mibovu kama hii kuendelea kwenye nchi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine inayoainishwa kutekelezwa kwa njia ya *PPP* haina tija na inaweza kusababisha hasara kubwa mfano Daraja la Pili la Kigamboni (Magogoni - Kivukoni). Daraja hili linapendekezwa kujengwa wakati tunalo Daraja la Nyerere (Kigamboni) lilojengwa na Mfuko wa *NSSF* hivyo kujengwa daraja lingine la kulipia litaua biashara ya daraja lililopo na kushindwa kurejesha mtaji wa uwekezaji wa shirika hilo, lakini pia eneo linalopendekezwa kujengwa daraja la pili kuingilia meli katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifute michakato inayoendelea wa kutafuta mkandarasi wa kujenga mradi wa barabara ya kulipia kutoka Kibaha hadi Dodoma kwa utaratibu wa *PPP* na badala yake ifanye tathmini upya kubaini maeneo na miradi yenye faida kiuchumi kutekelezwa kwa utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Innocent Bashungwa anashauriwa kuwa makini katika uandaaji wa bajeti na kuepuka kurudia miradi iliyokwishatekelezwa miaka ya nyuma, kutokuorodhesha miradi ambayo haina kasma ya fedha na kujiepusha kuanzisha miradi isiyo na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona mipango mibovu kiasi hiki wakati tuna Tume ya Mipango, Wizara inayotekeleza miradi mikubwa ya madaraja, barabara za lami na changarawe, viwanja vya ndege na vivuko kutengewa fedha ndogo kiasi cha shilingi trilioni 1.6 tu huku miradi mingi ya kimkakati iliyokuwa inachukua fedha nyingi imekamilika na mingine iko hatua za mwisho kukamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, ifahamike kuwa mipango mibovu inaliangamiza Taifa letu kwa kiasi kikubwa, hivyo kupitia Tume ya

Mipango ni lazima kufuatilia upya na kuongeza fedha katika Wizara hii na miradi yote isiyo na tija ifutwe katika vitabu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ni mepesi hayahitaji hesabu ngumu, ni rahisi mno, *it does not need hot calculations to do it like calculus, statistics, combination and permutation, it is a low hanging fruit*. Ni lazima mipango yetu iwe ya wazi na uwajibikaji katika kuliletea Taifa letu maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara. Nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika uchangiaji wangu naomba kujikita katika eneo moja tu ambalo kwa utafiti na ufuatiliaji wangu nimeona kuna changamoto kubwa. Eneo ambalo nataka kuchangia ni kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)*.

Mheshimiwa Spika, Wakala huyu anakabiliwa na changamoto kadhaa zinazoweza kuathiri ufanisi wake na utoaji wa huduma bora na hapa nimeainisha baadhi ya changamoto kuu ambazo *TEMESA* inakumbana nazo ambayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu wa rasilimalifedha; *TEMESA* inakabiliwa na upungufu wa fedha za kuendesha shughuli za kila siku, kufanya matengenezo ya vifaa na kuboresha miundombinu. Hali hii imekuwa ikiathiri utendaji kazi wa taasisi na kuleta malalamiko kwa wadau ambao ni taasisi za Serikali. Ikumbukwe kuwa ukosefu

wa bajeti ya kutosha kutoka Serikalini unakwamisha utekelezaji wa miradi mikubwa na muhimu. Hivyo, ninaitaka Wizara kuangalia namna kuongeza fedha katika taasisi hii.

(ii) Vifaa na vitendea kazi vya kisasa; wakala huu pamoja na umuhimu kwa Serikali bado anakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa na vya kutosha kwa ajili ya matengenezo na ufundi. Hali hii kwa ujumla wake inarudisha nyuma ndoto na mipango ya taasisi.

(iii) Rasilimali watu; upungufu wa wataalamu wenye ujuzi na uzoefu unaohitajika kwa huduma bora. Changamoto nyingine inaendelea kuumiza taasisi hii ni ukosefu wa wataalamu wenye ujuzi na maarifa kulingana na mahitaji ya sasa. Hali hii imefanya baadhi matengenezo ya magari na mitambo kuchukua muda mrefu kwa sababu ya kutegemea makampuni binafsi hasa katika utambuzi wa matatizo ya magari na kutatua. Ili taasisi hii iweze kujitegemea na kutekeleza majukumu yake ipasavyo Serikali inapaswa kuhakikisha inaajiri wataalamu ambao wana sifa na uwezo.

(iv) Mikopo na madeni; utafiti niliofanya unaonesha kuwa *TEMESA* inakumbana na changamoto za kudhibiti mikopo na madeni ambayo inaweza kuathiri uwezo wake wa kujiendesha. *TEMESA* inadai taasisi za umma kiasi kikubwa cha fedha zilizotokana na matengenezo ya magari na mitambo. Kucheleweshwa kwa fedha hizi kunaathiri mwenendo wa taasisi kutekeleza majukumu yake.

(v) Utaratibu mbovu wa kazi na urasimu unaochelewesha utoaji wa huduma kwa wakati; Wakala anakabiliwa na changamoto ya matumizi ya kisasa ya mifumo ya kiteknolojia katika kufanya kazi zake. Matumizi duni ya teknolojia mpya na za kisasa katika kutoa huduma za ufundi na umeme imefanya kazi nyingi za Wakala kuchukua muda mrefu kukamilika na kuleta malalamiko kwa wadau. Kutokana na hali hiyo, yapo malalamiko juu ya ubora wa huduma zinazotolewa ikiwa ni pamoja na muda wa kukamilisha matengenezo na kiwango cha matengenezo hayo.

(vi) Wakala kukosa mikakati ya kibiashara; taarifa za Wakala zinaonesha wazi kwa namna gani Wakala amekosa mikakati ya kibiashara ili kuhimili ushindani na kuongeza mapato yake. Hali hii imefanya Wakala kujiendesha kwa hasara ikilinganishwa na washindani wake katika soko.

(vii) Miundombinu na mazingira duni ya kazi; Kamati ya Bunge ya Miundombinu imetembelea na kukagua baadhi ya miundombinu ya Wakala na kubainisha mazingira yasiyoridhisha kama vile karakana za matengenezo na ofisi ambayo inaweza kuathiri ubora wa kazi. Aidha, mazingira ya kazi kwa watumishi ni duni kiasi cha kuathiri afya na usalama wa wafanyakazi. Kutokana na chagamoto hizi nashauri hatua zifuatazo kuchukuliwa na Wizara:-

(a) Kuhakikisha bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli na uwekezaji wa vifaa na teknolojia mpya;

(b) Mafunzo na maendeleo; kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi;

(c) Ufanisi wa usimamizi; kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji wa wakala; na

(d) Kuboresha mawasiliano na ushirikiano na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, *TEMESA* inahitaji mikakati madhubuti na jitihada za pamoja ili kukabiliana na changamoto hizi na kuboresha utoaji wa huduma zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Njombe - Songea imeharibika vibaya, barabara ilijengwa zamani na Kampuni ya *Buffer Beat* ya Marekani ambao walijenga kwa

kiwango. Sasa hivi barabara inahitaji siyo ukarabati bali ujenzi uanze upya.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Songea - Tunduru imejengwa na ina umri wa miaka karibu sita, leo hii ukienda barabara imekwishabomoka kwa sababu ya magari makubwa ya mkaa wa mawe. Barabara zinajengwa kwa kufuata *design* zinazowekwa, lakini magari yanaruhusiwa kupita na uzito wa ajabu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa reli Mtwara-*Mbamba Bay* unasuasua mno, ni ahadi tu, hii inasababisha barabara itumike hovyo. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inabidi wakae pamoja ili kunusuru na kuzuia upotevu wa fedha za ukarabati. Wakati mwingine ni hujuma au kitu gani ili wenye magari labda waendelee kufaidika na reli isijengwe kwa ajili ya usafiri. Barabara zitazidi kubomoka kama Serikali haitakuwa makini kwenye kusimamia matumizi mazuri ya barabara. Tunahitaji reli Kusini ili kuokoa barabara zetu.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya ya kuweza kuwepo kwenye Bunge lako Tukufu. Naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu na baada ya kuunga mkono hoja naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walio chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Rukwa Mhandisi Mwanga kwa

kazi kubwa anayoifanya ndani ya mkoa wetu, hakika mwanamama huyu amekuwa msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo machache kama ifuatavyo nikianza na suala la kumlipa kwa wakati mkandarasi anayejenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Matai kwenda *Kasesya Border* ambayo ni barabara muhimu sana kiuchumi kwa Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla. Kukamilika kwa barabara hii itapunguza kwa kiasi kikubwa msongamano wa malori katika mpaka wa Tunduma na pia kwa wasafiri wanaoelekea nchi za Uganda, Burundi na Rwanda ikiwa ni pamoja na kuelekea mikoa yote ya Kanda ya Ziwa kwa kutokea nchi zote zilizo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kusaidia bandari yetu ya Dar es salaam kuwa na ufanisi na kupunguza msongamano katika mpaka wa Tunduma ni pamoja na kujenga kipande cha barabara kwa kuanzia Mji Mdogo wa Laela kwenda Mwimbi hadi kwenda kuunganisha barabara ya kwenda Kasesya kipande ambacho Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wametembelea na kujiridhisha na umhimu wa barabara hii kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pia kufanya marekebisho maeneo yaliyoharibika kutokana na mvua nyingi iliyonyesha katika Wilaya na Jimbo la Kalambo na hivyo kuharibu barabara nyingi na hasa zinazotumika kusafirisha mazao ya wananchi na hivyo kukosa bei yenye tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kwa heshima na taadhima kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Bashungwa kwa kazi kubwa wanayofanya katika kujenga na kuimarisha miundombinu hasa ya barabara katika mkoa wetu wa Iringa na nchi nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kwa kuendelea kuufungua Mji wa Iringa ambao ulikuwa haupitiki kutokana na kupitiwa na barabara kubwa mbili, yaani Mbeya-Dar es Salaam na Mbeya-Dodoma. Hii ilisababisha msongamano mkubwa Mjini Iringa, lakini ujenzi wa *Iringa Bypass* na ujenzi wa Daraja la Kitwiru - Isakalilo na Ipogolo - Kilolo. Hizi tunaomba zikamilike kwa kweli zitatoa changamoto kubwa sana ndani ya Mji wa Iringa. Ahsanteni sana!

Pili, ninaomba barabara ya Iringa - Pawaga ijengwe pia kama ambavyo tuliomba wakati wa ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, lakini pia imo kwenye Ilani kwa zaidi ya miaka 30. Aidha, tunashukuru kwa kilometa ambazo tumepewa kwa barabara hiyo. Barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi na usafari kwa majimbo yote matatu au Manispaa na Halmashauri ya Iringa Vijijini. Tunaomba hata kilometa tano kuanzia mjini, kwa sababu wananchi wa Kata ya Kiwele na Mkwawa wanapata shida sana hasa wanapofuata huduma za matibabu, shule mjini.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunaomba eneo la upande wa mto wa barabara ya Mbeya -Dar es Salaam, eneo la Iyofi zisifanyike shughuli za ujenzi au kilimo hatarishi, maeneo hayo yatunzwe ili kulinda hizo barabara, kwa mazingira yake hiyo barabara itamegeka.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, watendaji wote walio chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kutengeneza mitandao ya barabara na madaraja maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu changamoto za barabara zinazojengwa na *TANROADS* katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara ya Kiboriloni - Tsuduni - Kidia kwa kiwango cha lami.

Barabara hii inajengwa na *TANROADS* na bado haijakamilika. Tuliwahi kutembelea barabara hii na Kamati ya Siasa ya Wilaya baada ya chama kupokea malalamiko kwamba ujenzi ulikuwa umelegalega. Pamoja na maelekezo na ahadi kwamba ujenzi ungeendelea, hadi leo ujenzi umekwama na mkandarasi hajaonekana *site*.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu mbaya sana kwenye barabara hii na wananchi wanailaumu sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Uru - Kishumundu - Materuni inajengwa kwa kiwango cha lami. *TANROADS* inajenga barabara hii kwa niaba ya *TARURA*. Kero kubwa ni kwamba kasi ya ujenzi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Moshi Vijijini, Barabara ya Kwa Rafaeli - Mto Sere inahudumiwa na *TANROADS*. Wameshaweka mitaro katika baadhi ya maeneo, na haijajengwa hata kidogo kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu kwani ni sehemu ya kusafirisha watalii kwenda Mlima Kilimanjaro kupitia njia ya Umbwe.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibosho Shine - Kwa Rafaeli ilikuwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi toka mwaka 2005 na inajengwa na *TANROADS* lakini hadi leo haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Rau - Uru - Shimbwe yenye urefu wa zaidi ya kilometa 13 ilikuwa kwenye ahadi za viongozi wa Kitaifa kujengwa kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umeanza kwa kasi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya hapo juu, naishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaiomba Serikali itenge kiasi cha fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Kiboriloni - Kikarara - Tsuduni - Kidia kwa kiwango cha lami, kwani wananchi wanalalamika sana.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaishauri Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Uru - Kishumundu - Materuni.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaiomba Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha kwa kiwango cha lami kipande cha Barabara ya Kwa Rafaeli - Mto Sere. Vilevile ninaishauri Serikali ifikirie kujenga kwa kiwango cha lami kipande cha Sere hadi Geti la Umbwe la kupanda Mlima Kilimanjaro. Barabara hii ni mbovu mno pamoja na kwamba hutumika kusafirisha watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro kupitia njia ya Umbwe na kuiingizia Serikali kipato kupitia sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nne, ninaiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa Barabara ya Kibosho Shine - Kwa Rafaeli - *International School* kwa kiwango cha lami kama ilivyoanishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi toka mwaka 2005. Ujenzi wa barabara hii umechukua zaidi ya miaka 13.

Mheshimiwa Spika, tano, ninaishauri Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Rau - Uru - Shimbwe kwa kiwango cha lami yenye urefu wa zaidi ya kilometa 13 kama wananchi walivyoahidiwa na wagombea Urais wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri niliotoa hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa katika ujenzi wa barabara nchini ni fedha. Tunayo mahitaji mengi kuliko uwezo wetu kifedha na hasa uwezo wa ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu juu ya namna ya kupambana na hali hii hasa kwa kuongeza mapaato kwenye Mfuko wa Barabara:-

(i) Kuongeza tozo ya mafuta kutoka shilingi 263 ya mwaka 2013 na kupunguzwa hadi shilingi 158 ya sasa mpaka angalau shilingi 300 kwa lita ya petroli na dizeli;

(ii) Kurejesha tozo ya angalau shilingi 100 kwa kila laini moja ya simu kwa mwaka na angalau shilingi 50 kwa mwezi ili kuongeza urari kwenye mfuko;

(iii) Kuweka asilimia kidogo ya nyongeza kwenye *CIF* ili kupata fedha angalau kama ile ya reli;

(iv) Kutengeneza barabara za kimkakati kwa ushirikiano na sekta binafsi kwa kuweka *Road Tolls* na kuingia mikataba kama ile ya *EPC+F;* na

(v) *Infrastructure bond.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote ni muhimu sana kwa mapato husika kulindwa kisheria na Serikali kuweka *discipline* ya kukusanya na kulinda vyanzo husika na mapato yake.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Bashungwa ambaye ni Waziri mwenye dhamana ya Miundombinu, pamoja na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lushoto lina barabara za *TANROADS* mbili tu ambazo ni Magamba hadi Mlola kilometa 40 na kilometa sita a,bazo zimeshajengwa kwa lami, kwa hiyo bado kilometa 34 na hizi kilometa 34 zimeshaingizwa kwenye utaratibu wa kuanza kujengwa, lakini toka iingizwe kwenye mfumo wa kujengwa mwaka jana mpaka sasa bado haijatengewa fedha kwa ajili kujengwa kwa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaiomba Serikali katika kipindi hiki cha Bajeti itengewe fedha kwani barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, barabara ya kuanzia Nyasa Darajani kupitia Gare hadi Magamba ambayo ina kilometa 19 na hii ni barabara muhimu sana kwani ndiyo mkombozi hasa pale Barabara ya Magamba - Lushoto inapopata changamoto. Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana na ni ya changarawe kwa baadhi ya maeneo, niiombe Serikali kwa kipindi hiki cha bajeti barabara hii itengewa angalau kilometa kumi za lami ili zijengwe hasa kwenye maeneo korofi.

Mheshimiwa Spika, barabara yetu ya kuanzia Mombo kupitia Soni hadi Lushoto yenye urefu wa kilometa 32 barabara hii imekuwa nyembamba sana na kupelekea magari makubwa kupita kwa shida na kuongeza gharama za bidhaa madukani kuwa za ghali kwa sababu ya kupita magari ya tani kumi na changamoto hii nimeshaisemea hapa Bungeni kwa muda mrefu tangu mwaka 2016 kwa ajili ya kupanuliwa hasa kwenye zile kona.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa adha ya wananchi wangu wanayoendelea kuipata, sambamba na hayo naomba kwenye bajeti ya hii barabara hii itengewe fedha kwa ajili ya kuanza kutanua kona pamoja na kuongeza upana wa makalavati.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Meneja wa *TANROADS Engineer* Singano anafanya kazi kubwa mno. *Engineer* huyu halali, hata umpigie simu usiku, atapokea na kisha muda huo huo anatatua changamoto yako bila kusahau kuipongeza na timu yake pia wanafanya kazi kwa ushirikiano wa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kazi kubwa ya kuwatumikia Watanzania, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amebainisha ujenzi wa Barabara ya Handeni kwenda Mafuleta kilometa 20, mkandarasi huyu anafanya kazi kwa kusuasua sana, ipo haja asimamiwe kwa karibu Wana-Kilindi wanataka kipande kiishe kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi huyu pia Serikali imempa kujenga kipande cha Mafuleta had Kileguru kilometa 30, je, ni lini ataanza kujenga kipande hiki? Naomba Mheshimiwa Waziri kupata majibu leo.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kipindi cha mvua ya *El-Nino* iliharibika sana, hivyo ipo haja kipande chote kijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, niombe pia barabara ya Kibirashi – Songe - Kweluguru ifanyiwe ukarabati, nayo haipo sawa baada ya mvua zilizonyesha kupita kiwango.

Mheshimiwa Spika, mwisho ipo ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. Magufuli ya ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa tano, ni kilometa 0.9 tu zimejengwa Makao Makuu ya Wilaya, je, ni lini ahadi hii itakamilika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUAKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kupitia Wizara hii ya Miundombinu kwa kukamilika kwa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo madaraja, barabara pamoja na *SQR*.

Mheshimiwa Spika, aidha nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kusimamia miradi mbalimbali pia tumeona wakati

wa mafuriko namna mlivyojitoa kufika katika maeneo yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara hii lazima kuongeza kipaumbele kwa makandarasi wa kike pamoja na vijana, hii itasaidia kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Wizara kushughulikia alama za barabara kuepusha ajali.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuimarisha sekta hii ya ujenzi kwa kuimarisha miundombinu mbalimbali ikiwemo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, aidha nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kusimamia na kutekeleza vyema majukumu yao ambayo yanaleta matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa imefanyika katika kuendeleza Mradi wa *SGR,* kujenga madaraja ndani ya wilaya, lakini pia kazi kubwa imefanyika katika kujenga barabara mbalimbali, licha ya kuwa miundombinu katika maeneo mengi yameharibika kutokana na mvua nyingi zilizonyesha.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara hii, kuangalia na kufikiria kwa umakini namna ya kujenga barabara na madaraja ambayo yataweza kudumu hata kama kutatokea mabadiliko ya hali ya hewa basi yaweze kubaki salama na kuepusha hasara kwa Serikali na kupunguza kero kwa wananchi.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kipenzi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kujenga nchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ujenzi na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja zangu. Kwanza naiomba Serikali kuwalipa fidia wananchi wa Tarafa ya Rulenge, Wilayani Ngara ambao walifanyiwa tathmini ili kupisha ujenzi wa barabara inayopita maeneo hayo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuna ahadi ya kipindi kirefu tangu Awamu ya Nne, Barabara ya Nyakahura – Murusagamba – Murugarama - Tembo Nickel hadi Rulenge. Naomba majibu ni lini ujenzi wa barabara hii ambayo ni ya muhimu sana kwa wananchi wa Ngara inayoleta uchumi katika wilaya yetu na mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba malipo ya wakandarasi yapewe kipaumbele kwa sababu wanategemea mikopo ya mabenki na wanapocheleweshewa malipo riba inazidi kupanda mwisho wa siku wanaishia kufa na *pressure* kwa sababu ya madeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe na Mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nichangie. Jambo la kwanza ninaunga mkono hoja ambayo imewekwa mezani. Jambo la pili, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge tunajadili bajeti ya Wizara ya Ujenzi katika kipindi ambacho barabara zimeharibiwa sana na mvua ambazo zimeendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Wabunge kwa kuwa wameitendea haki bajeti hii. Wamewatendea haki Watanzania kwa sababu wamejadili wameonesha uhitaji wa kuzirekebisha

barabara hizo, ndiyo maana ninaipenda CCM kwa sababu inaleta viongozi wanaojali masilahi ya Watanzania na hiyo ndiyo sifa kubwa ya Chama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali tumepokea hoja hizi ambazo Wabunge wamezisema na kwa ajili ya muda sitaenda kwenye hoja nyingi. Moja imeongelewa nyongeza ya bajeti, hata Serikali tunaiona bajeti hiyo na tunauona uhitaji huo. Uhitaji haupo tu kwenye nyongeza ya ukubwa wa bajeti, kuna uhitaji wa bajeti ambayo inahitaji marekebisho tu ya barabara ambazo zimeharibika. Tunalifanyia kazi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea tunatarajia tutakapokuja kwenye Bajeti Kuu tutatoa tamko kuhusu bajeti ya dharura mahsusi kuhusu kurejesha barabara zilizoharibika na tulivyokaa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi wametuambia, kwa upande wa ujenzi tu inahitajika takribani shilingi bilioni 700 mpaka shilingi trilioni moja, kwa upande wa barabara za ujenzi, kwa upande wa *TARURA* zinahitajika takribani shilingi bilioni 300, kwa hiyo uhitaji huu Wizara ya Fedha tumeushapokea na tunaendelea kuongea na wadau wenzetu ili tuweze kupata fedha hizo ambazo zitakuwa mahsusi kwa ajili ya kurejesha miundombinu hii ambayo imeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ambao umefanyika kwenye miundombinu hii ni takribani shilingi trilioni 40. Serikali haiwezi ikaacha tu uwekezaji wa aina hiyo ukapotea hivi hivi. Kupoteza miundombinu hii ni kuangusha uchumi, hatuwezi tukaruhusu jambo la aina hiyo. Kwa hiyo, kipengele cha kwanza ambacho tunakifanyia na tutatoa tamko kinahusisha fedha ambazo zinahitaji kurejesha miundombinu iliyoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni nyongeza ambayo inazingatia chanzo kipya mahsusi. Tunao upande wa mahitaji na tunao upande wa upatikanaji wa fedha. Mmeongelea mahitaji na sisi tunafanyia kazi upande wa upatikanaji wa fedha. Hili nalo tutakuja na chanzo, tutaleta pendekezo, Bunge lako litupitishie pendekezo la chanzo kipya mahsusi ambacho tutaenda

kuongeza kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Tunaangalia uwezekano, ikiwezekana kianze kufanya kazi mwaka huu lakini miaka mingine kitumike kama chanzo cha kushughulikia masuala ya dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mimi ninamwonea huruma Mheshimiwa Waziri mwenzangu Mheshimiwa Bashungwa, anafika *site* barabara imeharibika wananchi wamekwama, anasema Waziri wa Fedha niletee fedha lakini fedha hizo ambazo zinatakiwa zipatikane kimsingi si za dharura, tunalazimika kukata kutoka maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, sasa hii ambayo imetokea na kwa kuwa imekuwa ikijirudia, itupe funzo kwamba tunahitaji chanzo ambacho kitakuwa kinajilimbikiza wakati wa amani, wakati wa dharura kiweze kutumika kwa ajili ya dharura. Kwa hiyo, hilo la lenyewe ni eneo lingine na tutakuja na pendekezo. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, mpitishieni Mheshimiwa Bashungwa bajeti yake lakini tutakuja kujadiliana kwenye bajeti ambayo itakuwa inaongelea vyanzo, tujadiliane vyanzo na mapendekezo mengine yote haya tumeyapokea na tutayajadili kwa upana tutakapokuwa tunajadiliana kuhusu *Finance Bill*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni *EPC+ F*, tuliongea vizuri kuhusu jambo hili la *EPC + F* na wala hatujakurupuka. Ni jambo ambalo hata kwenye reli tunafanya, ni hivyo hivyo na kwenye reli. Mkandarasi anakuja, anakuja *in pair*, anakuja na *financier* wake, anakuja na mtoa fedha ambaye watafanya naye kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya hivyo kwenye reli, *lot* ya Kwanza ilikuwa na mkandarasi na mtoa fedha na kwenyewe ilikuwa *EPC + F* lakini tulipofika hapa, ukianzia *Lot 3, Lot 4* na *Lot 5*, mkandarasi na mtoa fedha ni *Standard Chartered* pamoja na CCCC.

Mheshimiwa Spika, hata hiyo *Lot 3, Lot 4* na *Lot 5* alivyoenda sokoni amekutana na tatizo, yule mtafuta fedha ambaye

amesaini pamoja na mkandarasi amekutana na tatizo kwenye soko la fedha, yule *financier* wa mkandarasi amekutana na tatizo. Ndugu zangu ukiambiwa ni *EPC + F*, ile '*F*' siyo fedha za familia ni fedha za mabenki, uchumi wa dunia umeyumba, amekutana na shida kule. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, wanasema kwa nini tumesainiana mkataba, sasa angempata wapi *Financier* bila yeye kupata kazi kwanza? Ni lazima apate kazi na wanaleta *in pair*, wamekuja *in pair*. Tumeangalia *financial terms* zao ziko sawa. Kwa hiyo, mkandarasi amemleta *Standard Chartered Bank*, kwamba ndiyo atakaye-*mobilize*. Jamani, hizi kilometa zaidi ya 2,000 ni kama *lot* ya reli. Ni fedha nyingi, hizi hazitoki kwenye familia moja, zinatoka kwenye mabenki, tena siyo benki moja ni *syndication*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wameenda kule wenzetu yule *financier* ameenda kwenye dunia ambayo na sisi tunaishi hiyo, amekutana na shida ya fedha. Sasa tunafanyaje? Tumwambie lete za urithi wa Babu yako? Hapana! Atasubiri uchumi utengemae, atafanya *syndication* halafu ujenzi utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata sasa tulikwama kwama kwenye reli kwa sababu ya shida hiyo, wakati UVIKO iko juu sana, wakati masuala ya siasa zile za Russia na Ukraine yako juu sana lakini sasa hivi ameanza ku-*mobilize resources* hizo. Haya ndiyo mambo ya kiuchumi yanavyofanyika na kwa sababu ni soko la dunia limeharibika, siyo sisi tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninadhani hawa wenzetu wanaochangia wanatakiwa wamtie moyo Mheshimiwa Rais kwa *courage* yake kwamba, licha ya msukosuko wa uchumi duniani, alisema miradi iendelee. Nchi zingine kwa ajili ya sababu hiyo hiyo wame-*withdraw* miradi, wameacha kutekeleza miradi lakini sisi miradi yote imetekelezwa katika kipindi hicho hicho ambacho dunia iko kwenye msukosuko. Tumetekeleza katika kipindi hicho hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mwalimu Nyerere linakamilika, msukosuko tu ungetosha kusema hatuwezi kutekeleza bwawa kwa sababu soko la dunia la masuala ya kifedha limeharibika lakini Rais akasema hapana, hakuna mradi utakaosimama! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika moja malizia.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwenye reli hivyo hivyo. Sasa hivi imefika hapa na kule kwingine inaendelea na soko linaenda linafunguka, hata hili la barabara patakapoimarika huo ndiyo taratibu wa *EPC + F*.

Mheshimiwa Spika, sasa niambieni, kama tumesaini *EPC+ F*, ndiyo mkataba uliopo na soko limeharibika, ninyi mnashaurije? Kwamba tubadilishe tuende kuchukua kwenye bajeti ya Wizara ya Afya? Mnataka tukachukue kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu? Mnataka tukachukue kwenye bajeti ya Wizara ya Maji? Huu siyo utaratibu. Hautakuwa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao tumesainiana mikataba kuna siku wanaweza wakatushtaki, wakasema *no,* tulishaingia mkataba, ninyi mnataka kuchukua fedha kutoka kwenye bajeti ya afya huku tulishaingia mkataba au tulishaweka *lining* benki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninawaomba Waheshimiwa Wabunge ninawaomba, pana mambo ambayo ni ya dharura tunayafanya kwa dharura, pana mambo ambayo ni ya kidunia na sisi tunaishi kwenye dunia hiyo hiyo inabidi tuyaelewe, lakini si nia mbaya ya Serikali kwenye jambo hili, si nia mbaya ya Serikali, Serikali nia yake ni hiyo hiyo njema na tutaendelea kukaa na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivi sasa hivi nimepokea barua, ninakaa nao wale watu wa *Standard Chartered*, inawezekana

watasema sasa hali inafunguka. Kwa hiyo, tuendelee nalo na tumuunge mkono Mheshimiwa Bashungwa bajeti yake ipite na tutaendelea kupeana taarifa katika mambo haya na yale yote ya madeni tunaendelea kulipa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ana sehemu kwenye bajeti yake na sehemu nyingine iko Mfuko Mkuu wa Serikali, hivyo ndivyo ambavyo huwa tunafanya.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha umesema hapo kitu kipya kuhusu kuanzisha Mfuko wa Dharura. Kifungu cha 39 cha Sheria yetu ya Bajeti, wakati mkiyatazama hayo kwa sababu umesema utakuja kuzungumza zaidi kwenye Bajeti Kuu, ukatazame kile Kifungu ili tujue huo Mfuko utakuwa tofauti na huu ama ni huu Mfuko ambao umetajwa kwenye Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, mtoa hoja ajiandae. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuunga hoja bajeti hii ambayo ipo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kuiletea maendeleo Tanzania na hasa jinsi anavyopigania miundombinu yetu kufanya iwe ni kati ya nchi zinazokuwa na miundombinu bora na mingi katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu. Nikushukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti ambao mnatuongoza vizuri sana katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Kamati ya Miundombinu chini ya Mheshimiwa Kakoso - Mwenyekiti wetu na Mheshimiwa Anne Kilango - Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote jinsi ambavyo wamekuwa wakitusimamia na kutupa miongozo. Nawashukuru sana Wabunge wote kwa michango yenu lakini pia kwa ushauri wenu na tunaahidi tu kwamba michango tutaichukua, ushauri tutauchukua na tutayatekeleza yote yale ambayo kwa kweli yanatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Ujenzi. Sina haja ya kueleza nini Mheshimiwa anafanya Wajumbe wameshaeleza, hongera sana Mheshimiwa. Sisi tunajivunia kuwa na wewe na tunaona jinsi Wizara inavyokwenda kasi. Kwa shukurani tu na mimi niishukuru familia yangu kwa kunipa ushirikiano mkubwa ili niweze kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu inasimamia taasisi kubwa tatu: *TANROADS, TBA* na *TEMESA*. Nitaanza na *TANROADS* na kwenye *TANROADS* naomba kwa kweli Wabunge na wananchi wa Tanzania tukubaliane kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa kujitolea kwake lakini na kujitoa kwake kukabiliana na changamoto kubwa ambalo lilikuwa ni janga kubwa ambalo kama nchi tumeweza kwa kweli kukabiliana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alitutahadharisha kama Serikali lakini na wananchi kupitia *TMA* kwamba kutakuwa na changamoto. Bahati nzuri alituandaa vizuri sana watu wa Serikali lakini pia na wananchi kwamba kutakuwa na janga. Changamoto ilikuwa ni kupima uzito huo utakuaje wa changamoto ambao nadhani hakuna aliyeota ama kutabiri changamoto itakuwa vipi. Tukianzia Katesh - Hanang, Mheshimiwa Rais aliacha shughuli zake zote akaenda kule. Ukitaka kujua wema, shukurani kwa Mheshimiwa Rais, mtu yeyote aende akaulize wana-Katesh Mheshimiwa Rais wanamsemaje au wanamuonaje? Walikuwa wamekata tamaa lakini leo amerudisha maisha ya wana-Hanang na wanaona

kwamba kweli Serikali ipo, hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuishia hapo, tumeona changamoto kubwa sana ambayo imekumba mikoa yetu ya Dar es Salaam, Lindi, Rukwa, Morogoro na mikoa mingine. Takriban mikoa yote 26 Tanzania Bara imepata changamoto kubwa lakini pongezi hizi wanazotoa Waheshimiwa Wabunge kwa mameneja wetu kwa kweli na mimi niwapongeze *managers* wetu. Kila palipotokea changamoto walikuwa haraka kurejesha miundombinu. Tunavyoongea sehemu kubwa hapakuwa na bajeti ya hiyo *emergency* kubwa lakini leo tumerejesha na kama mlivyomsikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Rais anatafuta fedha kuhakikisha kwamba miundombinu inarudi katika hali yake ya kawaida ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Lindi Kibiti ni kweli imechakaa na imeathirika sana. Serikali kwa kweli tunajipanga kuhakikisha kwamba barabara ile ijengwe upya lakini kabla ya kujenga upya maeneo yote yaliyoharibika yarejeshwe katika hali yake ya kawaida. Barabara nyingi za Tanzania zinaharibika haraka kutokana na ukweli kwamba kumekuwa na ukuaji mkubwa sana wa uchumi. Hatukufikiria kutakuwa na Dangote wakati tunajenga, kwa hiyo barabara kiwango kilichojengwa hakikuwa kikubwa kwa kubeba magari yale. Ukienda barabara za Kusini makaa ya mawe wanapo-*design* barabara mara nyingi wanaangalia magari ya aina gani yatapita lakini kutokana na ukuaji wa uchumi ndiyo maana barabara nyingi kwa kweli zimeenda kuchoka mapema tofauti na ilivyokuwa ime-*design*-iwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tumejifunza kwamba kila barabara inayo *design*-iwa iwe ina-*design*-iwa kwamba itabeba mizigo mikubwa. Niwahakikishie wana-Mtwara kwamba kupitia mradi wa *TanTIP* kuanzia Mtwara - Mingoyo hadi Masasi barabara inaenda kujengwa. Songea, *TanTIP* barabara ambayo imeongeleWa sana ya Makambako Songea, tunaanza Songea mpaka Lutukila pamoja na *bypass,* ni *World Bank* watafadhili. Tuna barabara

nyingi ikiwepo ya Mheshimiwa Waziri wangu Jenista, Likuyufusi - Mkenda kilometa 60 pamoja na daraja la Mitomoni. Mheshimiwa Benaya Kapinga unajua wakandarasi wapo ndani. Suala la mkandarasi yupo *site* nadhani changamoto tutazirekebisha na barabara hii tutaikamilisha kuanzia Kitai - Litui mpaka Ndumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameongea sana Mheshimiwa Kunambi lakini na Mheshimiwa Reuben. Kutokana na umuhimu wa barabara na kuunganisha mikoa, Mheshimiwa Waziri ameamua kupandisha hadhi ya barabara ya kutoka Kibena – Lupembe - Mlimba hadi Ifakara iende kwenye *trunk*, iwe *trunk road*. Sambamba na hiyo, kutoka Mikumi kwenda Dumila, kwenda Turiani, Mziha hadi Handeni ipande ili hiyo barabara iwe na uwezo wa kuunganisha mpaka bandari ya Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Reuben, Mbunge wa Handeni naomba usishike shilingi. Katika bajeti hii kama umeipitia barabara hii tunaendelea kuijenga. Tumeshajenga kilometa 45 kuanzia hapa Dumila mpaka Turiani na sasa tutaanza kujenga kilometa 30 kutoka Handeni kuja upande wa Mziha.

Mheshimiwa Spika, yote hiyo ni kuiunganisha Tanga, Handeni, Kilosa hadi Ifakara. Kwa hiyo mpango upo na tumeshaanza kujenga na mwaka huu tumeweka kwenye mpango huo wa kuijenga.

Mheshimiwa Spika, nikija Ifakara, Lupilo hadi Malinyi barabara imeathirika sana kwa Mheshimiwa Mgungusi. Hii barabara ipo kwenye *EPC* mimi nimeitembelea. Tulichokubaliana hata kama tutaanza kwa *EPC* ama kwa namna yoyote lakini maeneo yote yale ambayo ni makorofi hata kama yaanze kujengwa madaraja pamoja na maeneo korofi ili wananchi hawa hata wakati barabara inajengwa lakini yaweze kuwa yanapitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie barabara ya jiji la Mbeya, dada yangu Mheshimiwa Suma Fyandomo ameiongelea lakini na mimi pia ni mnufaika kwa sababu ili nifike Ileje lazima nipite Mbeya. Tunajua changamoto kubwa ukiwa unasafiri kwenda huko ndiyo unajiuliza nitapitaje?

Mheshimiwa Spika, kweli kumekuwa na kuchelewa lakini kuna sababu mbili kubwa. Barabara iliyokuwa inajengwa ndiyo kulikuwa na miundombinu ya maji, miundombinu ya umeme na miundombinu ya simu ambayo imechukua muda sana kuiondoa kwa sababu ilikuwa lazima uiondoe kwanza, uiunganishe ndiyo uitoe na ndiyo barabara zijengwe lakini kukaja pia na mvua ikanyesha sana. Nina hakika kwa jinsi ulivyochangia Mheshimiwa Suma Fyandomo tumesikia na kwa sababu mkandarasi yupo *site* sasa hivi ni kumsukuma aweze kwenda kwa kasi inayostahili ili hizo kilometa 29 ziweze kukamilisha na nikumbushe tu ndiyo barabara ambayo inapeleka magari yote yanayotoka Dar es Salaam kwenda Tunduma. Kwa hiyo ni moja tu katika Jiji la Mbeya. Kwa hiyo Wizara inatambua na ndiyo maana ilikuja na huo mpango wa kuijenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wanawake na vijana tumekuja na mpango mpya, tuliona wanawake wengi wanaachwa nyuma. Tunavyoongea hizo kilometa 20 tulishatangaza na kuna kandarasi tano zitakazo kuwepo hapo ambazo tayari tupo kwenye manunuzi kuwajengea uwezo. Tutakachokifanya kama Wizara pamoja na *TANROADS* ni kuwasaidia kwenye *management* namna ya kuendesha miradi mikubwa kama hiyo. Pia, tulichofanya Wizara yetu pamoja na Wizara ya Fedha kwamba sasa tutoke wazawa kuwa na miradi inayoishia thamani ya shilingi bilioni 10 twende shilingi bilioni 50 ikiwa ni kuwajengea uwezo lakini pia kuhakikisha kwamba fedha nyingi na miradi mingi inajengwa na wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusu *TBA;* kuna watu wamegusia *TBA*. *TBA* ni wakala wa nyumba. *TBA* kazi iliyokuwa inafanya ni kujenga majengo ya viongozi wa Serikali na watumishi. Haikuwa inafanya biashara. Mheshimiwa Rais

alipoingia akasema hapana toka nje ya *box* na hasa baada ya kuona *Magomeni Quarters*. Tumebadilisha muundo na sasa hivi *TBA* watafanya kazi na *private sector.* Kwa hiyo yale mawazo mliyokuwa nayo watafanya biashara na watapangisha. Kwa hiyo tunahakika watakuwa na uwezo mkubwa wa kujenga majengo mengi hususan katika Mji wa Dodoma, kwa sababu ilikuwa siyo rahisi kufanya hivyo kutokana na sheria yake ya muundo.

Mheshimiwa Spika, *TEMESA* kwa wakazi wa Dar es salaam. Julai *TEMESA* watakubaliana ama wataingia makubaliano na Azam kuendesha kwa *PPP* ama kwa *JV* ili kuhakikisha kwamba sasa watu wengine *private* wanaweza wakaendesha vivuko pale kupunguza changamoto iliyopo. Pia, itakuwa ni kusaidia kuboresha uendeshaji wa kile kivuko ambacho tumeona kwamba kwa utaratibu uliopo hauwezi kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe tu kabla sijamaliza kwamba wakati tunapata uhuru mwaka 1961, Tanzania tulikuwa na barabara za lami kilometa 1,360 lakini katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga na kukamilisha kilometa 1,198.5. Unaweza ukaona kazi lakini kilometa tulizonazo ni kilometa 12,000 za lami. Kwa hiyo unaweza ukaona kazi kubwa ambayo ameifanya katika kipindi hiki kifupi na bado tuna miradi mingi mikubwa ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, tuna miradi ya kimkakati ya hapa Dodoma na Mheshimiwa Waziri alieleza vizuri sana nini kinaendelea kuhusu *ring road*, *inner* na *medium*. Pia, tuna-*decongest* mji wa Dar es salaam. Tunatakaku- *decongest* mji wa Mwanza kuhakikisha kwamba watu wanakwenda kwa uharaka sana na tuna miradi ya kielezi ambayo tumeeleza vizuri sana Kigongo Busisi ambayo tuna uhakika Disemba itakamilika. Kwa hiyo kazi zote hizo zinaendelea kufanyika na tuna hakika tutafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la fidia, niongelee kidogo kuhusu fidia. Tuna mambo mawili; fidia kutokana na sheria yetu ambayo imetupeleka kwenye meta 60. Meta 7.5 ndiyo limekuwa

tatizo kubwa sana na Serikali kupitia Wizara tunafanya uchambuzi kuona; je, ni kweli maeneo yote tunahitaji hizo meta 60? Kama siyo, sheria yetu lakini inatuelekeza tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mipango ya ku-*divert* kwenye miji na kuangalia maeneo *specific* ambayo tutayaona kama kweli tunahitaji halafu tutapeleka Serikalini watayapitia kwa maana ya viongozi wa Kiserikali tuone halafu Serikali itakuja na tamko tufanye nini kuhusu fidia kwa watu wanaopisha barabara kulingana na sheria yetu ilivyo. Kwa sababu tumeona ni kweli watu wamesimamishiwa majengo yao kwa muda mrefu na imekuwa ni changamoto lakini kwa 22.5 kwa maana ya 45 lazima tuwafidie, tuwalipe ndiyo waweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, miradi ya *TanTIP*. Tunayo miradi sita ya *TanTIP* ambayo inatekelezwa na *World Bank* ambayo ni barabara za Iringa Msembe, Kiwanja cha Ndege cha Iringa, Kiwanja cha *Lake Manyara* na Kiwanja cha Tanga. Miradi hii yote ipo kwenye hatua za manunuzi na tupo kwenye *evaluation*, kwa hiyo muda wowote miradi hiyo itaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho niendelee kuwasihi Waheshimiwa Wabunge, ili tuweze kufanya shughuli zozote tunahitaji barabara. Kwa hiyo tunaomba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha mtupitishie bajeti ili tuendelee na kazi yetu kuhakikisha kwamba Tanzania inatembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona dhamira ya Mheshimiwa Rais ipo, anaiunganisha nchi na anaifungua nchi. Kwa hiyo niwashawishi tunaomba bajeti yetu ipitishwe tukatekeleze na kupitisha bajeti ya ujenzi maana yake umesaidia pia kwamba sekta zote, wakina mama waende wakatibiwe, watoto waende shuleni lakini pia mazao yatoke shambani yafike kwenye masoko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Ujenzi aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa nyingine ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuhitimisha hoja ya Bajeti ya Wizara yetu ya Ujenzi ambayo niliwasilisha jana. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kupita salama katika kipindi kigumu cha mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya. Nitumie nafasi hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano ambao mlitupa kipindi hiki ambacho kilihitaji subira na ushirikiano. Pia, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge katika majimbo yenu mlitupa ushirikiano mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa namna ambavyo unaongoza Bunge letu Tukufu kwenye mjadala wa bajeti yetu kuanzia jana tumekuwa pamoja nawe. Pia, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wenyeviti, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika pamoja na Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama kwa namna ambavyo walikusaidia katika mjadala ambao umekuwa wa siku mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana rafiki yangu, ndugu yangu Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya - Naibu Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kunisaidia katika majukumu ambayo Mheshimiwa Rais ameniamini kumsaidia kama Waziri wa Ujenzi pale ambapo ninafanya vizuri ni kwa sababu nina Naibu Waziri ambaye ananipa ushirikiano wa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru mbele yako pamoja na Waheshimiwa Wabunge wezangu, Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya nakushukuru sana na niendelee kuwaomba wananchi wa Jimbo la Ileje wamepata jembe kweli kweli. Mheshimiwa

Mhandisi Kasekenya tunamuamini ni mchapakazi na ni mzalendo; nawaomba wananchi wa Jimbo la Ileje waendelee kukulea na kukutunza na mwakani wakurejeshe hapa Bungeni ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa ufafanuzi mzuri ambao amenisaidia kutoa kwenye hoja hii. Mheshimiwa kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile, niwashukuru wasaidizi wetu ndani ya Wizara. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Kasekenya lakini niendelee kumshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Taasisi na Watumishi wote ndani ya Wizara na taasisi zake kwa namna ambavyo wanaendelea kuchapa kazi ili kutusaidia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kusimamia Dira ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ndani ya Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Wale ambao mmechangia kwa kuzungumza mlikuwa 77 na wale ambao mmechangia kwa maandishi mlikuwa wa nne kwa hiyo jumla hoja yetu imechangiwa na Wabunge 81. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana, hata wale ambao hamjapata nafasi ya kuchangia tunawashukuru kwa ushirikiano wenu, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge letu ya Miundombinu inayoongozwa na kaka yangu Mheshimiwa Selemani Kakoso, akisaidiwa na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti mama yetu Mama Anne Kilango Malecela na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa sana ambao wanatupatia Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninyi ndio *think tank* ya Wizara yetu, mnatushauri vizuri, mnatuelekeza vizuri, tunashirikiana vizuri,

tunawashukuru sana na tunawahidi tutaendelea kuwapa ushirikiano. Maoni na ushauri wa Kamati ambao mmetupatia tunakwenda kuutekeleza. Ahsanteni sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia na kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa. Hata kipindi kigumu cha mvua za *El-Nino* na Kimbunga cha Hidaya. Mheshimiwa Rais na sisi Wizara ya Ujenzi tuendelee kushukuru kwa kuwekeza na kuwezesha Taasisi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa kuwa ya kisasa, kwa sababu uwezo wa taasisi hii umetuepushia madhara makubwa ambayo yangetokea kwa mvua hizi kubwa ambazo tumezipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ya Mamlaka ya Hali ya Hewa imeweza kuwa inatoa utabiri sahihi na kutusaidia kuchukua tahadhari. Kwa hiyo, tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji huu kwa Mamlaka ya Hali ya Hewa. Tunamshukuru pia kwa shilingi bilioni 72 ambazo alituwezesha ili kuweza kuwanusuru Watanzania pale miundombinu ilipoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hiki ambacho Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekisema. Mheshimiwa Rais aliagiza Wizara ya Fedha wakae na sisi tubainishe mahitaji ya kurudisha barabara ambazo zimeharibika baada ya mvua kwisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimeona ametupa habari njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, tulipopata madhara ya *Covid* hakuna aliyejua kwamba Serikali hii bunifu yenye Mheshimiwa Rais mwenye *vision* tungepata shilingi trilioni 1.2 za *IMF*. Kipindi hicho tofauti na nchi nyingine ambazo zilitumia mabilioni ya pesa kwenye kununua vitakasa mikono na barakoa, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa dira yake aliona fedha hizi tuzitumie kwa kujenga miundombinu ambayo inadumu kizazi hiki

na vizazi vijavyo na akaelekeza tujenge shule za msingi, sekondari, vituo vya afya na tununue vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hizi fedha za dharura ambazo Mheshimiwa Rais ameelekeza Wizara ya Fedha watafute fungu, sisi tumewasilisha shilingi trilioni moja ya kurudisha miundombinu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema hapa. Sisi tumejipanga kwamba fedha hizi tutakazozipata hatutakwenda kukwangua barabara na kuziba mashimo, kwa sababu baada ya mwaka mmoja, miaka miwili ukiuliza mabilioni haya ambayo tutapata yametumika wapi? Itakuwa ni ngumu ku-*point* mahali ambapo fedha hizi zimetumika.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kurudisha madaraja na makalavati katika maeneo ambayo yamekatika ili hata mwakani Mwenyezi Mungu azuie, ikitokea tumepata mvua kubwa tunakwama, kwa sababu mvua ikisomba daraja huwezi ukalirudisha ndani ya wiki moja wala ndani ya mwezi. Kwa hiyo, fedha hizi ambazo Wizara ya Fedha inaziandaa kwa ajili ya kurudisha miundombinu ambayo imeharibilka Wizara ya Ujenzi tumejipanga kuhakikisha tunazipeleka kwenye kujenga madaraja na makalavati na itakuwa ni nchi nzima kulingana na uharibifu ulivyotokea.

Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, sisi kile ambacho Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekisema tayari tumeanza kujiandaa kwa ajili ya fedha ikipatikana na kiangazi kinapoingia basi tuingie katika kurudisha miundombinu ambayo imeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kujibu hoja za jumla, lakini nimeona, Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtupitishie bajeti hii kwa sababu tunazo barabara ambazo zipo juu ya 70% katika utekelezaji, haziwezi zikaishia njiani. Hii hii hela ambayo tumewezeshwa tunaomba mtupitishie ili tukaweze kukamilisha barabara 12 ambazo utekelezaji upo juu ya 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Noranga – Itigi – Mlongoji kilometa 25 ipo 72%, Ruangwa – Nanganga kilometa 50 ipo 76%, Tanga - Pangani kilometa 50 ipo 72%, Kidatu – Ifakara kilometa 66.9 ipo 88%, Itigi – *Township Road* kilometa 10 ipo 98%, *Kanyani Junction* – Mvugwe, kilometa 70.5 ipo 78% na Mvungwe – *Nduta Junction* kilometa 59 ipo 73%, *Nduta Junction – Kibondo Junction* – Kabingo kilometa 62.5 ipo 97%, *Lot I* Nala – Veyula – Mtumba – *Ihumwa Dry Port* kilometa 52.3 ipo 71%, Muheza – Amani kilometa nne ipo 98%, *BRT I Improvement* kilometa 20.3 ipo 99% na *BRT II* ipo 99%. Kipande cha bajeti ni kwenda kukamilisha hii miradi 12 ambayo ipo juu ya 70% kwenye utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna *JP Magufuli Bridge* lipo 89%, tunahitaji sehemu ya bajeti hii tukakamilishe daraja hili ili Disemba kama tulivyowaahidi Watanzania tuweze kulikamilisha daraja hili. *(Makofi)*)

Mheshimiwa Spika, tuna viwanja wa ndege; Kiwanja cha Ndege cha Iringa kipo 86%. Miradi ambayo ipo kwenye utekelezaji chini ya 70% inabidi tuitoe ilipo tuipeleke kwenye kuikamilisha 100%. Tuna barabara Ntendo – Muse – Kilyamatundu sehemu ya Tendo – Kizungu kilometa 25 ipo 44%, kuna barabara ya Matai – *Kasesya Road, Lot I,* Matai - Tatanda kilometa 25 ipo 34% na kuna barabara ya Isonje - *Makete Road* sehemu ya Kitulo – Iniho kilometa 36.3 ipo 4.2%, kuna barabara ya Itoni – Lusitu kilometa 50 ipo 22%, kuna barabara ya Mogabiri – Nyamongo kilometa 25 ipo 41%, kuna barabara ya Uvinza-Malagarasi kilometa 51.1 ipo 51%, kuna barabara ya Kumnazi – Kasuro – Bugene – Kyaka – Mtukula *(Lot II),* Bugene – Burigi – Chato kilometa 60 ipo 31%.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya Mnivata – Mnitesa kilometa 100 tupo kwenye maandalizi ya ujenzi, kuna barabara ya Mitesa – Masasi kilometa 60 tupo kwenye maandalizi ya ujenzi, kuna barabara ya Tamko – Mapiga kilometa 13.59 tupo kwenye maandalizi ya ujenzi kuna barabara ya Iringa – Ipogolo – Kilolo kilometa 33.61, Mheshimiwa Nyamoga nimekusikia, tumeanza maandalizi ya barabara hii, *Kagera Sugar Junction* – Kakunyi

kilometa 25 tupo kwenye maandalizi ya ujenzi, Tarime – Mogabiri kilometa 61, tupo kwenye maandalizi ya ujenzi Sabasaba – Sepuka – Ndago kilometa 77.4 tupo kwenye maandalizi ya ujenzi, Amani – Makoro – Luanda kilometa 35 utekelezaji tupo 25%, Mheshimiwa Benaya nimekusikia, tutakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua mkandarasi huyu ameharibu mahali pengine, barabara ambazo alikuwa ameshasaini tumemnyang'anya tumewapa wakandarasi wengine ambao wanaweza wakafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tungamaa – Mkange kilometa 95.2 tupo 31.3%, barabara ya Mianzini – Ngaramtoni kilometa 18 tupo 42%, barabara ya Ifakara – Mbingu kilometa 62.5 maandalizi ya ujenzi *(advance payment)*, Mheshimiwia Kunambi nimekusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbulu – Garbabi kilometa 25 tupo 28%, maandalizi ya kujenga barabara ya Labay – Haydom kilometa 25 tupo kwenye maandalizi, Lusahunga – Rusumo kilometa 92 tupo asilimia tano, Utete – Nyawage kilometa 33.7 tupo asilimia mbili, Kasulu – Manyovu na Kasulu *town links* kilometa 68.67 tupo 63%, *Ihumwa Dry Port* – Matumburu – Nala kilometa 60 tupo 60%, *Kikombo Junction* – Chochoro – Mapinduzi – *Ntyuka Junction* – Mvumi – Makulu kilometa 25 tupo 47%, Sanzate – Nata kilometa 40 tupo 44%, Vikonge – Luhafe kilometa 25 tupo 57% na Luhafe – Mishamo kilometa 37 tupo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kibaoni – Mlele kilometa 50 tupo 14%, *Nduta Junction – Kibondo Town – Kibondo Junction* kilometa 25.9 tupo 63%, Kibondo – Bambamba kilometa 47.9 tupo 10%, Itigi – Mkiwa kilometa 31.6 tupo asilimia mbili, Handeni – Mafuleta kilometa 20 tupo 41%, *Iringa By Pass* kilometa 7.3, inakwenda kwa awamu lakini tumeanza, Uyole – Ifisi kilometa 29 tupo 12.5%, kwa Mheshimiwa Spika, lakini tunakwenda kuongeza kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *BRT III* kilometa 23.3 tupo 26.5%, *BRT IV* kilometa 30 maandalizi ya ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Spika, kuna Sengerema – Nyehunge kilometa 54.5, mkandarasi yule ambaye ameshindwa kwa kina Mheshimiwa Kinanasi tumefuata hatua za kimkataba, tumemnyang'anya barabara hii. Tumeweka mkandarasi ambaye atakwenda kufanya kazi na kule Sengerema – Nyehunge vivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *rehabilitation* ya Ibanda – Kajunjumele, Kajunjumele – *Kiwira Port* na *rehabilitation* ya Kajunjumele – *Itungi Port* kilometa 32 kwa asilimia mbili, Kizota – Zuzu – *SGR* kilometa 14 tupo 25%, Maneromango – Kisarawe kilometa 3.1 tupo 30%, Goba – Matosa – Temboni kilometa tatu, tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi kilometa 3.7 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Chanika – Mbande kilometa 3.8 tupo 55% hatua hiyo, Morogoro – Bigwa – Mvuha kilometa 78, tunaanza maandalizi ya kujenga, Nachingwea – Ruangwa kilometa 57.6, tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kibada – Mwasonga kule Kigamboni kilometa 26.7 tunaanza maandalizi ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ubena Zomozi – Ngerengere kilometa 11.6 tunanza maandalizi ya ujenzi, Luanda - *Ndumbi Port* kilometa 50 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Mbingu – Chita kilometa 37.5 tunaanza maandalizi ya ujenzi, *Kizengi Weight Bridge* Tabora kule Nyahua Chaya maandalizi ya ujenzi wa daraja na *Kogwa Junction* – Nghambi – Mpwapwa kilometa 32 tunaanza maandalizi ya ujenzi. Kagwila – Kasekese kilometa 54 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kasekese – Ikola kilometa 56.9 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Ndungu – Mkomazi kilometa 36 tunaanza maandalizi ya ujenzi, *Isongole Two* - Ndembo kilometa 46.5 tunaanza maandalizi ya ujenzi. Katumba – Lupaso kilometa 35.3 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Mbaka – Kibanja kilometa 20.7 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kyerwa – Murushaka kilometa 50 tunaanza maandalizi ya ujenzi Ntyuka – *Mvumi Hospital* – Kikombo kilometa 53 tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kahama – Bulyanhulu

– Kakola kilometa 73 tunaanza maandalizi ya ujenzi na Tatanda – Kasesya kilometa 25 tunanaza maandalizi ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hizi ni barabara ambazo zipo katika hatua mbalimbali utekelezaji wake upo chini ya 70%, lakini kipande cha bajeti hii ni kwenda kuendelea na kazi. Tunaomba mtu-*support* Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madaraja, Daraja la Pangani – Tanga tupo 23%, Mbambe – Pwani tupo 15%, Simiyu – Mwanza tupo 15%, Lowa – Mpiji (Dar es Salaam) tupo asilimia mbili na mkandarasi huyu ameshindwa kazi kwa hiyo tunafuta hatua za kimkataba kumuondoa tumuweke mkandarasi mwingine. Daraja hili kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi mto umepanuka, hivyo nimeelekeza tufanye usanifu mpya ili mkandarasi tutakayempata atujengee daraja ambalo litakuwa na kizazi hiki na vizazi vijavyo. Mheshimiwa Subira Mgalu nimekusikia, kile kipande cha kwenda Mapinga tutafanya utaratibu ili kije *TANROADS* ili barabara hiyo yote iweze kuhudumiwa na *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambazo zinaingiliana, unakuta kipande hiki kipo *TARURA* na kipande kingine kipo *TANROADS,* Mheshimiwia Waziri Mchengerwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kaka yangu tumekubaliana, tumeunda timu ipitie barabara hizo tuangalie ni barabara zipi ziwe za *TARURA* na barabara zipi ziwe za *TANROADS* kulinga na uhalisia na uhitaji, tunafanya hilo kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Daraja la Milumba kule Katavi tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kibakwe hapa Dodoma tunaanza maandalizi ya ujenzi, Kelema Maziwa Dodoma tunaanza maandalizi ya ujenzi na Sukuma kule Mwanza tunaanza maandalizi ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyo viwanja vya ndege ambavyo vipo katika hatua za ujenzi chini ya 70%; *Msalato Airport,* Musoma,

Tabora, Shinyanga, Sumbawanga na Kigoma. Vilevile tuna miradi iliyosainiwa ambayo inahitaji malipo ya awali *(advance payment)* Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema hapa, lakini kuna vifungu vimeshikilia ili *advance* tutakavyoipata kupitia bajeti hii ambayo tunaomba tukatekeleza miradi ya barabara 26 ambazo tayari tumesaini.

Mheshimiwa Spika, muda ungekuwa unatosha ningezisema barabara hizi ili kila mmoja wenu aone kazi kubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge mmefanya katika kufuatilia barabara hizi zikafanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu wa kina zikaingia kwenye manunuzi mpaka hatua za kusainiwa. Ni hatua kubwa ninaomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ni hatua na miaka yote barabara hatujazijenga kwa wakati mmoja…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri dakika tatu malizia. Muda wetu umekwenda.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, zipo barabara ambazo mmepambana zimefika hatua tumemaliza upembuzi yakinifu, tumefanya usanifu wa kina na sasa zipo kwenye hatua ya kuingia kwenye manunuzi. Kadiri tunavyopata fedha kila mwaka wa fedha, kile kinachopatikana wakandarasi wanajenga katika awamu tofauti. Huyu ana-*raise certificate,* huyu anasaini. Hivyo hivyo *TRA* wanakusanya na Serikali inaongea na wafadhili wa maendeleo. Mtandao wote wa barabara za *TANROADS* ambao tumeujenga, tumeujenga kwa utaratibu huu. Kwa hiyo, niwaombe mtuamini na ninawashukuru kwa pongezi.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa kupambana katika kusimamia ujenzi ninaona mna imani na sisi. Kwenye suala la

upatikanaji wa fedha Wizara ya Ujenzi, niwape mfano, *Road Fund* kwa mwaka inapokea takribani trilioni moja, lakini *cash flow* hiyo tunaongea na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, ukichukua hela hiyo kwa wakati mmoja labda hela ya miaka mitano hizo ni kama trilioni tano.

Mheshimiwa Spika, kuna benki, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango wakiridhia tutaangalia namna ambavyo tunaweza tukapata hiyo *future cash flow* ya *Road Fund* tukaipata sasa hivi. Tukajenga barabara kwa wakati mmoja, halafu kwa vile *TRA* ikikusanya hela ipo kwa mujibu wa sheria inaenda kwenye *Road Fund,* basi hiyo hela, kama ni *infrastructure bond* inakuwa inatumika hiyo ambayo inakusanywa kila mwaka kwenda kuhudumia ile *bond* ambayo tayari tuliipa *future cash flow,* tukapata *lump sum* moja, tutajenga barabara zetu zika-*support* uchumi, tukatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Ujenzi, tumepeleka *proposal* yetu Wizara ya Fedha, Wizara ya Uwekezaji na Mipango. Kwa hiyo, mtuamini tuendelee na hatua hizi ambazo tumewaletea huku mengine tuliendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaomba sasa nitoe hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hela tunachukua hizi zilizopo kwenye kitabu. Toa hoja Mheshimiwa, sema natoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.................Sh. 2,125,597,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na kuna majina mengi mengi hapa yanayotaka ufafanuzi. Pengine kwa sababu yaliletwa majina kabla ya Mheshimiwa Waziri, hajatoa ufafanuzi labda kuna ambao wameelewa wakati akihitimisha hoja. Kwa hiyo, pengine wanajitoa.

Mheshimiwa Charles Muguta Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika bajeti ya mwaka huu ambayo inakamilika mwezi wa sita Wizara imetengewa shilingi 1, 419,843,057,000 lakini mpaka muda huu imeshapokea zaidi ya 1,421,842,330,490.81 yaani kuna ziada ya zaidi ya 2,000,000,000 lakini bado kuna malalamiko ya wakandarasi kutokulipwa pesa zao. Je, pesa hizi zimeenda wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Kajege kwa swali lake, kwa mfumo wa bajeti yetu, bajeti ya maendeleo huwa tunaitumia kulipa madeni. Kwa hiyo, inaonesha tumelipa asilimia 100 lakini tumelipa ile *portion* ya deni kwa kiasi hicho ambacho kimetengwa lakini bado tunaendelea kulipa madeni kama takwimu tulivyozionesha kwenye bajeti. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege naona umesimama.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia kwamba nitakamata shilingi yake kama hatokuja na mazuri. Kumekuwa na madeni yanaongezeka kila mwaka; na hapa sijaona mpango mahususi wa Wizara hii kulipa haya madeni, sasa haya madeni yatalipwa namna gani?

**MWENYEKITI:** Sawa, uzuri wake umeshakaa kabla haujatoa hoja, kwa hiyo umefanya jambo la heri. Ulishaketi Mheshimiwa ulishaketi lakini wacha nimpe fursa, Mheshimiwa Waziri afafanue, Waziri wa Fedha naona umeshika shika kisemeo sasa ukishika sina hakika ndiyo unaashiria unataka kusema ama? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Sekta Mheshimiwa Bashugwa kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wakienda wakafuatilia vitabu watatambua kwamba madeni ya sekta hii tulishayalimbikiza kwa muda mrefu sana na kwamba tungeamua katika mwaka wa fedha mmoja kushughulika na madeni tu maana yake tusingeweza kutekeleza miradi mipya. Kwa hiyo, tunachokifanya tunalipa madeni na kwa kuwa wakandarasi wapo *site* miradi inayoendelea tunailipia kwa *certificate* na ndiyo maana tumepanga fungu linakuwepo kwenye Wizara ya Kisekta lakini pia utaona tutakapokuja kwenye Wizara ya Fedha kwenye mfuko mkuu tunaweka pia bajeti ya kulipia madeni yakiwemo madeni ya Wizara ya Ujenzi pamoja na madeni ya watoa huduma na watoa huduma wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tangia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie mnaona kwamba bajeti ile ya kulipia madeni iliongezeka mwaka hadi mwaka na hata sasa imeongezeka. Kwa hiyo, mpango mkakati mkubwa tunaofanya, moja ni kuendelea kutokuyazalisha madeni ndiyo maana mnaona tunajaribu ku-*align* sana bajeti lakini pili kuendelea kuyalipa yale ambayo tulishayatengeneza. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kadri tunavyoongeza hali ya kifedha tutaendelea yale madeni ya nyuma na vile vile kuendelea ku-*align* kazi pamoja na upatikanaji wa fedha ili tusitengeneze madeni mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, ili na sisi Bunge tuwe tumekaa sawa kama bajeti iliyokuwa imetengwa kwa mwaka wa fedha huu tunaomalizia imetolewa kwa ukamilifu na kuzidi maana yake kilichokuwa kinatarajiwa kufanywa ndani ya mwaka wa fedha uliopita kilipaswa kuwa kimefanyika. Hii sehemu ya madeni ilikuwa ni sehemu ya ile bajeti? Au madeni haya yote ya bilioni 900 ni ya kuanzia 2023, 2022 kurudi nyuma? Yaani haya ya mwaka huu mpya ya fedha hatujazalisha madeni kwa sababu fedha zote mlizoomba mmepewa na Wizara ya Fedha kwa mujibu wa takwimu hizi kama zipo sahihi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni mfumo ambao upo wa Wizara na Hazina, malimbikizo ya madeni kila mwaka tunapewa *sealing* ya kuendelea kulipa kiasi cha deni ambalo ni *accumulative*. Kwa hiyo, kwenye mwaka huu wa fedha hicho ndicho kiasi tulitengewa kwa ajili ya *development,* lakini kulipa madeni ambayo ni *accumulative* ya miaka ya nyuma.

**MWENYEKITI:** Haya Waheshimiwa nadhani mmeelewa namna madeni yatakavyolipwa. Haya, mwingine anayetaka ufafanuzi. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, sera yetu ya Kitaifa kwenye ujenzi wa barabara ni kuunganisha Mikoa yote Tanzania Bara kwa kiwango cha lami. Ipo mikoa mpaka sasa ambayo haijaunganishwa kwa kiwango

cha lami ukiwepo Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Morogoro kwa barabara ya Handeni – Mziha - Turiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti yao na kwenye kitabu chao wamesema taratibu za kumpata mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa Ujenzi sehemu hii zinakwenda kufanyika. Imekuwa ikiripotiwa hivi toka bajeti ya mwaka 2021/2022, imeripotiwa hivyo 2022/2023, imeripotiwa hivyo 2023/2024 na leo inaripotiwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wasipotoa ufafanuzi unaoridhisha hapa, dhamira yangu ya kushika shilingi ipo pale pale. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sawa sasa ngoja nielewe vizuri, kama nimeelewa vizuri maelezo unayoyatoa ni kuhusu hiyo barabara ambayo ipo Jimboni kwako, nimeelewa sawa sawa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaja kwamba kuna mikoa mingi ambayo haijaunganishwa kwa lami kinyume na matakwa ya sera na kwa sababu ya muda sikuweza kutaja, lakini kama unanipa muda naweza nikataja mikoa ambayo haijaunganishwa kwa lami. Nimetolea mfano wa barabara hiyo kwa sababu ni mfano ambao nimependa niuzungumzia katika hizo barabara nyingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimuombe kaka yangu Mheshimiwa Reuben asishikilie shilingi moja kwa moja kwa sababu nilishatembelea jimbo lake, barabara ya Tanga - Handeni kuja mpaka Dumila anajua mipango ambayo tunayo ndani ya Wizara. Lakini ningependa kumuomba hatua ambayo tumefanya kwanza barabara ya kutoka Tanga - Handeni kuja Mziha - Dumila - Mikumi mpaka kule Ifakara kuifanya *trunk road* kwenda mpaka Mlimba - Lupembe mpaka kule Njombe - Kibena ni katika kutayarisha barabara hii iwe na hadhi inayostahili kuwa *trunk road.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari nilishatangaza na sasa hivi tunaendelea na huo utaratibu lakini pia kwenye vipaumbele vyetu tumekiri kwamba maendeleo ni hatua. Bado tunaendelea kuunganisha nchi yetu mikoa kwa mikoa. Nadhani ni kipaumbele kama cha pili au cha tatu kwenye mapendekezo ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Reuben nchi yetu tunajitahidi kuijenga kwa kadri rasilimali fedha zinavyopatikana. Hata hii halitatushinda Mheshimiwa Reuben. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Reuben amekaa kwa hivyo ameelewa. Mheshimiwa Halima James Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ningeomba Mheshimiwa Waziri unijibu wewe kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amejibu sijamwelewa, kwa hiyo, naamini wewe nitakuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPC+F* hii inasimama kwa *engineering* (uhandisi) pia inasimama *for procurement* (Ununuzi) C inasimama *for construction* (Ujenzi) na F inasimama kwa *funds* (Ufadhili). Kwa hiyo, kwa lugha nyingine ni kwamba kuna watu wanakuja ambao wana jukumu ya kufanya haya majukumu mengine manne. *TANROAD* wanachofanya ni usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niitaka nisaidiwe, kwa mujibu wa Taarifa ya Mkaguzi ya Mwaka huu inasema hivi masharti ya zabuni katika nyaraka za zabuni za *EPC+F* zilizochapishwa kwenye *TANEPs.* Wazabuni walitakiwa kuwasilisha angalau mapendekezo ya wafadhili wawili wa zabuni husika. Kwa hiyo, zabuni yenyewe mtu hadi anashinda zabuni maana yake ni kwamba tayari ana uhakika wa wafadhili, ana uhakika wa chanzo cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali mkaenda mkasaini mikataba na mkasema katika 129 wamekidhi wanne. Sasa tunataka utuambie tu kiukweli kwamba kwenye hili

tulikwama kwa sababu kitu kinachonitatiza ni nini? Sisi tunafata hotuba yako, ukurasa wa 36 inasema Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *EPC+F* kwanza Serikali sasa hivi si inatafuta wafadhili, inatafuta mikopo kwa miradi ambayo mnaitekeleza nyie. Hii *EPC+F* ilikuwa ni wakandarasi wanashindanishwa wamekidhi vigezo vinne unawapa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima sekundi 30 malizia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumalizia nataka tu ufanunuzi kwa kwamba kwa maelezo ya Waziri wa Fedha maana yake ni hivi, yale maneno ambayo Mheshimiwa Mbarawa alituambia mwaka jana kwamba kuna hiki kitu kinachoitwa *EPC+F* tumefeli na sasa Serikali tunaanza kufadhili miradi wenyewe kwa sababu lugha ya *EPC+F* na kilichozungumzwa kwenye hotuba na anachozungumza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni vitu vitatu tofauti. Naomba kama Waziri wa dhamana unijibu.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Usiponijibu vizuri nitashika shilingi yako, ukinijibu vizuri sitashika shilingi yako kwa sababu nataka ufafanunuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ili ni jambo la kifedha na *instrument* inanitaka nilielezee. Haya maneno ya kiingereza yasituchanganye. *EPC+F* ni namna hii, kwamba unaweza ukampa mkandarasi akujengee hata kama ni nyumba kwa utaratibu wa *material* yote na kila kitu na *design* wewe unamlipa kazi tu ile ya ukandarasi lakini unaweza ukampa

akujengee kila kitu halafu wewe unabeba mzigo wa kumlipa yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika Mheshimiwa Halima anasema kwa nini Serikali inasema inajadiliana? Sasa nakuuliza wakati tunaingia mkataba, riba kwenye soko la dunia ilikuwa kati ya asilimia nne mpaka tano. Tunavyoongea sasa hivi riba zipo kwenye asilimia 10 -12. Mheshimiwa Halima wewe ndiyo ungekuwa Serikali ungemwambia endelea tu kwa sababu mzigo huo utabebwa na Watanzania? Huwezi ukafanya hivyo, Serikali yoyote makini, Serikali yoyote inayowajibika kwa wananchi wake haiwezi ikawabebesha tu mzigo wananchi kwa sababu kulikuwa na mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa soko limechafuka tunaendelea kuona kwamba hii hali si ya kudumu itarejea katika hali ya kawaida. Kwa maana hiyo wana wajibu ule ambao walitakiwa kuleta fedha lakini riba zimeshabadilika tofauti na tulivyo sasa hivi. Kama hivyo ndivyo sisi tukaona kwa kuwa ambavyo wanasema watapata fedha na soko la dunia limeharibika sisi kama Serikali ambayo inawajibika, tumeona ni vyema wataendelea kutafuta fedha zile watapata katika masharti ambayo yapo sambamba na yale ambayo tuliwapitia. Lakini si kwamba jambo hili sasa sisi tunaenda kutafuta fedha hizo ili tuweze kutafuta kwenye bajeti, la hasha. *EPC+F* itaendelea na masharti yale yale lakini katika masharti ambayo hayawabebeshi Watanzania mzigo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *EPC+F* ikiwa Serikali ndiyo itatafuta hizo fedha je, watapewa wakandarasi hawa au mtafuata utaribu wa kisheria ambao upo wa kupata wajenzi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPC+F engineer* anafanya hii kazi ya ku-*design* pamoja na kujenga lakini *financier* atakuwa anapeleka fedha kwenye kulipia yale *material;* na kwa sababu kunakuwepo na masharti kwenye *financing* ambayo yanahusisha upatikanaji wa fedha na *material* ambazo

zinatakiwa ziende kwenye fedha. Ile fedha haiendi mfuko mkuu ndiyo itolewe kwenda…

**MWENYEKITI:** Hapo hapo uliposimama, Mimi nataka tuelewane kabla sijamrejeshea mwenye hoja, sisi wote Bunge tuwe tumeelewa hii *EPC+F* ni nini? Kama zile fedha inatafuta Serikali, zitaendaje kule moja kwa moja bila kupita huku Serikalini? Kama zinakuja Serikalini kwa nini wapewe hawa? Si tufuate utaratibu wa kawaida wa kwamba Serikali imeshakusanya fedha? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPC+F* ile *F* hatafuti Serikali, anatafuta…

**MWENYEKITI:** Maelezo yaliyopo kwenye Kitabu cha Waziri yanaleta hiyo changamoto. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayaleti changamoto kwa sababu hata kwenye reli nawapa mfano ulio hai…

**MWENYEKITI:** Huo tumeshaujua, Mheshimiwa unacho kitabu chako hapo? Hebu leta hicho kitabu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuelezea hiki.

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa inaonekana yale maneno hujayapata hasa yameandikwa nini.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo hotuba na mimi.

**MWENYEKITI:** Kama hayo ndiyo yaliyoandikwa mbona yana tofauti na hicho unachosema wewe? Serikali inaendaje kutafuta fedha ili impe nani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikilizane vizuri. Utaratibu wa *financing*, niwape mifano iliyo hai, *Lot 3* na *Lot 4* na *Lot 5…*

**MWENYEKITI:** Hapana, wewe tupe hapo kwenye vitabu kwa sababu utatuchanganya na hizo *Lot*. Tupe tu hii ya ujenzi halafu tusome. Tukishaelewa tu hatuna neno, tupe tu hayo maneno aliyotoa Mheshimiwa Waziri hapo yanamaanisha nini halafu tunatoka hapa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma kipengele cha 36 na msikatae kupokea mifano kwa sababu hata Yesu alifundisha kwa mifano.

**MWENYEKITI:** Hapana, sasa Mheshimiwa Hapana Hapana, wewe tupe mfano huo tunaotaka sisi. Sisi tunataka barabara zijengwe, reli tumeshamwelewa Mheshimiwa Dkt. Samia na zinajengwa kule hamna changamoto, changamoto ipo kwenye barabara. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninachosema.

**MWENYEKITI:** Haya endelea tusomee hapo uliposema unataka kutusomea.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo napenda kulihakikishia, kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa dhamira ya Serikali ni kutekeleza miradi hiyo ya *EPC+F* bado ipo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa inafanyikaje? Tunatoa *mandate* kwa yule anayefanya *financing*, Hivi ndivyo ambavyo tunafanya. Lakini tukishatoa *mandate* tuna-*engage ECA's,* anaye-*guarantee* hawa watu ni Serikali.

**MWENYEKITI:** *On whose behalf Mr. Minister? On whose behalf?* Kwa sababu nyinyi hawa watu mmewapa kazi na wao wameonesha uwezo wao. Baada ya kuonesha uwezo, ndiyo maelezo tuliyopewa kwenye kitabu cha mwaka jana alichotusomea Mheshimiwa Waziri. Sasa hapa ukitueleza kwamba Serikali ndiyo inatafuta fedha sisi tunaona kwa nini Serikali itafute fedha ili impe huyu? Serikali ikatafute fedha, turudi kwenye taratibu wa kawaida wa sheria zetu. Kwa nini apewe huyu? Maana yake yeye alionesha ana uwezo, kama uwezo hana sisi Serikali tutafute fedha tujenge kwa utaratibu wetu. Kwa nini tutumie hii ambayo yeye katudanganya? Haya Mheshimiwa Waziri umeshaeleweka. Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimsaidie Waziri kwamba mikataba ilivyosainiwa lengo lilikuwa hao mliowasainia ndiyo walete pesa sio Serikali ilete pesa. Sasa ngoja nikusomee kidogo Taarifa ya Mkaguzi halafu nitoe hoja. Mkaguzi ameseme hivi, ya Taarifa ya Ukaguzi wa Mwaka 2024. "sababu ya kuchelewa kuanza kwa mradi ni kutokana na wakandarasi kushindwa kuwasilisha dhamana ya benki ya utendaji kazi yenye dhamani ya shilingi bilioni 375.5".

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Kwamba mliingia mkataba nao waliwaambia wana vyanzo vya fedha mkasaini mkataba likataka kwamba wawasilishe dhamana ili utaratibu wa kazi uanze, wakashindwa ndiyo maana tumefeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba *access* ya *government funding* haipo. Kwa hiyo, ninaomba kutoa hoja hili jambo tulijadili kwa mapana yake kwa sababu tunakoelekea tutapotezana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kumi wamefika?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo tumefika na tumezidi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sawa lakini ngoja tuelewane jambo moja. Nimeshawaona, hoja imeungwa mkono. Subirini kwanza. Hoja imeungwa mkono. Nataka nimpe fursa Mheshimiwa Waziri ambaye ndiyo ametusomea hii hotuba yake ili atoe ufafanuzi wa haya maneno kabla hamjaanza kuchangia halafu tukaanza humu ndani kila mtu analeta elimu yake kila mtu alivyoelewa. Yaani wote tuwe na uelewa unaofafana ili tunapoingia kwenye mchango basi tujue tunachangia nini.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi ambao ameutoa. Neno 'Ufadhili' kwenye kitabu nadhani ni *limitation* ya *vocabulary* kwenye Kiswahili chetu lakini haimaanishi kwamba tunatafuta wafadhili. Ni kwamba kupitia huo utaratibu wa *EPC+F*, *EPC+F* ni *vehicle* moja wapo ya kupata *financing*, kuna *vehicle* ya *PPP* ambayo nayo tuna i-*promote*. Kuna *vehicle* hii ya *EPC+F*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPC+F* ni *pure loan* ambayo unaichukua kutoka *private sector* kwenda kujenga barabara kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa dhamira njema ya Serikali ya kuchelewesha jambo hili ili tulifanye katika namna ambayo haitaturudisha kama wiki mbili zilizopita, humu humu Bungeni tulikuwa tunalalamika mikopo kausha damu. Sasa tukikopa kwa *rate* ambazo tukaenda tukajenga barabara, unakuta barabara ambayo tungeijenga kwa hela ya kujenga kilometa tano, unajenga kilometa moja; si Bunge hili hili mtahoji kwamba kwa nini mlichukua mikopo hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo dhamira ya Serikali ni njema. Tunatafuta tukope wakati sahihi kwa riba sahihi. Tusije tukajenga barabara hizi kwa sababu ya *pressure* ya kujenga barabara haraka halafu humu humu, hata Mheshimiwa Halima

jana ulijenga hoja kwamba riba ambayo ime-*accumulate* kama ingeenda kujenga barabara, zingekuwa ni barabara kilometa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende haraka na hii miradi ya *EPC+F* tukope kwa gharama yenye riba kubwa halafu unakuta badala ya ukuijenga barabara kwa kiasi cha kujenga kilometa moja katika *conventional methods* za ujengaji wa barabara zetu, unakuta mkopo huo yaani kwenye kilometa tano ambazo zingejegwa katika riba ambayo ni *reasonable*, unajenga kilometa moja kwa huu utaratibu wa *EPC+F*. Kwa hiyo, Serikali tunachelewa ili tuweze kukopa katika riba sahihi. Watanzania wasije wakatuuliza kwamba mlichukua hii mikopo katika mazingira yapi? Kwa hiyo, hiyo ndiyo dhamira, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Mheshimiwa Waziri kwenye hii hotuba yako kwenye aya ya 40 kwenye haya maneno ya hapa mwisho, kwa sababu haya ndiyo yameleta kidogo changamoto. Hapo mwishoni kabla ya aya ya 41. Sijajua kama aya zinafanana, nenda ukurasa wa 36 juu kabisa hapo. Umefika? Inasema; "Serikali inaendelea na mazungumzo na wafadhili ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi hiyo."

Hii sentensi yaani huku mwanzoni huku ilivyoenda haina shida na sentensi inayofuata baada ya hapo kwa sababu ni Serikali inatoa *commitment* kwamba hiyo miradi itatekelezwa; hii haina shida. Shida iko hapa kwamba, Serikali ni kama vile kwa huo huo mlengo kwamba maneno ya Kiswahili labda ni machache, sentensi hii ikisomeka hivi ilivyo, inaashiria kwamba Serikali inazungumza na wafadhili ili fedha zipatikane ili miradi ya *EPC+F* iweze kutekelezwa. Hiyo ndiyo changamoto ya hii sentensi. *(Makofi)*

Sijui kama umeelewa kwa nini sentensi inaleta changamoto. Mheshimiwa Waziri, kama umeelewa tusaidie, uweke vizuri sasa hii kwa maneno yoyote utakayotumia ili tutoke hapa tuvuke. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, ni *limitation* ya *vocabulary* kwenye Kiswahili. Kwa hiyo, naomba nisahihishe kwamba tunaweza tukasema; "Serikali inaendelea kuwafuatilia wakandarasi walioingia mikataba ya *EPC+F* katika kupata mikopo ambayo iko katika kiwango ambacho ni *acceptable*."

**MWENYEKITI:** Haya. Maneno ya hiyo sentensi atayatafuta vizuri. Waheshimiwa Wabunge, si mmemwelewa Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Nadhani tunaweza kusonga hapo. Serikali haitawatafutia watu wa *EPC+F* fedha isipokuwa inaweza ikaweka hayo mazingira ya wao kwenda kupata fedha huko kwingine. Kwa sababu kwa utaratibu wetu wa kisheria, Serikali ikitafuta fedha itatakiwa ifuate ule utaratibu wa kutangaza, kufanya nini ili watu waombe na siyo kumpa huyu kwa sababu yeye aliingia mkataba kabla. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya kusema hayo, nadhani tunaweza kusonga. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto.

**MWENYEKITI:** Jamani si mmeelewa sentensi ile ameirekebisha Mheshimiwa?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto.

**MWENYEKITI:** Bado hamjaelewa hii *EPC+F?*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Haya sawa. Basi Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia wasimame. Haya watachangia Waheshimiwa Wabunge wachache sana kwa sababu muda wetu umekwenda. Kwa hiyo, niende na waliokuwa wamesimama mwanzo ama niliowaona mimi mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Olelekaita. Huku inabidi nigeuke nimwone mmoja. Mheshimiwa Mohamed Issa. Mheshimiwa Profesa Mbarawa... *(Makofi/Kicheko)*

Haya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Haya nani mwanamama? Hamna neno Waheshimiwa, sisi wote tunajenga nyumba moja. Sasa hapa mmesimama wengi kwa hiyo tukubaliane. Muda wetu umekwenda, Mheshimiwa Olelekaita, Mheshimiwa Mohamed Issa, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, hapa inabidi awakilishwe na mwanamama Mheshimiwa Kunti. Halafu tutafunga hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umesimama mwanzo kwa kuzungumza. Nawaona wote. Mimi sina neno tukubaliane tusonge. Mimi sina neno tukubaliane tusonge, maana nawaona wengi bado mmesimama na muda wetu mnauona pale. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatosha hao.

**MWENYEKITI:** Haya wanatosha si ndiyo? Wote wamesema wanatosha jamani. Haya Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi niseme nimesimama kwa sababu kuna mambo fulani ya kisheria sheria hapa yamezungumzwa ambayo tunataka tujadili ili tuweze kuishauri nchi yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kwamba hii *paragraph* imeleta mkakanganyiko mkubwa sana. Nakushukuru kwa hilo.

Alivyokuwa anaongea Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tumesaini mikataba tarehe 16 Mwezi wa Sita mwaka jana na kwa mujibu wa mkataba kama utakuwa umeandikwa vizuri, maana yake riba itakuwa imeandikwa vilevile. Sasa kama imetokea mabadiliko ya riba kwa sababu ya uchumi wa dunia, hiyo mpya itaingiaje kwenye mkataba ambayo ilishakuwa *negotiated*. Kwa hiyo, kuna *issue* hapa ya kisheria *unless* Mheshimiwa Waziri angekuwa anatuambia kwa sababu ingeweza kuwa ni hasara ya wale waliosaini. *Unless*, angesema kwamba hawa wanakataa kuendelea kwa sababu wanasema wanataka tu-*renegotiate* ile riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo sentensi *is not coming clear*. Sasa tutaonekana kama hapa mkataba ulikwisha kusainiwa halafu riba mpya inakuja halafu *automatically* itaingiaje kwenye mkataba. *There is an issue* ya kisheria hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu mikataba, Mimi ni *beneficiary* wa barabara hizi. Tulisaini na ulikuwepo muda maalumu wa kumaliza mikataba hii. *It is almost one year now* unakwisha na *actually*, ni kama Serikali inaelekea kuvunja mkataba. Kwa hiyo, *already we are in problems* kama hizi *delay* zitaendelea kuwepo na muda unakwenda, kwa hiyo, *we are likely to be sued.* Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani kuna issue hizi za kisheria tuweke sawa ili mambo yaende vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa, wachangiaji mnaofuata, hoja ya riba haimo kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri hoja ya riba haipo na ninasema hivyo vziuri tu ili tuwe tumeelewana vizuri. Hata kama wametoa ufafanuzi hapa lakini ile hoja ilikotokea, hoja ya riba na kwa namna tunavyoielewa wote hapa wote uelewa ni kawaida. Mimi siyo mtaalamu wala wengine pia pengine siyo wataalamu ni jambo jipya. Hii *EPC+F* hii hoja ya riba imekuja kwenye ufafanuzi lakini hapo kwamba ndiyo jambo lililozuia hii mikataba kufanya kazi. *(Makofi)*

Sasa tusije sisi ndiyo tukawa tume... Mheshimiwa Waziri amesema kwenye ufafanuzi lakini pia na Mheshimiwa Waziri amesema. Ninachojaribu kusema ni kwamba kwenye kitabu chao haipo kwamba hiyo ndiyo sababu. Hawajasema kwamba hiyo ndiyo sababu, hawajasema.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani walisema kwamba *the reason* kwa nini hizi barabara haziendelei ni kwa sababu riba imekuwa kubwa.

**MWENYEKITI:** Wametoa maelezo hapa. Nilikuwa naweka hiyo tofauti kwamba, hapa ndani Mawaziri wote wawili wametoa maelezo lakini kwenye kitabu chao hayapo...

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ifutwe pia hiyo kwenye labda... *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, uzuri watapata nafasi ya kuzungumza. Nitawaita kwa hiyo wao wenyewe wataamua kama wafute yale ya mwanzo ama bado yanasimama.

Mheshimiwa Mohamed Issa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwanza sisi Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa tufahamu kwamba sisi ni wawakilishi wa wananchi lakini wale walioko kule mtaani siyo kwamba hawafahamu tunachokijadili, siyo kwamba hawafahamu Kiingereza kama alivyosema Mheshimiwa Mwigulu. Wanafahamu na wanatufuatilia lakini wanaangalia kwenye *system* na kwenye mitandao, wanajua kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo lililowazi kabisa kwamba tunapoingia mkataba, tukishindwa ku-*meet conditions* za mkataba tunaadhibiwa. Sasa basi tusiende mbali sana kusema

kwamba soko la kimataifa au soko la dunia limeharibika. Tulikuwa na mfumo wetu ambao ulikuwa unafahamika *CPC* ambapo fedha tulikuwa tunatafuta wenyewe. Hii tulikuwa tunakwenda hivyo hivyo tunajikokota. Sasa Mheshimiwa Waziri pale akaja na suala linguine CPC + F. Maana yake yule...

**MBUNGE FULANI:** *EPC+F*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** ... *EPC+F*, ni ulimi tu. Maana yake ni nini? Kwamba yule *contractor* wetu atakuja na *financer* wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoingia mkataba maana yake nini? Ni kwamba yule sasa anachukua nguvu ya kushinda ile *tender*. Wale wakandarasi wetu ambao wapo hapa hawana *financer* washindwa kupata zile. Sasa mimi nashangaa kwa nini tunaenda sasa kufuatilia tena fedha, mtu ambaye alisema ana fedha. Hii inaonesha kwamba hii *EPC+F* ina njia fulani ya rushwa. Hili ambo linatakiwa liangaliwe na lichunguzwe kwa sababu siyo jambo la kawaida kusema kwamba *EPC+F* halafu tuseme tunatafuta fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachokisema ni kwamba...

**MWENYEKITI:** Haya naambiwa hapa kengele imeshagonga.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** ...tuendelee na mkataba kama ilivyokuwa mwanzo.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ameshaketi. Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru. Serikali inatuchanganya, mwaka jana Mheshimiwa Profesa Mbarawa alikuja hapa akatuambia kwa kuwa sisi kama Taifa vyanzo vyetu vya mapato hatuwezi kujenga barabara hizi kwa pesa zetu za ndani. Kwa hiyo, tunachokifanya kama Taifa, tunakwenda kutangaza tupate wakandarasi ambao watakuwa

na wafadhili watakao wapatia fedha, wajenge barabara hizo sisi tuje tuendelee kuwalipa kidogo kidogo. Ndicho tulichoambiwa hapa na tukahakikishiwa kwamba barabara hazi zitakwenda zote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo wanakuja tena na kigeugeu kingine kwamba, Serikali inakwenda sasa kutafuta, kujadiliana mazungumzo na mkandarasi ni namna gani tunakwenda kutafuta fedha tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatuchanganya.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ukija hata kwenye mazungumzo yao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mchango mzuri anaoutoa. Ninafikiri labda kwa maelezo aliyoyaeleza Mheshimiwa Waziri niongezee. Nina-*feel* nia yake anayoumia lakini pia kwa sababu zile fedha hata hawa wakienda kukopa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alikuwa amesema, bado Serikali itatakiwa iwalipe wale waliokopa. Kwa hiyo, Serikali lazima iwe kwenye mazingira ya kuona itakuja kulipa kiasi gani? Kama wamekopa kwa wakati ambao ni mbaya, *interest rate* ziko juu, bado na sisi tutatakiwa kulipa kwa *interest rate* ambazo ziko juu. Nilipenda kumwongezea tu wifi yangu hilo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa yake siipokei kwa sababu sisi suala la riba tulishasaini mkataba kwa riba iliyokuwepo, tuliyokuwa tumekubaliana. Sasa suala tena na kigeugeu hapa kwamba riba imebadilika sijui vitu gani, yaani mimi...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kengele imegonga. *(Kicheko)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nahitaji maelezo ya kina kwenye suala hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Mheshimiwa Nchemba ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu ambayo yamejibiwa leo na Serikali ni majibu ya tatu. La kwanza tuliambiwa kwamba miradi hii imechelewa kwa sababu ya *detail design* inafanyika upya na wakandarasi na majibu hayo yako kwenye *Hansard*. La pili tukaja tukaelezwa na hawa Mawaziri kwamba 10% tunatakiwa kuwalipa wakandarasi ndiyo waanze kujenga miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jibu la leo tena la kwamba wanatafuta *financing* ni jibu la tatu. Kwa sababu Mawaziri hawa wameshaji-*contradict* kwa kila jambo na wameshafeli kwenye hii miradi ya *EPC+F*, tunaomba mambo mawili yafanyike. Moja, wakiri kwamba walilidanganya Bunge. La pili, ile miradi ifutwe kwenye vitabu vya Serikali na mikataba hiyo ivunjwe, kwa sababu kama hawa wakandarasi tulioingia nao mkataba wameshindwa kukidhi takwa la kisheria la jinsi tulivyosaini nao mkataba na leo ni mwaka wa pili sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara tunayoyapata sisi ambao tunapitiwa na hii miradi, tumeondolewa kwenye mipango ya Serikali kwa sababu sisi tuko kwenye *EPC+F*. Moja, maana yake ni kwamba Serikali hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele imegonga.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba ni jambo moja kwamba, kwa sababu tunapata hasara kubwa, mwaka 2023 tuliondolewa, mwaka huu 2024/2025 tumeondolewa, sasa bajeti hii ifumuliwe na hii *EPC+F* ifutwe kwenye vitabu vya Serikali ili mipango ipangwe upya na sisi tuweze kuingizwa kwenye mipango ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Mbarawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Nchemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, ajiandae.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru sana na mimi kunipa fursa hii kuzungumzia hili jambo letu la *EPC+Finance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPC+Finance* kama walivyosema wenzangu, *Engineering Procurement na Construction plus Financing, means* ni kutafuta fedha na wajibu wa kutafuta fedha ni wa mkandarasi. Kwanza iwe *very clear*. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi tunazungumza *in terms* na *conditions* sisi Serikali, kwa sababu hatuwezi tu kumruhusu mkandarasi akaleta riba ya asilimia 10, hatuwezi tu kumruhusu Mkandarasi akaleta *grace period* ya miaka miwili ndiyo tulipe hilo deni, lazima kuna utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote ya *EPC+ Finance* si mara ya kwanza nchi hii kuingia, tuna *lot three, lot two* na *lot four* hivi sasa toka tume-*sign* zaidi ya miaka...

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarawa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

## TAARIFA

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yasichanganywe, hatujawahi nchi hii kutumia mfumo wa *EPC+F* na kama Mheshimiwa Waziri anayasema haya kwa maana ya kutuchanganya atuletee ushahidi tuliyoutumia kwenye *SGR EPC+F* hatujawahi kufanya huu mchezo na utaratibu huu wa *financing* ulishakataliwa hapa nchini miaka yote, Mheshimiwa Waziri Mbarawa ndiyo kauleta hapa katudanganya na kututapeli sisi, sijui alikuwa na maslahi gani katika mkataba huo.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Profesa Mbarawa unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siipokei kwa sababu *EPC+ finance* sijauleta mim,i huo ni utaratibu ambao duniani kote unatumika. Hasa hilo la kwanza kwa vile hatua inayofuata sasa naamini Wizara ya Fedha...

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarawa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ulenge.

## TAARIFA

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa mchango mzuri wa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Nenda tu moja kwa moja kwenye taarifa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amezungumza kwamba utaratibu wa *EPC+F* unafanyika Dduniani kote, duniani kote wanapofanya *EPC+ F* hii *F* kweli analeta yule mkandarasi lakini vigezo na masharti vya nchi husika kwenye suala la mikopo inazingatiwa. Kwa maana kwamba...

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa Mwanaisha, hicho si ndicho anakisema Mheshimiwa Waziri?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima itaangaliwa kama Taifa kwenye masharti ya kukopesheka *at that particular moment* mnakopesheka? Nakumbuka nilichangia hapa mwaka jana kwamba wenzetu wa nchi kama ya South Africa huwa haikopi Serikali bali inakopa taasisi inayotengeneza barabara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulenge unatupeleka kwingine tena Serikali yetu, yaani nchi yetu sasa hivi hatukopesheki?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo watuambie labda Serikali inawezekana hilo ndiyo sharti ambalo hawataki kuliweka wazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aisha sasa, Waheshimiwa Wabunge naona jambo linakua linaleta na mambo mengine sasa hapa tena jamani. Haya Mheshimiwa Mbarawa taarifa hiyo unaipokea?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Ni maneno yale yale ambayo nilikuwa nayazungumza tu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa vile utaratibu anaozungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri ni sahihi, Mkandarasi anaenda kutafuta hiyo mikopo halafu sisi tunakaa naye kuangalia *terms and conditions* za hiyo pesa yenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngoja tukae sawa. Ni usahihi baada ya yale marekebisho kwenye ile sentensi tupo sawa sawa, fedha inatafutwa na Mkandarasi ndiyo umeanza hapo kwa kueleza vizuri si ndivyo?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi.

**MWENYEKITI:** Haya malizia mchango wako.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna makosa tu kwenye hizo *wording* za kwenye kitabu kama alivyosema mwenyewe Mheshimiwa Waziri hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Halima Mdee amezungumzia *performance bond*. Mradi wowote wa aina yoyote lazima *performance bond* iwepo, kama *EPC+ Finance*, kama *GOT Government* sijui, kama *PPP* lazima *performance bond* iwepo. Kwa vile hawa makandarasi kabla hatujafika huku kuleta hiyo hela lazima wataleta *performance bond*.

**MWENYEKITI:** Ambayo ndiyo Mheshimiwa anasema hawajaleta mpaka leo?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mapema lakini wakati ukifika lazima ataleta, inategemea lazima ataleta. Naamini sasa hivi bado na wakati ukifika *performance bond* italetwa.

**MWENYEKITI:** Jamani ile mikataba hatujaipitia kujua imeandikwa utekelezaji ni lini, labda tuliingia mikataba utekelezaji wake bado maana wewe ndiyo ulikuwa Waziri, utekelezaji wake unaanza lini wa zile *EPC+F* tulizoingia kama nchi.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mkataba sasa hivi sikumbuki ni lini lakini kuna utaratibu ambao unatakiwa kufanywa. Utaratibu wa kwanza wa kufuata *performance bond* itawekwa halafu mkopo utachukuliwa, vilevile makandarasi hao wataleta *design* kwa sababu *design* ya ile miradi inakuwa haipo na ndiyo maana *EPC+Finance,* Mkandarasi mwenyewe anaenda kufanya *design* halafu analeta, sisi tunaipitia kama *TANROADS*.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma subiri kidogo. Mheshimiwa Waziri kama hivyo ndivyo kwa nini tusingeambiwa kwamba hawa wakandarasi sasa hivi wapo kwenye hizi hatua, na siyo kwamba imeshindikana kuna sababu fulani yaani kwa nini tusingeambiwa wapo kwenye hii *engineering* hawajaingia bado *procurement,* ingetusaidia sana hata hapa tusingefika sasa hivi, kuliko sisi tunajua wangekuwa *site* hawapo *site,* kumbe wapo kwenye *engineering* halafu tutaingia *procurement,* halafu tutaingia *construction,* yaani kwa nini hatukuambiwa hivyo, mbona ingeturahisishia?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Naomba nisaidie kidogo.

**MWENYEKITI:** Ngoja amalize mchango wake Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisaidie kidogo.

**MWENYEKITI:** Ngoja amalize mchango wake. Mheshimiwa Mbarawa au kengele imeshagonga, naambiwa kengele imeshagonga, haya tumalizie wachangiaji niliokuwa nimewataja hapa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Bashungwa halafu mtoa hoja utahitimisha hoja yako.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yote ya Bunge lako Tukufu naomba tukubaliane, naomba tukubaliane, hivi vitu tunavyoongea na Watanzania wanatufuatilia ni vitu *technical*. Kuna *technicalities* nyingi mno ambazo hapa tunavyoongea tunapita juu juu sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tuliwahi kupata changamoto huko nyuma, wewe turahisishie kwa uelewa wetu hapa ndani, wewe turahisishie.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wetu wa kisera moja, *EPC+F* ile *F* siyo msaada, siyo msaada. Siyo kwamba ukimpata yule *financier* na mkandarasi wake wanaenda kujenga tu halafu wanatukabidhi wanaondoka zao ni mkopo, lakini mkopo anapewa *mandate* yule *financier* anapewa *mandate* ya kufanya *syndication,* yaani kuya-*align* mabenki mengi hivi ili aweze kuleta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hizo *arrangement* Serikali ni lazima ikubaliane na ile iliyompa *mandate* kuhusu zile *technical issues* za *financing,* siyo tu anasema nawaletea fedha na kwamba ndiyo ameshakubaliana na *contractor* halafu ndiyo imeishia hapo! Ukienda popote ambapo nchi zimelalamikiwa kwa kujenga miradi yenye gharama za juu sana ni pale waliposema *contractor* na *financier* wake wanatosha kuleta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kazi ya *financier* itabakia kuleta fedha lakini Serikali na nchi wanalazimika na wana wajibu huo wa kuhakikisha kwamba hicho kitakacholetwa ni kile ambacho hakiwapi mzigo wananchi wa nchi hiyo husika. Kwa hiyo, tunatumia fursa pia ya kujibu, Mheshimiwa Mpina alikuwa anasema haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikiliza, mwanzoni wakati tumeanza kuenga reli, wakati tunatumia bajeti, kabla ya *financier* kabla ya *contractor* kupata fedha kutoka kwa *financier* utaratibu uliotumika...

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ngoja amalize anachosema basi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliotumika kwenye reli ni huu huu wa *EPC+F,* utaratibu huu ulikuwa mpya tu kwenye barabara lakini kwenye miradi hii mingine ndicho kinachotumika.

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Dkt. Nchemba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Waziri anayezungumza aelewe kwamba tunachokizungumza hiyo *technical* anayoisema tuna ufahamu wa kutosha kuhusu hiyo *technical*. Pili, mikopo anayoizungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwanza ile fedha trilioni 3.7 haipo kwenye kasma ya mikopo tuliyoi-*approve* Serikali kwenda kukopa. Ndiyo maana kwenye vitabu vyetu vyote tuna mikopo iliyoruhusiwa kwenda kukopwa kwa maana ya bajeti ya mwaka wa fedha, hii anayoizungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya mikopo ya EPC+F ni mikopo ambayo ipo nje ya utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, Mheshimiwa Mbunge ametoka nje.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya mikopo hii ya *EPC+F* ni mikopo ambayo ipo nje ya utaratibu. Kwa hiyo, huu utaratibu anaoueleza kwamba eti tulishawahi kutumia *EPC+F* katika miradi ya *SGR*, kama kweli hilo analolisema atuletee ushahidi wa hilo jambo hapa Bungeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Dkt. Nchemba unapokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei kwa sababu Mheshimiwa Mpina anachanganya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mikopo ambayo huwa yanapitishwa na Bunge ni ya bajeti kwa bajeti kwa mwaka wa fedha husika. Miradi hii tunayoiongelea ni miradi ambayo haifanywi kwenye mwaka mmoja, hauwezi uka-*approve* kwenye Bunge miradi ambayo utatumia zaidi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo na kwenye reli, tunaenda *pace* kwa *pace* lakini fedha ile ambayo tunaipitisha inakuwa ile ambayo inapangwa katika mwaka husika. Kwa hiyo, kile ambacho huwa kinapitishwa na Bunge ni kile kitakachotumika katika mwaka wa fedha husika, yeye anataka kutaja limradi lote kwa ukubwa wake kwamba halijawahi kuwa *approved* kwa hiyo hiyo siipokei.

Mheshimiwa Spika, nimalizie.

**MWENYEKITI:** Sekunde 10.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge....

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Waziri ameomba kumalizia na nimempa muda sasa tena anapewa na taarifa tena!

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa tu.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua una nia njema na Serikali, lakini shida iliyopo hizi harakati ambazo zinafanywa leo na Serikali, kuhakikisha kwamba Serikali isiingie hasara, kwa nini inafanya baada ya ku-*sign* mikataba? Maana mikataba ile tumeshasaini, ina maana tulisaini mikataba ambayo hatujui kwamba *fluctuation* yoyote ya riba ikitokea tutaenda kuingia kwenye chaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atuambie tuliingiaje kwenye mikataba hii ambayo *fluctuation* yoyote ile ya riba tunakwenda kuingia kwenye chaka, leo haya mambo yote,

mijadala hii yote ilitakiwa ifanywe kabla ili tujue kwamba huyu anaekuja kujenga hii barabara fedha anazitoa wapi, *financer* wake atakuja na riba kiasi gani, tukisharidhika kwamba inakwenda na viwango vyetu, na kwenye ile *standard* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana tulivyoambiwa mimi nilikuwa kwenye Kamati, tulichoambiwa ni kwamba huyu atakuja na fedha Mkandarasi huyu, sisi tutakachokifanya ni kuangalia je, atajenga kwa *rate* ya kwetu na je, ubora utakuwa ule ule ndiyo hivyo vitu viwili tu ili utakapoenda kulipa tulipe barabara ambayo tumeijenga kulingana na kiwango chetu cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wameshatuingiza chaka!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu taarifa nyingine hiyo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa pia siipokei kwa sababu amechanganya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatujasema popote kwamba riba zimepanda kwenye mkataba.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mkataba ule haujabadika, sisi tulichosema narudia tena na naweka herufi kubwa, tulichosema kwenye soko la dunia pamechafuka, kwa hiyo yule mleta fedha anapata changamoto ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba mleta fedhani kwamba hazipo kwenye *briefcase*. Kama anafanya *syndication* na hicho ndicho ambacho ninachokisema kwamba mleta fedha anapata *challenge* kwenye soko la fedha.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu ile busara yako ya mwanzo uliyoionesha kumwambia Mheshimiwa Waziri wetu wa Ujenzi afafanue, kwa akili ya kawaida nadhani kuna makosa kwenye maandiko, lakini tukienda anavyosema 'dokta' mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hapa, yeye mwenyewe kazungumza kwamba kule duniani uchumi umebadilika, hivi siyo vigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa Wazungu tuangalie na hapa kwetu, tulikuwa na wakati wa *Corona*, tulikuwa na wakandarasi wazawa ambao walikuwa tayari wameingia mikataba waliumia hivyo hivyo mpaka leo. Sasa kama mtu tumeshasaini mikataba, mmefanya *due diligence* mmemaliza kila kitu, leo katikati tena kupanda kwa dola? Kuna *clause* ambayo mliiweka kwenye mkataba kwamba tutarudi tena kukaa kujadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa busara ya kawaida Waheshimiwa Wabunge, mimi ningeomba tukampa nafasi Mheshimiwa Waziri kama kuna marekebisho, hii tuje tukutane nayo kwenye bajeti kuu ndiyo tujadili hiki kitu kwenye bajeti kuu, atueleze vizuri tumpe muda tusimsulubu Mjomba wangu hapa kwa sababu tumeshaelewa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewataja hapa kwamba kuna watu tuendelee nao lakini nadhani wote tumeelewa hoja eti, si tumeielewa hii hoja na Mheshimiwa Halima pia ameelewa, haya hitimisha hoja yako Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri sentensi hapa, kwanza haya maneno hayajawekwa bahati mbaya inawezekana Mheshimiwa Waziri siyo wewe labda waliokuzunguka hawajaweka bahati mbaya, kwa sababu

wanataka ku-*shift burden* kutoka kwa wale waliyosema wanaweza kufanya kazi kutafuta vyanzo vyao kuingiza jumumu kwa Serikali, haijawekwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilikuwa nashauri yafutwe, unajua kwa nini? Kifungu cha 14 cha huu mkataba ambao Mheshimiwa Mbarawa amezungumza hapo, kwamba lazima *performance bond* iwepo. Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anasema mpaka Machi, 2024 hawa wakandarasi saba, wakandarasi wanne waliopata jukumu la kujenga hizi barabara za kilomita 2,035 wameshindwa kuweka *performance bond* ya asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia Mheshimiwa Waziri atasema, kwa sababu wameshindwa kutekeleza upande wao wa mkataba tunavunja mikataba tunaanza upya, mkianza upya ndiyo mtazingatia hayo ambayo unazungumza maslahi ya nchi na kutokukurupuka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Hii mikataba ya kilomita 2,035 kwa mujibu ya maaelezo ya Mheshimiwa Waziri Mbarawa wakati wanaazindua utekelezaji wake ni miaka mitano, ndiyo maana anajifanya hapa hawakumbuki. Kwa hiyo, mmeingia *commitment* hizi barabara zote zikamilike miaka mitano, sasa hivi mnakuja hamjui chochote halafu unasema tuangalie wataendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mimi kama nilivyosema sina shida na Mheshimiwa Waziri ni mtu mwema, tunataka tumsaidie, rekebisha haya maneno kwa mantiki ya kwamba tulioingia nao mkataba wameshindwa, na kwa sababu wameshindwa tutatangaza ili tupate wengine maisha yaendelee lakini siyo kwa hizi lugha ambazo mmeziweka.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge amehitimisha hoja yake kwa sura hiyo, kwa hivyo hakuna haja ya kuwahoji kasharejesha shilingi. *(Makofi)*

Katibu tutapitisha kwa Mafungu, tusomee Mafungu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi**

Kifungu1001– *Administration and Human Resources Management*……………..Sh. 2,125,597,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………….Sh. 749,196,600
Kifungu1003 – *Policy and Planning Division*................Sh. 738,312,500
Kifungu1004 – *Government Communication Unit*.....Sh. 249,127,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 367,092,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 324,019,800
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*..............................Sh. 303,253,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*....................................Sh. 196,216,500
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*............Sh. 94,367,400
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*.............Sh. 22,424,571,000
Kifungu 2005 – *Roads Division*.................................Sh. 53,148,257,000
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*.............Sh. 377,778,600
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*....................Sh. 309,649,600

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE – MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*…………Sh. 246,371,400

Kifungu 2002 – *Technical Services Division*............Sh. 53,105,214,000
Kifungu 2005 – *Roads Division*……………..……Sh. 1,523,448,632,100
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*..........Sh. 1,370,147,000
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*.............Sh. 109,718,349,500

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa Hoja, Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake, hivyo naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa

Waziri wa Ujenzi kuhusu Wizara yake juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki kwa hivyo wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na ninyi kuafiki niseme sasa rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge.

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Wakuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri mnazozifanya ambazo zimesifiwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, pia kwa kupokea changamoto ambazo zimesemwa na Wabunge katika maeneo mbalimbali ambayo wanawakilisha wananchi tunaamini mmezichukua na mtaendelea kuzifanyia kazi. Sasa kwa upande wa taarifa hii ya ujumla, kwa sababu ilishaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge nafikiri ni jambo la kuendelea kujifunza matumizi ya yale maneno ili yasilete huo mkanganyiko ambao unatupeleka kwa muda kwa sura hii.

Jambo lingine ni kutazama namna ambavyo, kwa sababu lugha ya mazungumzo Waheshimiwa Wabunge siyo sawa na lugha ya maandishi, kwa hiyo wakati mwingine mtu anaweza kutumia neno fulani lakini ni kwa sababu anatumia Kiswahili analitafuta kutoka Kingereza kwa hiyo na mambo kama hayo. Kwa hiyo, wakati mwingine tuchukuliane kwa sababu lugha ya mazungumzo siyo lugha ya maandishi. Lakini kwenye yale mambo mengine ambayo Mheshimiwa ameahidi hapa kwamba

wanayafanyia kazi, basi tuamini ameyachukua na atayafanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, bila shaka changamoto zote mlizozisema baadhi ya hizo changamoto zimesemwa kwenye taarifa ya Kamati ambayo Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri na Kamati yetu. Kwa hiyo, tunaamini hayo nayo ameyachukua na bila shaka kutakuwa na hayo marekebisho ya hapa na pale katika utekelezaji wa ile bajeti inayokuja. Kwa yale ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameyasema kwamba wantafuta utaratibu mzuri wa kuhakikisha Wizara hii inakuwa na fedha za kutosha kwanza upande wa madeni lakini pia upande wa miradi inayoendelea na ile miradi mipya basi nafikiri ni kipindi sasa kwa sababu tumeshapitisha hii, tutakuwa na hayo matazamio sasa ya kuona ile Bajeti Kuu ya Serikali itakapokuja itakuwa inazungumza nini kuhusu mambo haya ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anameyasema hapa ndani.

Kwa muktadha huo huo, nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, pamoja na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii mnafanya kazi nzuri, pamoja na changamoto mlizozieleza humu lakini tunawashukuru kwamba mnaendelea kuisimamia vizuri Wizara hii mpaka inafika mahali ambapo inapata pongezi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nawashukuru sana wote kwa ushirikiano katika kuhakikisha jambo hili tunalifikisha pale ambapo tumelifikisha leo.

Baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.44 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 31 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*